# *GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR*

*(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)*

**Sehemu ya CXII Nam. 6482** **8 Julai, 2013** **Bei Shs. 15,000/=**
*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* *Hutolewa kila Ijumaa*

**YALIYOMO** *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya kufuta na kuandika Sheria inayohusu Kampuni na Jumuiya nyengine, kuweka masharti madhubuti zaidi ya Uratibu na Udhibiti wa Kampuni, Jumuiya na mambo yanayohusiana na hayo.......................................................................................... 17

**SEHEMU YA SHERIA**

Tangazo la Mswada uliyotajwa hapo chini umetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili

**Tangazo la Mswada**

Nam. :- Mswada wa Sheria ya kufuta na kuandika Sheria inayohusu Kampuni na Jumuiya nyengine

---

**T A N G A Z O**

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 12 Juni, 2013 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

**ZANZIBAR** (Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
8 Julai, 2013 ***Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi*.**

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

# MSWADA
*wa*
# SHERIA YA KUFUTA NA KUANDIKA SHERIA INAYOHUSU KAMPUNI NA JUMUIYA NYENGINE, KUWEKA MASHARTI MADHUBUTI ZAIDI YA URATIBU NA UDHIBITI WA KAMPUNI, JUMUIYA NA MAMBO YANAYOHUSIANA NAYO

## KIFUNGU CHA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina fupi na tarehe ya kuanza.

**1.** Sheria hii itajuilikana kama Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2012 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri, kwa tangazo katika Gazeti Rasmi, ataiteua, na Waziri anaweza kuteua tarehe tafauti kwa utekelezaji wa vifungu tafauti vya Sehemu za Sheria hii.

Tafsiri.

**2.-**(1) Katika Sheria hii, isipokuwa ielezwa vyenginevyo:-

"hesabu" inajumuisha hesabu za pamoja za kampuni ama zilizotayarishwa katika mfumo wa hesabu au zisizotayarishwa katika mfumo huo;

"wakala" haijumuishi mshauri wa mtu anayefanya kazi kwa madhumuni hayo;

"marejesho ya mwaka" maana yake ni marejesho yanayotakiwa kutayarishwa na kampuni yenye mtaji wa hisa kwa mujibu wa kifungu cha 129 na, kwa kampuni ambayo haina mtaji wa hisa kwa mujibu wa kifungu cha 130;

"kanuni" maana yake ni kanuni za mashirikiano za kampuni, kama ambavyo imetayarishwa kiasili au kama ambavyo imerekebishwa kwa azimio maalum, ikijumuisha kwa kadiri inavyotumika kwenye kanuni za kampuni zilizomo katika Jadweli A katika Sheduli ya Kwanza;

"mkaguzi" maana yake ni mhasibu aliyethibitishwa wa Serikali anayefanya kazi katika sekta ya umma kama anavyotambuliwa na wizara yenye dhamana ya fedha;

"muflisi" na "kufilisika" zinajumuisha muflisi na kufilisika kama ilivyo katika Sheria ya Ufiflisi;

"kitabu na waraka" na "kitabu au waraka" inajumuisha hesabu, hati, maandishi na nyaraka;

"daftari la tawi" ina maana kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 125(1);

"kampuni" maana yake ni kampuni iliyoanzishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria hii;

"kampuni yenye ukomo wa dhima kwa dhamana" na "kampuni yenye ukomo dhima kwa hisa" zina maana kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 3(2);

"mchangiaji" ina maana kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Ufilisi;

"mahakama" inapotumika kuhusiana na kampuni maana yake ni mahakama yenye mamlaka ya kuifunga kampuni;

"ufungaji wa hiari wa wakopeshaji" ina maana iliyoelezwa katika Sheria ya Ufilisi;

"dhamana" inajumuisha dhamana ya hisa, dhamana na dhamana nyengine za kampuni ziwe zinagharimiwa na raslimali za kampuni au hazigharimiwi;

"faini ya ukiukwaji" ina maana iliyoelezwa katika kifungu cha 255(1);

"mkurugenzi" inajumuisha mtu yeyote ambaye anashika wadhifa wa mkurugenzi kwa jina lolote lile;

"waraka" inajumuisha samoni, taarifa, amri, na maandiko mengine ya kisheria na madaftari;

"kampuni binafsi iliyosamehewa" maana yake ni kampuni binafsi iliyosamehewa kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 134(4);

"mwaka wa fedha" maana yake, kuhusiana na shirika lolote lile, ni kipindi kilichowekwa ambacho hesabu za faida na hasara za shirika zinazowasilishwa kwake kwenye muktano mkuu zinatayrishwa, kama kipindi hicho ni mwaka mmoja au si mwaka mmoja;

"hesabu za vikundi" maana yake ni kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 160(1);

"kampuni miliki" ni kampuni miliki kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 160;

"iliyotolewa kwa ujumla" kuhusiana na muhtasari wa ununuzi wa hisa, maana yake ni iliyotolewa kwa watu ambao hawamo katika kampuni au ambao si wamilki wa dhamana ya kampuni;

"ufungaji wa hiari wa wanachama" ina maana iliyoelezwa katika Sheria ya Ufilisi;

"katiba" maana yake ni katiba ya ushirikiano ya kampuni, kama ambavyo iliandikwa kiasili au kama ambavyo imerekibishwa kulingana na sheria yoyote;

"kima cha chini cha michango" maana yake ni kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 55(2);

"ofisa" kuhusiana na shirika inajumuisha mkurugenzi, meneja au katibu;

"zilizowekwa" maana yake, kuhusiana na vifungu vya Sheria hii kuhusu ufungaji wa kampuni, kama ilivyowekwa na Taratibu zilizowekwa na Mahakama Kuu, na kuhusiana na vifungu vyengine vya Sheria hii, kama vilivyowekwa na Kanuni zilizotungwa na Mrajis;

"kampuni binafsi" maana yake ni kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 30(1);

"muhtasari wa ununuzi wa hisa" maana yake ni muhtasari wa ununuzi wa hisa, taarifa, sakula, tangazo au mwaliko mwengine, unaotoa fursa kwa umma kuchangia au kununua hisa au dhamana za kampuni;

"Mrajis" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji anayeteuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali;

"azimio la kupunguza mtaji wa hisa" maana yake ni kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 74(2);

"azimio la ufungaji kwa hiari" maana yake ni kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Kufilisika;

"taratibu" maana yake ni taratibu zilizowekwa na Jaji Mkuu kwa madhumuni ya kuratibu mwenendo wa ufungaji kwa mujibu wa Sheria ya Kufilisika, na inajumuisha fomu;

"hisa" maana yake ni sehemu katika mtaji wa hisa wa kampuni, na inajumuisha raslimali, isipokuwa iwe tafauti baina ya raslimali na hisa imeelezwa bayana au inachukuliwa kuwa ipo;

"waranti wa hisa" maana yake ni kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 90(2);

"mkutano wa kisheria" maana yake ni mkutano unaotakiwa kufanyika kwa mujibu wa kifungu cha 136(1);

"ripoti ya kisheria" maana yake ni kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 137(2);

"tawi" ni tawi kama ilivyolezwa katika kifungu cha 161;

"Jadweli A" maana yake ni Jadweli A katika Sheduli ya Kwanza;

"muda wa kufungua orodha za uchangiaji" maana yake ni kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 58(1);

"kampuni isiyokuwa na ukomo" maana yake ni kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 3(1).

(2) Mtu hatahesabiwa kuwemo katika maana yeyote ya masharti ya Sheria hii mtu ambae kwa mujibu wa maelekezo yake wakurugenzi wa kampuni wamezoea kuyatekeleza, kwa sababu tu wakurugenzi wa kampuni wanachukua uamuzi kwa kufuata ushauri unaotolewa naye kwa mujibu wa wadhifa wake wa kitaalamu.

(3) Marejeo katika Sheria hii kwa shirika au shirika itachukuliwa kuwa haijumuishi shirika peke yake bali kuwa inajumuisha kampuni iliyoungana na kampuni nyengine iliyo nje ya Zanzibar.

(4) Kifungu chochote cha Sheria hii kinachotawala au kinachofasiri mikataba ya kampuni pia itatumika kuhusiana na katiba yake kama inavyotumika kuhusiana na mikataba yake.

## KIFUNGU YA II
## USAJILI WA KAMPUNI NA MASUALA YANAYOHUSIANA NAYO

Katiba ya Ushirikiano Namna ya kuunda kampuni iliyoandikishwa

**3.**-(1) Watu saba wowote au zaidi, au ambapo kampuni itakayoundwa itakuwa kampuni binafsi, watu wawili au zaidi, walioshirikishwa kwa madhumuni yoyote halali, wanaweza kwa kuandika majina yao kwenye katiba ya ushirikiano na vyenginevyo kutekeleza mahitaji ya Sheria hii, kuhusiana na fomu ya usajili ya kuunda kampuni yenye dhima yenye ukomo au isiyokuwa na dhima yenye ukomo. Kwa madhumuni ya kifungu hiki kampuni binafsi inajumuisha kampuni yenye mwanachama mmoja.

(2) Kampuni kama hiyo inaweza kuwa ama:-

(a) kampuni yenye dhima ya wanachama wake iliyowekewa ukomo na katiba kwa kima, kama kipo, ambacho hakikulipwa kwenye hisa zinazomilikiwa na kila mmoja wao (katika Sheria hii inaitwa "kampuni yenye ukomo wa hisa"), au

(b) kampuni yenye dhima ya wanachama wake iliyowekewa ukomo na katiba kwa kiasi ambacho wanachama wake wanaweza kuchangia kwenye raslimali za kampuni itokeapo kampuni kufungwa (katika Sheria hii inaitwa "kampuni yenye ukomo wa dhamana"), au

(c) kampuni ambayo haina ukomo juu ya dhima ya wanachama wake (katika Sheria hii inaitwa "kampuni isiyokuwa na ukomo").

Matakwa kuhusiana na Katiba.

**4.**-(1) Katiba ya kila kampuni itachapishwa kwa lugha ya Kiingereza au lugha ya Kiswahili na itaeleza:-

(a) jina la kampuni, liwe na "limited" kama neno la mwisho la jina la kampuni yenye ukomo wa hisa au wa dhamana;

(b) malengo ya kampuni.

(2) Katiba ya kampuni yenye ukomo wa hisa au wa dhamana pia itaeleza kuwa dhamana ya wanachama wake ni yenye ukomo.

(3) Katiba ya kampuni yenye ukomo wa dhamana pia itaeleza kuwa kila mwanachama atawajibika kuchangia katika raslimali za kampuni

itokeapo kampuni kufungwa wakati yeye ni mwanachama, au ndani ya mwaka mmoja baada ya yeye kuacha kuwa mwanachama, kwa ajili ya kulipia deni ambazo kampuni zilitiliana saini mkataba kabla ya yeye kuacha kuwa mwanachama, na ya gharama, malipo na matumizi ya ufungaji wa kampuni, na kwa ajili ya marekebisho ya haki za wachangiaji miongoni mwao, kiasi ambacho kinahitajika, kisichozidi kiasi kilichoainishwa.

(4) Kwa kampuni yenye mtaji wa hisa:-

(a) katiba pia, isipokuwa kampuni iwe ni kampuni isiyokuwa na ukomo, itaeleza kiasi cha hisa ya mtaji ambacho kampuni inapendekeza kusajiliwa na mgawanyiko wake wa hisa zenye kima kisichobadilika;

(b) hakuna mchangiaji kwenye katiba anaweza kuchukua chini ya hisa moja;

(c) kila mchangiaji ataandika penye jina lake idadi ya hisa ambazo anachukua.

(5) Ambapo katiba ya kampuni inaeleza kwamba madhumuni ya kampuni ni kuendesha biashara kama kampuni ya kibiashara kiujumla:-

(a) lengo la kampuni ni kuendesha biashara yoyote au kufanya shughuli yeyote yoyote; na

(b) kampuni ina uwezo wa kufanya mambo yote ambayo ni muafaka au mazuri kwa ajili ya kuendesha biashara au shughuli yoyote.

Uthibitisho na saini ya Katiba.

**5.** Katiba itathibitishwa na mwanasheria anayefanya kazi za kisheria na kutiwa saini na kila mchangiaji.

Katiba kutobadilishwa.

**6.** Kampuni haitaweza kubadilisha masharti yaliyomo katika katiba yake isipokuwa katika hali, katika namna na kwa kiasi ambacho masharti hayo yamewekwa na Sheria hii.

Namna na kiasi ambacho malengo ya kampuni yanaweza kubadilishwa.

**7.**-(1) Kampuni inaweza, kwa azimio maalumu, kubadilisha vifungu vya katiba yake kuhusiana na malengo ya kampuni, kwa kiasi kinachohitajika ili kuiwezesha:-

(a) kuendesha biashara yake kiuchumi zaidi au kwa ufanisi zaidi; au;

(b) kufikia lengo lake kuu kwa njia mpya au bora; au

(c) kupanua au kubadilisha mahali inapofanyia shughuli zake; au

(d) kuendesha biashara ambayo katika hali iliyopo inaweza bila ya matatizo au kwa faida kuchanganywa na biashara ya kampuni; au

(e) kuzuia au kuachana na lengo lolote lililoainishwa katika katiba; au

(f) kuuza au kuondoa yote au sehemu ya biashara ya kampuni; au

(g) kuungana na kampuni yoyote au taasisi yoyote au mtu yeyote.

(2) Maombi chini ya kifungu hiki yanaweza kufanywa na wamiliki wasiopungua asilimia kumi na tano ya thamani ya mtaji wa hisa wa kampuni au kundi lolote linalohusika au, kama kampuni si yenye ukomo wa hisa isiwe chini ya asilimia kumi na tano ya wanachama wa kampuni.

Isipokuwa kwamba maombi hayatafanywa na mtu yeyote ambaye ameridhia au amepiga kura kuunga mkono mabadiliko isipokuwa kampuni iwe ni kampuni binafsi yenye mwanachama mmoja.

(3) Maombi chini ya kifungu hiki yatafanywa ndani ya muda wa siku ishirini na moja baada ya tarehe ambayo azimio la kubadilisha malengo ya kampuni lilipitishwa, na yanaweza kufanywa kwa niaba ya watu wenye haki ya kufanya maombi na mmoja au zaidi ya idadi yao kama watakavyowateua kwa maandishi kwa madhumuni hayo.

(4) Kutokana na maombi chini ya kifungu hiki mahakama inaweza kutoa amri ya kuthibitisha mabadiliko ama yote au sehemu yake na kwa masharti ambayo inafikiri yanafaa, na inaweza, ikiwa inafikiri inafaa, kuakhirisha kesi ili utaratibu ufanywe wenye kuiridhisha mahakama kwa maslahi ya wanachama ambao hawakuridhika, na yaweza kutoa maagizo hayo na kufanya amri hiyo kama inaweza kutoa miongozo na maagizo kadiri itakavyoona inahitajika ili kurahisisha utekelezaji wa utaratibu huo

Isipokuwa kwamba hakuna sehemu ya mtaji wa kampuni utakaotumiwa katika ununuzi wowote wa namna hiyo.

(5) Kwa upande wa kampuni ambayo, kwa mujibu wa leseni iliyotolewa na Waziri, imesamehewa kutokana na wajibu wa kutumia neno "limited" kama sehemu ya jina lake, azimio la kubadilisha malengo ya kampuni litahitaji pia kutoa taarifa hiyo kwa Mrajis kama inavyohitajika kwa wanachama wa kampuni.

(6) Pale ambapo kampuni itapitisha azimio la kubadilisha malengo yake:-

(a) Kama hakuna maombi yaliyofanywa kwa mujibu wa kifungu hiki kampuni ndani ya muda wa siku kumi na tano kutoka mwisho wa kipindi kwa ajili ya kufanya maombi hayo kuwasilisha kwa Mrajis nakala moja iliyochapishwa ya katiba iliyobadilishwa; na

(b) Kama maombi hayo yamefanywa:-

(i) Mara moja itatoa taarifa kuhusu jambo hilo kwa Mrajis, na

(ii) Ndani ya siku kumi na tano kutoka tarehe iliyotolewa amri yoyote ya kufuta au ya kuthibitisha mabadiliko,

kuwasilisha kwa Mrajis nakala iliyothibitishwa ya amri, na kuhusu amri ya kuthibitisha mabadiliko nakala iliyochapishwa ya katiba kama ilivyobadilika,

Isipokuwa kwamba Mahakama inaweza kutoa amri wakati wowote ya kuongeza muda wa kuwasilisha nyaraka kwa Mrajis kwa mujibu wa paragrafu (b) ya kijifungu hiki kuhusu muda huo kama mahakama itakavyoona inafaa.

(7) Kama kampuni inakiuka kutoa taarifa au kuwasilisha hati yoyote kwa Mrajis kama inavyotakiwa na kijifungu cha (6), kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji huo atatozwa faini kwa ukiukaji.

(8) Uhalali wa mabadiliko ya masharti ya katiba ya kampuni kuhusiana na malengo ya kampuni hautahojiwa kwa misingi kwamba haikuidhinishwa kwa mujibu wa kijifungu cha (1) cha kifungu hiki isipokuwa katika hatua zilizochukuliwa kwa madhumuni (kama chini ya kifungu hiki au vyenginevyo) kabla ya kumalizika muda wa siku ishirini na moja baada ya tarehe ya azimio kuhusiana na hatua hiyo; na ambapo hatua zozote zimechukuliwa kinyume na kifungu hiki vifungu viwili vilivyopita vitatumika kuhusiana na jambo hilo kama vile zimechukuliwa chini ya kifungu hiki na kama vile amri ya kutangaza kwamba mabadiliko yaliyofanywa ni batili ilikuwa ni amri ya kuyafuta na kama kwamba amri iliyoyafuta ilikuwa ni amri ya kuthibitisha mabadiliko.

Kanuni za Ushirikiano Kanuni zinazoeleza taratibu za kampuni.

**8.** Inawezekana kwa kampuni yenye ukomo wa hisa, na kwa kampuni yenye ukomo wa dhamana au isiyokuwa na ukomo, kusajiliwa ikiwa na katiba na kanuni za ushirikiano zilizotiwa saini na wachangiaji kwenye katiba na taratibu zilizoweka kwa kampuni.

Kanuni zinazohitajika kwa kampuni isiyokuwa na ukomo au kampuni yenye ukomo wa dhamana

**9.**-(1) Kwa kampuni isiyokuwa na ukomo kanuni zitaeleza idadi ya wanachama wa kampuni ambao inapendekeza kusajiliwa na, kama kampuni ina mtaji wa hisa, kiasi cha hisa ambazo kampuni inapendekeza kusajiliwa.

(2) Kwa kampuni yenye ukomo wa dhamana, kanuni lazima zieleze idadi ya wanachama ambao kampuni inapendekeza kusajiliwa.

(3) Pale ambapo kampuni isyokuwa na ukomo au kampuni yenye ukomo wa dhamana imeongeza idadi ya wanachama wake zaidi ya idadi iliyosajiliwa, itatoa taarifa kwa Mrajis ndani ya siku kumi na tano tokea uamuzi wa kuongeza ulipotolewa au ulipotekelezwa, na Mrajis ataweka rikodi ya ongezeko hilo.

Iwapo utekelezaji wa kifungu hiki utakiukwa, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye atahusika na ukiukaji huo atatozwa faini kwa ukiukaji huo.

Kukubali na kuitumia Jadweli A

**10.**-(1) Kanuni za ushirikiano zinaweza kukubali kanuni zote au kanuni yoyote iliyomo katika Jadweli A.

(2) Kwa kampuni yenye ukomo wa hisa, iwapo kanuni hazikusajiliwa, au, kama kanuni zimesajiliwa, kwa kadiri ambavyo kanuni hazizibadilishi au haziziengui kanuni zilizomo katika Jadweli A, kanuni hizo, kadiri zinavyoweza kutumika, zitakuwa kanuni za kampuni kwa namna ile ile na kwa kiwango sawa kama vile zilikuwa zimesajiliwa kabla katika kanuni.

Uchapishaji na utiaji saini kwenye kanuni.

**11.** Kanuni ziwe:-

(a) zimechapishwa kwa lugha ya Kiingereza au lugha ya Kiswahili;

(b) zimegawiwa katika paragrafu zenye nambari za kufululiza;

(c) zimeshuhudiwa na mwanasheria anayefanya kazi na kutiwa saini na kila mchangiaji kwenye katiba ya ushirikiano.

Kubadilisha kanuni kwa azimio maalumu.

**12.**-(1) Kwa kuzingatia Sheria hii na masharti yaliyomo katika katiba yake, kampuni inaweza kwa azimio maalumu kubadilisha au kuongeza vifungu kwenye kanuni zake.

(2) Mabadiliko yoyote au nyongeza iliyofanywa katika kanuni zitakuwa, bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, halali kama kwamba tokea awali zilikuwemo humo, na kuwa zinaweza kubadilishwa kwa namna ile ile kwa azimio maalumu.

Fomu ya Katiba na Kanuni Fomu za kisheria za katiba na kanuni.

**13.** Fomu ya:-

(a) Katiba ya ushirikiano ya kampuni yenye ukomo wa hisa;

(b) Katiba na kanuni za ushirikiano za kampuni yenye ukomo wa dhamana na isiyokuwa na mtaji wa hisa;

(c) Katiba na kanuni za ushirikiano za kampuni yenye ukomo wa dhamana na yenye mtaji wa hisa;

(d) Katiba na kanuni za ushirikiano za kampuni isiyokuwa na ukomo na yenye mtaji wa hisa, zitakuwa na fomati zilizoelezwa kwenye Majadweli B, C, D E na F katika Sheduli ya Kwanza, au fomati inayokaribiana na hizo kama hali itakavyoruhusu.

Isipokuea, Waziri anaweza, katika vipindi tofauti, kurekebisha Jadweli yoyote kati ya hizo.

Usajili wakatiba na kanuni.

**14.** Katiba na kanuni, kama zipo, zitawasilishwa kwa Mrajis ambaye atazisajili na kubakia nazo.

Usajili Athari za usajili.

**15.**-(1) Wakati wa usajili wa katiba ya kampuni Mrajis atathibitisha kwa kutia saini kwamba kampuni imeandikishwa na, kwa kampuni yenye ukomo, kwamba kampuni ni yenye ukomo.

(2) Kuanzia siku ya kuandikishwa iliyotajwa katika hati ya uandikishaji, wachangiaji wa katiba, pamoja na watu wengine ambao wanaweza kuwa wanachama wa kampuni kila baada ya muda, watakuwa ni shirika lenye jina lililomo katika katiba, lenye uwezo, kuanzia hapo, wa kutekeleza shughuli zote za kampuni iliyoandikishwa, na uwezo wa kumiliki ardhi na kuwa na uhai wa kudumu na muhuri, lakini yenye dhima kwa upande wa wanachama kuchangia kwenye raslimali za kampuni itokeapo kampuni kufungwa kama ilivyoelezwa katika Sheria hii.

Uthabiti wa hati ya kujiandi-kisha.

**16.**-(1) Hati ya kuandikishwa iliyotolewa na Mrajis kuhusiana na jumuiya yoyote itakuwa ndiyo ushahidi wa mwisho kwamba matakwa yote ya Sheria hii kuhusiana na usajili na mambo yanayohusiana nao yamezingatiwa, na kwamba jumuiya ni kampuni iliyoruhusiwa kusajiliwa kihalali hisa na iliyosajiliwa chini ya Sheria hii.

(2) Tamko la kisheria lililotolewa na wakili wa Mahakama Kuu aliyeshiriki katika kuunda kampuni, au na mtu aliyetajwa katika kanuni kuwa ni mkurugenzi au katibu wa kampuni, kwa kufuata matakwa yote au shemu yake yawasilishwe kwa Mrajis, na Mrajis anaweza kukubali tamko kama vile ushahidi wa kutosha wa kutekeleza.

Usajili wa kampuni isiyokuwa na ukomo kuwa yenye ukomo.

**17.**-(1) Kulingana na masharti ya kifungu hiki, kampuni iliyosajiliwa kama si yenye ukomo inaweza kujiandikisha kama ni yenye ukomo, lakini usajili wa kampuni isiyokuwa na ukomo kama kampuni yenye ukomo hautaathiri haki au dhima kuhusiana na deni au jukumu lililochukuliwa na kampuni, au mkataba wowote ulioingiwa na, kwa, pamoja au kwa niaba ya kampuni kabla ya kusajiliwa.

(2) Wakati wa kusajili kwa mujibu wa kifungu hiki Mrajis atafunga usajili wa zamani wa kampuni, na anaweza kutumia nakala za hati zozote zilizowasilishwa kwake wakati wa usajili wa awali wa kampuni, lakini, ila kama ilivyoelezwa mwanzo, usajili utafanyika katika hali ile ile na utakuwa na athari kama kwamba ni usajili wa kwanza wa kampuni.

Masharti Yanayohusu Kubadilisha la Kampuni Mabadiliko ya jina.

**18.**-(1) Kampuni inaweza kwa azimio maalumu na kwa idhini ya maandishi ya Mrajis kubadilisha jina lake.

(2) Pale ambapo kampuni itabadilisha jina lake chini ya kifungu hiki, Mrajis ataingiza jina jipya kwenye orodha ya usajili katika nafasi ya jina la zamani, na atatoa hati ya kuandikishwa kulingana na hali ya mabadiliko ilivyo.

(3) Mabadiliko ya jina yaliyofanywa na kampuni chini ya kifungu hiki, hayataathiri haki yoyote au wajibu wowote wa kampuni au kuathiri taratibu zozote za kisheria za au dhidi ya kampuni, na taratibu zozote za kisheria ambazo zinaendelezwa au kuanzishwa dhidi ya kampuni kwa jina lake la zamani zinaweza kuendelezwa au kuanzwa dhidi yake kwa jina lake jipya.

Uwezo wa kuacha neno *"limited"* katika jina la kampuni ya hisani na nyenginezo.

**19.-**(1) Pale ambapo imethibitika kwa kumtoshelezeka Mrajis kuwa jumuiya itakayoundwa kama kampuni yenye ukomo itaundwa kwa madhumuni ya kukuza biashara, sanaa, sayansi, dini, sadaka, au jambo jengine lolote muhimu, na inakusudia kutumia faida yake, kama ipo, au mapato mengine katika kukuza malengo yake, na kuzuia malipo ya gawio lolote kwa wanachama wake, Mrajis anaweza kuagiza kuwa jumuiya hiyo inaweza kusajiliwa kama kampuni yenye ukomo wa dhima, bila ya kuongezea neno "limited" kwenye jina lake, na jumuiya inaweza kusajiliwa ipasavyo na, ikishasajiliwa, itanufaika na fursa zote na (chini ya masharti ya kifungu hiki) itakuwa na majukumu yote ya kampuni yenye ukomo.

(2) Itakapothibitika na Mrajis kutoshelezeka kwamba:-

(a) malengo ya kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria hii kama kampuni yenye ukomo yamefungika kwenye yale yaliyoainishwa katika kijifungu cha (1) na kwenye malengo yanayohusiana nayo; na

(b) kwa katiba yake kampuni inatakiwa kutumia faida yake, kama ipo, au mapato mengine katika kukuza malengo yake na inakatazwa kulipa gawio lolote kwa wanachama wake;

Mrajis atatoa idhini kwa kampuni ya kufanya mabadiliko kwa azimio maalumu katika jina lake ikiwa ni pamoja na kuingiza au kuondoa neno *"limited"*, na vifungu vya 18(2) na (3) vitatumika kwa mabadiliko ya jina chini ya kijifungu hiki kama vile yanavyotumika kwa mabadiliko ya jina chini ya kifungu kile.

(3) Kibali cha Mrajis chini ya kifungu hiki kinaweza kutolewa kwa masharti na kwa mujibu wa kanuni kama vile Mrajis atakavyoona inafaa, na masharti hayo na kanuni hizo zitakuwa zinamfunga mtu ambaye amepewa kibali, na (ambapo kibali kimetolewa chini ya kijifungu cha (1) kitaingizwa, ikiwa Mrajis ameelekeza hivyo, katika katiba na kanuni, au katika mojawapo ya hati hizo.

(4) Shirika ambalo limepewa kibali chini ya kifungu hiki litasamehewa kutoka masharti ya Sheria hii yanayohusiana na matumizi ya neno *"limited"* kuwa ni sehemu ya jina lake, kuchapisha jina lake na kuwasilisha orodha ya wanachama wake kwa Mrajis.

(5) Kibali kilichotolewa chini ya kifungu hiki kinaweza kufutwa wakati wowote na Mrajis, na kitakapofutwa Mrajis ataingiza neno "limited" mwisho wa jina la shirika lililopewa kibali, na shirika litakoma kunufaika na misamaha na fursa au, kama hali itakavyokuwa, misamaha inayotolewa na kifungu hiki.

Isipokuwa kwamba, kabla ya kibali kufutwa, Mrajis atatoa taarifa kwa maandishi kwa shirika kuhusu nia ya kukifuta, na atalipa fursa ya kusikilizwa upinzani wake dhidi ya kufutwa huko.

(6) Iwapo shirika, kwa mujibu wa kifungu hiki, kibali chake kinatumika halitaweza kubadilisha masharti ya katiba yake au kanuni zake

kuhusiana na matakwa yaliyotajwa katika kijifungu cha (2) bila ya idhini ya Mrajis, isipokuwa kwamba Mrajis anaweza kukibadilisha kibali na kukiweka chini ya masharti na kanuni kama Mrajis atakavyoona inafaa, badala ya au pamoja na masharti na kanuni, kama zipo, ambazo kabla zilikuwa kwenye kibali.

(7) Pale ambapo kibali kilichotolewa chini ya kifungu hiki kwa shirika ambalo jina lake lina maneno "Baraza la Biashara" kinafutwa, shirika litabadilisha jina lake kwa jina ambalo halina maneno hayo, ndani ya muda wa wiki sita tangu kufutwa kibali au ndani ya muda zaidi ya huo kama Mrajis atakavyoona inafaa kuruhusu, na:-

(a) taarifa inayopaswa kutolewa kwa shirika chini ya masharti ya kijifungu cha (5) cha kifungu hiki itajumuisha taarifa ya athari za vifungu vilivyotangulia kifungu kidogo hiki; na

(b) vijifungu vya (3) na (4) vya kifungu cha 19 vitatumika kwa mabadiliko ya jina chini ya kifungu kidogo hiki na vinatumika kwa mabadiliko ya jina chini ya kifungu hicho.

(8) Kama shirika litakiuka kutekeleza matakwa ya kijifungu cha (7), shirika hilo na kila ofisa wa shirika atatozwa faini na kwa kila siku ambayo ukiukaji unaendelea itapaswa kutozwa faini ya ukikukaji.

Uwezo wa kuitaka kampuni kuacha jna linalo-potosha.

**20.-**(1) Kama Mrajis ataona kwamba jina ambalo kampuni imesajiliwa linapotosha maumbile ya shughuli zake na kuna uwezekano wa kusababisha madhara kwa umma, anaweza kuielekeza kubadilisha jina lake.

(2) Maelekezo, kama hayakutolewa maombi mahakamani kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3), yatatekelezwa ndani ya kipindi cha wiki sita tangu tarehe yalipotolewa maelekezo au ndani ya muda zaidi ya huo kama Mrajis atakavyoona inafaa kuruhusu.

(3) Kampuni inaweza, katika kipindi cha wiki tatu kuanzia tarehe maelekezo yalipotolewa, kuomba mahakama kuyaweka kando; na mahakama inaweza kuyaweka maelekezo kando au kuyathibitisha na, kama itayathibitisha maelekezo, itaainisha kipindi ambacho ndani yake lazima yatekelezwe.

(4) Kama kampuni inakiuka katika kutekeleza maelekezo chini ya kifungu hiki, itatozwa faini na, kwa kuendelea kukiuka, faini ya kukiuka.

(5) Endapo kampuni itabadilisha jina lake chini ya kifungu hiki, Mrajis ataingiza jina jipya kwenye orodha ya usajili katika nafasi ya jina la zamani, na atatoa hati ya usajili ya mabadiliko kulingana na hali, na mabadiliko ya jina yataanza kutumika kutoka tarehe ambayo hati ya mabadiliko imetolewa.

(6) Mabadiliko ya jina la kampuni chini ya kifungu hiki hayaathiri haki yoyote au wajibu wowote wa kampuni, au kuathiri taratibu zozote za kisheria kwake au dhidi yake; na taratibu zozote za kisheria ambazo zinaweza

kuendelea au kuanza dhidi yake kwa jina lake la zamani zinaweza kuendelea au kuanzwa dhidi yake kwa jina lake jipya.

**21.**-(1) Kama mtu yeyote anauza au anendesha biashara yoyote au taaluma yoyote chini ya jina au lakabu ambayo ina neno *"limited"*, au ufupisho wowote au kuiga neno hilo, kuwa ni neno la mwisho, mtu huyo, isipokuwa kihalali kabla alikuwa ameandikishwa kwa dhima yenye ukomo, atakuwa amefanya kosa.

Adhabu kwa matumizi yasiyofaa ya "ukomo".

(2) Mtu ambaye si kampuni ya umma atakuwa amefanya kosa kama anauza bidhaa, taaluma au anaendesha biashara yoyote chini ya jina ambalo linajumuisha, kama sehemu yake ya mwisho, maneno "kampuni ya umma yenye ukomo" au ufupisho wake wowote.

(3) Kampuni ya umma yenye ukomo itakuwa imefanya kosa kama katika hali ambayo ukweli ni kwamba ni kampuni ya umma inayomilikiwa na mtu yeyote, inatumia jina ambalo linaweza kimantiki kutoa hisia kwamba ni kampuni binafsi.

(4) Mtu anayetenda kosa chini ya kifungu kidogo cha (1), (2), au (3), na kama mtu huyo ni kampuni, ofisa yeyote wa kampuni ambayo imekiuka masharti, anaweza kutozwa faini na, kwa kuendelea kukiuka, kutozwa faini ya ukiukwaji.

**22.**-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, katiba na kanuni, zikishasajiliwa, zitaifunga kampuni na wanachama wake kwa kiwango sawa kama kwamba zilitiwa saini na kila mwanachama, na makubaliano yaliyomo ya kila mwanachama kuzingatia masharti yote ya katiba na ya kanuni.

Masharti ya Jumla Kuhusu Katiba na Kanuni Athari ya katiba na kanuni.

(2) Fedha zote zinazopaswa kulipwa na mwanachama yeyote wa kampuni kwa mujibu wa katiba au kanuni zitakuwa ni deni kutokana na yeye kwa kampuni hiyo.

**23.**-(1) Kwa kampuni yenye ukomo wa dhamana na ambayo haina mtaji wa hisa, kila kifungu katika katiba au kanuni au katika azimio lolote la kampuni kinachompa mtu yeyote asiyekuwa mwanchama wa kampuni haki ya kushiriki katika faida inayogawika ya kampuni kitakuwa batili.

Masharti ya katiba na kanuni za kampuni zenye ukomo wa dhamna.

(2) Kwa madhumuni ya masharti ya Sheria hii kuhusiana na katiba ya kampuni yenye ukomo wa dhamana na kwa mujibu wa kifungu hiki, kila kifungu katika katiba au kanuni, au katika azimio lolote, la kampuni yenye ukomo wa dhamana, kinachodai kugawanya jukumu la kampuni katika hisa au riba kitachukuliwa kuwa ni sharti la mtaji wa hisa, bila ya kujali kwamba kiasi cha kima au idadi ya hisa au riba hakikuainishwa.

Mabadiliko katika katiba au kanuni kuongeza dhima ya kuchangia mtaji wa hisa kutowafunga wanachama waliopo bila ya ridhaa.

**24.** Bila ya kuathiri kitu chochote katika katiba au kanuni za kampuni hiyo, mwanachama yeyote wa kampuni hatafungwa na mabadiliko yaliyofanywa katika au kanuni baada ya tarehe ambayo yeye amekuwa mwanachama, iwapo na kwa kadiri ambavyo mabadiliko yaliyofanywa yanamtaka achukue au achangie hisa zaidi kuliko idadi aliyonayo katika tarehe ambayo mabadiliko yamefanyika, au kwa njia yoyote yanaongeza dhima yake kuanzia tarehe ile ya kuchangia kwenye mtaji wa hisa wa, au vyenginevyo kulipa fedha kwa, kampuni;

Isipokuwa kwamba kifungu hiki hakitatumika katika hali yoyote ambapo mwanachama anakubali kwa maandishi, ama kabla au baada ya mabadiliko kufanywa, kufungika nayo.

Uwezo wa kubadilisha masharti katika katiba ambayo yangeweza kuwamo katika kanuni

**25.**-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 24 sharti lolote lililomo katika katiba ya kampuni ambalo lingeweza kisheria kuwemo katika kanuni za kujiunga badala ya kuwemo katika katiba linaweza, chini ya masharti ya kifungu hiki, kubadilishwa na kampuni kwa azimio maalum:-

Isipokuwa kwamba kama maombi yamefanywa kwenye mahakama kwa ajili ya mabadiliko kufutwa, hayatakuwa na athari isipokuwa kama yamethibitishwa na mahakama.

(2) Kifungu hiki hakitatumika ambapo katiba yenyewe inaruhusu au inakataza mabadiliko ya yote au yoyote ya masharti yaliyotajwa, na hayataruhusu mabadiliko yoyote au kufutwa haki maalumu za wanachama wa kundi lolote.

(3) Kifungu cha 7(2), (3), (4), (6) na (7) kitatumika kuhusiana na mabadiliko yoyote na kwa maombi yoyote yaliyofanywa chini ya kifungu hiki kama kinavyotumika kuhusiana na mabadiliko na maombi yaliyotolewa chini ya kifungu hicho.

Nakala za katiba na kanuni kupewa wanachama

**26.**-(1) Kampuni itapeleka, itakapotakiwa kufanya hivyo na mwanachama yeyote, nakala ya katiba na kanuni, kama zipo, kwa malipo kama kampuni itakavyoagiza.

(2) Kama kampuni itakiuka katika kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika na ukiukaji huo atatozwa faini ya ukiukwaji kwa kila kosa.

Nakala za katiba zilizotolewa kuingiza mabadiliko.

**27.**-(1) Pale ambapo mabadiliko yamefanywa kwenye katiba ya kampuni, kila nakala ya katiba iliyotolewa baada ya tarehe ya mabadiliko itakuwa kulingana na mabadiliko.

(2) Kama, pale ambapo mabadiliko yoyote yamefanyika, kampuni wakati wowote baada ya tarehe ya mabadiliko inatoa nakala ya katiba ambayo si kulingana na mabadiliko, itatozwa faini ya ukiukwaji kwa kila nakala iliyotolewa hivyo, na kila ofisa wa kampuni ambaye ameshiriki katika ukiukaji atatozwa faini kama hiyo.

**28.-**(1) Wachangiaji wa katiba ya kampuni watachukuliwa kuwa wamekubaliana kuwa wanachama wa kampuni, na mwanachama katika usajili wake anaweza kuingizwa kama mwanachama katika daftari la wanachama.

Uanachama wa Kampuni Fasili ya mwanachama.

(2) Kila mtu mwengine ambaye anakubaliana kuwa mwanachama wa kampuni na ambaye jina lake limeingizwa katika daftari la wanachama, atakuwa mwanachama wa kampuni.

**29.-**(1) Isipokuwa katika hali ambayo katika kifungu hiki itatajwa, shirika haliwezi kuwa mwanachama wa kampuni ambayo kampuni yake yenye kumiliki hisa, na mgao wowote au uhamisho wa hisa katika kampuni kupeleka kwenye kampuni yake tanzu utakuwa batili.

Uanachama wa kampuni yenye kumiliki hisa.

(2) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitatumika iwapo kampuni tanzu inahusika kama mwakilishi binafsi, au ambapo inahusika kama mdhamini, isipokuwa kwamba kampuni yenye kumiliki hisa au kampuni tanzu yake inanufaika kwa faida kama mdhamini na hainufaiki hivyo kwa sababu tu ya dhamana kwa madhumuni ya manunuzi yaliyofanywa nayo katika mwenendo wa kawaida wa biashara ambayo ni pamoja na kukopesha fedha.

(3) Bila kuathiri kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, kijifungu cha (1) cha kifungu hiki kitatumika kuhusiana na mteule kwa ajili ya shirika ambalo ni kampuni tanzu, kama kwamba marejeo kwenye kifungu kidogo cha (1) kwa shirika hilo yalijumuisha marejeo ya mteule kwa ajili yake.

(4) Kuhusiana na kampuni yenye ukomo kwa dhamana au isiyokuwa na ukomo ambayo ni kampuni yenye kudhibiti dhamna, marejeo katika kifungu hiki kwa hisa, kama ina au haina mtaji wa hisa, yatachukuliwa kama kwamba yanajumuisha marejeo kwenye riba kwa wanachama wake kama hivyo, haidhuru ni riba ya aina gani.

**30.-**(1) Kwa madhumuni ya Sheria hii, neno "kampuni binafsi" maana yake ni kampuni ambayo kwa kanuni zake:-

Makampuni Binafsi Maana ya kampuni binafsi.

(a) inazuia haki ya kuhamisha hisa zake;

(b) inaweka mipaka ya idadi ya wanachama wake kutozidi khamsini, bila ya kuingiza watu walio katika ajira ya kampuni na watu ambao, kabla wamekuwa katika ajira ya kampuni hiyo, walikuwa wakati wakiwa katika ajira hiyo, na wameendelea baada ya uamuzi wa kuwa katika ajira hiyo, kuwa wanachama wa kampuni; na

(c) inakataza mwaliko wowote kwa wananchi kujiunga katika hisa zozote au dhamana za kampuni.

(2) Iwapo watu wawili au zaidi wanamiliki hisa moja au zaidi katika kampuni kwa pamoja, watachukuliwa, kwa madhumuni ya kifungu hiki, kama mwanachama mmoja.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kijifungu cha (1)(b) na (2), idadi ya wanachama kwa ajili ya Kampuni Binafsi ya Mwanachama Mmoja haitakuwa zaidi ya mwanachama mmoja na hakutakuwa na hisa inayomilikiwa na zaidi ya mtu mmoja.

Matokeo ya kukiuka kufuata masharti ya katiba ya kampuni binafsi.

**31.** Ambapo kanuni za kampuni zina masharti ambayo, chini ya kifungu cha 31, yanatakiwa kuingizwa katika kanuni za kampuni ili kuiunda kuwa kampuni ya binafsi lakini ukiukaji unafanyika katika kufuata lolote katika masharti hayo, kampuni itakoma kuwa na haki ya upendeleo na misamaha inayotolewa kwa kampuni binafsi chini ya masharti yaliyomo katika kifungu cha 33 na 135(1) na hivyo masharti yaliyomo katika kifungu cha kwanza, cha tatu na cha nne cha kanuni hizo yatatumika kwa kampuni kama vile si kampuni binafsi na masharti yaliyomo katika kifungu cha pili cha kanuni hizo zitakoma kutumika kwa kampuni:

Isipokuwa kwamba mahakama, kama imeridhika kwamba kushindwa kufuata masharti kulikuwa kwa bahati mbaya au kutokana na uzembe au kutokana na sababu nyengine ya kutosha, au kwamba kwa misingi myengine ni haki na usawa kutoa nafuu, inaweza, kwa kuombwa na kampuni au mtu mwengine yeyote anayependa na kwa maelekezo na masharti kama vile yanavyoonekana na mahakama kuwa ya haki na yenye kufaa, kuamuru kwamba kampuni iondolewe kwenye matokeo kama yalivyoelezwa kabla.

Kampuni kukoma kuwa kampuni binafsi.

**32.**-(1) Kama kampuni, kwa kuwa ni kampuni binafsi, inabadilisha kanuni zake kwa namna ambayo haiingizi tena masharti ambayo, chini ya kifungu cha 30, yanatakiwa kuingizwa katika kanuni za kampuni ili kuiunda kuwa kampuni binafsi, kampuni itakoma, kutoka tarehe ya mabadiliko, kuwa kampuni binafsi na, katika kipindi cha siku kumi na nne baada ya tarehe iliyotajwa, itawasilisha kwa Mrajis, kwa ajili ya usajili taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa katika mfumo ulioelezwa na yenye maelezo yaliyowekwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Kila taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa iliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo kilichotangulia, ambapo mtu anayetoa ripoti kama vile ilivyoelezwa kabla atakuwa amefanya humo au, bila ya kutoa sababu, ameonesha humo marekebisho yoyote kama yalivyoelezwa katika kanuni, itathibitisha humo au kuambatanisha humo maelezo ya maandishi yaliyotiwa saini na wale watu waliofanya marekebisho na kutoa sababu juu yao.

(3) Kama ukiukaji umefanywa katika kutekeleza kifungu kidogo cha (1) au cha (2) cha kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye ameshiriki katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

(4) Iwapo taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa imewasilishwa kwa Mrajis chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki ina taarifa yoyote ambayo si ya kweli, mtu yeyote ambaye aliruhusu uwasilishaji wa taarifa au tamko kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa ajili ya usajili itampasa akitiwa hatiani kifungo cha jela kwa muda usiozidi miaka miwili au faini isiyozidi shilingi milioni moja, au yote mawili, isipokuwa akithibitisha ama kwamba taarifa iliyokuwa si kweli haina maana

yoyote au alikuwa na sababu ya kuamini na alifanya hivyo hadi wakati wa uwasilishaji kwa ajili ya usajili wa taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa aliamini kwamba taarifa ambayo haikuwa ya kweli ilikuwa taarifa ya kweli.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki:-

(a) taarifa iliyoingizwa katika taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa itahesabika kuwa si ya kweli kama ni ya kupotosha katika umbo na mazingira ambayo imeingizwa; na

(b) taarifa hiyo itachukuliwa kuwa imeingizwa katika taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa ikiwa imo humo au katika ripoti yoyote au mkataba unaonekana kwenye uso wake au kwa kumbukumbu iliyomo humo.

Wanachama kuwa na dhima ya pamoja ya madeni biashara inapoemdeshwa na chini ya wanachama saba, au kwa kampuni binafsi wawili.

**33.**-(1) Kama wakati wowote idadi ya wanachama wa kampuni imepunguzwa, kwa kampuni binafsi, chini ya mmoja, au, kwa kampuni nyengine yoyote, chini ya saba, na inaendelea na biashara kwa zaidi ya miezi sita wakati idadi imepungua hivyo, kwa kampuni binafsi, kila ofisa na kwa kampuni nyengine yoyote kila mtu ambaye ni mwanachama wa kampuni wakati wa kuendesha biashara baada ya miezi sita hiyo na anaelewa ukweli kwamba anaendesha biashara na mwanachama chini ya mmoja, au wanachama saba, kama hali itakavyokuwa watakuwa kwa pamoja na dhima ya kulipa madeni yote ya kampuni iliyotiliana mkataba wakati huo, na kwa pamoja wanaweza kushitakiwa kwa hilo.

Isipokuwa kwamba kifungu hiki hakitatumika kwa kampuni yenye ukomo wa dhima yenye mwanachama mmoja.

(2) Mmiliki wa hisa mmoja pekee anaweza binafsi kuwa na dhima na kushitakiwa kwa jina lake mwenyewe ambapo anakiuka masharti ya Sheria hii.

**34.**-(1) Kutaingizwa katika daftari la kampuni ya wanachama, jina na anuani ya mwanachama pekee, taarifa kwamba kampuni ina mwanachama mmoja tu.

(2) Iwapo kampuni inaundwa na watu wawili au zaidi chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii na idadi ya wanachama wa kampuni yenye ukomo inapungua hadi mmoja, au kama kampuni isiyokuwa na ukomo yenye mwanachama mmoja tu inakuwa kampuni yenye ukomo wakati wa kujisajili tena, kwa kutokea tukio hilo itaingizwa katika daftari la wanachama la kampuni, pamoja na jina na anuani ya mwanachama pekee:-

(a) taarifa kuwa kampuni ina mwanachama mmoja tu, na

(b) tarehe ambayo kampuni ilikuwa kampuni yenye mwanachama mmoja tu.

(3) Pale ambapo kampuni inaundwa na watu wawili au zaidi na idadi ya wanachama wa kampuni yenye ukomo inapungua hadi mmoja kampuni inaweza kugeuzwa na kuwa ya mmiliki wa hisa mmoja kwa kuhamisha kampuni teule kwa aliyekuwa mmiliki pekee bila ya kuhitaji kusajiliwa tena.

(4) Endapo uanachama wa kampuni yenye ukomo ya mwanachama mmoja unaongezeka kutoka mwanachama mmoja hadi wanachama wawili au zaidi, kwa kutokea tukio hilo litaingizwa katika daftari la wanachama la kampuni, pamoja na jina na anwani ya mtu ambaye alikuwa zamani mwanachama pekee:-

(a) taarifa kwamba kampuni imesita kuwa na mwanchama mmoja tu; na

(b) tarehe ambayo hali hiyo ilitokea.

(5) Kama kampuni inakiuka katika kutekeleza kifungu hiki, itakuwa ni kosa kwa:-

(a) kampuni, na

(b) kila ofisa wa kampuni ambaye yumo katika ukiukaji.

(6) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa chini ya kifungu hiki atatozwa faini.

## SEHEMU YA III
## UWEZO WA KAMPUNI NA MASUALA YANAYOHUSIANA NAO

Uwezo wa Kampuni Uwezo wa kampuni na uwezo wa wakurugenzi kuwafunga.

**35.** Uhalali wa kitendo kilichofanywa na kampuni hautahojiwa kwa msingi ya kukosa uwezo kwa sababu ya kitu chochote katika katiba ya kampuni.

Uwezo wa wakurugenzi kuifunga kampuni.

**36.**-(1) Kwa upendeleo mtu anayeshughulika na kampuni kwa nia njema, nguvu ya wakurugenzi wa kuifunga kampuni, au kuwaidhinisha wengine kufanya hivyo, utakuwa huru bila ya kikomo chochote kwa mujibu wa katiba ya kampuni.

(2) Kwa madhumuni hayo:-

(a) mtu "anahusika na" kampuni kama yeye ni mshiriki kwenye shughuli yoyote au tendo lolote ambalo kampuni ni mshiriki,

(b) mtu anayeshughulika na kampuni:-

(i) hafungiki kuuliza kuhusu mpaka wa uwezo wa wakurugenzi wa kuiwajibisha kampuni au kuwaidhinisha wengine kufanya hivyo;

(ii) huchukuliwa kuwa ametenda kwa nia njema isipokuwa ithibitishwe kinyume chake; na

(iii) asionekane kama anafanya kwa nia mbaya kwa sababu tu ya kujua kwamba kitendo kiko juu ya uwezo wa wakurugenzi kwa mujibu wa katiba ya kampuni.

(3) Marejeo ya hapo juu kuhusu upungufu kwenye uwezo wa wakurugenzi chini ya katiba ya kampuni ni pamoja na upungufu unaotokana na:-

(a) azimio la kampuni au la kundi lolote la wamiliki wa hisa, au

(b) makubaliano yoyote baina ya wanachama wa kampuni au wa kundi lolote la wamiliki wa hisa.

(4) Kifungu hiki hakitaathiri haki yoyote ya mwanachama wa kampuni ya kuleta mashauri kuzuia kufanya kitendo kilicho nje ya uwezo wa wakurugenzi.

Lakini mashauri hayo hayatahusu kitendo kinachofanyika katika kutimiza wajibu wa kisheria kilichotokana na kitendo kilichopita cha kampuni.

(5) Kifungu hiki hakiathiri dhima iliyochukuliwa na wakurugenzi, au mtu mwengine yeyote, kwa sababu ya wakurugenzi kupindukia uwezo wao.

(6) Kifungu hiki kinaathari kwa mujibu wa kifungu cha 37 (shughuli zinazowahusisha wakurugenzi au washirika wao), na kifungu cha 38 (kampuni ambazo ni za hisani).

Mipaka ya kikatiba: shughuli zinazowa-husisha wakurugenzi au washirika wao.

**37.**-(1) Kifungu hiki kinatumika kwa shughuli kama au kwa kiasi kwamba uhalali wake unategemea kifungu cha 36 (uwezo ya wakurugenzi kuwa huru na hauna mipaka kwa mujibu wa katiba ya kampuni hiyo katika kumpendelea mtu anayeshughulika na kampuni kwa nia njema).

Hakuna chochote katika kifungu hiki kitasomeka kuwa kinaondoa utekelezaji wa sheria nyengine yoyote au utawala wa sheria ambayo shughuli inaweza kuhojiwa au dhima yoyote kwa kampuni inayoweza kutokea.

(2) Pale ambapo:-

(a) kampuni inaingia katika manunuzi hayo, na

(b) na washiriki katika manunuzi ni pamoja na:-

(i) mkurugenzi wa kampuni au ya kampuni yake yenye kudhibiti hisa, au

(ii) mtu anayehusiana na mkurugenzi yeyote wa aina hiyo, manunuzi hayo yataweza kubatilishwa kwa mnasaba wa kampuni hiyo.

(3) Kama imeepukwa au haikuepukwa, mshirika wowote katika shughuli kama ilivyoelezwa katika kifungu cha (2)(b)(i) au (ii), na mkurugenzi yeyote wa kampuni ambaye aliidhinisha manunuzi, atakuwa na dhima ya:-

(a) kuieleza kampuni kuhusu faida yoyote aliyofanya moja kwa moja au si moja kwa moja kutokana na manunuzi hayo, na

(b) kuilipa fidia kampuni kwa hasara au uharibifu unaotokana na manunuzi.

(4) Manunuzi husita kuwa batili kama:-

(a) urudishaji wa fedha yoyote au raslimali nyengine ambayo ilikuwa ndilo jambo lililojadiliwa la biashara hauwezekani tena, au

(b) kampuni hiyo imelipwa fidia kwa hasara au uharibifu wowote unaotokana na shughuli hiyo, au

(c) haki zilizopatikana moja kwa moja kwa ajili ya thamani na bila ya taarifa halisi ya wakurugenzi kuzidiwa uwezo wao na mtu ambaye si mshiriki katika shughuli zitaathirika kwa kuepukwa, au

(d) manunuzi yameidhinishwa na kampuni.

(5) Mtu nmweengine zaidi ya mkurugenzi wa kampuni hana dhima kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3) kama atathibitisha kuwa wakati manunuzi yalipofanywa hakujua kwamba wakurugenzi walikuwa wanapindukia uwezo wao.

(6) Hakuna chochote katika masharti yaliyotangulia ya kifungu hiki kitakachathiri haki za mshiriki yeyote katika shughuli ambayo hayamo ndani ya kifungu cha (2)(b)(i) au (ii).

Lakini mahakama inaweza, kutokana na maombi ya kampuni au mshiriki yeyote yule, kutoa amri kuthibitisha, kupunguza au kuweka kando shughuli kwa masharti kama yanavyoonekana na mahakamani kuwa ni ya haki.

(7) Katika kifungu hiki:-

(a) "shughuli" ni pamoja na tendo lolote, na

(b) marejeo kwa mtu anayehusiana na mkurugenzi ina maana sawa na ile ya katika Kifungu ya V (wakurugenzi wa kampuni).

**38.**-(1) Kifungu cha 35 na cha 36 (uwezo wa kampuni hiyo na nguvu za wakurugenzi wa kuzifunga kampuni) havitatumika kwa matendo ya kampuni ambayo ni ya hisani isipokuwa kwa upendeleo wa mtu ambaye:- Mipaka ya kikatiba: kampuni ambazo ni za hisani.

(a) hajui wakati lilipotokea tendo lilipofanyika kuwa kampuni ni ya hisani, au

(b) anafanya mazingatio kamili katika fedha au thamani ya fedha kuhusiana na kitendo kinachohusika na hajui (kadiri hali inavyoweza kuwa):-

(i) kwamba kitendo hakiruhusiwi na katiba ya kampuni, au

(ii) kwamba kitendo kiko zidi ya uwezo wakurugenzi.

(2) Pale ambapo kampuni ambayo ni ya hisani inadai kuhamisha au kutoa riba katika mali, ukweli kwamba (kama hali itakavyojitokeza):-

(a) kitendo hakikuruhusiwa na katiba ya kampuni, au

(b) wakurugenzi waliohusika na kitendo kilichopindukia nguvu zao kwa mujibu wa katiba ya kampuni hawataathiri cheo cha mtu ambaye hatimaye atapata mali au maslahi yoyote ndani yake kwa kuzingatia kamili bila ya taarifa halisi ya hali yoyote ile inayoathiri uhalali wa kitendo cha kampuni.

(3) Katika kesi yoyote itokanayo na kifungu cha (1) au cha (2) wajibu wa kuthibitisha:-

(a) kwamba mtu alijua kuwa kampuni ilikuwa ya hisani, au

(b) kwamba mtu alijua kwamba kitendo hakikuruhusiwa na katiba ya kampuni au kilikuwa zaidi ya uwezo wa wakurugenzi, unakuwa juu ya mtu anayelishikilia jambo hilo.

(4) Kwa kampuni ambayo ni ya hisani uthibitisho wa shughuli ambayo kifungu cha 37 kinatumika (shughuli zinazowahusu wakurugenzi au washirika wao) hautakuwa na nguvu bila idhini ya Waziri ya maandishi iliyotolewa kabla.

**39.**-(1) Mkataba unaweza kufanywa:- Mikataba ya kampuni.

(a) na kampuni kwa maandishi yenye muhuri, au

(b) kwa niaba ya kampuni, na mtu anayekaimu chini ya mamlaka yake, moja kwa moja au kwa kuchukulia.

(2) Taratibu zozote zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria kuhusu mkataba uliofanywa na mtu binafsi pia zitatumika, isipokuwa pawe na madhumuni mengine, kwa mkataba uliofanywa na au kwa niaba ya kampuni.

Utekelezaji wa nyaraka.

**40.**-(1) Hati itatekelezwa:-

(a) na kampuni kwa kuipiga muhuri wake, au

(b) kwa kutiwa saini kwa mujibu wa masharti yafuatayo.

(2) Hati itatekelezwa kihalali na kampuni iwapo imetiwa saini kwa niaba ya kampuni:-

(c) na watia saini wawili walioidhinishwa, au

(d) na mkurugenzi wa kampuni mbele ya shahidi ambaye anaithibitisha saini.

(3) wafuatao ni "watia saini walioidhinishwa" kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2):-

(e) kila mkurugenzi wa kampuni, na

(f) kwa kampuni binafsi yenye katibu au kampuni ya umma, katibu (au katibu mwenza yeyote) wa kampuni.

(4) Hati iliyotiwa saini kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) na kuelezwa, kwa maneno yawayo yoyote, kutekelezwa na kampuni ina athari sawa kama kwamba imetekelezwa chini ya muhuri wa kampuni.

(5) Kwa kumpendelea mnunuzi hati inachukuliwa kuwa imetekelezwa kihalali na kampuni kama inadai kutiwa saini kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2);

Kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki "mnunuzi" ina maana ya mnunuzi mwenye nia njema kwa kuzingatia thamani na ni pamoja na muuzaji, muekewa rahani au mtu mwengine yeyote ambaye kwa kuzingatia thamani anapata riba katika mali.

(6) Pale ambapo hati inapaswa kutiwa saini na mtu kwa niaba ya kampuni zaidi ya moja, haitatiwa saini kihalali na mtu huyo kwa madhumuni ya kifungu hiki isipokuwa aitie saini tafauti kwa kila kampuni.

(7) Marejeo katika kifungu hiki kuhusu waraka kutiwa saini (au kudaiwa kutiwa saini) na mkurugenzi au katibu isomeke, katika hali ambapo ofisi hiyo inashikiliwa na kampuni, kama marejeo ya kutiwa kwake saini (au kudaiwa kutiwa saini) na mtu binafsi aliyeidhinishwa na kampuni kutia saini kwa niaba yake.

(8) Kifungu hiki kinatumika kwa hati ambayo inatekelezwa (au inadaiwa kutekelezwa) na kampuni kwa jina la au kwa niaba ya mtu mwengine kama mtu huyo pia ni kampuni au si kampuni.

Muhuri.

**41.**-(1) Kampuni itakuwa na muhuri ambao jina lake limeandikwa kwa hati zinazosomeka.

(2) Kama kampuni inashindwa kutekelza kifungu cha (1) kosa litakuwa limefanywa na:-

(a) kampuni, na

(b) kila ofisa wa kampuni ambaye amashiriki katika ukiukaji.

(3) Ofisa wa kampuni, au mtu yeyote anayefanya jambo kwa niaba ya kampuni, atatenda kosa kama atatumia, au ataidhinisha matumizi ya, muhuri unaodaiwa kuwa muhuri wa kampuni ambao jina la kampuni kama inavyotakiwa na kifungu kidogo cha (1).

(4) Mtu anayetenda kosa chini ya kifungu hiki anaweza moja kwa moja kutiwa hatiani na kutozwa faini.

**42.**-(1) Waraka unaweza kutekelezwa kihalali na kampuni kuwa ni hati ikiwa:- Utekelezaji wa hati

(a) umetekelezwa kihalali na kampuni, na

(b) umewasilishwa kama hati.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1)(b) waraka unachukuliwa kuwa umewasilishwa unapokuwa umetekelezwa, isipokuwa nia iliyo kinyume na hivyo imethibitishwa.

**43.**-(1) Kampuni inaweza, kwa waraka uliotekelezwa kama hati, kumpa uwezo mtu, ama kwa jumla au kwa mambo maalumu yaliyoainishwa, kama mwanasheria wake ili kutekeleza matendo au hati nyengine kwa niaba yake. Utekelezaji wa hati au nyaraka nyengine na mwanasheria.

(2) Hati au waraka mwengine uliotekelezwa namna hiyo, katika Zanzibar au mahali pengine, utakuwa na athari kama vile umetekelezwa na kampuni.

**44.** Hati au mashauriano yanayohitaji uthibitisho wa kampuni itatiwa saini na mkurugenzi, katibu au ofisa mwengine wa kampuni aliyeidhinishwa, na muhuri wake. Uthibitisho wa nyaraka.

## SEHEMU YA IV
## MTAJI WA HISA NA DHAMANA

**45.**-(1) Katika Kifungu hii, vifungu vya 46 mpaka 56 na kifungu cha 63 vitatumika kwa makampuni ya umma tu. Muhtasari wa Ununuzi wa Hisa Kampuni za umma na za binafsi.

(2) Kampuni binafsi (zaidi ya kampuni yenye ukomo wa dhamana na isiyokuwa na mtaji wa hisa) itatenda kosa kama:-

(a) inatoa kwa umma (kama kwa fedha taslimu au vyenginevyo) hisa zozote au dhamana za kampuni, au

(b) inagawa au kukubaliana na kugawa (iwe kwa fedha au vyenginevyo) hisa zozote au dhamana za kampuni kwa lengo kuwa hisa hizo au dhamana zote au zozote zinazotolewa kwa ajili ya kuuza kwa umma.

(3) kampuni itakuwa inatenda kosa chini ya kifungu cha (2) na ofisa yeyote ambaye ameshiriki katika ukiukaji, anaweza kutozwa faini.

(4) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachoathiri uhalali wa ugawaji wowote au uuzaji wa hisa au dhamana, au makubaliano yoyote ya kugawa au kuuza hisa au dhamana.

Muhtasari wa ununuzi wa hisa.

**46.** Muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotolewa na au kwa niaba ya kampuni au kuhusiana na kampuni inayokusudiwa utakuwa na tarehe, na tarehe hiyo, isipokuwa ithibitishwe vyenginevyo, itachukuliwa kama tarehe ya uchapishaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa.

Mambo ya kuelezwa na ripoti za kuwekwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa.

**47.**-(1) Kila muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotolewa na au kwa niaba ya kampuni, au kwa niaba ya mtu yeyote ambaye ni au amekuwa akifanya au ana nia ya kuunda kampuni hiyo, ni lazima kueleza mambo yaliyotajwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Hali inayohitaji au kumfunga muombaji wa hisa au dhamana za kampuni kwa ajili kuondoa sharti la kufuata matakwa yoyote ya kifungu hiki, au inayodai kumuathiri na taarifa yoyote ya mkataba, waraka wowote, au jambo ambalo halikutajwa makhsusi katika muhtasari wa ununuzi wa hisa, itakuwa batili.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 48, itakuwa si halali kutoa aina yoyote ya fomu ya maombi kwa ajili ya hisa au dhamana za kampuni isipokuwa fomu hiyo iwe imetolewa pamoja na muhtasari wa ununuzi wa hisa ambao unafuata matakwa ya kifungu hiki:

Isipokuwa kwamba kifungu kidogo hiki hakitatumika kama imethibitishwa kuwa fomu ya maombi ilitolewa ama:-

(a) kuhusiana na mwaliko wa moja kwa moja kwa mtu kuingia katika makubaliano ya maandishi kuhusiana na hisa au dhamana, au

(b) kuhusiana na hisa au dhamana ambazo hazikutolewa kwa umma.

Kama mtu yeyote atafanya jambo linalokiuka masharti ya kifungu kidogo hiki, atakuwa na hatia ya kutozwa faini.

(4) Itokeapo kutofuata au kukiuka matakwa yoyote ya kifungu hiki, mkurugenzi au mtu mwengine mwenye kuwajibika na muhtasari wa ununuzi wa hisa hatakuwa na dhima yoyote kwa sababu ya kutofuata au kukiuka huko, kama:-

(a) kuhusu jambo lolote ambalo halikuwekwa bayana, anathibitisha kuwa hakulijua, au

(b) anathibitisha kuwa kutokufuata au kukiuka kulitokana na kukosea ukweli kuhusu jambo kwa upande wake, au

(c) kutofuata au kukiuka kulihusu mambo ambayo kwa maoni ya mahakama inayoshughulika na kesi yalikuwa hayana maana yoyote, kwa maoni ya mahakama hiyo, baada ya kuzingatia mazingira yote ya kesi, yanapaswa kusamehewa;

Isipokuwa kwamba, katika tukio la kushindwa kuingiza katika muhtasari wa ununuzi wa hisa taarifa kuhusu mambo yaliyotajwa katika kanuni, hakuna mkurugenzi au mtu mwengine atakuwa na dhima kuhusiana na kushindwa huko isipokuwa kuwa ikithibitishwa kuwa alikuwa anaelewa masuala ambayo hayakuwekwa wazi.

(5) Kifungu hiki haitatumika kwa suala la wanachama waliopo au wamiliki wa dhamana za kampuni, muhtasari wa ununuzi wa hisa au fomu ya maombi yanayohusiana na hisa au ya dhamana za kampuni, kama mwombaji wa hisa au dhamana ana haki au hana haki ya kujinyima kwa kuwapendelea watu wengine, lakini, kwa kulingana na yaliyoelezwa kabla, kifungu hiki kitatumika kwa muhtasari wa ununuzi wa hisa au fomu ya maombi kama ilitolewa kuhusu au kwa kuzingatia uundaji wa kampuni au baadaye.

(6) Hakuna jambo lolote katika kifungu hiki, kitaweka kikomo au kupunguza dhima yoyote ambayo mtu yeyote anaweza anaweza kubeba chini ya sheria za kawaida au Sheria hii mbali na kifungu hiki.

Ridhaa ya mtaalamu kutoa muhtasari wa ununuzi wa hisa yenye maelezo yake.

**48.**-(1) Muhtasari wa ununuzi wa hisa unaoalika watu kujiunga katika hisa au dhamana za kampuni ikiwamo taarifa inayodai kufanywa na mtaalamu haitatolewa isipokuwa kama:-

(a) ametoa na, kabla ya kuwasilisha nakala ya muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa ajili ya usajili, hajaondoa ridhaa yake ya maandishi kuhusu suala hilo na maelezo yake yaliyomo katika fomu na mazingira ambayo yaliingizwa; na

(b) taarifa ya kuwa ametoa na hajaiondoa ridhaa yake kama ilivyoelezwa kabla inaonekana katika muhtasari wa ununuzi wa hisa.

(2) Kama muhtasari wa ununuzi wa hisa yoyote unatolewa kwa kukiuka kifungu hiki kampuni na kila mtu ambaye huku akijua ameshiriki katika suala hilo atatozwa faini.

(3) Katika kifungu hiki neno "mtaalamu" linajumuisha mhandisi, mtathmini, mhasibu na mtu mwengine yeyote ambaye taaluma yake inalipa mamlaka tamko lililotolewa na yeye.

Usajili wa muhtasari wa ununuzi wa hisa.

**49.**-(1) Hakutakuwa na muhtasari wa ununuzi wa hisa yoyote itakayotolewa na au kwa niaba ya kampuni au kwa kampuni iliyokusudiwa isipokuwa katika au kabla ya tarehe ya kuchapishwa kwake, kumewasilishwa kwa Mrajis kwa ajili ya usajili nakala yake iliyosainiwa na kila mtu ambaye ametajwa humo kuwa ni mkurugenzi au mkurugenzi anayependekezwa wa kampuni, au na wakala wake aliyeidhinishwa kwa maandishi, na akiwa amethibisha humo au ameambatanisha:-

(a) ridhaa yoyote kuhusu suala la muhtasari wa ununuzi wa hisa inayohitajika kwa mujibu wa kifungu cha 48 kutoka kwa mtu yeyote kama ni mtaalamu; na

(b) kwa muhtasari wa ununuzi wa hisa iliyotolewa kwa jumla, pia:-

(i) nakala ya mkataba wowote inayotakiwa na kanuni zilizowekwa chini ya Sheria, kuelezwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa au, kwa mkataba usiokuwa katika maandishi, mkataba wenye kutoa maelezo kamili ndani yake; na

(ii) pale ambapo watu wanafanya ripoti yoyote inayotakiwa na kanuni zilizowekwa chini ya Sheria, wamefanya humo, au wameeleza humo, bila ya kutoa sababu, marekebisho yoyote kama yalivyotajwa katika kanuni, taarifa ya maandishi iliyotiwa saini na wale watu waliofanya marekebisho na kutoa sababu kuhusu marekebisho hayo.

Marejeo katika paragrafu ndogo ya (i) na paragrafu (b) ya kifungu kidogo hiki kwa nakala ya mkataba unaotakiwa kuandikwa au kuambatanishwa kwenye nakala ya muhtasari wa ununuzi wa hisa yatachukuliwa, kwa mkataba ambao wote au sehemu yake ni wa lugha ya kigeni, kama marejeo kwa nakala ya tafsiri ya mkataba kwa Kiingereza au Kiswahili nakala inayoingiza tafsiri kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili ya kifungu zilizomo katika lugha ya kigeni, kama hali itakavyokuwa, ikiwa ni tafsiri iliyothibitishwa kwa namna iliyowekwa kuwa ni tafsiri sahihi, na kumbukumbu ya nakala ya mkataba inatakiwa kuwa inapatikana kwa ajili ya ukaguzi zitakuwa ni pamoja na kumbukumbu ya nakala ya tafsiri yake au nakala inayoingiza tafsiri ya kifungu zake.

(2) Kila muhtasari wa ununuzi wa hisa:-

(a) utaeleza kuwa nakala imewasilishwa kwa ajili ya usajili kama inavyotakiwa na kifungu hiki, na

(b) kuainisha, au kurejea maelezo ambayo yaliingizwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa ambayo yanaainisha, na nyaraka zinazohitajika na kifungu hiki kuandikwa juu au kuambatanishwa kwenye nakala iliyowasilishwa.

(3) Mrajis hataandikisha muhtasari wa ununuzi wa hisa isipokuwa uwe na tarehe na nakala yake iwe imetiwa saini kwa mujibu wa kifungu hiki na isipokuwa kama umethibitisha au umeambanishwa na hati (kama zipo) zilizoainishwa kama ilivyoelezwa kabla.

(4) Kama muhtasari wa ununuzi wa hisa unatolewa bila ya nakala yake iliyowasilishwa kwa mujibu wa kifungu hiki kuthibitishwa au kuambatanishwa na nyaraka zinazohitajika, kampuni, na kila mtu ambaye kwa kujua anahusika katika suala la muhtasari wa ununuzi wa hisa, atakuwa na hatia na atatozwa faini kwa kila siku kuanzia tarehe ambayo muhtasari wa ununuzi wa hisa ulitolewa mpaka pale ambapo nakala yake imewasilishwa na nyaraka zinazohitajika zilizothibitishwa au kuambatanishwa nao.

Uzuiaji wa kubadilisha masharti yaliyotajwa katika muhtasari au tamko linalohusu muhtasari.

**50.**-(1) Kampuni yenye ukomo wa dhamana ya hisa au ukomo wa dhamana na yenye jumla ya hisa haitabadilisha kabla ya mkutano uliowekwa kwa mujibu wa sheria masharti ya mkataba yaliyotajwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa, au tamko linalohusu muhtasari wa ununuzi wa hisa, isipokuwa kwa kibali cha mkutano uliowekwa kwa mujibu wa sheria.

(2) Kifungu hiki hakitatumika kwa kampuni binafsi.

Dhima kwa matamko yaliyokosewa katika muhtasari.

**51.**-(1) Kulingana na masharti ya kifungu hiki, ambapo muhtasari wa ununuzi wa hisa unakaribisha watu kujiunga kwenye hisa au kwenye dhamana za kampuni, watu wafuatao watakuwa na dhima ya kulipa fidia kwa watu wote waliojiunga kwenye hisa yoyote au dhamana yoyote kwa imani ya muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa hasara au uharibifu wanaoweza kupata kwa sababu ya tamko lolote lisilokuwa la kweli lililomo ndani yake, yaani;

(a) kila mtu ambaye ni mkurugenzi wa kampuni wakati wa kutolewa muhtasari wa ununuzi wa hisa;

(b) kila mtu ambaye ameidhinisha mwenyewe kutajwa jina lake na jina lake limetajwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa kama mkurugenzi au amekubali kuwa mkurugenzi ama mara moja au baada ya muda kupita;

(c) kila mtu ambaye ni promota wa kampuni; na

(d) kila mtu ambaye ameidhinisha utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa;

Isipokuwa kwamba ambapo, kwa mujibu wa kifungu cha 48 ridhaa ya mtu inatakiwa kuhusu utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa na kuwa ametoa idhini, hatakuwa na dhima kwa sababu ya kuitoa ridhaa hiyo kwa mujibu wa kifungu hiki kidogo kama mtu ambaye ameidhinisha utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa isipokuwa kuhusiana na tamko lisilokuwa la kweli linalodaiwa kutolewa na yeye kama mtaalamu.

(2) Hakuna mtu atakayekuwa na hatia chini ya kifungu kidogo cha (1) kama atathibitisha:-

(a) kwamba, baada ya kuridhia kuwa mkurugenzi wa kampuni, aliondoa idhini yake kabla ya kutolewa muhtasari wa ununuzi wa hisa, na kwamba ilitolewa bila ya idhini yake au ridhaa yake; au

(b) kwamba muhtasari wa ununuzi wa hisa ulitolewa bila ya yeye kujua au bila ya idhini yake, na kwamba baada kufahamu kutolewa kwake palepale alitoa taarifa ya kuridhisha kwa umma kwamba ulitolewa bila ya yeye kujua au ridhaa yake; au

(c) kwamba, baada ya kutolewa muhtasari wa ununuzi wa hisa na kabla ya mgao wake, yeye, baada ya kufahamu tamko ambalo si la ukweli, aliondoa ridhaa yake palepale na alitoa taarifa ya kuridhisha kwa umma ya uondoaji huo na sababu za uondoaji huo; au

(d) kwamba:-

(i) kuhusu kila taarifa ambayo si ya kweli isiyodaiwa kutolewa kwa idhini ya mtaalamu au waraka rasmi wa serikali au tamko, alikuwa na sababu ya kuridhisha ya kuamini, na aliamini hadi wakati wa mgao huo wa hisa au dhamana, kadiri hali itakavyokuwa, kuamini, kwamba taarifa ilikuwa ni ya kweli; na

(ii) kuhusu kila taarifa ambayo si ya kweli inayodaiwa kuwa taarifa iliyotolewa na mtaalamu au iliyomo katika nakala au sehemu kutoka kwenye ripoti au tathmini ya mtaalamu, kwa kiasi kinachoridhisha iliwakilisha taarifa, au ilikuwa ni nakala sahihi na ya kuridhisha kutoka kwenye ripoti au tathmini, naye alikuwa na sababu za kuridhisha ya kuamini na aliamini hivyo hadi wakati wa kutolewa muhtasari wa ununuzi wa hisa kwamba mtu aliyetoa taarifa alikuwa na uwezo wa kufanya hivyo na kwamba mtu huyo alikuwa ametoa idhini iliyohitajika kwa mujibu wa kifungu cha 48 kuhusu utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa na kwamba hakuiondoa idhini hiyo kabla ya uwasilishaji wa nakala ya muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa ajili ya usajili au, kwa welewa wa mshtakiwa, kabla ya mgao huo; na

(iii) kuhusu kila taarifa isiyokuwa ya kweli inayodaiwa kuwa tamko lililotolewa na mtu rasmi au iliyomo katika nakala au dondoo kutoka hati rasmi ya serikali, ilikuwa ni kiwakilishi sahihi na cha kuridhisha cha taarifa au nakala ya au dondoo kutoka hati hiyo.

Isipokuwa kwamba kifungu hiki kidogo hakitatumika kwa mtu mwenye dhima, kwa sababu ya kutoa kwake ridhaa, iliyotakiwa kutoka

kwake kwa mujibu wa kifungu cha 48, kama mtu ambaye alikuwa ameidhinisha utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa kuhusiana na taarifa isiyokuwa ya kweli inayodaiwa kutolewa na yeye kama mtaalamu.

(3) Mtu ambaye, mbali na kifungu kidogo hiki atakuwa na dhima kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), kwa sababu ya kutoa ridhaa yake, aliyotakiwa na kifungu cha 48, kama mtu ambaye ameidhinisha utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa kuhusiana na taarifa ambayo si ya kweli inayodaiwa kutolewa na yeye kama mtaalamu atakuwa hana dhima kama atathibitisha:-

(a) kwamba, baada ya kutoa ridhaa yake kwa mujibu wa kifungu cha 48 kuhusu utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa, aliiondoa kwa maandishi kabla ya uwasilishaji wa nakala ya muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa ajili ya usajili; au

(b) kwamba, baada ya uwasilishaji wa nakala ya muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa ajili ya usajili na kabla ya mgao huo, yeye, baada ya kuijua taarifa iliyokuwa si ya kweli, aliondoa ridhaa yake kwa maandishi na kutoa taarifa yenye kuridhisha kwa umma ya uondoaji na sababu ya kufanya hivyo, au

(c) kwamba yeye alikuwa na uwezo wa kutoa taarifa na kwamba alikuwa na sababu ya kuridhisha kuamini na aliamini hadi wakati wa mgao huo wa hisa au dhamana, kadiri hali ilivyokuwa, kwamba taarifa ilikuwa ya kweli.

(4) Endapo:-

(a) muhtasari wa ununuzi wa hisa una jina la mtu kama mkurugenzi wa kampuni, au ambaye amekubali kuwa mkurugenzi wake, na ambaye hajatoa ridhaa ya kuwa mkurugenzi au ameondoa ridhaa yake kabla ya kutoa muhtasari wa ununuzi wa hisa, na hajaidhinisha au kukubali utoaji huo; au

(b) ridhaa ya mtu inatakiwa chini ya kifungu cha 48 kuhusu utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa na yeye ama hajatoa idhini hiyo au ameiondoa kabla ya utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa;

(c) wakurugenzi wa kampuni, isipokuwa yeyote ambaye bila kujua kwake au ridhaa yake muhtasari wa ununuzi wa hisa ulitolewa, na mtu mwengine yeyote ambaye aliidhinisha utoaji huo atakuwa na dhima ya kumlipa fidia mtu aliyetajwa kama ilivyoelezwa kabla au ambaye ridhaa yake ilitakiwa kama ilivyoelezwa kabla, kadiri hali itakavyokuwa, dhidi ya uharibifu wote, gharama na matumizi ambayo anaweza kuwa na dhima nayo kutokana na kuwa jina lake limeingizwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa au kwa kuingizwa ndani yake taarifa inayodaiwa kutolewa na yeye

kama mtaalamu, kadiri hali itakavyokuwa, au katika kujitetea dhidi ya hatua yoyote au mashauri ya kisheria yaliyoletwa dhidi yake kuhusiana nayo:

Isipokuwa kwamba mtu hatahesabiwa kwa madhumuni ya kifungu hiki kuwa ameidhinisha utolewaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa sababu tu ya kutoa ridhaa yake, kwa mujibu wa kifungu cha 48 kwa kuingizwa ndani yake taarifa inayodaiwa kutolewa na yeye kama mtaalamu.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki:-

(a) neno "promota" maana yake ni promota ambaye alikuwa mshiriki katika maandalizi ya muhtasari wa ununuzi wa hisa, au sehemu yake yenye taarifa isiyokuwa ya kweli, lakini halijumuishi mtu yeyote kwa sababu ya kukaimu kwake katika cheo cha kitaalamu kwa watu wanaohusika katika uundaji wa kampuni; na

(b) neno "mtaalamu" lina maana kama katika kifungu cha 48.

Dhima ya jinai kwa taarifa zisizokuwa za kweli katika muhtasari.

**52.**-(1) Pale ambapo muhtasari wa ununuzi wa hisa unajumuisha taarifa yoyote ambayo si ya kweli, mtu yeyote ambaye aliidhinisha utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa akitiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kwa muda usiozidi miaka miwili, au atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni moja, au adhabu zote mbili, isipokuwa kama atathibitisha kwamba taarifa ilikuwa haina maana yoyote au kuwa alikuwa na sababu ya msingi kuamini hivyo na, hadi wakati wa utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa, aliamini kwamba taarifa ilikuwa kweli.

(2) Mtu hatahesabiwa kwa madhumuni ya kifungu hiki kuwa ameidhinisha utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa sababu tu ya kutoa ridhaa inayotakikana na kifungu cha 48 kwa kuingizwa ndani yake taarifa inayodaiwa kutolewa na yeye kama mtaalamu.

Waraka wenye kutoa hisa au dhamana kwa ununuzi kuhesabiwa kama muhtasari.

**53.**-(1) Pale ambapo kampuni inagawa au kukubaliana kugawa hisa zozote au dhamana za kampuni kwa lengo la hisa hizo zote au dhamana zinazotolewa kwa ajili ya kuuzwa kwa umma, hati yoyote ambayo kwayo uuzaji kwa umma utafanywa utahesabiwa kwa madhumuni yote kuwa ni muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotolewa na kampuni.

(2) Sheria zote na kanuni zote za sheria kuhusiana na mihutasari ya ununuzi wa hisa na dhima kuhusiana na taarifa za ndani na upungufu kutoka mihutasari ya ununuzi wa hisa, au vyenginevyo zinazohusiana na mihutasari ya ununuzi wa hisa, zitatumika na kuwa na athari ipasavyo, kama kwamba hisa au dhamana zimetolewa kwa umma kwa ajili ya kuchangia na kama kwamba watu wanaokubali hisa au dhamana kuhusiana na hisa zozote au dhamana zozote kuhusiana na hisa au dhamana walikuwa wanachama kwa hisa hizo au dhamana hizo, lakini bila ya kuathiri dhima, kama zipo, kwa watu ambao wametoa fursa hiyo kuhusiana na taarifa zilizokosewa zilizomo katika hati au vyenginevyo kuhusiana nayo.

(3) Kwa madhumuni ya Sheria hii, isipokuwa imethibitishwa vyenginevyo, utakuwa ni ushahidi kwamba mgao wa, au makubaliano ya kugawa, hisa au dhamana yalifanywa kwa lengo la hisa au dhamana kutolewa kwa ajili ya kuuzwa kwa umma kama itaoneshwa:-

(a) kwamba utoaji wa hisa au dhamana au yoyote kati yao kwa ajili ya kuuza kwa umma ulifanywa ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya mgao au makubaliano ya kugawa; au

(b) kwamba katika tarehe ambayo utoaji ulifanywa mazingatio kamili ya kupokewa na kampuni kuhusiana na hisa au dhamana hazikupokewa kama zilivyopaswa.

(4) Kifungu cha 47 kama kilivyo katika kifungu hiki kitakuwa na athari kama kwamba kilihitaji muhtasari wa ununuzi wa hisa kutaja pamoja na masuala yanayohitajika na kifungu hicho kuelezwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa:-

(a) kiasi halisi cha mazingatio yaliyopokewa au yatakayopokewa na kampuni kuhusiana na hisa au dhamana ambazo utoaji huo unahusiana nao; na

(b) mahali na wakati ambapo mkataba ambao kwao hisa au dhamana zilizotajwa zimegawiwa au zitagawiwa unaweza kukaguliwa;

na kifungu cha 49 kama kinavyotumika katika kifungu hiki kitakuwa na athari kama kwamba watu wanaotoa fursa walikuwa watu waliotajwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa kama wakurugenzi wa kampuni.

(5) Iwapo mtu anayetoa fursa kwa mujibu wa kifungu hiki ni kampuni au shirika, itatosha kama waraka uliotajwa kabla umetiwa saini kwa niaba ya kampuni au shirika na wakurugenzi wawili wa kampuni au si chini ya nusu ya washirika, kadiri hali itakavyokuwa, na mkurugenzi yoyote au mshirika anaweza kutia kusaini kwa wakala wake kuidhinishwa kwa maandishi.

Tafsiri ya vifungu vinavyohusiana na muhtasari.

**54.** Kwa madhumuni ya masharti yaliyotangulia ya Sehemu hii:-

(a) taarifa iliyoingizwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa itahesabika kuwa si ya kweli kama ni ya kupotosha katika umbo na muktadha ambamo imeingizwa;

(b) taarifa itachukuliwa kuwa imeingizwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa ikiwa imo humo au katika ripoti yoyote au mkataba unaonekana kwenye uso wake au kwa kumbukumbu ya kuingizwa humo au iliyoingizwa humo.

Mgao Uzuiaji wa ugawaji isipokuwa mchango wa msingi umetolewa.

**55.**-(1) Hautafanywa mgao wowote wa mtaji wa hisa wa kampuni zilizotolewa kwa umma kwa ajili ya michango isipokuwa kwamba kiasi kilichotajwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa kuwa ni kiasi cha msingi ambacho, kwa maoni ya wakurugenzi, lazima zikusanywe kutokana na utoaji

wa hisa ili kwa ajili ya mambo yaliyotajwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii yametekelezwa, na kiasi kinachopaswa kulipwa kwa maombi kwa kiasi kilichotajwa kimelipwa na kupokewa na kampuni.

Kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki kiasi hicho kitahesabika kuwa kimelipwa kwa kupokewa na kampuni kama hundi kwa kiasi hicho imepokewa na kampuni na wakurugenzi wa kampuni wakawa hawana sababu ya kutuhumu kwamba hundi haitalipwa.

(2) Kiasi kilichotajwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa kitahesabiwa peke yake kutoka kiasi chochote kilicholipwa kwa namna nyengine isiyokuwa ya fedha taslimu na katika Sheria hii inajuilikana kama "mchango wa msingi".

(3) Kima cha fedha cha kulipa baada ya kuombwa kisiwe chini ya asilimia tano ya kima cha chini cha hisa.

(4) Kama masharti yaliyoelezwa kabla hayakutekelezwa baada ya kumalizika muda wa siku mia moja na ishirini baada ya toleo la kwanza la muhtasari wa ununuzi wa hisa, fedha zote zilizotoka kwa waombaji wa hisa zitalipwa mara moja bila ya riba, na, kama fedha hizo hazikulipwa ndani ya siku mia moja na thelathini baada ya utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa, wakurugenzi wa kampuni kwa pamoja na mmoja mmoja watakuwa na dhima ya kulipa fedha hizo pamoja na riba kwa kiwango cha asilimia tano kwa mwaka baada ya kumalizika siku ya mia na thalathini:

Isipokuwa kwamba mkurugenzi hatakuwa na dhima kama atathibitisha kuwa ukosefu katika ulipaji wa fedha ulikuwa si kutokana na utovu wa nidhamu wowote au kwa uzembe kutokana upande wake.

(5) Sharti lolote linalomtaka au linalomfunga muombaji yeyote wa hisa kuondoa kufuata matakwa yoyote ya kifungu hiki litakuwa batili.

(6) Kifungu hiki, isipokuwa kifungu kidogo chake cha (3), hakitatumika kwa mgao wa hisa wowote utakaofanywa baada ya mgao wa kwanza wa hisa zinazotolewa kwa umma kwa ajili ya michango.

Uzuiaji wa mgao katika hali maalumu isipokuwa taarifa kuhusu muhtasari iwe imewasilishwa kwa Mrajis.

**56.**-(1) Kampuni yenye mtaji wa hisa ambayo haikutoa muhtasari wa ununuzi wa hisa kuhusu au kwa kuzingatia kuundwa kwake, au ambayo imetoa muhtasari wa ununuzi wa hisa lakini bado haijafanya mgao wowote wa hisa zinazotolewa kwa umma kwa ajili ya michango, haitagawa hisa zake zozote au dhamana zake isipokuwa angalau siku tatu kabla ya mgao wa kwanza wa ama hisa au dhamana kuwe kumewasilishwa kwa Mrajis kwa ajili ya usajili taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa iliyotiwa saini na kila mtu ambaye jina limetajwa humo kama mkurugenzi au mkurugenzi anayependekezwa wa kampuni au na wakala wake aliyeidhinishwa kwa maandishi, katika namna na yenye maelezo yaliyoainishwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, na kuweka ripoti zilizoainishwa humo.

(2) Kila taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa iliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo kilichopita, itaainisha, ambapo mtu anayefanya ripoti kama hiyo yoyote kama ilivyoelezwa kabla kuwa alifanya humo au ameingiza humo, bila ya kutoa sababu, marekebisho yoyote kama yalivyotajwa katika kanuni za Sheria hii, kuwa amethibitisha juu yake au kuambatanisha humo taarifa yoyote ya maandishi iliyosainiwa na wale watu waliofanya marekebisho na kutoa sababu ya kufanya hivyo.

(3) Kifungu hiki hakitatumika kwa kampuni binafsi.

(4) Kama kampuni itafanya kitendo kinyume na kifungu kidogo cha (1) au cha (2), kampuni na kila mkurugenzi wa kampuni ambaye anajua na kwa makusudi anaidhinisha au anaruhusu ukiukaji huo atakuwa na hatia na atatozwa faini.

(5) Iwapo taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa uliowasilishwa kwa Mrajis chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki inaingiza taarifa yoyote ambayo si ya kweli mtu yeyote ambaye ameidhinisha utoaji wa taarifa hiyo kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa ajili ya usajili itampasa akitiwa hatiani kupewa adhabu ya kifungo cha jela kwa muda usiozidi miaka miwili, au kutozwa faini isiyozidi milioni moja, au yote mawili, isipokuwa kama atathibitisha ama kwamba taarifa iliyokuwa si ya kweli haina maana yoyote au kuwa alikuwa na sababu ya msingi ya kuamini na aliamini hivyo hadi wakati wa uwasilishaji kwa ajili ya usajili taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa kwamba taarifa ilikuwa ya kweli.

(a) taarifa iliyoingizwa katika taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa itahesabika kuwa inapotosha kama ni ya kupotosha katika umbo na mazingira ambayo imeingizwa; na

(b) taarifa itachukuliwa kuwa imeingizwa katika taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa ikiwa imo humo au katika ripoti yoyote au katiba yenye kuonekana kwenye uso wake au kwa kumbukumbu yenye kuingizwa humo.

Athari ya ugawaji usiokuwa wa kawaida.

**57.**-(1) Mgao uliofanywa na kampuni kwa muombaji kwa kukiuka masharti ya vifungu vya 55 na 56 utakuwa batili kwa muombaji ndani ya mwezi mmoja baada ya kufanyika mkutano wa kisheria wa kampuni na si baada ya hapo, au, katika hali yoyote ambapo kampuni haikutakiwa kufanya mkutano wa kisheria, au ambapo mgao huo unafanywa baada ya kufanyika mkutano wa kisheria, ndani ya mwezi mmoja baada ya tarehe ya kufanya mgawo huo, na si baada ya hapo, na utakuwa batili bila ya kujali kwamba kampuni imo katika hatua za kufungwa.

(2) Kama mkurugenzi yeyote wa kampuni kwa kujua anakiuka, au anaruhusu au anaidhinisha ukiukaji wa masharti yoyote ya vifungu vilivyotajwa kuhusu mgao, atakuwa na dhima ya kulipa fidia kwa kampuni na mgawiwaji kwa upotevu, uharibifu, au gharama ambazo kampuni au mgawiwaji inaweza kuwa amezipata au ameingia.

Isipokuwa kwamba kesi za kurejesha hasara yoyote, uharibifu, au gharama hazitaanza baada ya kumalizika muda wa miaka miwili kuanzia tarehe ya mgao huo.

Maombi ya, na mgao wa, hisa na dhamana.

**58.**-(1) Hakuna mgao utakaofanywa wa hisa zozote au dhamana za kampuni kulingana na muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotolewa kwa jumla na hakuna hatua zitakazochukuliwa juu ya maombi yaliyotolewa kulingana na muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotolewa, hadi mwanzo wa siku ya tatu baada ya ile ambayo muhtasari wa ununuzi wa hisa ulitolewa kwa mara ya kwanza au wakati mwengine baada ya hapo (kama upo) kama itakavyoainishwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa.

Isipokuwa kwamba mwanzo wa siku ya tatu iliyotajwa au wakati mwengine baada ya hapo kama ilivyoelezwa kabla inakusudiwa kuanzia sasa katika Sheria kuwa ni "wakati wa ufunguzi wa orodha ya michango".

(2) Katika kifungu kidogo cha (1), marejeo kwenye siku ambayo muhtasari wa ununuzi wa hisa unatolewa kwa mara ya kwanza kwa jumla itafahamika kama inamaanisha siku ambayo umetolewa kama tangazo kwenye gazeti.

Isipokuwa kwamba, kama haukutolewa kama tangazo kwenye gazeti kabla ya siku ya tatu baada ya siku ya kwanza ulipotolewa kwa njia nyengine yoyote, marejeo yaliyoelezwa yatafahamika kwamba yanarejea kwenye siku ambayo ni ya kwanza kutolewa kwake katika namna nyengine yoyote.

(3) Uhalali wa mgao hautaathiriwa na ukiukwaji wowote wa masharti yaliyoelezwa kabla ya kifungu hiki lakini, katika tukio la ukiukaji wowote wa namna hiyo, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye ni mshiriki katika ukiukaji atatozwa faini.

(4) Katika matumizi ya kifungu hiki kwa muhtasari wa ununuzi wa hisa au dhamana kwa ajili ya kuuza, vifungu vilivyotangulia vitakuwa na athari juu ya kubadilisha marejeo ya uuzaji kwa marejeo ya mgao huo, na kubadilisha marejeo ya kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anakiuka na marejeo ya mtu yeyote ambaye au kupitia kwake marejeo yamewekwa na ambaye anajua na kwa makusudi anaidhinisha au anaruhusu ukiukwaji.

(5) Maombi ya hisa au dhamana za kampuni ambayo yamefanywa kulingana na muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotolewa kwa jumla hayataweza kufutwa mpaka baada ya kumalizika muda wa siku ya tatu baada ya wakati wa ufunguzi wa orodha ya michango, au utoaji kabla ya kupita siku ya tatu iliyoelezwa, na mtu mwenye dhamana chini ya kifungu cha 51 kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa, wa tangazo kwa umma lenye athari chini ya kifungu hicho ya kuondoa au kupunguza wajibu wa mtu aliyelitoa.

(6) Katika kuhesabu kwa madhumuni ya kifungu hiki na kifungu cha 59 siku ya tatu baada ya siku nyengine, siku yoyote ya katikati ambayo ni Jumamosi au Jumapili au ambayo ni siku ya mapumziko ya serikali au mapumziko ya benki haitahisabiwa, na kama siku ya tatu (kama itakavyohisabiwa) yenyewe ni Jumamosi au Jumapili au ni ya mapumziko

ya serikali au mapumziko ya benki itabadilishwa kwa madhumuni yaliyotajwa na siku ya kwanza baada ya hapo ambayo si mojawapo ya hizo.

Ugawaji wa hisa na dhamana kushughu-likiwa kwenye soko la hisa.

**59.**-(1) Ambapo muhtasari wa ununuzi wa hisa, iwe iliyotolewa kwa ujumla au la, inaeleza kuwa maombi yamefanywa au yatafanywa kuhusu ruhusa kwa hisa au dhamana zinazotolewa humo kushughulikiwa kwenye soko la hisa lolote, mgao wowote uliotolewa juu ya maombi kulingana na muhtasari wa ununuzi wa hisa utakuwa batili, wakati wowote ukifanywa, kama ruhusa haikuombwa kabla ya siku ya tatu baada ya toleo la kwanza la muhtasari wa ununuzi wa hisa au kama ruhusa imekataliwa kabla ya kumalizika muda wa wiki tatu kuanzia tarehe ya mwisho ya kuorodhesha michango au muda mrefu zaidi usiozidi wiki sita kama itakavyoweza kutolewa taarifa, ndani ya wiki tatu zilizoelezwa, kwa muombaji kwa ajili ya ruhusa ya au kwa niaba ya soko la hisa.

(2) Ambapo ruhusa haikuombwa kabla kama ilivyoelezwa awali, au kama imekataliwa kama ilivyoelezwa kabla, kampuni italipa mara moja bila ya riba fedha zote zilizopokelewa kutoka kwa waombaji kulingana na muhtasari wa ununuzi wa hisa, na, kama fedha zozote hazikulipwa ndani ya siku nane baada ya kampuni kuwa na dhima ya kuzilipa, wakurugenzi wa kampuni watakuwa kwa pamoja na mmoja mmoja na dhima ya kulipa fedha hizo pamoja na riba kwa kiwango cha asilimia tano kwa mwaka kutoka kumalizika siku ya nane.

Isipokuwa kwamba mkurugenzi hatakuwa na dhima kama atathibitisha kuwa ukiukaji katika ulipaji wa fedha ulikuwa si kutokana na utovu wa nidhamu wowote au kwa uzembe kwa upande wake.

(3) Fedha zilizopokewa kama ilivyoelezwa kabla zitatunzwa katika akaunti ya benki tafauti madamu kampuni ina dhima ya kuzilipa kwa mujibu wa kifungu cha (2), na, ukiukwaji utafanywa kwa kuzingatia kifungu kidogo hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye ameshiriki katika ukiukaji atatozwa faini.

(4) Sharti lolote linalomtaka au linalomfunga muombaji wa hisa au dhamana kutofuata matakwa yoyote ya kifungu hiki litakuwa batili.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, ruhusa haitahesabiwa kuwa imekataliwa kama imearifiwa kuwa maombi kwa ajili yake, ingawa bado haijatolewa, yatazingatiwa zaidi.

(6) Kifungu hiki kitatumika:-

(a) kuhusiana na hisa yoyote au dhamana iliyokubaliwa kuchukuliwa na mtu aliyeahidi kuchukua hisa hiyo kwa muhtasari wa ununuzi wa hisa kama kwamba alikuwa ameomba kulingana na muhtasari wa ununuzi wa hisa; na

(b) kuhusiana na muhtasari wa ununuzi wa hisa unaotoa hisa kwa ajili ya kuuza pamoja na marekebisho yafuatayo, yaani:-

(i) marejeo ya kuuza yatabadilishwa kuwa marejeo ya mgao;

(ii) watu ambao wanapewa hisa, na si kampuni, watakuwa na dhima chini ya kifungu kidogo cha (2) kulipa fedha zilizopokewa kutoka kwa waombaji, na marejeo ya dhima ya kampuni hiyo chini ya kifungu hicho yatafahamika ipasavyo; na

(iii) kwa marejeo ya kifungu kidogo cha (3) kwa kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye ameshiriki katika ukiukaji atawekewa mbadala wa marejeo kwa mtu yeyote au kupitia mtu yeyote anayepewa hisa ambaye kwa kujua na kwa makusudi ameidhinisha au ameruhusu ukiukaji.

Marejesho kuhusu ugawaji

**60.**-(1) Kila ambapo kampuni yenye ukomo wa hisa au marejesho ya kampuni kama yenye ukomo wa dhamana na yenye mtaji wa hisa inafanya ugawaji wa hisa zake, kampuni ndani ya siku sitini baada ya hapo itawasilisha kwa Mrajis kwa ajili ya usajili:-

(a) marejesho ya ugawaji, yakieleza idadi na kima cha hisa zilizomo katika mgao huo, majina, anwani na maelezo ya wagawiwaji, na kiasi, kama kipo, kilicholipwa au kinachopaswa kulipwa na kulipwa kwa kila hisa, na

(b) kwa hisa zilizogawiwa kama kwamba zimelipiwa kamili au sehemu yake kinyume na fedha taslimu, mkataba kwa maandishi wenye cheo cha mgawiwaji pamoja na mkataba wowote wa kuuza, au kwa ajili ya huduma au mazingatio mengine ambayo yalifanywa kuhusiana na mgao huo, mikataba hiyo ikiwa imepigwa muhuri, na maelezo yenye kueleza idadi na kiasi kilichogawiwa, kiwango ambacho kinapaswa kuchukuliwa kuwa kimelipwa, na mazingatio yaliyofanywa katika kugawiwa kwake.

(2) Endapo mkataba kama uliotajwa hapo juu haukuwekwa kwa maandishi, kampuni ndani ya siku sitini baada ya kutoa mgao huo itawasilisha kwa Mrajis, kwa ajili ya usajili taarifa zilizotakiwa za mkataba zikipigwa muhuri ule ule wa ushuru wa stempu kama ambavyo ungelipwa kama mkataba ungewekwa kwa maandishi, na taarifa hiyo itahesabika kuwa hati ndani ya maana ya Sheria ya Ushuru wa Stempu, na Mrajis anaweza, kama masharti ya kutunza taarifa, kutaka ushuru unaolipwa uamuliwe kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria hiyo.

(3) Kama ukiukaji utafanywa katika kutekeleza kifungu hiki, kila ofisa wa kampuni ambaye ameshiriki katika ukiukaji itampasa kutozwa faini kwa kila siku ambayo ukiukaji unaendelea:

Isipokuwa kwamba, kwa ukiukaji wa kuwasilisha kwa Mrajis ndani ya siku sitini baada ya mgao huo hati yoyote inayotakiwa kuwasilishwa kwa mujibu wa kifungu hiki, kampuni, au ofisa yeyote mwenye dhima kwa

ukiukaji, anaweza kuomba mahakama kwa ajili ya msamaha, na mahakama, ikiridhika kwamba kukosa kuwasilishwa hati kulikuwa kwa bahati mbaya au kulitokana na hali ambayo haikutarajiwa au kwamba ni haki na usawa kutoa msamaha, inaweza kutoa amri ya kuongeza muda kwa ajili ya kuwasilisha hati kwa kipindi ambacho mahakama inaona kinafaa.

Kamisheni na Punguzo Uwezo wa kulipa baadhi ya kamisheni na kukataza kulipa kamisheni nyengine zote, punguzo, n.k.

**61.**-(1) Itakuwa halali kwa kampuni kulipa kamisheni kwa mtu yeyote kwa kuzingatia mchango wake au kukubali kwake kuchangia, iwe moja kwa moja au kwa masharti, kwa hisa zozote katika kampuni, au kununua au kukubali kununua michango, iwe moja kwa moja au kwa masharti, kwa hisa zozote katika kampuni kama:-

(a) malipo ya kamisheni yaimeidhinishwa na kanuni; na

(b) kamisheni inayolipwa au inayokubaliwa kulipwa haizidi asilimia kumi ya bei ambayo hisa zinatolewa au kiasi au kiwango kilichoidhinishwa na kanuni, chochote kilicho kidogo; na

(c) kiasi au kiwango cha asilimia ya kamisheni kinacholipwa au kinachokubaliwa kulipwa ni:-

(i) kwa hisa zinazotolewa kwa umma kwa ajili ya kuchangia,

(ii) kilichoelezwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa; au

(iii) kwa hisa ambazo hazikutolewa kwa umma kwa ajili ya kuchangia, zilizoelezwa katika taarifa kuhusiana na muhtasari wa ununuzi wa hisa, au katika taarifa ya fomu iliyoainishwa iliyotiwa saini katika namna hiyo hiyo kama taarifa kuhusiana na muhtasari wa ununuzi wa hisa na kuwasilishwa kabla ya malipo ya kamisheni kwa Mrajis kwa ajili ya usajili, na, pale ambapo sakula au taarifa, isiyokuwa muhtasari wa ununuzi wa hisa, inayokaribisha michango kwa ajili ya hisa imetolewa, pia imeelezwa katika sakula au taarifa hiyo; na

(d) idadi ya hisa ambazo watu wamekubaliana kwa ajili ya kamisheni kuchangia moja kwa moja imewekwa wazi katika namna iliyoelezwa kabla.

(2) Isipokuwa kama ilivyoelezwa kabla, hakuna kampuni itakayotumia hisa zake zozote au pesa za mtaji ama moja kwa moja au si moja kwa moja katika malipo ya kamisheni yoyote, punguzo, au posho kwa mtu yeyote kwa mazingatio ya kuchangia kwake au kukubali kwake kuchangia, iwe moja kwa moja au kwa masharti, kwa ajili ya hisa zozote katika kampuni, au kununua au kukubali kununua michango, iwe moja kwa moja au kwa masharti, kwa hisa zozote katika kampuni, kama hisa au fedha

zitatumika hivyo kwa kuongezwa kwenye fedha za ununuzi wa mali yoyote inayonunuliwa na kampuni au kwa bei ya zabuni ya kazi yoyote ya kutekelezwa kwa ajili ya kampuni, au fedha za kulipwa nje ya fedha ya msingi ya ununuzi au bei ya zabuni, au vyenginevyo.

(3) Muuzaji kwa, promota wa, au mtu mwengine ambaye anapata malipo kwa fedha au hisa kutoka, kampuni itakuwa na na itachukuliwa daima kuwa ilikuwa na uwezo wa kutumia sehemu yoyote ya fedha au hisa zilizopokewa katika malipo yoyote ya kamisheni hiyo, malipo ambayo, kama yangefanywa moja kwa moja na kampuni, yangekuwa halali chini ya kifungu hiki.

(4) Endapo ukiukwaji umefanywa katika kutekeleza masharti ya kifungu hiki kuhusiana na uwasilishaji kwa Mrajis wa taarifa katika fomu iliyoainishwa, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye ameshiriki katika ukiukaji itampasa kutozwa faini.

Ukatazaji wa utoaji wa misaada ya kifedha kwa kampuni kwa ajili ya ununuzi wa au michango kwa ajili yake yenyewe, au hisa za kampuni.

**62.**-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, haitakuwa halali kwa kampuni kutoa, iwe moja kwa moja au si moja kwa moja, na kama kwa njia ya mkopo, dhamana, utoaji wa dhamana au vyenginevyo msaada wowote wa kifedha kwa madhumuni ya au kuhusiana na ununuzi au mchango uliofanywa au utakaofanywa na mtu yeyote au kwa ajili ya hisa zozote katika kampuni, au, ambapo kampuni ni kampuni tanzu, katika kampuni yake ya hisa:

Isipokuwa kwamba hakuna kitu katika kifungu hiki kitachukuliwa kuwa kinakataza:-

(a) ambapo ukopeshaji ya fedha ni sehemu ya biashara ya kawaida ya kampuni; ukopaji wa fedha kwa kampuni katika utaratibu wa kawaida wa biashara yake;

(b) utoaji wa kampuni, kwa mujibu wa mpango wowote kwa sasa unaotumika, wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa, au michango kwa ajili ya, hisa zinazolipiwa kamili katika kampuni au kampuni yake ya hisa, kuwa ni ununuzi au michango na wadhamini wa au kwa hisa zitakazoshikiliwa na au kwa manufaa ya wafanyakazi wa kampuni; ikiwa ni pamoja na mkurugenzi yeyote mwenye ajira ya mshahara au cheo katika kampuni;

(c) kutolewa mikopo na kampuni kwa watu halisi, zaidi ya wakurugenzi, waliomo katika ajira ya kampuni kwa lengo la kuwawezesha watu hao kununua au kujisajili kwenye hisa za kulipwa kikamilifu katika kampuni au kampuni yake ya hisa kumilikiwa na wao wenyewe kwa njia ya umiliki wenye manufaa.

(2) Endapo kampuni itatekeleza kinyume na kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni aliyeshiriki katika ukiukaji atatozwa faini.

Ujenzi wa Marejeo ya Utoaji wa Hisa au Dhamana kwa Hisa za Umma Ujenzi wa kumbukumbu za utoaji wa hisa na dhamana kwa umma.

**63.**-(1) Marejeo yoyote katika Sheria hii kuhusu kutoa hisa au dhamana kwa umma, bila ya kuathiri masharti yoyote yaliyo kinyume yaliyomo humo, yatahesabika kuingiza marejeo ya kuyatoa kwa kundi lolote la umma, iwe wamechaguliwa kama wanachama au wamiliki wa dhamana wa kampuni wanaohusika au kama wateja wa mtu anayetoa muhtasari wa ununuzi wa hisa au kwa njia yoyote ile nyengine, na marejeo katika Sheria hii au katika kanuni nyengine zozote za kampuni kwa mialiko kwa umma kujiunga kwenye hisa au dhamana, bila ya kuathiri yaliyoelezwa kabla, yatahesabika vivyo hivyo.

Kifungu kidogo cha (1) hakitachukuliwa kwamba kinahitaji utoaji wowote au mwaliko kuchukuliwa kama ulifanywa kwa umma kama unaweza kuchukuliwa vyema, katika hali zote, kama haukufanyiwa hesabu na kusababisha, moja kwa moja au si moja kwa moja, katika hisa au dhamana kupatikana kwa ajili ya kuchangiwa au kununuliwa na watu wengine kuliko wale waliopewa fursa au mwaliko, au vyenginevyo kuwa ni jambo la ndani la wasiwasi kwa watu wanauofanya na kuupokea, na hasa:-

(a) sharti katika kanuni za kampuni linalozuia mialiko kwa umma kujiunga kwenye hisa au dhamana halitachukuliwa kama linazuia kutoa mialiko kwa wanachama au wamiliki wa dhamana ambayo inaweza kuonekana vyema kama ilivyoelezwa kabla; na

(b) masharti ya Sheria hii yanayohusu makampuni binafsi yatachukuliwa ipasavyo.

Utoaji wa Hisa Katika Malipo ya Msingi na Punguzo Kwenye Hisa za Upendeleo Zinazolipwa Matumizi ya malipo ya msingi yaliyopokewa katika utoaji wa hisa.

**64.**-(1) Pale ambapo kampuni inatoa hisa, iwe kwa ajili ya fedha au vyenginevyo, jumla sawa na kiasi au thamani ya jumla ya malipo kwenye hisa hizo kuhamishiwa kwenye akaunti, itakayoitwa "akaunti ya malipo ya msingi", masharti ya Sheria hii yanayohusiana na kupunguzwa mtaji wa hisa wa kampuni, isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki, yatatumika kama kwamba akaunti ya malipo ya msingi zilikuwa ni mtaji wa hisa uliolipwa wa kampuni.

(2) Akaunti ya malipo ya msingi inaweza, bila ya kujali kitu chochote katika kifungu kidogo cha (1), kutumiwa na kampuni katika kulipa hisa ambazo hazikutolewa za kampuni zinazotolewa kwa wanachama wa kampuni kama hisa za bonasi zilizolipiwa kamili, katika kufuta:-

(a) matumizi ya Awali ya kampuni; au

(b) matumizi ya, au kamisheni iliyolipwa au punguzo lililoruhusiwa kwenye, utoaji wowote wa hisa au dhamana za kampuni; au

(c) katika kutoa malipo ya msingi yanayolipwa katika kukomboa hisa zozote za upendeleo zinazokomboleka au ya dhamana zozote za kampuni.

Uwezo wa kutoa hisa kwa punguzo.

**65.-**(1) Ila kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki, itakuwa halali kwa kampuni kutoa hisa kwa punguzo kwenye kampuni za daraja ambayo tayari imetolewa. Isipokuwa kwamba:-

(a) utoaji wa hisa kwa punguzo utaidhinishwa kwa azimio lililopitishwa katika mkutano mkuu wa kampuni, na utaidhinishwa na mahakama;

(b) azimio litaainisha kiwango cha juu cha punguzo ambacho kitatolewa kwenye hisa;

(c) si chini ya mwaka mmoja tokea tarehe ya utoaji umepita tangu tarehe ambayo kampuni ilikuwa na haki ya kuanza biashara;

(d) hisa zitakazotolewa kwa punguzo zitatolewa ndani ya mwezi mmoja baada ya tarehe ambayo utoaji umeidhinishwa na mahakama au ndani ya muda wa zaida ulioongezwa kama mahakama itavyoruhusu.

(2) Pale ambapo kampuni inapitisha azimio linaloidhinisha utoaji wa hisa kwa punguzo, inaweza kuiomba mahakama kutoa amri juu ya utoaji huo, na juu ya ombi lolote kama hilo mahakama, ikiwa kwa kuzingatia mazingira yote ya suala lenyewe inafikiri inafaa kufanya, inaweza kutoa amri kuidhinisha utoaji kwa masharti kama inavyoona inafaa.

(3) Kila muhtasari wa ununuzi wa hisa kuhusiana na utoaji wa hisa utakuwa na maelezo ya punguzo lililoruhusiwa juu ya utoaji wa hisa au ya kiasi ambacho hakijafutwa cha punguzo hilo katika tarehe ya utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa.

Endapo ukiukaji utafanywa katika kufuata kifungu hiki kidogo, kampuni na kila ofisa wa kampuni aliyeshiriki katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

Nguvu ya kutoa hisa za upendeleo zinazoko-mboleka.

**66.-**(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, kampuni yenye ukomo wa hisa inaweza, ikiwa imeidhinishwa na kanuni zake, kutoa hisa za upendeleo ambazo zinatakiwa, au kwa chaguo la kampuni zinaweza, kukombolewa.

Isipokuwa kwamba:-

(a) hisa kama hizo zitakombolewa isipokuwa kutoka kwenye faida ya kampuni ambayo vyenginevyo ingekuwa inapatikana kwa ajili ya mgao au kutokana na mapato ya utoaji mpya wa hisa uliofanywa kwa madhumuni ya ukombozi;

(b) hisa zozote kama hizo hazitakombolewa mpaka ziwe zimelipwa zote;

(c) malipo ya msingi, kama yapo, yanayolipwa kwa kukomboa, yatatolewa kutokana na faida ya kampuni au kutokana na akaunti ya malipo ya msingi ya kampuni kabla ya hisa kukombolewa;

(d) ambapo hisa zozote kama hizo zinakombolewa kwa njia nyengine isiyokuwa kutokana na mapato ya utoaji mpya wa hisa, faida ambayo vyenginevyo ingepatikana kwa ajili ya mgao itahamishiwa kwenye mfuko wa akiba, utakaoitwa "mfuko wa wa akiba wa kukombolea mtaji", kiasi sawa na kiasi cha msingi wa hisa zilizokombolewa, na masharti ya Sheria hii yanayohusiana na kupunguzwa mtaji wa hisa wa kampuni yatatumika, isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki kuomba kama mfuko wa akiba wa ukombozi wa mtaji ulikuwa mtaji wa hisa uliolipwa wa kampuni.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, ukombozi wa hisa za upendeleo hizo unaweza kufanyika kwa masharti na kwa namna ambayo imewekwa na kanuni za kampuni.

(3) Ukombozi wa hisa za upendeleo chini ya kifungu hiki na kampuni hazitachukuliwa kama ni kupunguza kiasi cha mtaji wa hisa za kampuni zilizoidhinishwa.

(4) Endapo katika kutekeleza kifungu hiki kampuni imezikomboa au inataka kuzikomboa hisa zozote za upendeleo, itakuwa na uwezo wa kutoa hisa hadi kiasi cha hisa za msingi zilizokombolewa au zitakazokombolewa kama kwamba hisa hizo hazijawahipo kutolewa, na kwa mnasaba huo mtaji wa hisa wa kampuni kwa madhumuni ya sheria zozote zinazohusiana na ushuru wa stempu hautafahamika kuwa umeongezeka kwa kutoa hisa kwa mujibu wa kifungu hiki kidogo.

Isipokuwa kwamba, pale ambapo hisa mpya zinatolewa kabla ya ukombozi wa hisa za zamani, hisa mpya, kwa kadiri zinavyohusiana na ushuru wa stempu, hazitafahamika kuwa zimetolewa katika kutekeleza kifungu hiki kidogo isipokuwa hisa za zamani ziwe zimekombolewa ndani ya mwezi mmoja baada ya utoaji wa hisa mpya.

(5) Mfuko wa akiba wa ukombozi wa mtaji unaweza, bila ya kujali chcochote katika kifungu hiki, kutumiwa na kampuni katika kulipa hisa zisizotolewa za kampuni zinazotaka kutolewa kwa wanachama wa kampuni kama hisa za bonasi zilizolipwa kamili.

Masharti Mengineyo Kuhusiana na Mtaji wa Hisa

Uwezo wa kampuni wa kupanga viasi tafauti vya kulipwa juu ya hisa.

**67.** Kampuni, iwapo imeruhusiwa na kanuni zake, inaweza kufanya mojawapo lolote au zaidi ya mambo yafuatayo:-

(a) kufanya mipango juu ya utoaji wa hisa tafauti kati ya wanahisa katika kiasi na muda wa malipo ya maombi ya hisa zao;

(b) kukubali kutoka mwanachama yeyote yote au sehemu ya kiasi kilichobaki bila kulipwa kwenye hisa yoyote

inayomilikiwa naye, ingawa hakuna sehemu ya kiasi hicho kimeombwa;

(c) kulipa gawio kulingana na kima kilicholipwa kwa kila hisa ambapo kima kikubwa zaidi kinalipwa kwenye baadhi ya hisa kuliko kwenye nyengine.

Dhima ya akiba ya kampuni yenye ukomo.

**68.** Kampuni yenye ukomo inaweza kwa azimio maalumu kuamua kwamba sehemu yoyote ya mtaji wake wa hisa ambayo haijawahi kuombwa haitaweza kuombwa ila katika tukio na kwa madhumuni ya kampuni kufungwa, na katika hali hiyo sehemu hiyo ya mtaji wake wa hisa hautaweza kuombwa ila katika tukio hilo na kwa madhumuni yaliyoelezwa kabla.

Uwezo wa kampuni yenye ukomo wa hisa wa kubadilisha mtaji wake wa hisa.

**69.**-(1) Kampuni yenye ukomo wa hisa au kampuni yenye ukomo wa dhamana na yenye mtaji wa hisa, kama inaruhusiwa na kanuni zake, inaweza kubadilisha masharti ya katiba yake kama ifuatavyo, yaani, inaweza:-

(a) kuongeza mtaji wake wa hisa kwa hisa mpya kwa kima ambacho inahisi kinahitajika;

(b) kujumuisha na kugawanya zote au mtaji wake wa hisa wowote katika hisa za kima kikubwa kuliko hisa zake zilizopo;

(c) kubadilisha zote au yoyote katika hisa zake zilizolipwa katika hisa, na kuzibadilisha hisa katika hisa zilizolipwa za ukubwa wowote;

(d) kuzigawanya hisa zake, au yoyote kati yao, katika hisa za kiasi kidogo zaidi kuliko zilivyowekwa na katiba, ili, hata hivyo, katika ugawanyaji uwiano kati ya kiasi kilicholipwa na kiasi, kama kipo, ambacho hakijalipwa juu ya kila hisa iliyopunguzwa kitakuwa sawa kama kilivyokuwa katika hisa ambayo hisa iliyopunguzwa imatokea;

(e) kufuta hisa ambazo, katika tarehe ya kupitisha azimio kwa ajili hiyo, hazikuchukuliwa au kukubaliwa kuchukuliwa na mtu yeyote, na kupunguza kiasi cha mtaji wake wa hisa kwa kiasi cha hisa kilichofutwa.

(2) Uwezo uliotolewa na kifungu hiki utatumiwa na kampuni kwenye mkutano mkuu.

(3) Ufutaji wa hisa kwa mujibu wa kifungu hiki hautachukuliwa kumaanisha kupunguza mtaji wa hisa kwa mujibu wa Sheria hii.

Taarifa kwa Mrajis kuhusu ujumuishaji wa mtaji wa hisa, ubadilishaji wa hisa katika bidhaa, n.k.

**70.**-(1) Endapo kampuni yenye mtaji wa hisa:-

(a) imejumuisha na kugawanya mtaji wake wa hisa katika hisa za kima kikubwa kuliko hisa zake zilizopo; au

(b) imebadilisha hisa zozote kuwa bidhaa; au

(c) imebadilisha tena bidhaa kuwa hisa; au

(d) imezigawanya hisa zake au mojawapo yoyote; au

(e) imekomboa hisa yoyote iliyopendekezwa inayokomboleka; au

(f) imefuta hisa zozote, vyenginevyo isipokuwa kuhusiana na upunguzaji wa mtaji wa hisa kwa mujibu wa kifungu cha 74;

itatoa taarifa ndani ya mwezi mmoja baada ya kufanya hivyo kwa Mrajis inayobainisha, kama hali itakavyokuwa, hisa zilizojumuishwa, zilizogawanywa, zilizobadilishwa, zilizogawanywa kuwa ndogo zaidi, zilizokombolewa au kufutwa, au bidhaa zilizobadilishwa tena.

(2) Endapo ukiukaji utafanywa katika kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa aliyeshiriki katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji huo.

Taarifa ya ongezeko la mtaji wa hisa.

**71.**-(1) Pale ambapo kampuni yenye mtaji wa hisa, kama hisa zake zimebadilishwa au hazikubadilishwa katika bidhaa, imeongeza mtaji wake wa hisa kupindukia mtaji wake wa hisa uliosajiliwa, ndani ya siku kumi na tano baada ya kupitisha azimio lililoidhinisha ongezeko, itatoa taarifa kwa Mrajis ya ongezeko hilo, na Mrajis ataweka rikodi ya ongezeko hilo.

(2) Taarifa itakayotolewa kama ilivyoelezwa kabla itajumuisha maelezo kama yatakavyowekwa kuhusiana na daraja za hisa zilizoathirika na masharti ambayo hisa mpya zimetolewa au zitatolewa, na kutawasilishwa kwa Mrajis pamoja na taarifa hiyo nakala iliyochapishwa ya azimio lililoidhinisha ongezeko hilo.

(3) Endapo ukiukaji umefanyika katika kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni aliyeshiriki kwenye ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji huo.

Uwezo wa kampuni isiyokuwa na ukomo wa kuweka mtaji wa hisa wa akiba wakati wa kujisajili tena.

**72.** Kampuni yenye ukomo wa hisa inaweza, kwa azimio lake la kujisajili kama kampuni yenye ukomo kwa mujibu wa Sheria hii, kufanya mojawapo au yote mawili ya mambo yafuatayo ambayo ni:-

(a) kuongeza kiasi cha msingi cha mtaji wake wa hisa kwa kuongeza kiasi cha msingi cha kila hisa yake, lakini kwa kuzingatia sharti kuwa hakuna sehemu ya hisa iliyoongezwa itakuwa na uwezo wa kuombwa ila katika tukio na kwa madhumuni ya kampuni kufungwa;

(b) kuweka sharti kwamba sehemu maalumu ya mtaji wake wa hisa haitakuwa na uwezo wa kuombwa ila katika tukio hilo na kwa madhumuni ya kampuni kufungwa.

Uwezo wa kampuni kulipa riba kutoakana na mtaji wa hisa katika hali maalumu.

**73.** Ambapo hisa zozote za kampuni zinatolewa kwa madhumuni ya kulipia gharama za ujenzi wa kazi zozote au majengo au ununuzi wa mitambo yoyote ambayo haiwezi kutoa faida kwa muda mrefu, kampuni inaweza kulipa riba juu ya mtaji huo wa hisa kama ambavyo kwa sasa inalipwa kwa kipindi na kwa kufuata masharti na vizuizi vilivyotajwa katika

kifungu hiki, na inaweza kutoza ada kwenye kiasi kilicholipwa hivyo kwa njia ya riba kwenye mtaji kama sehemu ya gharama ya kazi ya ujenzi au jengo, au uwekaji wa mitambo.

Isipokuwa kwamba:-

(a) hakuna malipo kama hayo, kama yameidhinishwa na kanuni au kwa azimio maalumu, yatakayofanywa bila ya idhini ya kabla ya Mrajis ambayo idhini hiyo itakuwa ni ithibati ya mwisho kwa madhumuni ya kifungu hiki kwa hisa za kampuni ambazo idhini yake imetolewa kwa madhumuni yaliyotajwa katika kifungu hiki;

(b) kabla ya kuidhinisha malipo yoyote kama hayo Mrajis anaweza, kwa gharama ya kampuni, kumteua mtu kuchunguza na kuripoti kwake kuhusu mazingira ya suala hilo, na inaweza, kabla ya kufanya uteuzi, kuitaka kampuni kuweka dhamana kwa ajili ya malipo ya gharama za uchunguzi;

(c) malipo yatafanywa kwa kipindi kile tu kama itakavyoamuliwa na Mrajis na kipindi hicho katika hali yoyote hakitapindukia kumalizika nusu mwaka inayofuata baada ya nusu mwaka ambayoo kazi au majengo kweli yamekamilika au mitambo imewekwa;

(d) kiwango cha riba katika hali yoyote hakitazidi asilimia nne kwa mwaka au kiwango chengine kama Mrajis atakavyoweza kwa wakati huo kutangaza katika Gazeti la Serikali;

(e) malipo ya riba hayatapunguza kima kilicholipwa kwenye hisa ambazo kutokana na hisa hizo inalipwa.

Kupunguza Mtaji wa Hisa Azimio maalumu kwa kupunguza mtaji wa hisa.

**74.-**(1) Kampuni yenye ukomo wa hisa au kampuni yenye ukomo wa dhamana na yenye mtaji wa hisa inaweza, ikiwa imeidhinishwa na kanuni zake na kwa masharti yaliyomo humu, kwa azimio maalumu kupunguza mtaji wake wa hisa kwa namna yoyote, na hasa, inaweza:-

(a) kufuta au kupunguza dhima kwenye hisa zake zozote kuhusiana na mtaji wa hisa ambao haukulipwa; au

(b) ama kwa kuwa imefuta au bila ya kufuta au kupunguza dhima ya hisa zake zozote, kufuta mtaji wa hisa wowote ambao umepotezwa au usiowakilishwa na mali zilizopo; au

(c) ama kwa kuwa imefuta au bila ya kufuta au kupunguza dhima ya hisa zake zozote, kuilipa hisa yoyote iliyolipwa ambayo ni zaidi ya mahitaji ya kampuni;

(d) ikiwa na hadi sasa kama ni lazima, kubadilisha katiba yake kwa kupunguza kiasi cha mtaji wake wa hisa na hisa zake ipasavyo.

(2) Taarifa inayotolewa ya nia ya kupendekeza azimio maalumu la kupunguza mtaji wa hisa wa kampuni itakuwa imeambatanishwa na hati ya mkurugenzi ya kufilisika aliyopewa kwa mujibu wa kifungu cha 75 na, ambapo inafaa, ripoti ya wakaguzi wa hesabu kuhusiana na hilo.

(3) Bila ya kuathiri kifungu cha 76, azimio maalumu lililopitishwa kupunguza mtaji wa hisa wa kampuni halitatumika mpaka baada ya azimio kusajiliwa na Mrajis na azimio, katika hali yoyote, halitasajiliwa na Mrajis mpaka siku thalathini na tano kuanzia tarehe ambayo lilipitishwa.

(4) Azimio maalumu linalopunguza mtaji wa hisa wa kampuni litatangazwa katika Gazeti la Serikali, na kwa kampuni ya umma, gazeti la kitaifa, katika kila hali ndani ya siku tano za kazi baada ya azimio kupitishwa kama kampuni inashindwa kutekeleza kifungu kidogo hiki, wakurugenzi watatozwa faini.

Cheti cha wakurugenzi kwa kufilisika.

**75.**-(1) Pale ambapo inapendekezwa kupitisha azimio kupunguza mtaji wa hisa wa kampuni, wakurugenzi walio wengi watathibitisha kuwa walifanya uchunguzi kamili katika shughuli za kampuni, na kwamba, baada kufanya hivyo, wamekuwa na maoni kuwa kampuni itakuwa na uwezo wa kulipa madeni yake kamili ndani ya miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya leseni au, kama kampuni inafungwa ndani ya kipindi hicho, tarehe ya kuanza kuifunga.

(2) Kama kampuni ina wakaguzi, cheti cha wakurugenzi kitaambatana na ripoti kutoka kwa wakaguzi kuthibitisha kwamba wamechunguza hali ya shughuli za kampuni na hawafahamu chochote kinachoonesha kuwa hati ya wakurugenzi ya kufilisika haina mantiki.

(3) Kila mkurugenzi wa kampuni anayetoa cheti chini ya kifungu hiki bila ya kuwa na sababu za msingi kwa maoni yake, atapewa adhabu ya kifungo kwa muda usiozidi miezi sita au faini isiyozidi shilingi laki tatu, au adhabu zote mbili, na kama kampuni imefungwa kwa azimio lililopitishwa ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili baada ya kutoa cheti, lakini madeni yake hayakulipwa au kuwekewa utaratibu kamili ndani ya kipindi kilichoelezwa katika cheti, itachukuliwa isipokuwa imeoneshwa vyenginevyo kuwa mkurugenzi hakuwa na sababu za msingi kwa maoni yake.

Maombi kwa mahakama kwa wakopeshaji wanaopinga punguzo.

**76.**-(1) Kuhusu kupunguza mtaji wa hisa wa kampuni kwa madhumuni mengine kuliko yale yaliyotajwa katika kifungu cha 74(1)(b), mdai yeyote wa kampuni anaweza kuiomba mahakama kupinga mapendekezo ya kupunguza kwa misingi kwamba nafasi yake kama mdai itaathiriwa na upunguzaji.

(2) Ombi kwa mujibu wa kifungu hiki litatolewa:-

(a) ndani ya siku 28 za tangazo la azimio maalumu katika Gazeti la Serikali au, pale inapobidi, gazeti la kitaifa; au

(b) katika hali ya kushindwa kutangaza azimio maalumu kama inavyotakiwa na kifungu 74(4), ndani ya kipindi cha ziada kama mahakama itakavyoona inafaa.

(3) Juu ya maombi chini ya kifungu hiki mahakama inaweza kutoa amri ya kuzuia kupunguza au kuuoanisha upunguzaji ama wote au sehemu yake na kwa masharti na hali kama itakavyoona inafaa.

(4) Mabadiliko katika katiba ya kampuni yaliyofanywa kutokana na amri kwa mujibu wa kifungu hiki yatakuwa na athari sawa kama kwamba yalifanywa kwa azimio, na Sheria hii itatumika ipasavyo kwa Katiba hiyo iliyobadilishwa.

Dhima ya wanachama na wakurugenzi kuhusiana na hisa zilizopunguzwa.

**77.**-(1) Kuhusu kupunguza mtaji ambao haukuathirika kwa mujibu wa vifungu vya 74, 75 na 76, ikiwa ni pamoja na hali ambapo cheti kinatolewa na wakurugenzi chini ya kifungu cha 75 ambapo wakurugenzi hawakuwa na sababu za msingi za kuamini katika ukweli wake, mdai yeyote wa kampuni hiyo ambaye angekuwa na haki ya kupinga mapendekezo ya kupunguza chini ya kifungu cha 76 anaweza kuiomba mahakama kupinga punguzo kwa misingi kwamba nafasi yake kama mdai imeathirika kwa kupunguza huko.

(2) Juu ya maombi chini ya kifungu hiki mahakama inaweza kutoa amri kama inavyoona inafaa, ikiwa ni pamoja na amri kwamba kila mwanachama wa kampuni katika tarehe ya kupitishwa azimio maalumu la kupunguza mtaji wa hisa ambaye akijua kushindwa kwa kampuni na kifungu cha 75, 75 na 76 na, pale inapofaa, kila mkurugenzi aliyetoa cheti cha wakurugenzi chini ya kifungu cha 75 itampasa:-

(a) kuchangia katika malipo ya madeni au madai ya mdai, isipokuwa kwamba kwa mwanachama mchango huo utakuwa katika kiasi kisichozidi kiasi ambacho angepaswa kuchangia kama kampuni ilianza kufungwa katika siku kabla ya tarehe ya kupitishwa azimio maalumu; au

(b) kuchangia ulipaji wa kiasi ambacho mtaji wa hisa wa kampuni kilipunguzwa kutokana na kupitishwa azimio maalumu.

(3) Hakuna jambo katika kifungu hiki litakaloathiri haki za wachangiaji miongoni mwao.

Mabadiliko ya Haki za Wamilki wa Hisa Haki za wamiliki wa daraja maalumu za hisa.

**78.**-(1) Kama, katika kampuni ambayo mtaji wake wa hisa umegawanywa katika daraja mbali mbali za hisa, masharti yamewekwa na katiba au kanuni kuidhinisha mabadiliko ya haki zilizoambatana na masharti yoyote ya daraja ya hisa katika kampuni, kwa ridhaa ya uwiano wowote ulioainishwa ya wamiliki wa hisa zilizotolewa za daraja hiyo juu ya kuidhinisha azimio lililopitishwa katika mkutano mwengine wa wamiliki wa hisa hizo, na kwa mujibu wa masharti yaliyotajwa haki zilizoambatana na daraja yoyote ya hisa katika wakati wowote zilipobadilishwa, wamiliki si chini ya asilimia kumi na tano ya idadi ya hisa zilizotolewa za daraja

hiyo, kuwa ni watu ambao hawakuridhia au kupiga kura kuunga mkono azimio kuhusu mabadiliko, wanaweza kuiomba mahakama kufuta mabadiliko, na, ambapo maombi yoyote yamefanywa, mabadiliko hayatakuwa na athari isipokuwa na mpaka pale yatakapothibitishwa na mahakama.

(2) Maombi chini ya kifungu hiki yatafanywa ndani ya siku ishirini na moja baada ya tarehe ambayo ilitolewa idhini au azimio kupitishwa, kadiri hali itakavyokuwa, na yanaweza kufanywa kwa niaba ya wamiliki wa hisa walio na haki ya kufanywa maombi na mmoja wao au zaidi kama watakavyoteua kwa maandishi kwa madhumuni hayo.

(3) Juu ya maombi yoyote ya namna hiyo mahakama, baada ya kumsikiliza muombaji na watu wengine wowote ambao wameiomba mahakama kusikilizwa na wanaonekana na mahakama kuwa wana manufaa kwenye maombi, inaweza, ikiwa imeridhika, kwa kuzingatia mazingira yote ya kesi, kwamba yangekuwa si ya haki, yenye athari na wanahisa wa daraja lililowakilishwa na muombaji, kutoruhusu mabadiliko na, kama haikuridhika, kuthibitisha mabadiliko.

(4) Uamuzi wa mahakama juu ya ombi lolote la namna hiyo utakuwa ni wa mwisho.

(5) Kampuni ndani ya siku kumi na tano baada ya maamuzi ya mahakama juu ya maombi yoyote kama hayo itapeleka nakala ya hati iliyothibitishwa ya amri iliyotolewa kwa Mrajis, na, kama ukiukwaji utafanywa katika kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye ameshiriki katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji huo.

(6) Neno "mabadiliko" katika kifungu hiki linajumuisha ubatilishaji na neno "yenye kubadilishwa" litachukuliwa kwa mnasaba huo huo.

**79.** Hisa au maslahi mengine ya mwanachama yeyote katika kampuni itakuwa ni mali inayohamishika, inayohaulishika kwa namna ambayo inaelezwa na kanuni za kampuni. Uhamisho wa Hisa na Dhamana, Ushahidi wa Jina n.k. Aina ya hisa.

**80.-**(1) Soko la hisa lililothibitishwa linaweza kuanzisha kanzi ambayo ndani yake dhamana zilizotolewa zinaweza kutunzwa kwa sharti kwamba mamlaka au chombo chengine chenye uamuzi cha soko hilo kitaweka kanuni zinazohusiana na ulinzi wenye usalama, uhamishaji na ripoti za kutunzwa na Mrajis zinazohusiana na shughuli kuhusu dhamana zilizowekwa. Kanzi ya hisa.

(2) Kanuni zilizoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) zitamtosheleza Mrajis.

(3) Uhaulishaji wa dhamana zilizowekwa katika kanzi inayosimamiwa na soko la hisa lililokubaliwa utateklezwa.

**81.** Kila hisa katika kampuni yenye mtaji wa hisa itaainishwa kwa nambari yeke inayostahiki. Kutia nambari hisa.

Isipokuwa kwamba, kama katika wakati wowote hisa zote zilizotolewa katika kampuni, au hisa zote zilizotolewa humo za daraja fulani, zimelipwa kikamilifu sawasawa kwa madhumuni yote, hakuna haja ya hisa hizo baada ya hapo kuwa na idadi kubainisha madamu inabakia kuwa imelipwa kikamilifu na ina daraja sawia kwa madhumuni yote na hisa zote za daraja moja zilizotolewa kwa wakati huo na kulipwa kikamilifu.

Uhaulishaji kutosajiliwa isipokuwa kwa kutoa hati ya uhaulishaji.

**82.** Bila ya kujali chochote katika kanuni za kampuni, haitakuwa halali kwa kampuni kujiandikisha kwa uhaulishaji wa hisa au dhamana za kampuni isipokuwa hati sahihi ya uhaulishaji imewasilishwa kwa kampuni:
Isipokuwa kwamba hakuna kitu katika kifungu hiki kitaathiri mamlaka yoyote ya uhaulishaji ya kampuni kujiandikisha kama mmiliki wa hisa au mmiliki wa dhamana ya kampuni kwa mtu yeyote ambaye haki ya hisa zozote au dhamana za kampuni zimehaulishwa kwa kutumia sheria.

Uhaulishaji kwa mwakilishi wa kisheria.

**83.** Uhaulishaji wa hisa au maslahi mengine ya mwanachama wa kampuni ambaye amefariki uliofanywa na mwakilishi wake wa kisheria utakuwa, ingawa mwakilishi wa kisheria yeye mwenyewe si mwanachama wa kampuni, halali kama kwamba yeye amekuwa mwanachama wakati wa utekelezaji wa hati ya uhaulishaji.

Usajili wa uhaulishaji kwa maombi ya mhaulishaji.

**84.** Juu ya maombi ya mhaulishaji au hisa yoyote au maslahi katika kampuni, kampuni itaingiza katika daftari lake la wanachama jina la anayehaulishiwa kwa namna ile ile na kwa kufuata masharti sawa kama kwamba maombi kwa ajili ya kuingizwa yalifanywa na mhaulishiwaji.

Taarifa ya kukataa kusajili uhaulishaji.

**85.-**(1) Kama kampuni inakataa kuandikisha uhaulishaji wa hisa yoyote au dhamana, kampuni itapeleka, ndani ya miezi miwili baada ya tarehe ambayo uhaulishaji uliombwa kwa kampuni, kwa mhaulishiwaji taarifa ya kukataa huko.

(2) Endapo ukiukaji utafanywa katika kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

Utoaji wa vyeti vya uhaulishaji.

**86.-**(1) Utoaji wa vyeti kwa kampuni kwa hati ya uhaulishaji wa hisa au dhamana za kampuni utachukuliwa kama uwakilishi na kampuni kwa mtu yeyote kwa imani kwamba vyeti vilivyotolewa na kampuni ni hati zinazodhihirisha ushahidi wa mwanzo wa mmiliki wa hisa au dhamana ya mhaulishaji aliyetajwa katika hati ya uhaulishaji, lakini si kama uwakilishi kwamba mhaulishaji ana umiliki wowote katika hisa au dhamana.

(2) Iwapo mtu yeyote anchukua hatua kwa kutumia vyeti vya uongo vya kampuni vilivyofanywa kwa uzembe, kampuni itakuwa chini ya dhima ilie ile kama kwamba vyeti vimetolewa kwa udanganyifu.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki:-

(a) hati ya uhaulishaji itachukuliwa kuwa imethibitishwa kama ina maneno "cheti kilichoombwa" au maneno na yenye maana kama hiyo;

(b) uthibitisho wa hati ya uhaulishaji utachukuliwa kuwa umefanywa na kampuni kama:-

(i) mtu anayetoa hati ni mtu mwenye mamlaka ya kutoa hati zilizothibitishwa za uhaulishaji kwa niaba ya kampuni; na

(ii) uthibitisho umetiwa saini na mtu mwenye mamlaka ya kuthibitisha uhaulishaji kwa niaba ya kampuni au kwa ofisa yeyote au mtumishi ama wa kampuni au shirika lililoidhinishwa kufanya hivyo;

(c) uthibitisho utachukuliwa kuwa umetiwa saini na mtu yeyote kama:-

(i) unadai kuwa umethibitishwa kwa saini yake au hati zake (kama zimeandikwa kwa mkono au la); na

(ii) haikuoneshwa kuwa saini au hati haikutiwa au hazikuwekwa hapo ama na yeye mwenyewe wala na mtu yeyote aliyeidhinishwa kutumia saini au hati kwa madhumuni ya kuthibitisha uhaulishaji kwa niaba ya kampuni.

Majukumu ya kampuni kuhusiana na utoaji wa vyeti.

**87.**-(1) Kila kampuni itakamilisha, ndani ya miezi mitatu baada ya ugawaji wowote wa hisa zake, dhamana au bidhaa za dhamana na ndani ya miezi mitatu baada ya tarehe ambayo uhaulishaji wa hisa hizo, dhamana au bidhaa za dhamana zimeombwa kwenye kampuni, na kuwa tayari kwa ajili ya uwasilishaji vyeti vya hisa zote, dhamana na vyeti vya bidhaa za dhamana zote zilizogawiwa au kuhamishwa, isipokuwa masharti ya utoaji wa hisa, dhamana au bidhaa za dhamana yamewekwa mengine.

Kwa madhumuni ya kifungu hiki kidogo "uhaulishaji" maana yake ni uhaulishaji uliopigwa muhuri au vyenginevyo ni halali, na haujumuishi pamoja uhaulishaji kama ule ambao kampuni kwa sababu yoyote ina haki ya kukataa kuusajili na hakuusajili.

(2) Kama ukiukaji umefanyika katika kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye amehusika katika ukiukaji atatozwa faini ya ukiukwaji.

(3) Kama kampuni yoyote iliyopewa taarifa kuitaka kampuni kurekebisha ukiukaji wowote katika kutekeleza masharti ya kifungu kidogo cha (1) inashindwa kurekebisha ukiukaji huo ndani ya siku kumi baada ya kupewa taarifa, mahakama inaweza, juu ya maombi ya mtu mwenye haki ya kuwa na vyeti au dhamana zilizowasilishwa kwake, kutoa amri kuielekeza kampuni na ofisa yeyote wa kampuni ya kurekebisha ukiukaji ndani ya muda kama vile utakavyoainishwa katika amri, na amri yoyote kama hiyo inaweza kuweka masharti kwamba gharama zote zinazotokana na maombi zitalipwa na kampuni au na ofisa yeyote wa kampuni anayewajibika kwa ukiukaji huo.

Cheti kuwa ni ushahidi wa umiliki.

**88.** Cheti, chenye muhuri wa kampuni wa kawaida, kinachobainisha hisa zozote zinazomilikiwa na mwanachama yeyote, kitakuwa ni ushahidi wa kwanza wa hatimiliki ya mwanachama kwenye hisa.

Ushahidi wa utoaji wa hati ya wasia.

**89.** Uwasilishaji kwenye kampuni wa hati yoyote ambayo kwa sheria ni ushahidi wa kutosha kwamba:-

(a) hati ya wasia, au barua za usimamizi wa mali isiyohamishika, za marehemu umetolewa au zimetolewa kwa mtu fulani; au

(b) Msimamizi Mkuu amechukua usimamizi wa mali isiyohamishika chini ya kifungu cha 5 chaa Dikrii ya Msimamizi Mkuu.

utakubaliwa na kampuni, bila ya kujali kitu chochote katika kanuni hizi, kama ni ushahidi wa kutosha wa utoaji huo au ahadi.

Utoaji na utumikaji wa waranti za hisa kwa mmiliki.

**90.-**(1) Kampuni yenye ukomo wa hisa, kama inaruhusiwa na kanuni zake, inaweza, kuhusiana na hisa zozote zilizolipwa kamili, kutoa chini ya muhuri wake wa kawaida waranti unaoeleza kuwa mchukuaji wa waranti huo ana haki kwenye hisa zilizoainishwa humo, na inaweza kutoa, kwa kuponi au vyenginevyo, kwa ajili ya malipo ya gawio baadaye hisa zilizoingizwa kwenye waranti.

(2) Waranti huo kama ulivyoelezwa katika Sheria hii unaitwa "waranti wa hisa".

(3) Waranti wa hisa utampa haki aliyenao kwenye hisa zilizoainishwa ndani yake, na hisa zinaweza kuhaulishwa kwa kuwasilisha waranti huo.

Adhabu kwa kuijifanya mmiliki wa hisa.

**91.** Kama mtu yeyote kwa uongo na udanganyifu anaigiza mmiliki yeyote wa hisa yoyote au mwenye maslahi katika kampuni yoyote, au wa waranti wowote wa hisa au kuponi, iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria hii, na hivyo anapata au anajaribu kupata hisa yoyote ile au maslahi au waranti wa hisa au kuponi, au anapokea au anajaribu kupokea fedha yoyote inayomsatahikia mmiliki yoyote yule, kama kwamba mkosaji alikuwa mmiliki wa kweli na halali, atakuwa anatenda kosa, na akitiwa hatiani atahukumiwa kifungo kwa muda wowote usiozidi miaka saba.

Makosa kuhusiana na waranti za hisa.

**92.-**(1) Kama mtu yeyote:-

(a) kwa nia ya kutapeli, anaghushi au anabadilisha, au anatoa, anatamka, anatupa, au anazuia, akijua kwamba kwamba kughushiwa au kubadilishwa, hisa yoyote, waranti au kuponi, au hati yoyote inayodai kuwa ni waranti wa hisa au kuponi, iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria hii; au

(b) kwa njia ya waranti wa hisa ulioghushiwa au uliobadilishwa, kuponi, au unaodai kama ilivyoelezwa, matakwa au

majaribio ya kupata au kupokea hisa yoyote au maslahi katika kampuni yoyote chini ya Sheria hii, au kupokea gawio lolote au fedha inayolipwa kuhusiana na hayo, akijua hati, kuponi, au hati ya kughushiwa au kubadilishwa;

atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kifungo cha maisha au cha muda wowote usiopungua miaka mitatu.

(2) Ikiwa mtu yeyote bila mamlaka halali au udhuru, ambaye ushahidi utakuwa dhidi yake:-

(a) atachimbua au kufanya juu ya bango, ubao, jiwe, au kitu chengine chochote, hati yoyote ya hisa au kuponi inayodai kuwa:-

(i) hati ya hisa au kuponi iliyotolewa au kutengenezwa na kampuni fulani yoyote kwa mujibu wa Sheria hii; au

(ii) hati tupu ya hisa au kuponi iliyotolewa au kutengenezwa; au

(iii) sehamu ya hati hiyo ya hisa au kuponi; au

(b) anatumia bango, ubao, jiwe, au kitu chengine, kwa ajili ya kutengenezea au kuchapisha hati yoyote ya hisa au kuponi, au hati yoyote tupu ya hisa au kuponi, au sehemu yake yoyote kwa mtiririko huo; au

(c) kwa kujua, analo katika hifadhi yake au milki bango, ubao, jiwe, au kitu chengine ambacho juu yake hati yoyote ya hisa au kuponi, au sehemu yake yoyote kama ilivyoelezwa imechimbuliwa au kutengenezwa;

atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atafungwa jela kwa muda wowote usiozidi miaka kumi na nne na si chini ya miaka mitatu.

Masharti Maalumu Kuhusiana na Dhamana Masharti kuhusiana na usajili wa dhamana.

**93.**-(1) Kila kampuni ambayo, baada ya siku iliyowekwa, inatoa mfululizo wa dhamana itaweka katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni daftari la wamiliki wa dhamana hizo.

Isipokuwa kwamba:-

(a) ambapo kazi ya kutengeneza daftari hilo inafanyika katika ofisi nyengine isiyokuwa ofisi iliyosajiliwa, daftari hilo linaweza kuhifadhiwa kwenye ofisi hiyo; na

(b) ambapo kazi ya kutengeneza daftari hilo ni kwa makubaliano ya kampuni kufanywa na mtu fulani kwa niaba ya kampuni, daftari hilo linaweza kuhifadhiwa kwenye ofisi ya mtu ambayo kazi imefanywa.

(2) Kila kampuni itatoa taarifa kwa Mrajis ya mahali ambapo daftari linahifadhiwa na mabadiliko yoyote katika mahali hapo;

Isipokuwa kwamba kampuni haitalazimika kutoa taarifa chini ya kifungu kidogo hiki ikiwa daftari, wakati wote tangu lilipowekwa, limehifadhiwa katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni.

Haki ya Mrajis wa wamiliki wa dhamana kuwa na nakala za daftari na hati za uaminifu.

**94.**-(1) Kila daftari la wamiliki wa dhamana za kampuni, isipokuwa litakapokuwa limefungwa (lakini kwa mujibu wa vizuizi ambavyo kampuni inaweza kuweka katika Mkutano Mkuu, ili si chini ya aa mbili katika kila siku zitaruhusiwa kwa ajili ya ukaguzi), litakuwa wazi kwa ukaguzi wa mmiliki yeyote wa dhamana au mmiliki wa hisa katika kampuni bila ya ada, na kwa mtu mwengine yeyote kwa malipo ya ada kama yatakavyowekwa na kampuni.

(2) Mtu yeyote aliyesajiliwa kama mmiliki wa dhamana au mmiliki wa hisa kama ilvyoelezwa kabla au mtu mwingine yeyote anaweza kuhitaji nakala ya daftari la wamiliki wa dhamana za kampuni au sehemu yake yoyote kwa malipo ya senti khamsini kwa kila maneno mia yanayohitajika kunakiliwa.

(3) Nakala yoyote ya hati ya uaminifu kwa ajili ya kupata toleo lolote la dhamana itapelekwa kwa kila mmiliki wa dhamana kwa ombi lake kwa malipo, kuhusiana na hati ya uaminifu iliyochapishwa, ya shilingi moja au chini ya kima hicho kitakavyowekwa na kampuni, au, ambapo hati ya uaminifu haikuchapishwa, kwa malipo ya senti khamsini kwa kila maneno mia yanayotaka kunakiliwa.

(4) Kama ukaguzi umekataliwa kufanywa, au nakala inakataliwa kutolewa au kupelekwa, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye ameshiriki katika ukiukaji atatozwa faini.

(5) Pale ambapo kampuni imekiuka kama ilivyoelezwa kabla, mahakama inaweza kutoa amri kumlazimisha ukaguzi wa haraka wa daftari au kuagiza kwamba nakala zinazohitajiwa kwa mtu anayezihitaji.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, daftari litachukuliwa kuwa limefungwa kihalali ikiwa limefungwa kwa mujibu wa masharti yaliyomo katika kanuni au katika dhamana au, kwa dhamana za bidhaa, katika vyeti vya hisa, au kwa hati za uaminifu au hati nyengine za kupata dhamana au dhamana za bidhaa, wakati wa kipindi hicho au vipindi hivyo, usiozidi siku nzima thalathini katika mwaka wowote, kama itakavyoainishwa humo.

Dhima za wadhamini kwa wamiliki wa dhamana.

**95.**-(1) Bila ya kuathiri masharti yafuatayo ya kifungu hiki, sharti lolote lililomo katika hati ya uaminifu kwa ajili ya kupata toleo la dhamana, au katika mkataba wowote na wamiliki wa dhamana lililowekwa na hati ya uaminifu, litakuwa batili kwa kadri ambavyo lingekuwa na athari ya kumsamehe mdhamini wake kutoka au kumfidia dhidi ya dhima kwa uvunjaji wa uaminifu ambapo atashindwa kuonesha kiwango cha uangalifu na bidii inayohitajika kutoka kwake kama mdhamini, kwa kuzingatia masharti ya hati ya uaminifu inayompa madaraka yoyote, mamlaka au uamuzi.

(2) Kifungu kidogo cha (1) hakitabatilisha:-

(a) utoaji wowote ambao umetolewa kihalali katika kuhusiana na kitu chochote kilichofanywa au lililoacha kufanywa na mdhamini kabla ya toleo kutolewa; au

(b) sharti lolote linalowezesha utoaji huo kufanyika:-

(i) kwa makubaliano ya wengi ambao si chini ya robo tatu ya thamani za wamiliki wa dhamana waliohudhuria na kupiga kura wao wenyewe au, pale ambapo wawakilishi wanaruhusiwa na wakala, katika mkutano ulioitishwa kwa madhumuni hayo; na

(ii) ama kuhusiana na matendo au uachaji maalumu au mdhamini kufa au kukoma kufanya kazi.

(3) Kifungu kidogo cha (1) hakitafanya kazi:-

(a) kubatilisha sharti lolote linalotumika katika siku iliyoteuliwa madamu mtu yeyote ambaye wakati huo alikuwa na haki ya kunufaika na sharti hilo au baadaye amepewa fursa hiyo chini ya kifungu kidogo cha (4) bado anabakia kuwa mdhamini wa hati inayohusika; au

(b) kumuondolea mtu yoyote msamaha au haki ya kufidiwa kuhusiana na jambo lolote lililofanywa au lililoachwa kufanywa na yeye lote wakati sharti lolote kama hilo lilikuwa linatumika.

(4) Wakati mdhamini yeyote wa hati ya dhamana bado ana haki ya kufaidika na sharti lililowekwa na kifungu kidogo cha (3), faida ya vifungu hivyo inaweza kutolewa ama:-

(a) kwa wadhamini wote wa hati, wa sasa na wa baadaye; au

(b) kwa wadhamini wowote waliotjwa au wadhamini waliopendekezwa;

kwa azimio lililopitishwa na wengi ambayo si chini ya robo tatu ya thamani ya wamiliki wa dhamana waliohudhuria wao wenyewe au, pale ambapo wawakilishi wanaruhusiwa, ya wakala katika mkutano ulioitishwa kwa madhumuni hayo uliothibitishwa na mahakama.

**96.** Sharti lililomo katika dhamana zozote au katika hati yoyote kwa ajili ya kupata dhamana zozote halitakuwa batili kwa sababu tu kwamba dhamana hizo hazikomboleki au zinakomboleka panapotokea dharura tu, japo kwa mbali, au kwa kumalizika muda haidhuru wa urefu gani, bila ya kujali kanuni yoyote ya uwiano iliyo kinyume.

Dhamana za kudumu Dhamana zinazoendelea.

Uwezo wa kutoa tena dhamana zilizobadilishwa katika hali maalumu.

**97.**-(1) Pale ambapo kampuni imezikomboa dhamana zilizotolewa, kabla, basi:-

(a) isipokuwa kama kuna sharti lolote lililo kinyume, ama moja kwa moja au kwa kuchukulia, katika kanuni au katika mkataba wowote kampuni iliyoingiana nao; au

(b) isipokuwa kama kampuni, kwa kupitisha azimio kuhusiana na hilo au kwa tendo jengine, imeonesha nia yake kuwa dhamana zitafutwa;

kampuni itakuwa na mamlaka ya kutoa upya dhamana, ama kwa kutoa upya dhamana hizo au kwa kutoa dhamana nyengine katika nafasi zao.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 96, juu ya kutoa upya dhamana zilizokombolewa mtu mwenye haki ya dhamana atakuwa na vipaumbele sawa kama kwamaba dhamana hizo hazijawahi kukombolewa.

(3) Pale ambapo kampuni imeweka dhamana zake zozote kupata advansi kila baada ya muda kwenye akaunti ya biashara au vyenginevyo, dhamana hazitahesabiwa kuwa zimekombolewa kwa sababu tu ya akaunti ya kampuni kukoma kuwa katika deni wakati dhamana hizo zilipokuwa bado zimewekwa.

(4) utoaji upya wa dhamana au utoaji wa dhamana nyengine badala yake chini ya uwezo kwa mujibu wa kifungu hiki uliyopewa kampuni, utachukuliwa kama utoaji wa dhamana mpya kwa madhumuni ya ushuru wa stempu, lakini hautochukuliwa kuwa hivyo kwa madhumuni ya sharti lolote linaloweka ukomo wa kiasi au idadi ya dhamana zinazopaswa kutolewa.

Isipokuwa kwamba mtu yeyote anayekopesha pesa kwa ajili ya usalama wa ddhamana iliyotolewa chini ya kifungu hiki ambayo imepigwa muhuri anaweza kuitoa dhamana katika ushahidi katika kesi yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa dhamana yake bila kulipa ushuru wa stempu au adhabu yoyote inayohusiana nayo, isipokuwa kama alikuwa na taarifa au, lakini kwa uzembe wake, angeweza kugundua, kwamba dhamana haikupigwa muhuri, lakini katika hali kama hiyo kampuni itapasa kulipa ushuru wa stempu sahihi na adhabu.

Utekelezaji maalumu wa mikataba ya kuchangia dhamana.

**98.** Mkataba na kampuni wa kuchukua na kulipa kwa ajili ya dhamana zozote za kampuni unaweza kutekelezwa kwa amri kwa utekelezaji maalumu.

Ulipaji wa baadhi ya deni kutoka-na na raslimali kwa malipo yanayoelea kwa upendeleo dhidi ya madai juu ya malipo.

**99.**-(1) Yafuatayo yanatumika kwa kampuni ambapo dhamana za kampuni zinapatikana kwa malipo ambayo, kama yalivyowekwa, yalikuwa malipo yanayoelea.

(2) Pale ambapo ama mpewaji ameteuliwa kwa niaba ya wamiliki wa dhamana zozote za kampuni zilizopatikana kwa malipo yanayoelea, au umiliki unachukuliwa na au kwa niaba ya wamiliki wa dhamana yoyote ya mali yoyote yenye au chini ya malipo, na kampuni wakati huo haimo katika mwenendo wa kufungwa, deni za kampuni zilizopewa kipaumbele zitalipwa kutokana na mali zinazoingia kwenye mikono ya mtu anayechukua umiliki dhidi ya kipaumbele cha madai yoyote ya mtaji au riba zinazohusiana na dhamana.

(3) "Madeni ya kipaumbele" ina maana sawa kama ilivyo katika Sheria ya Kufilisika.

(4) Malipo yaliyofanywa chini ya kifungu hiki yatarejeshwa, kadiri itakavyowezekana, kutokana na mali ya kampuni inayopatikana kwa ajili ya malipo ya wadai wa kawaida.

## SEHEMU YA V
## UANDIKISHAJI WA MALIPO

Uuandiki-shaji wa Malipo kwa Mrajis Usajili wa malipo.

**100.**-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Kifungu hiki, kila mashtaka yanayofanywa na kampuni iliyosajiliwa katika Zanzibar na yakawa ni mashtaka ambayo kifungu hiki kinatumika, madhali dhamana yoyote juu ya mali ya kampuni imewekwa au ahadi imetolewa, yatakuwa batili dhidi ya mfilisi na mdai yeyote wa kampuni, isipokuwa taarifa zilizoainishwa za mashtaka pamoja na waraka, kama upo, ambao kwa mkataba huo mashtaka yamefanywa au kuthibitishwa, zinawasilishwa au zinapokewa na Mrajis kwa ajili ya usajili kwa namna inayotakiwa na Sheria hii ndani ya siku arubaini na mbili baada ya tarehe ya kufanywa kwake, lakini bila ya kuathiri mkataba wowote au wajibu wa kulipa tena fedha zilizopatikana na wakati mashtaka yanapokuwa batili chini ya kifungu hiki fedha zilizopatikana zitalipwa mara moja.

(2) Kifungu hiki kitatumika kwa mashtaka yafuatayo:-

(a) mashtaka kuhusu upatikanaji wa toleo lolote la dhamana;

(b) mashtaka kuhusu mtaji wa hisa wa kampuni ambao haujafutwa;

(c) mashtaka yaliyofanywa au yaliyothibitishwa na waraka ambao kama ungetekelezwa na mtu binafsi, ungepaswa kusajiliwa kama muswada wa kuuza;

(d) mashtaka kuhusu mali isiyohamishika, popote ilipo, au riba yoyote iliyo ndani yake, lakini si pamoja na malipo kwa ajili ya kodi yoyote au malipo mengine ya kipindi yanayotokana na mali isiyohamishika;

(e) mashtaka kuhusu madeni ya kampuni yaliyorikodiwa;

(f) mashtaka kuhusu ahadi au mali ya kampuni;

(g) mashtaka kuhusu maombi yaliyotolewa lakini hayakulipwa;

(h) mashtaka kuhusu meli au hisa yoyote katika meli;

(i) mashtaka kuhusu nia njema, kuhusu hataza au leseni chini ya hataza, kuhusu alama ya biashara au kuhusu hakimiliki au leseni chini ya hakimiliki.

(3) Kwa mashtaka yaliyofanywa nje ya Zanzibar kuhusu mali iliyo nje ya Zanzibar, uwasilishaji wa nakala ya hati ambayo mashtaka yamefanywa iliyohakikiwa kwa namna iliyowekwa kwa Mrajis na kupokewa nakala hiyo na Mrajis itakuwa na athari sawa kwa madhumuni ya kifungu hiki kama uwasilishaji na upokeaji wa hati yenyewe, na siku arubaini na mbili baada ya tarehe ambayo hati au nakala ingeweza, kwa posta, na ikiwa ilipelekwa kwa umakini, kupokewa Zanzibar zitabadilishwa na siku arbaini na mbili baada ya tarehe yaliyofanywa mashtaka kama wakati ambao ndani yake maelezo na hati zinapaswa kuwasilishwa kwa Mrajis.

(4) Pale ambapo mashtaka yamefunguliwa katika Zanzibar lakini yanajumuisha mali iliyo nje ya Zanzibar, waraka uliofungua au kudai kufungua mashtaka unaweza kupelekwa kwa ajili ya usajili chini ya kifungu hiki bila ya kujali kwamba taratibu zaidi zinaweza kulazimika kuyafanya mashtaka kuwa halali au kuweza kutekelezeka kulingana na sheria ya nchi ambayo mali hiyo iko.

(5) Endapo mashtka yanajumuisha mali zilizo nje ya Zanzibar na usajili katika nchi ambapo mali ipo ni wa lazima ili kuyafanya mashtaka yawe halali au yaweze kutekelezeka kwa mujibu wa sheria ya nchi hiyo, uuwasilishaji kwa na upokelewaji na Mrajis wa nakala iliyohakikiwa kwa namna iliyowekwa wa hati ambayo mashtaka yalifunguliwa au yalithibitishwa, pamoja na cheti katika umbo lililowekwa kinachoeleza kuwa mashtaka yaliwasilishwa kwa ajili ya usajili katika nchi ambapo mali iko katika tarehe ambayo aliwasilisha, kwa madhumuni ya kifungu hiki, utakuwa na athari sawa na uwasilishaji na upokeaji wa hati yenyewe.

(6) Pale ambapo hati inayoweza kubadilishwa kwa fedha imetolewa ili kupata malipo ya madeni yoyote ya kampuni yaliyorikodiwa uwekaji kama amana wa hati hiyo kwa ajili ya kupata rubuni, kwa madhumuni ya kifungu hiki, haitachukuliwa kama malipo ya madeni yaliyorikodiwa.

(7) Umiliki wa dhamana unamstahikia mmiliki malipo katika mali isiyohamishika hautahesabiwa, kwa madhumuni ya kifungu hiki, kuwa riba katika mali isiyohamishika.

(8) Pale ambapo mfululizo wa dhamana zenye, au zinazotoa kwa upendeleo kwa hati yoyote, mashtaka yoyote kwa manufaa ambayo wamiliki wa dhamana waliomo katika mfululizo huo wana haki sawasawa

yamefunguliwa na kampuni, kwa madhumuni ya kifungu hiki, itatosheleza kama zitawasilishwa au kupokewa na Mrajis, ndani ya siku arubaini na mbili baada ya utekelezaji wa hati yenye mashtaka au, kama hakuna hati kama hiyo, baada ya utekelezaji wa dhamana zozote za mfululizo huo, taarifa zifuatazo:-

(a) kiasi cha jumla kilichopatikana na mfululizo mzima; na

(b) tarehe za maazimio yaliyoidhinisha utoaji wa mfululizo huo na tarehe ya hati inayohusika, kama ipo, ambayo upatikanaji ulifanywa au kufafanuliwa; na

(c) maelezo ya jumla ya mali inayoshtakiwa; na

(d) jina la wadhamini, kama wapo, kwa ajili ya wamiliki wa dhamana; pamoja na hati yenye mashtaka, au, kama hakuna hati kama hiyo, dhamana moja ya mfululizo huo.

Isipokuwa kwamba, iwapo utoaji zaidi ya mmoja umefanywa wa dhamana katika mfululizo huo, kutawasilishwa kwa Mrajis kwa ajili ya kuingiza katika daftari taarifa kuhusu tarehe na kiasi cha kila toleo, lakini kuacha kufanya hivyo hakutaathiri uhalali wa dhamana zilizotolewa.

(9) Endapo kamisheni, posho au punguzo lolote limelipwa au kufanywa ama moja kwa moja au si moja kwa moja na kampuni kwa mtu yeyote kwa kuzingatia mchango wake au kukubali kwake kuchangia, iwe moja kwa moja au kwa masharti, kwa dhamana zozote za kampuni, au kununua au kukubali kununua michango, iwe moja kwa moja au kwa masharti, kwa dhamana zozote kama hizo, taarifa zinazohitajika kuwasilishwa kwa ajili ya usajili chini ya kifungu hiki zitakuwa ni pamoja na maelezo kuhusu kiasi au kiwango cha asilimia ya punguzo, au posho litakalolipwa au kufanywa, lakini kuacha kufanya hivyo hakutaathiri uhalali wa dhamana zilizotolewa.

Isipokuwa kwamba amana ya dhamana yoyote kama dhamana kwa ajili ya kulipa deni yoyote ya kampuni, kwa madhumuni ya kifungu hiki, haitahesabika kama utoaji wa dhamana kwa punguzo.

(10) Katika Sehemu hii neno "malipo" linajumuisha mikopo.

**101.**-(1) Utakuwa ni wajibu wa kampuni kuwasilisha kwa Mrajis kwa ajili ya usajili maelezo ya kila malipo yaliyobuniwa na kampuni na utoaji wa dhamana za mfululizo zinazohitaji usajili chini ya kifungu cha 100, lakini usajili wa malipo yoyote kama hayo unaweza kutekelezwa kwa maombi ya mtu yeyote ambye ana maslahi ndani yake. Wajibu wa kampuni kusajili malipo yaliyobuniwa na kampuni.

(2) Pale ambapo usajili umetekelezwa kwa maombi ya mtu mwengine asiyekuwa kampuni, mtu huyo atakuwa na haki ya kupata kutoka kampuni kiasi cha ada yoyote kilicholipwa na yeye kwa namna inayofaa kwa Mrajis kwa ajili ya usajili.

(3) Kama kampuni yoyote itakiuka kuwasilisha kwa Mrajis kwa ajili ya usajili maelezo yoyote kuhusu malipo yaliyobuniwa na kampuni au

ya utoaji wa dhamana za mfululizo zinazohitaji usajili kama ilivyoelezwa kabla, basi, isipokuwa kama usajili umefanywa kwa maombi ya mtu mwengine, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye amehusika na ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

Wajibu wa kampuni kusajili malipo yaliyopo kwenye mali iliyo-patikana.

**102.**-(1) Ambapo kampuni inapata mali yoyote ambayo inapaswa kutolewa malipo ya namna yoyote, ambayo kama yalibuniwa na kampuni baada ya upatikanaji wa mali, yangetakiwa kuandikishwa chini ya Sehemu hii, kampuni itatayarisha maelezo ya malipo yanayohitajika, pamoja na nakala (iliyothibitishwa katika namna iliyowekwa kuwa ni nakala sahihi) ya waraka, kama upo, ambao malipo yalibuniwa au yalithibitishwa, kupelekwa kwa Mrajis kwa ajili ya usajili kwa namna inayotakiwa na Sheria hii ndani ya siku ishirini na moja baada ya tarehe ambayo upatikanaji ulikamilika.

Isipokuwa kwamba, kama mali ipo na malipo yamebuniwa nje ya Zanzibar, siku ishirini na moja baada ya tarehe ambayo nakala ya hati baada ya kutiwa posta, na kama ilipelekwa kwa makini, ingeweza kupokewa katika Zanzibar zitakuwa badala ya siku ishirini na moja baada ya kukamilika ununuzi kama wakati ambao ndani yake maelezo na nakala ya hati zinapaswa kupelekwa kwa Mrajis.

(2) Kama ukiukaji utafanywa katika kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji itampasa kutozwa faini kwa ukiukaji.

Daftari la malipo kuwekwa na Mrajis.

**103.**-(1) Mrajis ataweka, kuhusiana na kila kampuni, daftari lililo katika umbo lililowekwa la malipo yote yanayohitaji usajili chini ya Sehemu hii, na baada ya kulipwa ada iliyowekwa, ataingiza katika daftari kuhusiana na malipo hayo taarifa zifuatazo:-

(a) Kwa malipo ambayo faida yake wamiliki wa dhamana za mfululizo wanastahiki, maelezo kama yale yaliyoainishwa katika kifungu cha 100(8);

(b) kwa malipo mengine yoyote:-

(i) kama malipo ni malipo yaliyobuniwa na kampuni, tarehe ya kubuniwa kwake, na kama malipo yalikuwa malipo yaliyo kwenye mali iliyopatikana na kampuni, tarehe ya upatikanaji wa mali; na

(ii) kiasi kilichopatikana kwa malipo; na

(iii) maelezo mafupi ya mali iliyolipishwa; na

(iv) watu wenye haki ya malipo.

(2) Mrajis atatoa cheti chenye saini yake cha usajili wa malipo yoyote yaliyosajiliwa kwa mujibu wa Sehemu hii, chenye kueleza kiasi kilichopatikana, na cheti kitakuwa ni ushahidi wa mwisho kwamba masharti ya Sehemu hii kuhusiana na usajili yametimizwa.

(3) Daftari lililowekwa kwa mujibu wa kifungu hiki litakuwa wazi kwa ukaguzi wa mtu yeyote kwa malipo ya ada iliyowekwa, kwa kila ukaguzi katika kiwango kitakachowekwa na Waziri katika Kanuni.

Uthibitisho wa cheti cha usajili wa dhamana.

**104.**-(1) Kampuni itawezesha nakala ya kila cheti cha usajili kilichotolewa chini ya kifungu cha 103 kuthibitishwa kwenye kila dhamana au cheti cha dhamana ya hisa ambayo imetolewa na kampuni na malipo ambayo yanapatikana kwa malipo yaliyosajiliwa.

Isipokuwa kwamba hakuna kitu katika kifungu hiki kitakachofahamika kama inahitajika kampuni kusababisha hati ya usajili ya malipo yoyote yaliyotolewa kuthibitishwa kwenye dhamana yoyote au cheti cha dhamana ya hisa zilizotolewa na kampuni kabla ya malipo kubuniwa.

(2) Ikiwa mtu yeyote kwa kujua na kwa makusudi anaidhinisha au anaruhusu utoaji wa dhamana yoyote au hati ya dhamana ya hisa ambayo chini ya masharti ya kifungu hiki inahitajika kuthibitishwa juu yake na nakala ya cheti cha usajili bila ya nakala hiyo kuthibitishwa juu yake, bila ya kuathiri dhima nyengine yoyote, atatozwa faini.

Taarifa za kutoshelezeka na utoaji wa mali kutoka kwenye malipo.

**105.** Mrajis, kutokana na ushahidi uliotolewa wenye kumridhisha kuhusiana na malipo yoyote yaliyosajiliwa: -

(a) kwamba deni ambalo malipo yalitolewa limelipwa au limetoshelezwa lote au baadhi yake; au

(b) kwamba sehemu ya mali au biashara iliyotozwa malipo imetolewa kwenye malipo au imesita kuwa sehemu ya mali ya kampuni au biashara;

anaweza kuingiza kwenye daftari maelezo ya kuridhika kamili au sehemu, au ukweli kwamba sehemu ya mali au biashara imetolewa kwenye malipo au imesita kuwa sehemu ya mali ya kampuni au biashara, kama itakavyokuwa, na pale ambapo anaingiza maelezo ya kuridhika kamili, kama inahitajika, ataipatia kampuni nakala yake.

Usahihishaji wa daftari la malipo.

**106.** Mahakama, juu ya kutosheka kuwa kuacha kusajili malipo ndani ya muda unaotakiwa na Sheria hii au kwamba kuacha au kueleza vibaya kuhusu malipo yoyote au katika maelezo ya kuridhika kulikuwa kwa bahati mbaya, au kutokana na kupitikiwa au kwa sababu nyengine ya kutosha, si ya namna ambayo inaweza kuathiri nafasi ya wadai au wanahisa wa kampuni, au kwamba kwa misingi myengine ni haki na usawa kutoa msaada wa ruzuku, inaweza, kwa maombi ya kampuni au mtu yeyote anayependa, na kwa masharti na hali ambayo yanaonekana na mahakama kuwa ni ya haki na yanahitajika, kuagiza kwamba wakati kwa ajili ya usajili utaongezwa, au, kama itakavyokuwa, kwamba kuacha au kueleza vibaya kutasahihishwa na inaweza kuagiza hivyo kwa gharama za maombi kama inavyoona inafaa.

Nakala za hati zinazobuni malipo kuwekwa na kampuni.

**107.-**(1) Kama mtu yeyote anapata agizo la uteuzi wa mpokeaji au meneja wa mali ya kampuni, au anamteua mpokeaji au meneja chini ya mamlaka yoyote yaliyomo katika hati yoyote, ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya agizo au kuteuliwa chini ya mamlaka yaliyoelezwa, kutoa taarifa kuhusu jambo hilo kwa Mrajis, na Mrajis, baada ya kulipwa ada iliyowekwa, ataingiza taarifa hiyo katika daftari la malipo.

(2) Iwapo mtu yeyote mwenye kuteuliwa mpokeaji au meneja wa mali ya kampuni chini ya uwezo uliomo katika hati yoyote anasita kuwa mpokeaji au meneja, kwa kusita huko, atatoa taarifa kwa Mrajis kuhusu jambo hilo, na Mrajis ataiingiza taarifa katika daftari la malipo.

(3) Iwapo mtu yeyote anakiuka katika kutekeleza matakwa ya kifungu hiki, atatozwa faini kwa kila siku ambayo ukiukaji unaendelea.

Masharti Kuhusu Daftari la Kampuni la Malipo na Kuhusu Nakala za Hati Zinazobuni Malipo Daftari la malipo la kampuni.

**108.** Kila kampuni itawezesha nakala moja ya kila hati inayobuni malipo yoyote yanayohitaji usajili chini ya Sehemu hii kuwekwa kwenye ofisi iliyosajiliwa ya kampuni:

Isipokuwa kwamba, kwa mfululizo wa dhamana zinazolingana, nakala ya dhamana moja katika mfululizo itatosheleza.

Haki ya kukagua nakala za hati zilizobuni mikopo na malipo na daftari la malipo la kampuni.

**109.-**(1) Kila kampuni yenye ukomo itaweka katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni daftari la malipo na kuingiza humo malipo yote hasa yanayoathiri mali ya kampuni na malipo yote yaliyoahidiwa katika biashara au mali yoyote ya kampuni, na kutoa kwa kila mojawapo maelezo mafupi ya mali inayolipiwa, kiasi cha malipo, na, isipokuwa katika dhamana za mtu binafsi, majina ya watu wenye haki.

(2) Ikiwa ofisa yeyote wa kampuni kwa kujua na kwa makusudi anaidhinisha au anaruhusu kuachwa kuingiza taarifa yoyote inayotakiwa kuingizwa kulingana na kifungu hiki, atatozwa faini.

Matumizi ya Sehemu ya IV kwa mali kulingana na malipo yanayopatikana, kwa kampuni iliyosajiliwa nje ya Zanzibar.

**110.-**(1) Nakala za hati zinazobuni malipo yoyote yanayohitaji usajili chini ya Sehemu hii kwa Mrajis, na daftari la malipo lililowekwa kwa mujibu wa kifungu cha 109, zitakuwa wazi wakati wa saa za kazi (lakini chini ya masharti yanayofaa kama kampuni katika mkutano mkuu yanavyoweza kuyaweka, ili si chini ya saa mbili katika kila siku zitaruhusiwa kwa ajili ya ukaguzi) kwa ukaguzi wa mdai yeyote au mwanachama wa kampuni bila ya ada, na daftari la malipo litakuwa pia wazi kwa ukaguzi wa mtu mwengine yeyote kwa malipo ya ada kwa ajili ya kila ukaguzi, kama kampuni itakavyoagiza.

(2) Kama ukaguzi wa nakala zilizotajwa au daftari umekataliwa, kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini na faini ya ziada kwa ajili ya kila siku ambayo ukataaji unaendelea na mahakama inaweza kutoa amri kulazimisha ukaguzi wa haraka wa nakala au daftari.

**111.** Masharti ya Sehemu hii yatahusu pia malipo juu ya mali zilizopo Zanzibar ambazo zinabuniwa, na malipo juu ya mali zilizopo Zanzibar ambazo zinapatikana, kwa kampuni (kama ni kampuni kwa maana ya Sheria hii au la) kusajiliwa nje ya Zanzibar ambayo ina mahali pa biashara panapojuilikana katika Zanzibar.

Matumizi ya Sehemu ya IV kwa Kampuni Zilizosajiliwa nje ya Zanzibar

## SEHEMU YA VI
## USIMAMIZI NA UTAWALA

Ofisi iliyosajiliwa ya kampuni.

**112.-**(1) Kampuni, kutoka siku ambayo inaanza na kuendesha biashara au kutoka siku ya kumi na nne kutoka tarehe ya kusajiliwa kwake, yoyote itakayokuwa ni ya mapema, itakuwa na ofisi iliyosajiliwa katika Zanzibar ambapo mawasiliano na taarifa zote zitapelekwa.

Ofisi Iliyosajiliwa na Jina Kampuni kuchaisha jina.

(2) Tangazo la mahali ilipo ofisi iliyosajiliwa, na mabadiliko yoyote yaliyomo humo, yatawasilishwa ndani ya siku kumi na nne baada ya tarehe ya kusajiliwa kampuni au ya mabadiliko kufanywa, kama itakavyokuwa, kwa Mrajis, ambaye atayarikodi.

Kuingizwa katika marejesho ya kampuni ya kila mwaka maelezo kuhusu anuani ya ofisi yake iliyosajiliwa hakutachukuliwa kukidhi wajibu uliowekwa na kifungu kidogo hiki.

(3) Kama ukiukaji umefanywa katika kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini.

**113.-**(1) Kila kampuni:-

Taarifa ya kiasi cha mtaji ulioandikishwa na kiasi kilicholipwa.

(a) itatia rangi au kubandika, na kuendelea kupaka rangi au kubandika, jina lake nje ya kila ofisi au mahali ambapo biashara yake inafanyika, katika pahali wazi, katika herufi za Kirumi zinazosomeka kwa urahisi;

(b) itakuwa na jina lililochimbuliwa kwa herufi za Kirumi zinazosomeka kwenye muhuri wake;

(c) itakuwa na jina lake lililotajwa kwa hati zinazosomeka za Kirumi katika barua zote za biashara za kampuni na katika matangazo yote na machapisho mengine rasmi ya kampuni, na katika hawala zote, hati za ahadi, hundi na maagizo kwa ajili ya fedha au bidhaa zinazotiwa saini na au kwa niaba ya kampuni, na katika bili zote za vifurushi, ankara, risiti na barua za mikopo za kampuni.

(2) Kama kampuni haikutia rangi au kubandika jina lake kwa namna ilivyoagizwa na Sheria hii, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini, na kama kampuni haikuweka au kubandika jina lake katika namna ilivyoagizwa, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

(3) Kama kampuni itashindwa kutekeleza paragrafu (b) au paragrafu (c) ya kifungu kidogo cha (1), kampuni itatozwa faini.

(4) Ikiwa ofisa wa kampuni au mtu yeyote kwa niaba yake:-

(a) anatumia au anaidhinisha matumizi yoyote ya muhuri unaodaiwa kuwa muhuri wa kampuni ambao juu yake jina lake halikuchimbuliwa kama ilivyoelezwa kabla; au

(b) anatoa au anaidhinisha barua yoyote ya biashara ya kampuni au taarifa yoyote au nyengine rasmi ya uchapishaji wa kampuni, au taarifa yoyote au chapisho jengine rasmi la kampuni, au anatia saini kwa niaba ya kampuni bili yoyote ya kubadilishana, hati ya ahadi, uthibitisho, hundi au agizo la fedha au bidhaa ambalo ndani yake jina lake halikutajwa katika namna iliyoelezwa kabla; au

(c) anatoa au anaidhinisha bili yoyote ya vifurushi, risiti ankara, au barua ya mikopo ya kampuni ambayo jina lake halikutajwa katika namna iliyoelezwa kabla;

atatozwa faini, na zaidi atakuwa yeye mwenyewe binafsi atawajibika kwa mmiliki wa hati ya kubadilishana, hati ya ahadi, hundi au agizo la fedha au bidhaa kwa kiasi kinachohusika isipokuwa kwamba kimelipwa kihalali na kampuni hiyo.

Taarifa ya Kiasi cha Mtaji Uliolipwa Vikwazo kuhusu uanzishaji wa biashara.

**114.**-(1) Pale ambapo taarifa yoyote, tangazo, au chapisho jengine rasmi la kampuni lina taarifa ya kiasi cha mitaji ulioidhinishwa wa kampuni, taarifa hiyo, tangazo, au chapisho jenghine rasmi litakuwa pia na taarifa katika nafasi sawa inayoonekana na katika maandishi sawa yanayosomeka ya kiasi cha mtaji ambao umeandikishwa na kiasi kilicholipwa.

(2) Kila kampuni ambayo inakiuka katika kutekeleza matakwai ya kifungu hiki na kila ofisa anayehusika na ukiukaji atatozwa faini.

Vikwazo Kuhusu Uanzishaji wa Biashara Daftari la wanachama.

**115.**-(1) Pale ambapo kampuni ambayo ina mtaji wa hisa imetoa muhtasari wa ununuzi wa hisa kuukaribisha umma kujiunga kwenye hisa zake, kampuni haitaanzisha biashara yoyote au kutumia uwezo wowote wa kukopa isipokuwa kwamba:-

(a) hisa zilizomilikiwa kwa sharti la kulipwa kiasi chake chote kwa fedha taslimu ziwe zimewekwa kwa kiasi kisichokuwa chini kwa ujumla kuliko michango ya kiwango cha chini; na

(b) kila mkurugenzi wa kampuni awe amelipa kwa kampuni, juu ya kila hisa iliyochukuliwa au iliyotiliwa saini mkataba kuchukuliwa na yeye na ambao yeye anapaswa kulipa fedha taslimu, uwiano sawa na uwiano unaolipwa wakati wa kuomba na mgao wa kwenye hisa zinazotolewa kwa ajili ya michango ya umma; na

(c) hakuna pesa ambayo ni au inayoweza kustahiki kulipwa kwa waombaji kwa hisa zozote au dhamana ambazo zimetolewa kwa ajili ya michango ya umma kwa sababu yoyote ya kushindwa kuomba au kupata kibali kwa ajili ya hisa au dhamana za kushughulikiwa katika soko la hisa; na

(d) kumewasilishwa kwa Mrajis kwa ajili ya usajili tamko la kisheria na katibu au na mmojawapo wa wakurugenzi, katika namna iliyowekwa, kwamba masharti yaliyoelezwa kabla yametekelezwa.

(2) Pale ambapo kampuni yenye mtaji wa hisa haijatoa muhtasari wa ununuzi wa hisa kuukaribisha umma kujiunga kwenye hisa zake, kampuni haitaanzisha biashara yoyote au kutumia madaraka yoyote ya kukopa isipokuwa kwamba:-

(a) kumewasilishwa kwa Mrajis kwa ajili ya usajili taarifa kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa; na

(b) kila mkurugenzi wa kampuni amelipa kwa kampuni, juu ya kila mojawapo ya hisa zilizochukuliwa au zilizotiliwa saini mkataba kuchukuliwa na yeye na ambazo anapaswa kuzilipia kwa fedha taslimu, uwiano sawa na uwiano unaolipwa wakati wa kuomba na mgao wa hisa zinazolipiwa kwa fedha taslimu; na;

(c) kumewasilishwa kwa Mrajis kwa ajili ya usajili tamko la kisheria na katibu au mmojawapo wa wakurugenzi, katika namna iliyowekwa, kwamba paragrafu (b) ya kifungu kidogo hiki imetekelezwa.

(3) Mrajis, baada ya kuwasilishwa kwake tamko la kisheria lililoelezwa na, kwa kampuni ambayo inahitajika kwa kifungu hiki kuwasilisha taarifa badala ya muhtasari wa ununuzi wa hisa, taarifa hiyo, atathibitisha kwamba kampuni inastahiki kuanza biashara, na kwamba ithibati hiyo itakuwa ushahidi wa mwisho kuwa kampuni inastahiki kufanya hivyo.

(4) Mkataba wowote uliotiwa saini na kampuni kabla ya tarehe ambayo inastahiki kuanza biashara utakuwa wa muda tu, na hautakuwa na nguvu ya kisheria juu ya kampuni hadi tarehe hiyo, na katika tarehe hiyo utakuwa na nguvu ya kisheria.

(5) Hakuna kitu katika kifungu hiki kitazuia kutoa sambamba mchango au mgao wa hisa yoyote na dhamana au upokeaji wa fedha yoyote inayolipwa kwenye maombi ya dhamana.

(6) Kama kampuni yoyote inaanza biashara au inatumia madaraka ya kukopa kinyume na kifungu hiki, kila mtu ambaye anahusika katika kukiuka, bila ya kuathiri dhima nyengine yoyote, atatozwa faini kwa kila siku ambayo ukiukaji unaendelea.

(7) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachotumika kwa kampuni binafsi.

Daftari la Wanachama Faharisi ya wanachama.

**116.**-(1) Kila kampuni itaweka daftari la wanachama wake na kuingiza humo taarifa zifuatazo:-

(a) Majina na anwani za wanachama, na. kwa kampuni yenye mtaji wa hisa taarifa za hisa zinazomilikiwa na kila mjumbe, ikitafautisha kila hisa kwa nambari yake madamu hisa ina namba, na kiasi kilicholipwa au kukubaliwa kuchukuliwa kama kimelipwa kwenye hisa za kila mwanachama;

(b) tarehe ambayo kila mtu aliingizwa katika daftari kama mwanachama;

(c) tarehe ambayo mtu yeyote alikoma kuwa mwanachama:

Isipokuwa kwamba, ambapo kampuni imezibadilisha hisa zake zozote katika bidhaa na kutoa taarifa ubadilishaji kwa Mrajis, daftari litaonesha kiasi cha bidhaa zinazomilikiwa na kila mwanachama badala ya kiasi cha hisa na maelezo kuhusu hisa zilizoainishwa katika paragrafu (a) ya kifungu kidogo hiki.

(2) Daftari la wanachama litawekwa katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni.

Isipokuwa kwamba:-

(a) ikiwa kazi ya kulifanya inafanyika katika ofisi nyengine ya kampuni, linaweza kuwekwa katika ofisi hiyo nyengine; na

(b) kama kampuni inapanga na mtu mwengine utengenezaji wa daftari ufanywe kwa niaba ya kampuni na huyo mtu mwengine, linaweza kuwekwa katika ofisi ya huyo mtu mwengine ambapo kazi inafanywa isipokuwa kwamba halitawekwa mahali nje ya Zanzibar.

(3) Kila kampuni itatuma taarifa kwa Mrajis ya mahali ambapo daftari la wanachama wake linawekwa na ya mabadiliko yoyote ya mahali hapo:

Isipokuwa kwamba kampuni haitalazimika kupeleka taarifa chini ya kifungu kidogo hiki ambapo daftari wakati wote tokea lilipotayarishwa limehifadhiwa katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni.

(4) Endapo kampuni inakiuka katika kutekeleza kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki au inafanya ukiukaji kwa siku kumi na nne katika kutekeleza kifungu kidogo cha mwisho kilichoelezwa, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

**117.-**(1) Kila kampuni yenye wanachama zaidi ya khamsini itaweka, isipokuwa kama daftari la wanachama limo katika umbo la kuwa lenyewe ni faharisi, faharisi ya majina ya wanachama wa kampuni na itafanya, ndani ya siku kumi na nne baada ya tarehe ambayo mabadiliko yoyote yalifanywa katika daftari la wanachama, mabadiliko yoyote muhimu katika faharisi.

Masharti kuhusu kuingiza taarifa katika daftari kuhusiana na hati za hisa

(2) Faharisi kuhusiana na kila mwanachama itakuwa na dalili za kutosha kuwezesha taarifa za mwanachama katika daftari kupatikana kwa urahisi.

(3) Faharisi itakuwa wakati wote inaendelea kuwekwa mahali pale pale kama daftari la wanachama.

(4) Iwapo ukiukaji utafanywa katika kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

**118.-**(1) Kuhusu utoaji wa hati ya hisa kampuni itafuta kwenye daftari lake la wanachama jina la mwanachama aliyeingizwa humo kama kuwa mmiliki wa hisa zilizoainishwa katika hati kama kwamba alikuwa amekoma kuwa mwanachama, na itaingiza katika daftari taarifa zifuatazo, yaani: -

Ukaguzi wa daftari na faharisi.

(a) tendo la kutolewa hati;

(b) taarifa ya hisa zilizojumuishwa katika hati, ikitafautisha kila hisa kwa nambari yake madhali hisa ina nambari; na

(c) tarehe iliyotolewa hati.

(2) Mwenye hati ya hisa atastahiki, chini ya kanuni za kampuni, baada ya kuisalimisha ili ifutwe, jina lake kuingizwa kama mwanachama katika daftari la wanachama.

(3) Kampuni itawajibika kwa hasara yoyote atakayopata mtu yeyote kwa sababu ya kampuni kuingiza katika daftari jina la mwenye hati ya hisa kuhusiana na hisa zilizoanishwa humo bila ya hati kusalimishwa na kufutwa.

(4) Mpaka kibali kitakaposalimishwa, taarifa zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) zitachukuliwa kuwa taarifa zinazotakiwa na Sheria hii kuingizwa katika daftari la wanachama, na, baada ya kusalimishwa, tarehe ya kusalimishwa itaingizwa.

(5) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, mwenye hati ya hisa, ikiwa kanuni za kampuni zinaruhusu, atachukuliwa kuwa mwanachama wa kampuni kwa maana ya Sheria hii, ama kamili au kwa madhumuni yoyote yanayoelezwa katika kanuni.

**119.-**(1) Isipokuwa wakati ambapo daftari la wanachama limefungwa chini ya masharti ya Sheria hii, daftari, na faharisi ya majina ya wajumbe wa kampuni wakati wa saa za biashara (chini ya vizuizi vinavyokubalika kama kampuni katika mkutano mkuu inavyoweza kuweka, ili si chini ya saa mbili kila siku kuruhusiwa kwa ajili ya ukaguzi) yatakuwa wazi kwa ukaguzi wa mwanachama yeyote bila malipo na wa mtu mwengine yeyote kwa malipo ya kiasi ambacho kampuni imeweka, kwa kila ukaguzi.

Matokeo ya kushindwa kutekeleza matakwa kuhusiana na daftari kutokana na ukiukaji wa wakala.

(2) Mjumbe yeyote au mtu mwengine anaweza kutaka nakala ya daftari, au sehemu yake yoyote, kwa malipo ya kiasi ambacho kampuni imeweka, kwa kila maneno mia moja au sehemu yake yanyohitaji kunakiliwa.

Kampuni itawezesha nakala yoyote iliyotakiwa na mtu yeyote kupelekwa kwa mtu huyo ndani ya kipindi cha siku kumi kuanzia siku ya pili baada ya siku ambayo maombi yamepokewa na kampuni.

(3) Kama ukaguzi wowote unaotakiwa chini ya kifungu hiki unakataliwa au kama nakala yoyote inayotakiwa chini ya kifungu hiki haikupelekwa katika kipindi kinachofaa, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa kila kosa.

(4) Kwa ukosaji au ukataaji wowote, mahakama inaweza kutoa amri kulazimisha ukaguzi wa haraka wa daftari na faharisi au kuelekeza kwamba nakala zilizotakiwa zipelekwe kwa watu waliozitaka.

Matokeo ya kushindwa kuzingatia mahitaji ya daftari la wanachama yanayotokana na uwakala.

**120.** Ambapo, kwa mujibu wa kifungu kidogo (b) cha kifungu cha 116(2) daftari la wanachama limewekwa katika ofisi ya mtu mwengine ambaye si kampuni, na kwa sababu ya ukiukaji wowote wa kampuni yake atashindwa kutekeleza kifungu kidogo cha 116(3) ya kifungu hicho, kifungu kidogo cha 117(3), au kifungu cha 119 au matakwa yoyote ya Sheria hii kuhusu utayarishaji wa daftari, mtu huyo mwengine atastahiki adhabu sawa kama vile angekuwa ofisa wa kampuni ambaye alihusika katika ukiukaji, na uwezo wa mahakama chini ya kifungu kidogo cha 119(4) kitatumika kutoa amri dhidi ya mtu huyo mwengine na maofisa wake na watumishi wake.

Uwezo wa kufunga daftari.

**121.** Kampuni inaweza, kwa kutoa taarifa kwa tangazo katika gazeti linalosambazwa katika wilaya ambapo ofisi iliyosajiliwa ya kampuni ipo, kulifunga daftari la wanachama kwa muda mfupi wowote au muda mrefu usiozidi kwa jumla siku thalathini katika kila mwaka.

Uwezo wa mahakama kurekebisha daftari.

**122.**-(1) Kama:-

(a) jina la mtu yeyote, bila sababu za kutosha, limeingizwa katika au limeachwa katika daftari la wanachama la kampuni; au

ukiukaji umefanywa au ucheleweshaji usiokuwa wa lazima unafanyika katika kuingiza kwenye daftari taarifa za mtu yeyote ambaye ameacha kuwa mwanachama; mtu aliyeathirika, au mwanachama yeyote wa kampuni, au kampuni, anaweza kuiomba mahakama kulifanyia marekebisho daftari.

(2) Pale ambapo maombi yamefanywa chini ya kifungu hiki, mahakama inaweza ama kukataa maombi au inaweza kuamuru marekebisho ya daftari na kampuni kulipa hasara aliyopata mtu aliyeathirika.

(3) Kuhusu maombi chini ya kifungu hiki mahakama inaweza kuamua suala lolote kuhusiana na hatimiliki ya mtu yeyote ambaye ni

mshiriki katika maombi kuingizwa au kutolewa jina lake katika daftari, kama suala limeibuka kati ya wanachama au wanachama wanaodaiwa, au baina ya wanachama au wanachama wanaodaiwa kwa upande mmoja na kampuni kwa upande mwengine, na kwa jumla inaweza kuamua suala lolote la lazima au linalofaa kuamuliwa kwa ajili ya marekebisho ya daftari.

(4) Kwa kampuni ambayo inatakiwa na Sheria hii kupeleka orodha ya wanachama wake kwa Mrajis, mahakama, wakati wa kutoa amri kwa ajili ya marekebisho ya daftari itaelekeza kwa amri yake taarifa ya marekebisho iwasilishwe kwa Mrajis.

Amana kutoingizwa katika daftari.

**123.** Hakuna taarifa ya amana yoyote, iliyoelezwa bayana, ya kuchukulia au ya kusaidia, itaingizwa kwenye daftari, au kupokewa na Mrajis.

Daftari kuwa ushahidi.

**124.** Daftari la wanachama litakuwa ni ushahidi wa kwanza kuhusiana na masuala yoyote ya Sheria au yaliyoidhinishwa kuingizwa humo Daftari la Tawi.

Uwezo wa kampuni wa kuweka daftari la tawi.

**125.**-(1) Kampuni yenye mtaji wa hisa inaweza, ikiwa inaruhusiwa na kanuni zake, kusababisha kuwekwa katika nchi yoyote nje ya Zanzibar daftari la tawi la wanachama wakaazi katika nchi ile (katika Sheria hii litaitwa "daftari la tawi").

(2) Kampuni itatoa taarifa kwa Mrajis kuhusu mahali ambapo ofisi ipo ambamo daftari la tawi lolote linawekwa na mabadiliko yoyote ya mahali pake, na kama limekoma kuhusu kukoma kwake, na taarifa yoyote ya aina hiyo itatolewa ndani ya mwezi mmoja ya ufunguzi wa ofisi au ya mabadiliko au kukoma, kama itakavyokuwa.

(3) Kama ukiukaji umefanywa katika kutekeleza kifungu kidogo cha (2), kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye amehusika katika ukiukaji atatozwa faini.

Kanuni kuhusu daftari la tawi .

**126.**-(1) Daftari la tawi litachukuliwa kuwa sehemu ya daftari la kampuni la wanachama (katika kifungu hiki litaitwa "daftari kuu").

(2) Litatunzwa kwa namna ile ile ambayo daftari kuu kwa Sheria hii linatakiwa kutunzwa, isipokuwa kwamba tangazo kabla ya kulifunga daftari litaingizwa katika gazeti linalosambazwa katika wilaya ambayo daftari la tawi lipo.

(3) Kampuni:-

(a) itapeleka kwenye ofisi yake iliyosajiliwa nakala ya kila taarifa iliyoingizwa katika daftari lake la tawi haraka iwezekanavyo baada ya taarifa kuingizwa; na

(b) itawezesha kuwekwa mahali ambapo daftari kuu la kampuni linawekwa nakala ya dafatari lake la tawi lililoingizwa taarifa kila baada ya muda.

Kila nakala ya namna hiyo kwa madhumuni ya Sheria hii itahesabika kuwa sehemu ya daftari kuu.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki kuhusiana na nakala ya daftari, hisa zilizosajiliwa katika daftari la tawi zitatafautishwa na hisa zilizosajiliwa katika daftari kuu, na hakuna shughuli kuhusiana na hisa zozote zilizosajiliwa katika daftari la tawi, wakati wa kuendelea na usajili, zitaandikishwa katika daftari jengine lolote.

(5) Kampuni inaweza kusitisha kuweka daftari la tawi, na kwa kufanya hivyo taarifa zote zilizoingizwa katika daftari hilo zitahaulishwa kwenye daftari kuu.

(6) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, kampuni yoyote inaweza, kwa kanuni zake, kuweka masharti kama inavyoona inafaa kuhusiana na utunzaji wa madaftari ya tawi.

(7) Kama ukiukaji umefanywa katika kutekeleza kifungu kidogo cha (3), kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji; na ambapo, kwa mujibu wa paragrafu (b) na kifungu kidogo cha cha 116(2), daftari kuu limewekwa katika ofisi ya mtu mwengine ambaye si kampuni na kwa sababu ya ukiukaji wake wowote atashindwa kutekeleza paragrafu (b) ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, atastahiki adhabu sawa kama vile angekuwa ofisa wa kampuni ambaye alihusika katika ukiukaji.

Ushuru wa stempu kwa hisa zilizosajiliwa katika madaftari ya tawi.

**127.** Hati ya uhaulishaji wa hisa iliyosajiliwa katika daftari la tawi, itachukuliwa kuwa uhaulishaji wa mali iliyo nje ya Zanzibar, na, isipokuwa iwe imetekelezwa katika sehemu yoyote ya Zanzibar, itasamehewa ushuru wa stempu unaotozwa Zanzibar.

Masharti kuhusu madaftari ya tawi ya kampuni yanayowekwa Zanzibar.

**128.** Kama kwa mujibu wa sheria inayotumika katika nchi yoyote ya nje kampuni zilizosajiliwa chini ya sheria hiyo zina uwezo wa kuweka katika tawi la Zanzibar, madaftari ya wanachama wao wakaazi wa Zanzibar, Mrajis anaweza kwa amri iliyochapishwa katika Gazeti la Serikali kuelekeza kuwa vifungu vya 120(2) na 123, chini ya mabadiliko yoyote na marekebisho yaliyoainishwa katika amri, vinatumika kwa na kuhusiana na daftari la tawi lolote linalowekwa katika Zanzibar kama zinavyotumika kwa na kuhusiana na madaftari ya kampuni kwa maana ya Sheria hii Marejesho ya Mwaka.

Marejesho ya mwaka kufanywa na kampuni yenye mtaji wa hisa.

**129.**-(1) Kila kampuni yenye mtaji wa hisa, angalau mara moja kila mwaka, itafanya marejesho yenye kuhusiana na ofisi iliyosajiliwa ya kampuni, madaftari ya wanachama na wamiliki wa dhamana, hisa na dhamana, madeni, wanachama wa zamani na wa sasa na wakurugenzi na katibu, mambo yaliyoainishwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii na na marejesho yaliyoelezwa yatakuwa katika fomu iliyowekwa katika Kanuni hizo au linalokaribiana na hilo kama hali inavyoruhusu.

Isipokuwa kwamba:-

(a) kampuni haihitaji kufanya marejesho chini ya kifungu kidogo hiki ama katika mwaka wa kusajiliwa kwake au,

kama haikutakiwa na kifungu cha 136 kuitisha mkutano mkuu wa mwaka katika mwaka unaofuata, katika mwaka huo;

(b) ambapo kampuni imebadilisha hisa zake zozote kuwa katika bidhaa na kutoa taarifa kuhusu ubadilishaji huo kwa Mrajis, orodha iliyotajwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii itaeleza kiasi cha bidhaa zinazomilikiwa na kila mmoja wa wanachama badala ya kiasi cha hisa na maelezo kuhusu hisa yanayotakiwa na paragrafu hiyo;

(c) marejesho yanaweza, katika mwaka wowote, kama marejesho kwa mmojawapo wa miaka miwili iliyopita imetoa kama tarehe ya marejesho hayo maelezo kamili yanayohitajika na paragrafu ya 5 iliyoelezwa, kutoa tu maelezo yanayotakiwa na paragrafu hiyo kuhusiana na watu waliokoma kuwa au waliokuwa wanachama tangu tarehe ya marejesho ya mwisho na hisa zilizohaulishwa tangu tarehe hiyo au mabadiliko kama yakilinganishwa na tarehe hiyo katika kiasi cha bidhaa kinachomilikiwa na mwanachama.

(2) Kwa kampuni inayoweka daftari la tawi:-

(a) marejeo katika paragrafu (c) ya kifungu kidogo cha (1) kuhusu taarifa zinazotakiwa na Kanuni hizo yatachukuliwa kama kwamba hayaingizi maelezo yoyote yaliyomo katika daftari la tawi madhali nakala za taarifa zilizoingizwa hazikupokewa katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni kabla ya tarehe ambayo marejesho yanayohusika yalifanywa; na

(b) ambapo marejesho ya kila mwaka yanafanywa kati ya tarehe ambazo taarifa zozote zinaingizwa katika daftari la tawi na tarehe ambayo nakala za taarifa hizo zimepokewa katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni, maelezo yaliyomo katika taarifa hizo zilizoingizwa, madhali zinafaa kwa marejesho ya kila mwaka, zitaingizwa katika marejesho yanayofuata au ya baadaye kama itakavyofaa baada ya kuzingatia taarifa zilizomo katika marejesho hayo kuhusiana na daftari la kampuni la wanachama.

(3) Kama kampuni itashindwa kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki na ya Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, maneno "mkurugenzi" na "ofisa" yatakuwa ni pamoja na mtu yeyote amabye maelekezo au maagizo yake wakurugenzi wa kampuni wamezoea kuyatekeleza.

Marejesho ya mwaka kufanywa na kampuni isiyokuwa na mtaji wa hisa.

**130.**-(1) Kila kampuni ambayo haina mtaji wa hisa itafanya marejesho angalau mara moja kila mwaka wa kalenda yakieleza:-

(a) anuani ya ofisi iliyosajiliwa ya kampuni;

(b) kama daftari la wanachama, chini ya masharti ya Sheria hii, linawekwa mahali pengine pasipokuwa ofisi hiyo, anuani ya mahali ambapo linawekwa;

(c) kama daftari lolote la wamiliki wa dhamana za kampuni au nakala yoyote ya daftari hilo au sehemu ya daftari hilo, chini ya masharti ya Sheria hii, linawekwa mahali pengine pasipokuwa ofisi iliyosajiliwa ya kampuni, anwani ya mahali ambapo linawekwa;

(d) taarifa zote hizo kuhusiana na watu ambao katika tarehe ya marejesho ni wakurugenzi wa kampuni na mtu yeyote ambaye katika tarehe hiyo ni katibu wa kampuni kama zinavyotakiwa na Sheria hii kuwemo kuhusiana na wakurugenzi na katibu katika daftari la wakurugenzi na makatibu wa kampuni;

Isipokuwa kwamba kampuni haihitaji kufanya marejesho chini ya kifungu kidogo hiki ama katika mwaka wa kusajiliwa kwake au, kama haikutakiwa na kifungu cha 136 kuitisha mkutano mkuu wa mwaka katika mwaka unaofuata, katika mwaka huo.

(2) Kutaambatanishwa kwenye marejesho maelezo yenye taarifa kuhusu jumla ya kiasi cha deni za kampuni kuhusiana na rahani zote na malipo ambayo yanatakiwa kusajiliwa na Mrajis chini ya Sheria hii.

(3) Kama kampuni itashindwa kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki maneno "ofisa" na "mkurugenzi" yatakuwa ni pamoja na mtu yeyote ambaye maelekezo au maagizo yake wakurugenzi wa kampuni wamezoea kuyatekeleza.

Muda wa kukamilisha marejesho ya mwaka.

**131.**-(1) Marejesho ya kila mwaka yatakamilishwa ndani ya siku arubaini na mbili baada ya mkutano mkuu wa mwaka katika mwaka unaohusika, kama mkutano huo ni wa kwanza au la au ni mkutano wa kawaida tu, wa kampuni katika mwaka huo, na kampuni baada ya hapo itapeleka kwa Mrajis nakala iliyotiwa saini na mkurugenzi na katibu wa kampuni.

(2) Kama kampuni itashindwa kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini ya ukiukwaji.

Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno "ofisa" litakuwa ni pamoja na mtu yeyote ambaye maelekezo au maagizo yake wakurugenzi wa kampuni wamezoea kuyatekeleza

**132.**-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, kutakuwa kumeambatanishwa na marejesho ya kila mwaka:-

Nyaraka za kuambatanishwa na marejesho ya mwaka.

(a) nakala iliyoandikwa, iliyothibitishwa na mkurugenzi na katibu wa kampuni kuwa ni nakala halisi, ya kila mizania uliowasilishwa mbele ya kampuni kwenye mkutano mkuu katika kipindi ambacho marejesho yanahusiana nacho (ikiwa ni pamoja na kila hati inayohitajika kwa sheria kuambatanishwa na mizania); na

(b) nakala, iliyothibitishwa kama ilivyoelezwa kabla, ya ripoti ya wakaguzi juu ya, na ya ripoti ya wakurugenzi inayoambatana na, kila mizania hiyo;

na ambapo mizania hiyo au hati inayotakiwa na sheria kuambatanishwa imo katika lugha nyengine yoyote isiyokuwa Kiswahili au Kiingereza, kutaambatanishwa na mizania hiyo tafsiri kwa Kiingereza au Kiswahili ya ya mizania au hati iliyothibitishwa katika namna iliyowekwa kuwa ni tafsiri sahihi.

(2) Kama mizania yoyote kama ilivyoelezwa kabla au hati inayotakiwa na sheria kuambatanishwa haikukidhi masharti ya sheria inayotumika katika tarehe ya ukaguzi kuhusiana na fomu ya mizania au nyaraka zilizoelezwa kabla, kama hali itakavyokuwa, kutafanywa nyongeza kwenye masahihisho na katika nakala kama ambayo yangetakiwa kufanywa katika mizania au waraka ili kuifanya ikidhi matakwa yaliyoelezwa, na ukweli kwamba nakala imefanyiwa marekebisho utaelezwa juu yake.

(3) Kama kampuni itashindwa kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini.

Kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki, neno "ofisa" litakuwa ni pamoja na mtu yeyote ambaye maelekezo au maagizo yake wakurugenzi wa kampuni wamezoea kuyatekeleza.

**133.** Kampuni binafsi itapeleka pamoja na marejesho ya kila mwaka yanayotakiwa na kifungu 129 cheti kilichotiwa saini na mkurugenzi na katibu wa kampuni kwamba kampuni, tangu tarehe ya marejesho ya mwisho, au, kwa marejesho ya kwanza, tangu tarehe ya kusajiliwa kampuni, haijatoa mwaliko wowote kwa umma kujiunga na hisa yoyote au dhamana za kampuni, na, ambapo marejesho ya kila mwaka yanaonesha kwamba idadi ya wanachama wa kampuni inazidi khamsini, pia cheti kilichotiwa saini kinachoeleza kwamba watu ambao wamezidi wote ni kwa mujibu wa kifungu cha 30(1)(b) na wasiingizwe katika idadi ya khamsini.

Vyeti vya kuwasilishwa na kampuni binafsi na marejesho ya kila mwaka.

**134.**-(1) Kampuni binafsi itapata msamaha kutokana na masharti yaliyowekwa na kifungu cha 133 kama, lakini tu kama:-

Msamaha, katika baadhi ya hali, ya kampuni binafsi, kutokana na masharti ya sehemu ya 133.

(a) masharti yaliyoelezwa katika kifungu cha pili kinachofuata yametoshelezwa katika tarehe ya marejesho na yametoshelezwa wakati wote tangu kampuni iliposajiliwa; na

(b) kumepelekwa pamoja na marejesho cheti, kilichotiwa saini na watu wanaotia saini vyeti ambavyo vinatakiwa kupelekwa kwa mujibu wa kifungu cha mwisho kilichotangulia, kwamba kwa kadiri wanavyojua wao na wanavyoamini masharti yaliyoelezwa yanatimizwa na yamekuwa yakitimizwa kama ilivyoelezwa kabla.

Isipokuwa kwamba kama wakati wowote imeoneshwa kwamba masharti yaliyoelezwa yemetimizwa kwa kampuni yoyote binafsi, Mrajis anaweza kwa maombi ya wakurugenzi wa kampuni kuamuru kwamba, kuhusiana na marejesho ya kila mwaka wowote wa baadaye ya kampuni, haitakuwa lazima kwa masharti yaliyoelezwa kuwa yametimizwa kabla ya wakati huo, na vyeti vilivyopelekwa na marejesho hayo, katika hali hiyo vitahusu kipindi tangu wakati huo tu.

(2) Masharti yaliyoelezwa ni:-

(a) kwamba masharti yaliyomo katika Kanuni yametimizwa kuhusu mtu anayetaka hisa za kampuni na dhamana; na

(b) kwamba idadi ya watu wanaomiliki dhamana za kampuni si zaidi ya khamsini (wamiliki wa pamoja watahesabiwa kama mtu moja); na

(c) kwamba hakuna shirika ambalo ni mkurugenzi wa kampuni na wala kampuni yoyote au yeyote wa wakurugenzi anahusika au ana mpango wowote ambapo sera ya kampuni inaweza kuamuliwa na watu wengine kuliko wakurugenzi, wanachama na wamiliki wa dhamna au wadhamini wa wamiliki wa dhamana.

(3) Marejeo yoyote katika Sheria hii kwa kampuni binafsi iliyosamehewa yatafahamika kumaanisha kampuni ambayo masharti yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (2) yametimizwa na yamekuwa yakitimizwa wakati wote tangu kampuni iliposajiliwa au tangu Mrajis alipotoa maelekezo chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1).

Mikutano na Kumbu-kumbu Mikutano ya kisheria na ripoti za kisheria.

**135.-**(1) Kila kampuni yenye ukomo wa hisa na kila kampuni yenye ukomo wa dhamana na yenye mtaji wa hisa, ndani ya kipindi si cha chini ya mwezi mmoja wala si zaidi ya miezi mitatu kuanzia tarehe ambayo kampuni ina haki ya kuanza biashara, itaitisha Mkutano Mkuu wa wanachama wa kampuni hiyo, ambao utaitwa "mkutano wa kisheria".

(2) Wakurugenzi, angalau siku kumi na nne kabla ya siku ambayo mkutano utafanyika, watapeleka ripoti (katika Sheria hii inajuilikana kama "ripoti ya kisheria") kwa kila mwanachama wa kampuni:

Isipokuwa kwamba iwapo ripoti ya kisheria itapelekwa baadaye kuliko inavyotakiwa na kifungu kidogo hiki, bila ya kujali ukweli kwamba, itafahamika kuwa imepelekwa kama imekubaliwa na wanachama wote wenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano.

(3) Ripoti ya kisheria itathibitishwa na si chini ya wakurugenzi wawili wa kampuni na itaeleza:-

(a) idadi ya jumla ya hisa zilizotolewa, zikitafautishwa hisa zilizotolewa na kulipiwa kikamilifu au zilizolipiwa sehemu vyenginevyo kuliko fedha taslimu, na kueleza kwa hisa zilizolipiwa sehemu kiwango ambacho zimelipiwa, na katika kila hali mazingatio yaliyofanywa katika kutengwa kwake;

(b) kiasi cha jumla ya fedha zilizopokewa na kampuni kuhusiana na hisa zote zilizotolewa, zikitafautishwa kama ilivyoelezwa kabla;

(c) muhtasari wa mapato ya kampuni na wa malipo yaliyofanywa kutoka mapato hayo, hadi tarehe ndani ya siku saba ya tarehe ya ripoti, ukionesha chini ya vichwa vya habari tafauti ya mapato ya kampuni kutoka hisa na dhamana na vyanzo vyengine, malipo yaliyofanywa kutokana na mapato hayo, na maelezo kuhusu bakaa iliyomo mikononi, na maelezo au makisio ya gharama za awali za kampuni;

(d) majina, anwani na maelezo ya wakurugenzi, wakaguzi, kama wapo, mameneja, kama wapo, na katibu wa kampuni; na

(e) maelezo ya mkataba wowote ambao marekebisho yake yatawasilishwa kwenye mkutano kupata idhini yake, pamoja na maelezo ya marekebisho au marekebisho yanayopendekezwa.

(4) Ripoti ya kisheria, madhali inahusiana na hisa zilizotolewa na kampuni, na fedha zilizopatikana kuhusiana na hisa hizo, na mapato na malipo ya kampuni kwenye akaunti ya mtaji, itathibitishwa kuwa ni sahihi na wakaguzi, kama wapo, wa kampuni.

(5) Wakurugenzi watawezesha nakala ya ripoti ya kisheria, iliyothibitishwa kama inavyotakiwa na kifungu hiki kuwasilishwa kwa Mrajis kwa ajili ya usajili mara baada ya kupelekwa kwa wanachama wa kampuni.

(6) Wakurugenzi watawezesha orodha unaonesha majina, maelezo na anwani za wanachama wa kampuni, na idadi ya hisa zinazomilikiwa na kila mmoja wao, kupatikana wakati wa kuanza mkutano na kubaki wazi na kupatikana kwa mwanachama yeyote wa kampuni wakati wa kuendelea na mkutano.

(7) Wanachama wa kampuni waliopo katika mkutano watakuwa na uhuru wa kujadili jambo lolote kuhusiana na uanzishaji wa kampuni, au linalotokana na ripoti ya kisheria, kama taarifa ya awali imetolewa au la, lakini hakuna azimio ambalo taarifa haikutolewa kwa mujibu wa kanuni linaweza kupitishwa.

(8) Mkutano unaweza kuakhirishwa kila baada ya muda, na katika mkutano wowote ulioakhirishwa azimio lolote ambalo taarifa imetolewa kwa mujibu wa kanuni, ama kabla au baada ya mkutano wa zamani, linaweza kupitishwa, na mkutano ulioakhirishwa utakuwa na mamlaka sawa kama mkutano wa awali.

(9) Katika tukio la ukiukaji wowote katika kutekeleza masharti ya kifungu hiki, kila mkurugenzi wa kampuni ambaye kwa kujua na kwa makusudi ametenda kosa la ukiukaji au, kwa ukiukaji kwa upande wa kampuni, kila ofisa wa kampuni ambaye amehusika katika ukiukaji atatozwa faini.

(10) Kifungu hiki hakitatumika kwa kampuni binafsi.

Mkutano mkuu wa mwaka.

**136.**-(1) Kila kampuni katika kila mwaka itafanya mkutano mkuu kama mkutano wake mkuu wa mwaka zaidi ya mikutano myengine yoyote katika mwaka huo, na itauainishaa mkutano kama hivyo katika matangazo ya kuuitisha; na si zaidi ya miezi kumi na tano itapita kati ya tarehe ya mkutano mkuu wa mwaka mmoja wa kampuni na ule wa pili.

Isipokuwa kwamba, madamu kampuni inafanya mkutano wake mkuu wa mwaka wa kwanza ndani ya miezi kumi na nane baada ya kusajiliwa kwake, hakutahitajika kuufanya katika mwaka wa usajili wake au katika mwaka uliofuata.

(2) Kama ukiukaji umefanywa katika kufanya mkutano wa kampuni kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), Mrajis anaweza, kwa maombi ya mwanachama yeyote wa kampuni, kuitisha, au kuagiza uitishaji wa, mkutano mkuu wa kampuni na kutoa maelekezo ya ziada au ya matokeo kama Mrajis anavyodhani yanahitajika ikiwa ni pamoja na maelekezo ya kubadilisha au ya nyongeza kuhusiana na uitishaji, ufanyaji na uendeshaji wa mkutano huo, utekelezaji wa kanuni za kampuni; na maelekezo ambayo yanaweza kutolewa chini ya kifungu kidogo hiki ni pamoja na maelekezo kwamba mwanachama mmoja wa kampuni ambaye yeye mwenyewe binafsi yupo au yupo kwa kutumia wakala utachukuliwa kuunganika katika mkutano.

(3) Mkutano mkuu uliofanyika kulingana na kifungu kidogo cha (2) utahesabika, chini ya maagizo yoyote ya Mrajis, kuwa mkutano mkuu wa mwaka wa kampuni lakini, ambapo mkutano uliofanyika hivyo haukufanyika katika mwaka ambao ukiukaji katika kuitisha mkutano mkuu wa mwaka wa kampuni ulitokea, mkutano uliofanyika hivyo hautachukuliwa kama mkutano mkuu wa mwaka kwa mwaka ambao umefanyika isipokuwa kwamba katika mkutano huo kampuni inaaamua kwamba utachukuliwa hivyo.

(4) Endapo kampuni itaamua kwamba mkutano huo uchukuliwe hivyo, nakala ya azimio hilo, ndani ya siku kumi na tano baada ya kupitishwa kwake, litapelekwa kwa Mrajis na kurikodiwa na yeye.

(5) Kama ukiukaji umefanywa katika kufanya mkutano wa kampuni kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), au katika kutekeleza maelekezo

yoyote ya Mrajis chini ya kifungu kidogo cha (2), kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini na kama ukiukaji umefanywa katika kutekeleza kifungu kidogo cha (4) kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye amehusika katika ukiukaji huo atatozwa faini.

Kuitisha mkutano mkuu wa dharura kwa maombi.

**137.-**(1) Wakurugenzi wa kampuni, bila ya kujali kitu chochote katika kanuni, kwa maombi ya wanachama wa kampuni yenye mtaji wa hisa katika tarehe ya kuwasilisha maombi si chini ya moja ya kumi ya mtaji uliolipwa wa kampuni katika tarehe ya kuwasilishwa walio na haki ya kupiga kura katika mikutano mikuu ya kampuni, au, kwa kampuni ambayo haina mtaji wa hisa, wanachama wa kampuni wanaowakilisha si chini ya moja ya kumi ya haki ya kupiga kura ya jumla ya wanachama wote ambao katika tarehe iliyoelezwa wana haki ya kupiga kura katika mikutano mikuu ya kampuni, wataendelea kuitisha mkutano mkuu wa dharura wa kampuni.

(2) Maombi lazima yaeleze malengo ya mkutano, na lazima yasainiwe na waombaji na yawasilishwe katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni, na inaweza kuwa na nyaraka nyingi katika fomu zinazofanana kila moja ikitiwa saini na muombaji mmoja au zaidi.

(3) Kama wakurugenzi ndani ya siku ishirini na moja kutoka tarehe ya kuwasilisha maombi wanaitisha mkutano, waombaji, au yeyote kati yao anayewakilisha zaidi ya nusu moja ya jumla haki za kupiga kura za wote wanaweza wenyewe kuitisha mkutano, lakini mkutano wowote ulioitishwa hivyo hautafanyika baada ya kumalizika muda wa miezi mitatu kuanzia tarehe iliyoelezwa.

(4) Mkutano ulioitishwa chini ya kifungu hiki na waombaji utaendeshwa kwa namna ile ile, kadiri iwezekanavyo, kama ile mikutano ambayo inaitishwa na wakurugenzi.

(5) Gharama zozote zinazokubalika zilizoingiwa na waombaji kwa sababu ya kushindwa wakurugenzi kuitisha mkutano italipwa kwa waombaji na kampuni, na kiasi chochote kilicholipwa hivyo kitabakia kwa kampuni kutokana na kiasi chochote ambacho kitatokana na kampuni kwa njia ya ada au malipo mengine kwa mujibu wa huduma zao kwa wakurugenzi kama ilivyokuwa katika ukiukaji.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki wakurugenzi, kwa mkutano ambao azimio litakalopitishwa litapendekezwa kuwa ni azimio maalumu, watafahamika kuwa hawakuitisha mkutano kihalali kama hawakutoa taarifa kuhusu mkutano huo kama inavyotakiwa na kifungu cha 146.

Urefu wa taarifa ya wito wa mikutano.

**138.-**(1) Kifungu chochote cha kanuni ya kampuni kitakuwa batili kwa kadri kinavyotoa wito wa mkutano wa kampuni (zaidi ya mkutano ulioakhirishwa) kwa taarifa fupi kuliko ile ya mikutano.

(a) kwa mkutano mkuu wa mwaka, taarifa ya maandishi ya siku ishirini na moja; na

(b) kwa mkutano mwengine zaidi ya mkutano mkuu wa mwaka au mkutano wa kupitisha azimio maalumu, taarifa

ya maandishi ya siku kumi na nne kwa kampuni nyengine isiyokuwa kampuni ambayo haina ukomo na taarifa ya siku saba ya maandishi kwa kampuni ambayo haina ukomo.

(2) Ila kwa kadiri ambavyo kanuni za kampuni zinaweka sharti jengine kwa ajili hiyo (si sharti lililoepukwa na kifungu kidogo cha (1)) katika mkutano wa kampuni (zaidi ya mkutano ulioakhirishwa) unaweza kuitishwa:-

(a) kwa mkutano mkuu wa mwaka, kwa taarifa ya maandishi ya siku ishirini na moja; na

(b) kwa mkutano mwengine zaidi ya mkutano mkuu wa mwaka au mkutano wa kupitisha azimio maalumu, kwa taarifa ya maandishi ya siku kumi na nne kwa kampuni nyengine zaidi ya kampuni isiyokuwa na na ukomo na kwa taarifa ya siku saba ya maandishi kwa kampuni isiyokuwa na ukomo.

(3) Mkutano wa kampuni, bila ya kujali kwamba umeitishwa kwa taarifa ya muda mfupi kuliko ule uliotajwa katika kifungu kidogo cha (2) au katika kanuni za kampuni, kama itakavyokuwa, utahesabiwa kuwa umeitishwa kihalali kama umekubaliwa:-

(a) kwa mkutano uliotishwa kama mkutano mkuu wa mwaka, na wanachama wote wenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura; na

(b) kwa mkutano mwengine wowote, na wanachama wengi kwa idadi wenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano, wakiwa ni wengi kwa pamoja wenye kumiliki si chini ya asilimia 95 katika thamani ya hisa zinazotoa haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano, au, kwa kampuni isiyokuwa na mtaji wa hisa, kwa pamoja, wanaowakilisha si chini ya asilimia 95 ya haki zote za kupiga kura kwenye mkutano huo wa wajumbe wote.

Masharti ya jumla kuhusu mikutano na kura.

**139.** Masharti yafuatayo yatatumika kwa kadiri ambavyo kanuni za kampuni haziweki masharti mengine kwa ajili hiyo:-

(a) taarifa ya mkutano wa kampuni atapewa kila mwanachama wa kampuni katika namna ambayo taaraifa zinatakiwa kutolewa kwa mujibu wa Jadweli A na kwa madhumuni ya paragrafu hii tamko "Jadweli A" lina maana ya Jadweli kwa wakati huu linalotumika;

(b) wanachama wawili au zaidi wanaomiliki si chini ya moja ya kumi ya mtaji wa hisa uliotolewa au, kama kampuni haina mtaji wa hisa si, si chini ya asilimia tano ya idadi ya wanachama wa kampuni wanaweza kuitisha mkutano.

(c) kwa kampuni binafsi wanachama wawili, na kwa kampuni nyengine yoyote wanachama watatu, waliopo wenyewe binafsi watakuwa ni akidi;

(d) mwanachama yeyote aliyechaguliwa na wanachama katika mkutano wa sasa anaweza kuwa mwenyekiti wake;

(e) kwa kampuni ambayo awali ilikuwa na mtaji wa hisa, kila mwanachama atakuwa na kura moja kuhusiana na kila hisa au bidhaa inayomilikiwa na yeye, na katika hali nyengine yoyote kila mwanachama atakuwa na kura moja.

Uwezo wa mahakama wa kuitisha mikutano.

**140.-**(1) Kama kwa sababu yoyote haiwezekani kuitisha mkutano wa kampuni kwa namna yoyote ambayo mikutano ya kampuni hiyo inaweza kuitishwa, au kufanya mkutano wa kampuni katika namna inayoelezwa na kanuni au Sheria hii, mahakama inaweza, ama kwa uamuzi wake yenyewe au kwa maombi ya mkurugenzi yeyote wa kampuni au ya mwanachama yeyote wa kampuni ambaye angekuwa na haki ya kupiga kura katika mkutano, kuamuru mkutano wa kampuni uitishwe na uendeshwe katika namna kama mahakama itakavyoona inafaa, na ambapo amri ya namna hiyo imetolewa inaweza kutoa maagizo ya ziada kama itakayoona yanahitajika; na maelekezo yanayoweza kutolewa chini ya kifungu hiki ni pamoja na muongozo kwamba mjumbe mmoja wa kampuni aliyehudhuria mwenyewe au kwa kutumia wakala atachukuliwa kuunganika kwenye mkutano.

(2) Mkutano wowote ulioitishwa, uliofanyika na ulioendeshwa kwa mujibu wa amri chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa madhumuni yote utachukuliwa kuwa mkutano wa kampuni ulioitishwa kihalali, uliofanyika na uulioendeshwa.

Wakala.

**141.-**(1) Mwanachama yeyote wa kampuni mwenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura katika mkutano wa kampuni atakuwa na haki ya kumteua mtu mwengine (kama mwanachama au si mwanachama) kama wakala wake kuhudhuria na kupiga kura badala yake, na wakala aliyeteuliwa kuhudhuria na kupiga kura badala ya mwanachama wa kampuni binafsi atakuwa pia na haki sawa kama mwanachama kuzungumza katika mkutano:

Isipokuwa kwamba, isipokuwa kanuni zinaelekeza vyenginevyo:-

(a) kifungu hiki kidogo hakitatumika kwa kampuni isiyokuwa na mtaji wa hisa; na

(b) mwanachama wa kampuni binafsi hatakuwa na haki ya kuteua zaidi ya wakala mmoja kuhudhuria kwenye tukio moja; na

(c) wakala atakuwa hana haki ya kupiga kura isipokuwa kwenye uchaguzi.

(2) Katika kila taarifa inayoitisha mkutano wa kampuni yenye mtaji wa hisa mtakuwa na tamko bayana kuwa mwanachama anayeruhusiwa

kuhudhuria na kupiga kura ana haki ya kumteua mwakilishi au, ambapo hilo linaruhusiwa, mwakilishi mmoja au zaidi kuhudhuria na kupiga kura badala ya yake, na kwamba wakala hahitajiki kuwa mwanachama, na kama ukiukaji umefanywa katika kutekeleza kifungu hiki kidogo kama kuhusiana na mkutano wowote, kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini.

(3) Sharti lolote lililomo katika kanuni za kampuni litakuwa batili maadamu litakuwa na athari ya kuhitaji hati ya kumteua wakala, au hati nyengine muhimu yoyote kuonesha uhalali wa au vyenginevyo zinazohusiana na uteuzi wa wakala, kupokewa na kampuni au mtu mwengine yeyote zaidi ya saa arubaini na nane kabla ya mkutano au kuakhirishwa mkutano ili kwamba uteuzi uweze kutumika hapo.

(4) Iwapo kwa madhumuni ya mkutano wowote wa kampuni mialiko ya kuteua kama wakala mtu au mmojawapo ya watu walioainishwa katika mialiko imetolewa kwa gharama za kampuni kwa baadhi tu ya wanachama wenye haki ya kupelekewa taarifa ya mkutano na kupiga kura kwa kutumia wakala, kila ofisa wa kampuni ambaye kwa kujua na kwa makusudi anaidhinisha au anaruhusu utoaji kama ilivyoelezwa atatozwa faini.

Isipokuwa kwamba ofisa huyo hatahusika chini ya kifungu hiki kwa sababu tu ya kutoa kwa mwanachama kwa ombi lake kwa maandishi la fomu ya uteuzi inayomtaja wakala au ya orodha ya watu walio tayari kuwa wakala iwapo fomu au orodha inapatikana kwa ombi la maandishi kwa kila mwanachama mwenye haki ya kupiga kura katika mkutano kwa wakala.

(5) Sehemu hii itatumika kwa mikutano ya daraja yoyote ya wanachama wa kampuni kama inavyotumika kwa mkutano mkuu wa kampuni.

Haki ya kutaka uchaguzi.

**142.**-(1) Sharti lolote lililomo katika kanuni ya kampuni litakuwa batili maadamu litakuwa na athari ama:-

(a) ya kuondoa haki ya kutaka uchaguzi katika mkutano mkuu juu ya suala lolote zaidi ya uchaguzi wa mwenyekiti wa mkutano au kuakhirishwa mkutano; au

(b) ya kufanya lisifae ombi la uchaguzi juu ya suala lolote lile ambalo limetolewa ama:-

(i) na wanachama wasiopungua watano wenye haki ya kupiga kura katika mkutano; au

(ii) na mwanachama au wanachama wanaowakilisha si chini ya moja ya kumi ya haki za kupiga kura za wanachama wote wenye haki ya kupiga kura katika mkutano; au

(iii) na mwanachama au wanachama wenye hisa katika kampuni zinazotoa haki ya kupiga kura katika mkutano huo, zikiwa hisa ambazo jumla ya pamoja

imelipwa sawa na si chini ya moja ya kumi ya jumla yote iliyolipwa kwa hisa zote zinazotoa haki hiyo.

(2) Hati inayomteua wakala wa kupiga kura katika mkutano wa kampuni itachukuliwa pia kutoa mamlaka ya kudai au kujiunga katika kudai uchaguzi, na kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) ombi la mtu kama wakala wa mwanachama litakuwa sawa na ombi la mwanachama.

Kupiga kura kwenye uchaguzi.

**143.** Kwenye uchaguzi unaofanywa katika mkutano wa kampuni au mkutano wa daraja yoyote la wanachama wa kampuni, mwanachama mwenye haki ya kupiga kura zaidi ya moja halazimiki, kama anapiga kura, kutumia kura zake zote au kuzipiga, na kura anazotumia katika namna ile ile.

Uwakilishi wa mashirika katika mikutano ya makampuni na ya wadai.

**144.**-(1) Shirika, kama ni kampuni ndani ya maana ya Sheria hii au la, linaweza:-

(a) Kama ni mwanachama wa shirika jengine, ambalo ni kampuni ndani ya maana ya Sheria hii, kwa azimio la wakurugenzi wake au chombo chengine cha uongozi, kumuidhinisha mtu huyo kama linavyoona inafaa kuwa mwakilishi wake katika mkutano wowote wa kampuni au katika mkutano wowote wa daraja yoyote ya wanachama wa kampuni;

(b) Kama ni mdai (ikiwa ni pamoja na mmiliki wa dhamana) wa shirika jengine, ambalo ni kampuni ndani ya maana ya Sheria hii, kwa azimio la wakurugenzi wake au chombo chengine cha uongozi, kumuidhinisha mtu huyo kama linavyoona inafaa kuwa mwakilishi wake katika mkutano wowote wa wadai wowote wa kampuni uliofanyika katika kutekeleza Sheria hii au kanuni zozote zilizotungwa chini yake, au kwa mujibu wa masharti yaliyomo katika dhamana yoyote au hati ya dhamana, kama itakavyokuwa.

(2) Mtu aliyeruhusiwa kama ilivyoelezwa kabla atakuwa na haki ya kutumia madaraka sawa kwa niaba ya shirika ambalo analiwakilisha kama ambavyo shirika lingeweza kuyatumia kama vile ni mmiliki binafsi wa hisa, mdai au mmiliki wa dhamana wa ile kampuni nyengine.

Usambazji wa maazimio ya wanachama n.k.

**145.**-(1) Bila ya kuathiri masharti yafuatayo ya kifungu hiki utakuwa ni wajibu wa kampuni, kwa maombi ya maandishi ya idadi ya wanachama kama ilivyoainishwa humu na (isipokuwa kwamba kampuni imeazimia vyenginevyo) kwa gharama ya waombaji:-

(a) Kutoa kwa wanachama wa kampuni wenye haki ya kupokea taarifa ya mkutano mkuu wa mwaka unaofuata taarifa ya azimio lolote ambalo linaweza kutolewa vizuri na limekusudiwa kutolewa katika mkutano huo;

(b) Kusambaza kwa wanachama wenye haki ya kuwa na taarifa ya mkutano wowote mkuu waliopelekewa taarifa

yoyote ya maneno yasiyozidi elfu moja kuhusiana na suala lililotajwa katika azimio lolote linalopendekezwa au shughuli itakayofanywa na mkutano huo.

(2) Idadi ya wanachama wa lazima kwa ombi chini ya kifungu kidogo cha (1) itakuwa:-

(a) idadi yoyote ya wanachama inayowakilisha si chini ya moja ya ishirini ya jumla ya haki za kupiga kura za wanachama wote wenye haki katika tarehe ya maombi ya kupiga kura katika mkutano ambao unahusiana na maombi; au

(b) si chini ya wanachama mia moja wenye hisa katika kampuni ambazo zimelipwa kima cha wastani, kwa kila mwanachama, si chini ya shilingi elfu mbili.

(3) Taarifa ya azimio lolote litatolewa, na taarifa yoyote kama hiyo itasambazwa, kwa wanachama wa kampuni wenye haki ya kupata taarifa ya mkutano iliyopelekwa kwao kwa kuwapelekea nakala ya azimio au taarifa kwa kila mwanachama katika namna yoyote inayoruhusiwa kwa ajili ya kutoa matangazo au mkutano, na taarifa ya azimio lolote la namna hiyo itatolewa kwa mwanachama yeyote wa kampuni kwa kutoa taarifa ya athari ya jumla ya azimio kwa njia yoyote ile inayoruhusiwa ya kutoa taarifa za mikutano ya kampuni.

Isipokuwa kwamba nakala itapelekwa, au taarifa ya athari ya azimio itatolewa, kama itakavyokuwa, kwa namna ile ile na, kwa kadiri iwezekanavyo kupelekwa au kutolewa kwa wakati huo, itapelekwa au kutolewa haraka iwezekanavyo baada ya hapo.

(4) Kampuni haitalazimika chini ya kifungu hiki kutoa taarifa ya azimio lolote au kusambaza tamko lolote isipokuwa:-

(a) nakala ya ombi lililotiwa saini na waombaji (au nakala mbili au zaidi ambazo zimetiwa saini na waombaji wote) inawasilishwa katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni:-

(i) kwa ombi linalohitaji taarifa ya azimio, si chini ya wiki sita kabla ya mkutano; na

(ii) kwa ombi jengine lolote, si chini ya wiki moja kabla ya mkutano; na

(b) kumewekwa amana au kuwasilishwa pamoja na ombi kima cha fedha kinachotosheleza kukidhi mahitaji ya kampuni kutekeleza hayo;

Isipokuwa kwamba iwapo, baada ya nakala ya ombi linalohitaji taarifa ya azimio imewasilishwa katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni, mkutano mkuu wa kila mwaka umeitishwa kwa tarehe wiki sita au chini yake baada ya nakala kuwasilishwa, nakala japokuwa haikuwasilishwa

ndani ya muda unaotakiwa na kifungu hiki kidogo itachukuliwa kuwa imewasilishwa ipasavyo kwa madhumuni hayo.

(5) Kampuni pia haitafungika chini ya kifungu hiki kusambaza taarifa yoyote kama, kwa maombi ya kampuni au ya mtu mwengine yeyote anayedai kuathiriwa, mahakama itaridhika kwamba haki zilizotolewa na kifungu hiki zinatumika vibaya kutoa tangazo lisilohitajika kwa suala la kukashifu, na korti inaweza kuamuru gharama ya kampuni kwa maombi chini ya kifungu hiki kulipwa kamili au sehemu na waombaji, bila ya kujali kwamba wao si wahusika katika maombi.

(6) Bila ya kujali kitu chochote katika kanuni za kampuni, shughuli ambayo inaweza kufanywa katika mkutano mkuu wa mwaka itakuwa ni pamoja na azimio lolote ambalo limetolewa taarifa kwa mujibu wa kifungu hiki, na kwa madhumuni ya kifungu hiki kidogo taarifa itachukuliwa kuwa imetolewa bila ya kujali kuachwa kwa bahati mbaya, katika kuitoa, mjumbe mmoja au zaidi.

(7) Katika tukio lolote la ukiukaji katika kutekeleza masharti ya kifungu hiki, kila ofisa wa kampuni anayehusika katika ukiukaji atatozwa faini.

Maazimio ya kawaida na ya dharura.

**146.**-(1) Azimio litakuwa azimio la dharura wakati limepitishwa na idadi kubwa ambayo si chini ya robo tatu ya wanachama, wanaostahiki kufanya hivyo, kupiga kura wenyewe, au ambapo wakala wanaruhusiwa, kwa wakala, katika mkutano mkuu ambao taarifa inayobainisha nia ya kupendekeza azimio kama azimio la dharura imetolewa ipasavyo.

(2) Azimio litakuwa azimio maalumu wakati limepitishwa na wengi kama inavyohitajika kwa ajili ya kupitisha azimio la dharura na katika mkutano mkuu ambao taarifa ya si chini ya siku ishirini na moja, inayobainisha nia ya kupendekeza azimio kama azimio maalumu, imetolewa ipasavyo;

Isipokuwa kwamba, imekubaliwa na wengi katika idadi ya wanachama wenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura katika mkutano wowote ule, wakiwa wengi kwa pamoja wanaomiliki si chini ya asilimia tisiini na tano katika thamani ya hisa zenye kutoa haki hiyo, au, kwa kampuni ambayo haina mtaji wa hisa, kwa pamoja wanaowakilisha si chini ya asilimia tisiini na tano ya haki zote za kupiga kura katika mkutano huo wa wajumbe wote, azimio linaweza kupendekezwa na kupitishwa kama azimio maalumu katika mkutano ambao taarifa ya chini ya siku ishirini na moja imetolewa.

(3) Wakati wowote mkutano wa kupitisha azimio la dharura au azimio maalumu linapowasilishwa kwa ajili ya kupitishwa, tamko la mwenyekiti kwamba azimio linachukuliwa, isipokuwa uchaguzi umeombwa, litakuwa ushahidi wa mwisho bila ya uthibitisho wa idadi au uwiano wa kura zilizorikodiwa kuunga mkono au kupinga azimio hilo.

(4) Katika kuhesabu wingi unaohitajika kwenye uchaguzi ulioombwa kuhusu suala ambalo azimio la dharura au azimio maalumu

litapitishwa, marejeo yatakuwa katika idadi ya kura zilizopigwa kuunga mkono na zilizopinga azimio.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, taarifa ya mkutano itachukuliwa kuwa imetolewa ipasavyo na mkutano kuwa umefanyika kihalali wakati taarifa inapotolewa na mkutano ukafanyika katika namna inayoelekezwa na Sheria hii au kanuni.

Maazimio yanayohitaji taarifa maalumu.

**147.** Ambapo sharti lolote lililomo katika Sheria hii taarifa maalumu inahitajika ya azimio, azimio halitakuwa na nguvu isipokuwa taarifa ya nia ya hoja hiyo imepewa kampuni si chini ya siku ishirini na nane kabla ya mkutano ambao itatolewa, na kampuni itawapa wanachama wake taarifa ya azimio lolote lile wakati huo huo na kwa namna ile ile kama inavyotoa taarifa ya mkutano, au kama hivyo haiwezekani, itawapa taarifa yake katika namna nyengine yoyote inayoruhusiwa na kanuni, si chini ya siku ishirini na moja kabla ya mkutano.

Isipokuwa kwamba iwapo, baada ya taarifa ya nia ya kutoa hoja ya azimio hilo imepewa kampuni, mkutano unaitishwa kwa tarehe ya siku ya ishirini na nane chini yake baada ya taarifa kutolewa, taarifa ingawa haikutolewa ndani ya muda unaotakiwa na kifungu kidogo hiki itahesabika kuwa imetolewa ipasavyo kwa madhumuni hayo.

Usajili na nakala za baadhi ya maazimio na mikataba.

**148.**-(1) Nakala iliyochapishwa ya kila azimio au makubaliano ambayo kifungu hiki kinatumika, ndani ya siku thalathini baada ya kupitishwa au kufanywa, itapelekwa kwa Mrajis na kurikodiwa na yeye:

Isipokuwa kwamba kampuni binafsi iliyosamehewa haitahitahitaji kupeleka nakala ya azimio lolote lililochapishwa au makubaliano ikiwa badala yake itapeleka kwa Mrajis nakala kwenye fomu nyengine iliyothibitishwa na yeye.

(2) Ambapo kanuni zimesajiliwa, nakala ya kila azimio au mkataba kwa wakati huo unaotumika utaingizwa katika au kuambatanishwa kwenye kila nakala ya kanuni zilizotolewa baada ya kupitishwa azimio au kufanywa makubaliano.

(3) Pale ambapo kanuni hazijasajiliwa, nakala iliyochapishwa ya kila azimio au mkataba itapelekwa kwa mwanachama yeyote kwa ombi lake kwa malipo kama vile kampuni itakavyoelekeza.

(4) Sehemu hii itatumika kwa:-

(a) maazimio maalumu;

(b) maazimio ya dharura;

(c) maazimio ambayo yamekubaliwa na wanachama wote wa kampuni, lakini ambayo, kama hayakukubaliwa, yasingeweza kutumika kwa madhumuni hayo isipokuwa, kama itakavyokuwa, yalikuwa yamepitishwa kama maazimio maalumu au kama maazimio ya dharura.

(d) maazimio au mikataba ambayo imekubaliwa na wanachama wote wa daraja fulani la wamiliki wa hisa lakini ambalo, kama halikukubaliwa hivyo, lisingetumika kwa madhumuni hayo ispokuwa kwamba yalikuwa yamepitishwa kwa wingi makhsusi au vyenginevyo kwa namna makhsusi, na maazimio yote au mikataba ambayo inawafunga wanachama wote wa daraja yoyote ya wamiliki wa hisa ingawa haikukubaliwa na wanchama wale wote.

(e) maazimio yanayoitaka kampuni kufungwa kwa hiari, yaliyopitishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kufilisika.

(5) Kama kampuni itashindwa kutekeleza kifungu kidogo cha (1), kampuni na kila ofisa wa kampuni anayehusika katika ukiukaji atatozwa faini ya ukiukwaji.

(6) Kama kampuni itashindwa kutekeleza kifungu kidogo cha (2) au kifungu kidogo cha (3), kamapuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa kila nakala ambayo ukiukaji umefanywa.

(7) Kwa madhumuni ya vifungu vidogo vya (5) na (6), mfilisi wa kampuni atahesabika kuwa ni ofisa wa kampuni.

Maazimio yaliyopitishwa kwenye mikutano iliyoakhirishwa.

**149.** Pale ambapo azimio limepitishwa katika mkutano ulioakhirishwa wa:-

(a) kampuni;

(b) wamiliki wa hisa za daraja yoyote katika kampuni;

(c) wakurugenzi wa kampuni, azimio kwa madhumuni yote litachukuliwa kama kwamba limepitishwa katika tarehe ambayo ndiyo lilipopitishwa, na halitachukuliwa kuwa lilipitishwa katika tarehe yoyote ya kabla.

Maazimio yaliyoandikwa.

**150.**-(1) Jambo lolote ambalo linaweza kufanywa kuhusu kampuni:-

(a) kwa azimio la kampuni katika mkutano mkuu; au

(b) kwa azimio la mkutano wa wanachama wa daraja yoyote wa kampuni,

(c) linaweza kufanywa, bila ya mkutano na bila ya taarifa ya kabla inayotakiwa, kwa azimio la maandishi lililotiwa saini na au kwa niaba ya wanachama wote wa kampuni ambao katika tarehe ya kupitisha azimio wangekuwa na haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano huo.

Isipokuwa kwamba hakuna kitu chochote katika kifungu hiki kitakachotumika kwa azimio lililopitishwa kwa mujibu wa kifungu cha (197(1) kumuondoa mkurugenzi kabla ya muda wake wa kushika ofisi

kumalizika au azimio chini ya kifungu cha 167(7) kumuondoa mkaguzi kabla ya kumaliza muda wake wa kushika ofisi.

(2) Saini si lazima iwe kwenye waraka mmoja iwapo kila moja iko kwenye waraka unaoeleza kwa usahihi masharti ya azimio.

Kumbukumbu za mwenendo wa mikutano ya kampuni na ya wakurugenzi na meneja.

**151.**-(1) Kila kampuni itawezesha kuweka kumbukumbu zote za mwenendo wa mikutano mikuu, mwenendo wa mikutano ya wakurugenzi wake na pale ambapo pana meneja, mwenendo wa mikutano yote ya meneja wake kuingizwa kwenye madaftari yaliyowekwa kwa madhumuni hayo.

(2) Kumbukumbu hizo zikiwa zinadai kuwa zimetiwa saini na mwenyekiti wa mkutano ambao shughuli za mkutano ulifanyika, au na mwenyekiti wa mkutano mwengine unaofuatia, zitakuwa ni ushahidi wa mwenendo wa mkutano.

(3) Pale ambapo kumbukumbu zimetayarishwa kwa mujibu wa msharti ya kifungu hiki kumbukumbu kwenye mkutano mkuu wowote wa kampuni au wa wakurugenzi au meneja, basi mpaka pale itakapothibitishwa vyenginevyo, mkutano utahesabika kuwa umefanywa kihalali na kuitishwa, na kumbukumbu zote za mkutano zilipatikana kihalali, na uteuzi wote wa wakurugenzi, meneja, au wafilisi utachukuliwa kuwa ni halali.

(4) Kama kampuni imeshindwa kutekeleza kifungu kidogo cha (1), kampuni na kila ofisa wa kampuni anayehusika na ukiukaji atatozwa faini ya ukiukwaji.

Ukaguzi wa vitabu vya kumbukumbu.

**152.**-(1) Vitabu vyenye kumbukumbu za mwenendo wa mkutano mkuu wowote vitawekwa kwenye ofisi iliyosajiliwa ya kampuni na vitakuwa wakati wa saa za kazi (kwa kufuata vizuizi vinavyoridhisha ambavyo kampuni kwa kanuni au mkutano mkuu inaweza kuweka), ili kwamba si chini ya saa mbili kila siku zitaruhusiwa kwa ukaguzi) vitakuwa wazi kwa ukaguzi wa mwanachama yoyote bila ya malipo.

(2) Kila mwanchama atakuwa na haki ya kupatiwa ndani ya siku saba baada ya kuwasilisha ombi kuhusiana na hilo kwa kampuni kopi ya kumbukumbu hizo kama ilivyoelezwa kabla kwa kiasi cha malipo ambacho kampuni inaweza kuweka.

(3) Kama ukaguzi wowote unaotakiwa chini ya kifungu hiki unakataliwa au kama nakala yoyote inayotakiwa chini ya kifungu hiki haikupelekwa ndani ya wakati muwafaka, kampuni na kila ofisa wa kampuni anayehusika katika ukiukaji atatozwa faini kuhusiana na kila kosa.

(4) Katika hali ya kukataliwa au kukiukwa huko, mahakama inaweza kwa amri kulazimisha ukaguzi wa haraka wa vitabu kuhusiana na mwenendo wote wa mikutano mikuu au kuelekeza kwamba nakala zinazohitajika zipelekwe kwa watu wanaozihitaji.

Hesabu na Ukaguzi Kuweka vitabu vya hesabu.

**153.**-(1) Kila kampuni itawezesha kuwekwa kwa Kiswahili au Kiingereza vitabu sahihi vya hesabu kuhusiana na:-

(a) pesa zote zilizopokelewa na kutumiwa na kampuni na mambo ambayo mapato na matumizi yamefanyika;

(b) uuzaji na ununuzi wote wa bidhaa wa kampuni;

(c) rasilimali na madeni ya kampuni.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo kilichotangulia, vitabu sahihi vya hesabu havitahesabiwa kuwa vimewekwa kuhusiana na mambo yaliyoelezwa kabla ikiwa hapakuwekwa vitabu vilivyo lazima kutoa hali ya kweli na ya kuridhisha ya hali ya shughuli za kampuni na kueleza shughuli zake za biashara.

(3) Vitabu vya hesabu vitawekwa katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni au mahali pengine kama wakurugenzi watakavyoona inafaa, va vitakuwa wazi wakati wote kwa ukaguzi wa wakurugenzi.

Isipokuwa kwamba kama vitabu vya hesabu vimewekwa mahali nje ya Zanzibar vitapelekwa na kuwekwa mahali katika Zanzibar na kuwa wazi wakati wote kwa ukaguzi wa wakurugenzi hesabu hizo na marejesho kuhusiana na shughuli zilielezwa katika vitabu vya hesabu zilizowekwa kwa namna ambayo zitadhihirisha kwa usahihi hali ya kifedha ya biashara hiyo kila baada ya muda usiozidi miezi sita na zitawezesha kutayarishwa kwa mujibu wa Sheria hii mizania ya kampuni, hesabu zake za faida na hasara au hesabu za mapato na matumizi, na kila waraka ulioambatanishwa na nyaraka hizo wenye kutoa taarifa zinazohitajiwa na Sheria hii na zinazoruhusiwa kutolewa hivyo.

(4) Kama mtu yeyote ambaye ni mkurugenzi wa kampuni anashindwa kuchukua hatua zote zinazofaa kutekelezwa na kampuni matakwa ya kifungu hiki, au kwa matendo yake ya hiari anasababisha ukiukaji wowote wa kampuni, kwa kila kosa, akitiwa hatiani atafungwa kwa muda usiozidi miezi sita au kutozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu.

Ispokuwa kwamba:-

(a) Katika mashtaka yoyote dhidi ya mtu kuhusiana na kosa chini ya kifungu hiki linalohusu kushindwa kuchukua hatua zinazofaa kuifanya kampuni kutekeleza matakwa ya kifungu hiki, utakuwa ni utetezi kuthibitisha kwamba alikuwa na sababu zinazokubalika kuamini na aliamini kwamba mtu mwenye uwezo na mwenye kuaminika alipewa jukumu la kuhakikisha kwamba matakwa hayo yanatekelezwa na alikuwa na nafasi ya kutekeleza jukumu hilo; na

(b) Mtu hatahukumiwa kufungwa kwa kosa kama hilo isipokuwa kwamba, kwa maoni ya mahakama inayoshughulikia kesi hiyo, kosa lilitekelezwa kwa kukusudia.

Hesabu ya faida na hasara na mizania.

**154**.-(1) Wakurugenzi wa kila kampuni katika tarehe si zaidi ya miezi kumi na nane baada ya kuandikishwa kampuni na baadaye angalau mara moja katika kila mwaka wa kalenda watawasilisha kwa kampuni katika mkutano mkuu hesabu ya faida na hasara au, kwa kampuni ambayo haiendeshi biashara kwa faida, hesabu ya mapato na matumizi kwa kipindi, kwa hali nyengine yoyote, tangu hesabu iliyotangulia, iliyofanywa hadi tarehe ambayo si mapema zaidi ya tarehe ya mkutano kwa zaidi ya miezi tisa, au, kwa kampuni inayoendesha biashara au yenye maslahi nje ya nchi, kwa zaidi ya miezi kumi na mbili:

Isipokuwa kwamba Mrajis, ikiwa kwa sababu yoyote maalumu anadhani inafaa kufanya hivyo, anaweza, kwa kampuni yoyote, kuongeza muda wa miezi kumi na nane ulioelezwa awali, na kwa kampuni yoyote na kuhusiana na mwaka wowote kupanua vipindi vya miezi tisa na miezi kumi na mbili vilivyoelezwa awali.

(2) Wakurugenzi watawezesha kutayarishwa katika kila mwaka wa kalenda, na kuwasilishwa kwenye kampuni katika mkutano mkuu, mizania kama ulivyo katika tarehe ambayo hesabu ya faida na hasara au hesabu ya mapato na matumizi, kama itakavyokuwa, imetengenezwa.

(3) Iwapo mtu yeyote akiwa ni mkurugenzi wa kampuni anashindwa kuchukua hatua zote zinazostahiki kutekeleza masharti ya kifungu hiki, atakuwa, kuhusiana na kila kosa, itampasa akitiwa hatiani hukumu ya kifungo cha muda usiozidi miezi sita au faini isiyozidi shilingi laki tatu.

Isipokuwa kwamba:-

(a) katika mashtaka yoyote dhidi ya mtu kuhusiana na kosa chini ya kifungu hiki itakuwa ni utetezi kuthibitisha kuwa alikuwa na sababu nzuri kuamini na aliamini kwamba mtu mwenye uwezo na mwenye kuaminika alipewa wajibu wa kuona kuwa masharti ya kifungu hiki yanatekelezwa na alikuwa katika nafasi ya kutekeleza wajibu huo; na

(b) mtu hatahukumiwa kifungo kwa kosa kama hilo isipokuwa kwamba, kwa maoni ya mahakama inayoshughulikia kesi, kosa lilitendwa kwa makusudi.

Sharti la jumla kuhusu maudhui na fomu za hesabu.

**155.**-(1) Kila mizania ya kampuni itatoa maoni ya kweli na ya haki kuhusu hali ya mambo ya kampuni kama ilivyo katika mwisho wa mwaka wake wa fedha, na kila hesabu ya faida na hasara ya kampuni itatoa maoni ya kweli na ya haki ya faida au hasara ya kampuni kwa mwaka wa fedha huo.

(2) Mizania ya kampuni na hesabu ya faida na hasara itazingatia matakwa ya Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, kwa kadiri zinavyoweza kutumika.

(3) Ila kama ilivyoelezwa waziwazi katika masharti yafuatayo ya kifungu hiki au katika kanuni za sheria hii, matakwa ya kifungu kidogo cha

(2) na Kanuni zilizotajwa yatakuwa hayaathiri ama matakwa ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki au matakwa yoyote mengine ya Sheria hii.

(4) Mrajis anaweza, kwa maombi au kwa idhini ya wakurugenzi wa kampuni, kurekebisha kuhusiana na kampuni hiyo matakwa yoyote ya Sheria hii kuhusiana na mambo yatakayoelezwa katika mizania ya kampuni au hesabu ya faida na hasara (ila matakwa ya kifungu kidogo cha (1) kwa madhumuni ya kuyaoanisha na hali ya mambo ya kampuni.

(5) Vifungu vidogo vya (1) na (2) havitatumika kwa hesabu ya faida na hasara ya kampuni kama:-

(a) kampuni hiyo ina matawi; na

(b) hesabu ya faida na hasara imetayarishwa kama hesabu ya pamoja ya faida na hasara inayoshughulikia yote au lolote la matawi ya kampuni pamoja na kampuni; na

(c) nakubaliana na matakwa ya Sheria hii yanayohusiana na hesabu za pamoja za faida na hasara; na

(d) inaonesha ni kiasi gani cha faida au hasara ya pamoja kwa mwaka wa fedha unaoshughulikiwa na katika hesabu za kampuni.

(6) Iwapo mtu yeyote akiwa ni mkurugenzi wa kampuni anashindwa kuchukua hatua zote zinazostahiki kuhakikisha utekelezaji na heasbu zozote zilizowasilishwa kwenye kampuni katika mkutano mkuu kwa masharti ya kifungu hiki na kwa matakwa mengine ya Sheria hii kuhusiana na mambo yanayopaswa kuelezwa katika hesabu, kuhusiana na kila kosa, akitiwa hatiani atafungwa kwa muda usiozidi miezi sita au faini isiyozidi shilingi laki tatu.

Isipokuwa kwamba:-

(a) katika mashtaka yoyote dhidi ya mtu kuhusiana na kosa chini ya kifungu hiki, itakuwa ni utetezi kuthibitisha kuwa alikuwa na sababu nzuri ya kuamini na aliamini kwamba mtu mwenye uwezo na mwenye kuaminika alipewa wajibu wa kuona kuwa masharti yaliyoelezwa au matakwa mengine yaliyoelezwa, kama itakavyokuwa, yanatekelezwa na alikuwa katika nafasi ya kutekeleza wajibu huo; na

(b) mtu hatahukumiwa kifungo au kosa lolote lile, isipokuwa kwa maoni ya mahakama inayoshughulikia kesi, kosa hilo liwe limetendwa kwa makusudi.

(7) Kwa madhumuni ya kifungu hiki na masharti yanayofuata ya Sheria hii, isipokuwa pale ambapo muktadha unahitaji vyenginevyo:-

(a) marejeo yoyote ya mizania au hesabu ya faida na hasara yatajumuisha maelezo yoyote yaliyomo humo au hati iliyoambatanishwa nayo inayotoa taarifa ambayo inahitajika na Sheria hii na inayoruhusiwa kutolewa hivyo; na

(b) marejeo yoyote ya hesabu ya faida na hasara itachukuliwa kwa kampuni isiyoendesha biashara kwa faida, kumaanisha hesabu yake ya mapato na matumizi, na marejeo ya faida au ya hasara na, kama kampuni ina matawi, marejeo ya faida ya pamoja na hesabu ya hasara itafahamika ipasavyo.

Wajibu wa kuwasilisha hesabu za vikundi kwenye kampuni ya hisa.

**156.**-(1) Pale ambapo mwisho wa mwaka wake wa fedha kampuni ina hesabu za matawi, au maelezo (katika Sheria hii zinajuilikana kama "hesabu za kikundi" zinazoshughulikia kama ilivyoelezwa badaaye na hali ya mambo na faida au hasara ya kampuni na matawi, chini ya kifungu kidogo cha (2), zitawasilishwa kwenye kampuni katika mkutano mkuu wakati mizania ya kampuni yenyewe na hesabu ya faida na hasara zinapowasilishwa.

(2) Bila ya kujali kitu chochote katika kifungu kidogo cha (1):-

(a) hesabu za vikundi hazitatakiwa wakati kampuni imo mwishoni mwa mwaka wake wa kifedha wa kampuni tanzu inayomilikiwa kamili na kampuni iliyoandikishwa katika Zanzibar; na

(b) hesabu za vikundi hazilazimiki kushughulikia tawi la kampuni kama wakurugenzi wa kampuni wana maoni kwamba:-

(c) haziwezekani, au zitakuwa hazina faida yoyote halisi kwa wanachama wa kampuni, kutokana na kiasi kidogo kinachohusika, au zingehusisha gharama au kucheleweshwa kusikowiana na thamani ya wanachama wa kampuni; au

(d) matokeo yangekuwa ya kupotosha, au hatari kwa biashara ya kampuni au kwa matawi yake; au

(e) biashara ya kampuni ya hisa na ile ya kampuni tanzu ni tafauti kiasi kwamba haziwezi kuchukuliwa kama biashara moja;

(f) na, kama wakurugenzi wana maoni kuhusu kila tawi la kampuni hiyo, hesabu za vikundi hazitahitajika;

Isipokuwa kwamba idhini ya Mrajis itatakiwa kwa kutokushughulikia hesabu za vikundi na kampuni tanzu kwa msingi kwamba matokeo yatakuwa na madhara au kwa msingi wa tafauti kati ya biashara ya kampuni ya hisa na ya kampuni tanzu.

(3) Iwapo mtu yeyote akiwa ni mkurugenzi wa kampuni anashindwa kuchukua hatua zote zinazofaa kuhakikisha utekelezaji wa kampuni kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki, kuhusiana na kila kosa, akitiwa hatiani, atafungwa gerezani kwa muda usiozidi miezi sita au faini isiyozidi shilingi laki tatu:

Isipokuwa kwamba:-

(a) katika mashtaka yoyote dhidi ya mtu kuhusiana na kosa chini ya kifungu hiki, itakuwa ni utetezi kuthibitisha kuwa alikuwa na sababu ya kuridhisha ya kuamini na aliamini kwamba mtu mwenye uwezo na mwenye kuaminika alipewa wajibu wa kuona kuwa matakwa ya kifungu hiki yanatekelezwa na alikuwa katika nafasi ya kutekeleza wajibu huo; na

(b) mtu hatahukumiwa kifungo kwa kosa chini ya kifungu hiki isipokuwa, kwa maoni ya mahakama inayoshughulikia kesi, kosa hilo liwe lilifanywa kwa makusudi.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki shirika litachukuliwa kuwa kampuni tanzu inayomilikiwa kamili na kampuni nyengine kama haina wanachama isipokuwa ile kampuni nyengine na ile kampuni tanzu inayomilikiwa na kampuni nyengine au wateuliwa wake au wao.

**157.**-(1) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (2), hesabu za vikundi zinazopelekwa kwenye kampuni ya hisa zitakuwa hesabu za pamoja zenye kujumuisha:- Fomu ya kundi akaunti.

(a) mizania jumuishi inayoeleza hali ya mambo ya kampuni na matawi yote yanayopasa kushughulikiwa katika hesabu za vikundi;

(b) hesabu ya pamoja ya faida na hasara yenye kueleza faida au hasara ya kampuni na matawi hayo.

(2) Kama wakurugenzi wa kampuni wana maoni kwamba ni bora kwa madhumuni:-

(a) ya kuwasilisha taarifa ile ile au inayolingana kuhusu hali ya mambo na faida au hasara ya kampuni na tanzu hizo; na

(b) ya kwamba kuwasilishwa hivyo kunaweza kukubaliwa kwa urahisi na wanachama wa kampuni;

hesabu za vikundi zinaweza kutayarishwa katika fomu nyengine zaidi ya ile inayotakiwa na kifungu kidogo cha (1), na hasa inaweza kujumuisha zaidi ya seti moja ya haesabu za pamoja kushughulikia kampuni na kundi moja la kampuni tanzu na vikundi vyengine vya kampuni tanzu au ya hesabu tafauti kushughulikia kila moja ya kampuni

tanzu, au ya maelezo yanayopanua taarifa kuhusu kampuni tanzu katika hesabu za kampuni yenyewe, au mchanganyiko wa fomu hizo.

(3) Hesabu za vikundi zinaweza zote au baadhi yake kuingizwa katika mizania ya kampuni yenyewe na heasbu ya faida na hasara.

Yaliyomo katika hesabu za vikundi.

**158.**-(1) Hesabu za vikundi zilizowasilishwa kwenye kampuni zitatoa maoni ya kweli na ya haki ya hali ya mambo na faida au hasara ya kampuni na matawi yake yaliyoshughulikiwa kwa jumla, kama inavyohusu wanachama wa kampuni.

(2) Pale ambapo mwaka wa fedha wa kampuni tanzu haulingani na ule wa kampuni ya hisa, hesabu za vikundi, isipokuwa Mrajis kwa maombi au kwa idhini ya wakurugenzi wa kampuni ya hisa aelekeze vyenginevyo, zitashughulikia hali ya mambo ya kampuni tanzu kama zilivyo katika mwisho wa mwaka wake wa fedha unaomalizika na au unaoishia kabla ya ule wa kampuni ya hisa, na pamoja na faida au hasara ya kampuni tanzu kwa mwaka ule wa fedha.

(3) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1), hesabu za vikundi, ikiwa zimetayarishwa kama hesabu za pamoja, zitazingatia matakwa ya Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, kadiri zinavyoweza kutumika, na kama hazikutayarishwa hivyo zitatoa taarifa sawa au zinazolingana:

Isipokuwa kwamba Mrajis anaweza, kwa maombi au kwa idhini ya wakurugenzi wa kampuni hiyo, kurekebisha matakwa yaliyoelezwa kuhusiana na kampuni hiyo kwa lengo la kuyaoanisha na hali ya mambo ya kampuni.

Mwaka wa fedha wa kampuni ya hisa na kampuni tanzu.

**159.**-(1) Wakurugenzi wa kampuni ya hisa watahakikisha kwamba isipokuwa pale ambapo kwa maoni yao kuna sababu za msingi dhidi yake mwaka wa fedha wa kila kampuni tanzu yake utaoana na mwaka wa fedha wa kampuni yenyewe.

(2) Pale ambapo inaonekana na Mrajis inahitajika kwa ajili ya kampuni ya hisa au kampuni tanzu yake kuupanua mwaka wake wa fedha ili mwaka wa fedha wa kampuni tanzu uweze kuishia na ule wa kampuni ya hisa, na kwa madhumuni hayo kuakhirisha uwasilishaji wa hesabu zinazohusika kwenye mkutano mkuu kutoka tarehe moja hadi nyengine, Mrajis anaweza kwa maombi au, kwa idhini ya wakurugenzi wa kampuni ambao mwaka wao wa fedha unaakhirishwa kuelekeza kwamba, kwa kampuni hiyo, kuwasilisha hesabu kwenye mkutano mkuu, kuitisha mkutano mkuu wa mwaka au kutayarisha marejeo ya kila mwaka hayatatakiwa katika mwaka wa kalenda uliotangulia wa miaka iliyoelezwa.

Maana ya "kampuni ya hisa" na "kampuni tanzu"

**160.**-(1) Kwa madhumuni ya Sheria hii, kampuni, chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (3), itachukuliwa kuwa kampuni tanzu ya nyengine kama:-

(a) ile nyengine ama:-

(i) ni mwanachama wa hiyo na inadhibiti muundo wa bodi ya wakurugenzi wake; au

(ii) inamiliki zaidi ya nusu katika thamani ya mtaji wa hisa; au

(b) kampuni ya kwanza iliyotajwa ni kampuni tanzu ya kampuni yoyote ambayo ni kampuni tanzu ya ile kampuni tanzu nyengine.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo kilichotangulia, muundo wa bodi ya wakurugenzi ya kampuni itachukuliwa kudhibitiwa na kampuni nyengine kama, lakini kama tu, kampuni ile nyengine kwa kutumia baadhi ya uwezo unaoweza kutumiwa nayo bila ya idhini au makubaliano na mtu mwengine yeyote inaweza kumteua au kuwaondoa wote au wengi wenye uongozi wa ukurugenzi; lakini kwa madhumuni ya sheria hii kampuni ile nyengine itachukuliwa kuwa na uwezo wa kumteua kwenye uongozi wa ukurugenzi mtu yeyote ambaye sharti lolote miongoni ya yanayofuata limetoshelezwa, yaani:-

(a) kwamba mtu hawezi kuteuliwa katika uongozi huo bila ya kuwa na uwezo katika ile kampuni nyengine kama ilivyoelezwa kabla; au

(b) kuwa uteuzi wa mtu kwenye yongozi huo lazima uwe unatokana na uteuzi wake kama mkurugenzi wa ile kampuni nyengine; au

(c) kwamba ukurugenzi unashikiliwa na ile kampuni nyengine yenyewe au na kampuni tanzu yake.

(3) Katika kuamua kama kampuni moja ni kampuni tanzu ya nyengine:-

(a) hisa yoyote iliyomilikiwa au uwezo wowote unaotumika na ile nyengine katika uwezo wa udhamini itahesabiwa kama kwamba haikumilikiwa au haukutumiwa nayo;

(b) chini ya paragrafu mbili zifuatazo, hisa zozote zinazomilikiwa au uwezo unaotumiwa:-

(i) na mtu yeyote kama mteuliwa kwa ajili ya ile nyengine (isipokuwa pale ambapo ile nyengine inahusika katika uwezo wa udhamini tu); au

(ii) na, au na mteuliwa kwa ajili ya, kampuni tanzu ya ile nyengine, isiyokuwa kampuni tanzu inayojishughulisha katika uwezo wa udhamini tu; itachukuliwa kama inamilikiwa au inatumika na ile nyengine;

(c) hisa zozote zinazomilikiwa au uwezo wowote unaotumiwa na mtu yeyote kwa kuzingatia masharti ya dhamana yoyote ya kampuni ya kwanza iliyotajwa au ya hati yoyote ya amana kwa ajili ya kupata utoaji wowote wa dhamana hizo yatapuuzwa;

(d) hisa zozote zinazomilikiwa au uwezo wowote unaotumiwa na, au na mteuliwa kwa ajili ya, ile nyengine au kampuni tanzu yake yake (isiyomilikiwa au kutumiwa kama ilivyoelezwa katika paragrafu (c) itachukuliwa kama haikumilikiwa au kutumiwa na ile nyengine kama biashara ya kawaida ya ile nyengine au kampuni yake tanzu, kama itakavyokuwa, ni pamoja na mikopo ya fedha na hisa zinamilikiwa au uwezo unatumiwa kama ilivyoelezwa awali kwa njia ya dhamana tu kwa madhumuni ya ununuzi unaofanywa katika mwenendo wa kawaida wa biashara hiyo.

(4) Kwa madhumuni ya Sheria hii, kampuni itachukuliwa kuwa ya kampuni nyengine ya hisa ikiwa, lakini ikiwa tu, ile nyengine ni kampuni tanzu yake.

(5) Katika kifungu hiki tamko "kampuni" ni pamoja na shirika lolote, na tamko "mtaji wa hisa za kawaida" maana yake, kuhusiana na kampuni, mtaji wake wa hisa iliyoutoa ukiondoa sehemu yake yoyote ambayo, haihusiani na gawio wala haihusiani na mtaji, inabeba haki yoyote ya kushiriki zaidi ya kiasi kilichoainishwa katika ugawaji.

Kusaini mizania.

**161.**-(1) Kila mizania ya kampuni itatiwa saini kwa niaba ya Bodi na wakurugenzi wawili wa kampuni, au, kama kuna mkurugenzi mmoja tu, na mkurugenzi huyo.

(2) Kwa kampuni ya benki mizania lazima itiwe saini na Katibu au Meneja, kama yupo, na ambapo kuna zaidi ya wakurugenzi wa kampuni watatu na angalau na watatu wa wakurugenzi hao, na ambapo hakuna zaidi ya wakurugenzi watatu na wakurugenzi wote.

(3) Iwapo jumla ya idadi ya wakurugenzi wa kampuni kwa wakati huo waliopo Zanzibar ni kidogo kuliko idadi ya wakurugenzi ambao saini zao zinatakiwa na kifungu hiki, mizania itatiwa saini na wakurugenzi wote kwa wakati huo waliopo Zanzibar au, kama kuna mkurugenzi mmoja tu kwa wakati huo katika Zanzibar, na mkurugenzi huyo, lakini katika hali kama hiyo yoyote, kutaambatanishwa kwenye mizania taarifa iliyotiwa saini na wakurugenzi hao au mkurugenzi kueleza sababu ya kutotekeleza masharti ya kifungu hiki.

(4) Iwapo nakala yoyote ya mizania ambayo haikutiwa saini kama inavyotakiwa na kifungu hiki imetolewa, kusambazwa au kuchapishwa, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini.

Hesabu na Ripoti ya Wakaguzi kuambatanishwa na mizania.

**162.-**(1) Hesabu ya faida na hasara na, kwa kadiri ambavyo haikuingizwa mizania au hesabu ya faida na hasara, hesabu zozote za vikundi zilizowasilishwa kwenye kampuni kwenye mkutano mkuu, zitaambatanishwa kwenye mizania, na ripoti ya wakaguzi itafunganishwa nayo.

(2) Hesabu zozote zilizoambanishwa hivyo zitathibitishwa na bodi ya wakurugenzi kabla ya mizania kutiwa saini kwa niaba yao.

(3) Kama nakala yoyote ya mizania imetolewa, kusambazwa au kuchapishwa bila ya kuambatanishwa nakala ya hesabu ya faida na hasara au hesabu zozote za vikundi zinazotakiwa na kifungu hiki kuambatanishwa hivyo, au bila ya kufangamanisha nakala ya ripoti ya wakaguzi, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini.

Ripoti ya Wakurugenzi kuambatanishwa na mizania.

**163.-**(1) Kutaambatanishwa kwenye kila mizania inayowasilishwa kwenye kampuni katika mkutano mkuu ripoti ya wakurugenzi kwa kuhusiana na hali ya mambo ya kampuni hiyo, kiasi, kama kipo, ambacho wanapendekeza kinapaswa kulipwa kwa njia ya gawio, na kiasi, kama kipo, ambacho wanapendekeza kubeba akiba ndani ya maana ya Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Ripoti iliyoelezwa itashughulikia, kadiri inavyofaa kwa ajili ya kutathmini hali ya mambo ya kampuni na wanachama wake na kwa maoni ya wakurugenzi kuwa haitakuwa na madhara kwa biashara ya kampuni au ya kampuni tanzu yake yoyote, na mabadiliko yoyote katika mwaka wa fedha katika hali ya biashara ya kampuni hiyo, au katika kampuni tanzu za kampuni hiyo, au katika daraja za biashara ambazo kampuni ina maslahi, iwe kama mwanachama wa kampuni nyengine au vyenginevyo.

(3) Iwapo mtu yeyote akiwa ni mkurugenzi wa kampuni anashindwa kuchukua hatua zote zinazostahiki kutekeleza masharti ya kifungu kidogo cha (1), kuhusiana na kila kosa, akitiwa hatiani atafungwa kwa muda usiozidi miezi sita au faini isiyozidi shilingi laki tatu.

Isipokuwa kwamba:-

(a) katika mashtaka yoyote dhidi ya mtu kuhusiana na kosa chini ya kifungu kidogo cha (1), itakuwa ni utetezi kuthibitisha kuwa alikuwa na sababu za msingi kuamini na aliamini kwamba mtu mwenye uwezo na mwenye kuaminika alipewa wajibu wa kuona kwamba masharti ya kifungu kidogo hicho yanatekelezwa na alikuwa katika nafasi ya kutekeleza wajibu huo; na

(b) mtu hatahukumiwa kifungo kwa kosa hilo isipokuwa, kwa maoni ya mahakama inayoshughulikia kesi, kosa lilifanywa kwa makusudi.

Haki ya kupokea nakala ya mizania na taarifa ya wakaguzi wa hesabu.

**164.-**(1) Nakala ya kila mizania, ikiwa ni pamoja na kila hati inayotakiwa na sheria kuambatanishwa nayo, ambayo itawasilishwa kwenye kampuni katika mkutano mkuu, pamoja na nakala ya ripoti ya wakaguzi, si chini ya

siku ishirini na moja kabla ya tarehe ya mkutano, itapelekwa kwa kila mwanachama wa kampuni (kama yeye ana haki au hana haki ya kupelekewa taarifa ya mikutano mikuu ya kampuni), kila mmiliki wa dhamana za kampuni (kama yeye ana haki au hana haki hiyo) na watu wote zaidi ya wanachama au wamiliki wa dhamana za kampuni, wakiwa ni watu wenye haki hiyo.

Isipokuwa kwamba:-

(a) kwa kampuni ambayo haina mtaji wa hisa kifungu kidogo hiki hakitataka kupeleka nakala za hati zilizoelezwa awali kwa mwanachama wa kampuni ambaye hana haki ya kupewa taarifa za mikutano mikuu ya kampuni au kwa mmiliki wa dhamana za kampuni ambaye hana haki hiyo;

(b) kifungu kidogo hiki hakitataka nakala za hati hizo kupelekwa:-

(i) kwa mwanachama wa kampuni au mmiliki wa dhamana za kampuni, akiwa katika kila hali ama ni mtu ambaye hana haki ya kupewa taarifa za mikutano mikuu ya kampuni na ambaye anuwani yake kampuni haiijui;

(ii) kwa zaidi ya mmoja wa wamiliki wa pamoja wa hisa yoyote au dhamana ambao hakuna mmoja wao mwenye haki ya kupelekewa taarifa hiyo; au

(iii) kwa wamiliki wa pamoja wa hisa zozote au dhamna ambao baadhi yao wana haki na baadhi yao hawana haki ya kupelekewa taarifa hiyo, kwa wale ambao hawana haki hiyo; na

(c) kama nakala za nyaraka zilizoelezwa awali zinapelekwa chini ya siku ishirini na moja kabla ya tarehe ya mkutano, bila ya kujali ukweli huo, zitachukuliwa kuwa zimepelekwa kihalali kama imekubaliwa hivyo na wanachama wote wenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano.

(2) Mwanachama yeyote wa kampuni, kama yeye ana haki au hana haki ya kupelekewa nakala ya mizania ya kampuni, na mmiliki yeyote wa dhamana za kampuni, kama yeye ana haki au hana haki hiyo, atakuwa na haki ya kupewa bila malipo nakala ya mizania ya mwisho ya kampuni, ikiwa ni pamoja na kila hati inayotakiwa na sheria kuambatanishwa nayo, pamoja na nakala ya ripoti ya wakaguzi kwenye mizania.

(3) Kama ukiukaji umefanywa katika kutekeleza kifungu kidogo cha (1), kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini, na kama, wakati mtu yeyote anaomba hati yoyote ambayo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) ana haki ya kupewa, ukiukaji unafanywa katika kutekeleza ombi ndani ya siku saba baada ya kupeleka ombi hilo, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika

ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji, isipokuwa ikithibitika kuwa mtu huyo aliomba kabla na alikwishapatiwa nakala ya hati hiyo.

Uteuzi na malipo ya wakaguzi.

**165.**-(1) Kila kampuni katika kila mkutano mkuu wa mwaka itateua mkaguzi wa kushikilia ofisi kutoka pale unapomalizika mkutano, mpaka utakapomalizika mkutano mkuu wa mwaka ujao.

(2) Katika mkutano mkuu wa mwaka wowote, mkaguzi anayestaafu, kwa namna yoyote aliyoteuliwa, atateuliwa tena bila ya kupitisha azimio lolote isipokuwa:-

(3) Iwapo katika mkutano mkuu wa mwaka hakuna wakaguzi wanaoteuliwa au kuteuliwa tena, Mrajis anaweza kumteua mtu kujaza nafasi.

(4) Kampuni, ndani ya wiki moja ya tarehe ambayo amri ya mahakama chini ya kifungu kidogo cha (3) ilianza kutekelezwa, itatoa taarifa kwa Mrajis kuhusu jambo hilo, na, kama kampuni inashindwa kutoa taarifa kama inavyotakiwa na kifungu kidogo hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

(5) Bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa baadaye wakaguzi wa kwanza wa kampuni wanaweza kuteuliwa na wakurugenzi wakati wowote kabla ya mkutano mkuu wa mwaka wa kwanza na wakaguzi walioteuliwa hivyo watashika wadhifa huo hadi mwisho wa mkutano huo.

Isipokuwa kwamba:-

(a) kampuni inaweza katika mkutano mkuu kuwaondoa wakaguzi wowote kama hao na kuteua katika nafasi zao mtu mwengine yeyote ambaye ameteuliwa kwa ajili ya uteuzi na mwanachama yeyote wa kampuni na ambaye taarifa ya uteuzi imepelekwa kwa wanachama wa kampuni si chini ya siku kumi na nne kabla ya tarehe ya mkutano; na

(b) kama wakurugenzi wanashindwa kutumia uwezo wao chini ya kifungu kidogo hiki, kampuni katika mkutano mkuu inaweza kuteua wakaguzi wa kwanza, na hapo mamlaka ya wakurugenzi yatakoma.

(6) Wakurugenzi wanaweza kujaza nafasi yoyote iliyoachwa wazi katika ofisi ya mkaguzi, lakini wakati nafasi hiyo inaendelea kuwa wazi, mkaguzi aliyepo au mkaguzi anayendelea, ikiwa yupo, anaweza kukaimu.

(7) Malipo ya wakaguzi wa kampuni:-

(a) kwa mkaguzi aliyeteuliwa na wakurugenzi au na Mrajis, yanaweza kuwekwa na wakurugenzi au na Mrajis kama itakavyokuwa;

(b) chini ya paragrafu iliyotangulia, yatawekwa na kampuni katika mkutano mkuu au kwa namna kama kampuni katika mkutano mkuu inavyoweza kuamua.

Kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki, kiasi chochote kinacholipwa na kampuni kuhusiana na matumizi ya wakaguzi yatachukuliwa kujumuishwa katika tamko "malipo".

Masharti kuhusu maazimio yanayohusiana na kuteuliwa na kuondolewa wakaguzi.

**166.**-(1) Taarifa maalumu itatakiwa kwa azimio katika mkutano mkuu wa mwaka wa kuteua mtu kuwa mkaguzi zaidi ya mkaguzi anayestaafu au kuelezwa wazi kwamba mkaguzi anayestaafu hatateuliwa tena.

(2) Baada ya kupokea taarifa ya azimio linalokusudiwa kama ilivyoelezwa awali, kampuni papo hapo itapeleka nakala yake kwa mkaguzi anayestaafu (kama yupo).

(3) Pale ambapo taarifa imetolewa ya azimio linalokusudiwa kama ilivyoelezwa awali na mkaguzi anayestaafu kuhusiana na azimio linalokusudiwa anawasilisha maoni yake kwa maandishi kwenye kampuni (yasiyozidi urefu unaokubalika) na kuomba waarifiwe kuhusu maoni hayo wanachama wa kampuni, kampuni, isipokuwa maoni yamepokelewa kwa kuchelewa mno kwa ajili ya kufanya hivyo:-

(a) katika taarifa yoyote ya azimio waliyopewa wanachama wa kampuni hiyo, itaeleza kwamba maoni yametolewa; na

(b) itapeleka nakala ya maoni kwa kila mwanachama wa kampuni ambaye taarifa ya mkutano alipelekewa (iwe kabla au baada ya kupokewa maoni na kampuni); na

(c) kama nakala ya maoni haikupelekwa kama ilivyoelezwa awali kwa sababu ilipokewa kwa kuchelewa mno au kwa sababu ya ukiukaji wa kampuni, mkaguzi anaweza (bila ya kuathiri haki yake ya kusikilizwa kwa mdomo) kutaka kwamba maoni yasomwe katika mkutano.

Isipokuwa kwamba nakala za maoni hazitahitajika kupelekwa na hayatalazimika kusomwa katika mkutano kama, kwa maombi ama ya kampuni au ya mtu mwengine yeyote anayedai kuathirika, mahakama itaridhika kwamba haki zinazotolewa na kifungu hiki zinatumika vibaya kupata umaarufu usiohitajika kwa jambo lenye kashfa; na mahakama inaweza kumuamuru mkaguzi wa kampuni, bila ya kujali kwamba yeye ni mshiriki kwenye maombi.

(4) kifungu kidogo cha (3) kitatumika kwa azimio la kuwaondoa wakaguzi wa kwanza kwa mujibu wa kifungu cha 165(5) kama kinavyotumika kuhusiana na azimio kwamba mkaguzi anayestaafu hatateuliwa tena.

Kukosa sifa za kuteuliwa kuwa mkaguzi.

**167.**-(1) Mtu hatakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa mkaguzi wa kampuni isipokuwa yeye awe ana sifa kama vile zitakavyowekwa chini ya sheria zinazohusika.

Isipokuwa kwamba kifungu hiki hakitatumika kwa kampuni binafsi ambayo wakati wa uteuzi wa mkaguzi ni kampuni binafsi yenye msamaha.

(2) Watu wafuatao hawataweza kuwa na sifa za kuteuliwa kama mkaguzi wa kampuni:-

(a) ofisa au mtumishi wa kampuni;

(b) mtu ambaye ni mwenza wa au yumo katika ajira ya ofisa au mtumishi wa kampuni;

(c) shirika.

Isipokuwa kwamba paragrafu (b) ya kifungu kidogo hiki haitatumika kwa kampuni binafsi ambayo wakati wa uteuzi wa mkaguzi ni kampuni binafsi yenye msamaha.

Marejeo katika kifungu kidogo hiki kwa ofisa au mtumishi itafahamika kuwa si pamoja na marejeo ya mkaguzi.

(3) Mtu pia hatakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa mkaguzi wa kampuni kama yeye ni, kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), hastahiki kuteuliwa kuwa mkaguzi wa shirika jengine lolote ambalo ni kampuni tanzu ya kampuni hiyo au kampuni ya hisa au kampuni tanzu ya kampuni ya hisa ya kampuni hiyo, au atakuwa hana sifa kama shirika lingekuwa kampuni.

(4) Shirika lolote ambalo linafanya kazi kama mkaguzi wa kampuni litatozwa faini.

Ripoti ya wakaguzi na haki ya kupata vitabu na kuhudhuria na kusikilizwa katika mikutano mkuu.

**168.**-(1) Wakaguzi watatayarisha ripoti kwa wanachama kuhusu hesabu zilizochunguzwa na wao, na kila mizania, kila hesabu ya faida na hasara na hesabu zote za vikundi zilizowasilishwa kwenye kampuni katika mkutano mkuu kwa kipindi cha uongozi wao, na ripoti itakuwa na maelezo kuhusiana na mambo yaliyotajwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Ripoti ya wakaguzi itasomwa kwenye kampuni katika mkutano mkuu na itakuwa wazi kwa ukaguzi wa mwanachama yeyote.

(3) Kila mkaguzi wa kampuni atakuwa na haki ya kupata wakati wote vitabu na hesabu na vocha za kampuni, na atakuwa na haki ya kutaka kutoka kwa maofisa wa kampuni taarifa na maelezo kama yeye anavyodhani ni muhimu kwa utendaji wa kazi ya wakaguzi.

(4) Wakaguzi wa kampuni watakuwa na haki ya kuhudhuria mkutano wowote mkuu wa kampuni na kupokea taarifa zote na mawasiliano mengine yanayohusiana na mkutano wowote mkuu ambao mwanachama yeyote wa kampuni ana haki ya kupata na ya kusikilizwa wakati wowote kwenye mkutano mkuu wowote ambao wanahudhuria kwenye sehemu yoyote ya shughuli ya mkutano ambayo inawahusu wao kama wakaguzi.

Utayarishaji wa kumbukumbu za nyaraka zilizoamba-tanishwa na hesabu.

**169.** Marejeo katika Sheria hii kwenye hati iliyoambatanishwa au inayotakiwa kuambatanishwa na hesabu za kampuni au yoyote kati yao hitajumuisha ripoti ya wakurugenzi au ripoti ya wakaguzi:

Isipokuwa kwamba maelezo yoyote ambayo yanatakiwa na Sheria hii kuwekwa katika hesabu, na yanaruhusiwa kuelezwa katika taarifa inayoambatanishwa, yanaweza kuelezwa katika ripoti ya wakurugenzi badala ya katika hesabu, na kama maelezo hayo yamewekwa hivyo, ripoti itaambatanishwa kwenye hesabu na Sheria hii itatumika ipasavyo kuhusianana nayo isipokuwa kwamba wakaguzi wataripoti juu yake kwa kiasi kile tu ambacho inatoa taarifa iliyoelezwa.

Kuchunguzwa na Mrajis.

**170.**-(1) Pale ambapo Mrajis katika kupitia hati yoyote ambayo kampuni inatakiwa kuwasilisha kwake chini ya masharti ya Sheria hii anadhani kwamba taarifa yoyote ni muhimu ili hati hiyo iweze kuwa na maelezo kamili ya jambo ambalo inadai kulihusisha, anaweza kwa amri ya maandishi kuitaka kampuni iliyowasilisha hati kuwasilisha kwa maandishi taarifa hiyo au maelezo ndani ya muda kama alivyouainisha katika amri yake.

(2) Baada ya kupokea amri chini ya kifungu kidogo cha (1), itakuwa ni wajibu wa watu wote ambao ni au wamekuwa maofisa wa kampuni kuwasilisha taarifa hiyo au maelezo kwa kadiri ya uwezo wao.

(3) Iwapo mtu yeyote anakataa au anapuuza kutoa taarifa yoyote kama hiyo au maelezo atatozwa faini kuhusiana na kila kosa.

(4) Kama taarifa hiyo au maelezo hayakutolewa ndani ya muda ulioainishwa, au kama baada ya kupitia taarifa hiyo au maelezo Mrajis anadhani kuwa hati inayohusika inafichua hali isiyoridhisha ya mambo, au kwamba haifichui taarifa kamili na ya haki ya mambo ambayo inadai kuyahusisha nayo, Mrajis atapeleka ripoti kwa maandishi ya mazingira ya jambo linalohusika mahakamani.

Uchunguzi wa masuala ya kampuni kwa maombi ya wanachama.

**171.**-(1) Mahakama inaweza kuteua mkaguzi mmoja au zaidi mwenye uwezo wa kuchunguza masuala ya kampuni na kuripoti juu yake kwa namna ambayo mahakama itakavyoelekeza kwa:-

(a) kampuni yenye mtaji wa hisa, juu ya maombi ya ama wanachama wasiopungua mia moja au ya wanachama ambao wanamiliki si chini ya sehemu moja ya sehemu kumi za hisa zilizotolewa; au

(b) kampuni ambayo haina mtaji wa hisa, juu ya maombi ya si chini ya moja ya tano ya idadi ya watu waliomo katika daftari la wanachama la kampuni; au

(c) maombi na kampuni.

(2) Maombi yatathibitishwa na ushahidi kama vile ambavyo mahakama itataka kwa madhumuni ya kuonesha kwamba waombaji wana sababu za msingi za kuhitaji uchunguzi, na mahakama inaweza, kabla ya kumteua mkaguzi yeyote, kuwataka waombaji kuweka dhamana kwa ajili ya malipo ya gharama ya uchunguzi.

Upelelezi wa masuala ya kampuni hiyo katika kesi nyengine.

**172.** Bila ya kuathiri madaraka yake chini ya kifungu cha 171 mahakama itateua mkaguzi mmoja au zaidi mwenye uwezo wa kuchunguza shughuli za kampuni na kuripoti juu yake kwa namna mahakama itakavyoelekeza,

kama kampuni kwa azimio maalumu inatangaza kwamba mambo yake lazima kuchunguzwa na mkaguzi aliyeteuliwa na mahakama;

(a) inaweza kufanya hivyo, ikiwa inaonekana na mahakama kutokana na ripoti ya Mrajis kwamba kuna mazingira yanayoashiria:-

(i) kwamba biashara ya kampuni inafanywa kwa nia ya kuwatapeli wadai wake au wadai wa mtu mwengine yeyote au vyenginevyo kwa lengo la ulaghai au linalokwenda kinyume na sheria, au kwa namna ya ukandamizaji wa sehemu yoyote ya wanachama wake, au kwamba iliundwa kwa madhumuni yoyote ya ulaghai au kinyume na sheria; au

(ii) kwamba watu wanaohusika na kuundwa kwake au na usimamizi wa mambo yake wametiwa hatiani kwa udanganyifu, utovu mwengine wa nidhamu kwa kampuni au wanachama wake; au

(iii) kwamba wanachama wake haujapewa taarifa zote kuhusiana na mambo yake ambazo kwa kawaida wangetarajia; au

(iv) kwamba inahitajika kufanya hivyo; na

(b) inaweza kufanya hivyo baada ya kupokea ripoti kutoka kwa Mrajis chini ya kifungu cha 170.

Uwezo wa wakaguzi kufanya uchunguzi katika mambo yanayohusiana na kampuni.

**173.** Kama mkaguzi aliyeteuliwa chini ya ama kifungu cha 171 au cha 172 kuchunguza shughuli za kampuni anadhani ni muhimu kwa madhumuni ya uchunguzi wake kuchunguza pia mambo ya shirika jengine lolote ambalo ni au limekuwa wakati wowote unaohusika kampuni tanzu au kampuni mama au kampuni tanzu ya kampuni mama yake au kampuni mama ya kampuni yake tanzu, atakuwa na uwezo wa kufanya hivyo, na atatoa taarifa juu ya mambo ya shirika jengine kwa kadiri anavyodhani kuwa matokeo ya uchunguzi wake ni muhimu kwa uchunguzi wa masuala ya kampuni ilyotajwa kwanza.

Utoaji wa nyaraka na ushahidi juu ya uchunguzi.

**174.**-(1) Itakuwa ni wajibu wa maofisa wote na mawakala wa kampuni na maofisa wote na mawakala wa mashirika mengine yoyote ambayo mambo yao yanachunguzwa kwa mujibu wa kifungu cha 173 kutoa kwa mkaguzi yeyote vitabu vyote vya na nyaraka za au zinazohusiana na kampuni au, kama itakavyokuwa, shirika jengine ambalo liko chini ya usimamizi au uwezo wao, kuhudhuria mbele ya mkaguzi wakati watakapotakiwa kufanya hivyo na vyenginevyo kutoa kwa mkaguzi misaada yote kuhusiana na uchunguzi ambayo kwa kawaida wana uwezo wa kutoa.

(2) Kama mkaguzi anadhani kwamba ofisa au wakala wa kampuni au shirika jengine la kampuni au mtu mwengine yeyote anazo au anaweza kuwa nazo taarifa zinazohusiana na jambo ambalo wanaamini kuwa ni muhimu kwa uchunguzi, wanaweza kumtaka:-

(a) kutoa kwa mkaguzi nyaraka zozote zilizo chini ya ulinzi wake au chini ya uwezo wake zinazohusiana na jambo hilo;

(b) kuhudhuria mbele ya wakaguzi;

(c) vyenginevyo kutoa kwa mkaguzi misaada yote katika kuhusiana na uchunguzi ambayo kwa kawaida ana uwezo wa kutoa.

(3) Mkaguzi anaweza kuchunguza kwa kiapo maofisa na mawakala wa kampuni au shirika jengine kuhusiana na biashara, na anaweza kuwaapisha ipasavyo.

(4) Ikiwa ofisa yeyote au wakala wa kampuni au shirika jengine anakataa kutoa kwa mkaguzi kitabu chochote au hati ambayo ni wajibu wake chini ya kifungu hiki kuitoa, au anakataa kuhudhuria mbele ya mkaguzi wakati anatakiwa kufanya hivyo, au anakataa kujibu swali lolote ambalo ameulizwa na mkaguzi kuhusiana na masuala ya kampuni au shirika jengine, kama itakavyokuwa, mkaguzi anaweza kuthibitisha kwa saini yake mahakamani, na mahakama inaweza, baada ya hapo kuchunguza suala hilo, na baada ya kusikiliza mashahidi wowote ambao wanaweza kuletwa dhidi ya au kwa niaba ya anayedaiwa kuwa mkosaji na baada ya kusikiliza taarifa yoyote ambayo inaweza kutolewa katika kujitetea, kumuadhibu mkosaji kwa namna kama kwamba alikuwa na hatia ya kudharau mahakama.

(5) Kama mkaguzi anadhani ni muhimu kwa madhumuni ya uchunguzi wake kwamba mtu ambaye hana uwezo wa kuchunguza kwa kiapo lazima kuchunguza, anaweza kuiomba mahakama na mahakama inaweza kama inaona inafaa kumuamuru mtu huyo kuhudhuria na kuchunguzwa kwa kiapo mbele ya mahakama juu ya jambo lolote muhimu kwa uchunguzi, na kwenye uchunguzi wowote kama huo:-

(a) mkaguzi anaweza kushiriki ama yeye mwenyewe au kwa wakili;

(b) mahakama inaweza kumuuliza maswali mtu anayechunguzwa kama mahakama inavyodhani inafaa;

(c) mtu anayeulizwa maswali atajibu maswali yote kama mahakama inavyoweza kumuuliza au kuruhusu kuulizwa, lakini anaweza kwa gharama zake mwenyewe kuajiri wakili, ambaye atakuwa na uhuru wa kumuuliza maswali ambayo mahakama itaona yanafaa kwa madhumuni ya kumwezesha kuelezea au kufafanua jawabu zozote alizotoa, na maelezo ya usaili yatawekwa kwa na yatasomwa kwa au na, na kutiwa saini na mtu anayechunguzwa, na baada ya hapo yanaweza kutumika katika ushahidi dhidi yake;

Isipokuwa kwamba, bila ya kujali kitu chochote katika paragrafu (c) ya kifungu hiki, mahakama inaweza kumruhusu mtu anayechunguzwa gharama kama vile zilizomo katika uamuzi wake, na gharama zozote zinazoruhusiwa hivyo zitalipwa kama sehemu ya gharama za uchunguzi.

(6) Katika kifungu hiki marejeo yoyote kwa maofisa au mawakala yatajumuisha pamoja na wa siku za nyuma, na wa sasa hivi, maofisa au mawakala, kama itakavyokuwa, na kwa madhumuni ya kifungu hiki tamko 'mawakala', kuhusiana na kampuni au shirika jengine litakuwa ni pamoja na wafanya biashara wa mabenki na mawakili wa kampuni au shirika jengine na watu wowote walioajiriwa na kampuni au shirika jengine kama wakaguzi, kama watu hao ni au si maofisa wa kampuni au shirika jengine.

Ripoti ya Mkaguzi.

**175.-**(1) Mkaguzi anaweza, na, kama anaelekezwa hivyo na mahakama, kutayarisha taarifa za muda mfupi kwa mahakama, na baada ya uchunguzi kukamilika atatayarisha ripoti ya mwisho kwa mahakama; na ripoti hiyo itakuwa ya maandishi au, kama mahakama inaagiza hivyo, itapigwa chapa.

(2) Mahakama itaamuru kwamba nakala ya ripoti yoyote kupelekwa kwa Waziri na inaweza, kwa uamuzi wake, kuamuru nakala ya ripoti yoyote kupelekwa:-

(a) kwa kampuni;

(b) kwa ombi na kwa malipo ya ada iliyowekwa kwa mtu mwengine yeyote ambaye ni mwanachama wa kampuni au wa shirika jengine lolote kama ilivyo hapo juu anaonekana na mahakama kuwa ameathirika, au ambaye mwenendo wake umeelezwa katika ripoti;

(c) kwa maombi kwa waombaji wa uchunguzi;

(d) kwa wakaguzi wa kampuni au shirika kama itakavyokuwa, na pia wanaweza kuwezesha ripoti kupigwa chapa na kuchapishwa.

Kesi kutokana na ripoti ya mkaguzi.

**176.-**(1) Kama kutokana na ripoti yoyote iliyotolewa chini ya kifungu cha 175, inaonekana na mahakama kwamba mtu yeyote, kuhusiana na kampuni au shirika lolote ambalo mambo yake yamechunguzwa kwa mujibu wa kifungu cha 173 ametiwa hatiani kwa kosa lolote ambalo ni la jinai, mahakama itapeleka nakala ya ripoti kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, na kama Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma akiona kwamba jambo hilo linapaswa kufunguliwa mashtaka, atafungua kesi ipasavyo, na itakuwa ni wajibu wa maofisa wote na mawakala wa kampuni hiyo, wa zamani na wa sasa (isipokuwa mshitakiwa katika kesi) kumpa misaada yote kuhusiana na upande wa mashitaka ambao wao wana uwezo wa kutoa, kifungu cha 174(5) kitatumika kwa madhumuni ya kifungu hiki kama kinavyotumika kwa madhumuni ya kifungu hicho.

(2) Kama, shirika lolote ambalo linaweza kufungwa chini ya Sheria hii, inaonekana na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, kutokana na ripoti yoyote kama ilivyo hapo juu kwamba ni afadhali kufanya hivyo kwa sababu ya hali yoyote kama ilivyoelezwa katika vifungu vidogo vya (i) au (ii) vya paragrafu (b) ya kifungu cha 172, Mwanasheria Mkuu anaweza, isipokuwa kama shirika tayari linafungwa na mahakama, kuwasilisha ombi kuwa lifungwe ikiwa mahakama inadhani ni haki na usawa kwamba ni lazima lifungwe au ombi la kutolewa amri chini ya kifungu cha 172 au yote mawili.

(3) Kama kutoka ripoti yoyote iliyotolewa au taarifa zilizopatikana chini ya Sehemu hii inaonekana na Mwanasheria Mkuu kwamba kesi yeyote ya madai lazima kwa maslahi ya umma iletwe na shirika, anaweza yeye mwenyewe kuwasilisha mashtaka kwa ajili hiyo kwa jina la shirika.

(4) Waziri atalifidia shirika dhidi ya gharama yoyote au gharama ilizotumia katika au kuhusiana na kesi yoyote iliyoletwa kwa mujibu wa kifungu cha (3).

Gharama za uchunguzi.

**177.**-(1) Gharama za na zinazotokana na uchunguzi zilizoingiwa na mkaguzi aliyeteuliwa na mahakama chini ya Sura hii katika tukio la kwanza zitalipwa na Waziri, lakini watu wafuatao, kwa kadiri walivyotajwa, watapaswa kumlipa Waziri:-

(a) mtu yeyote ambaye atapatikana na hatia juu ya upande wa mashtaka yaliyofunguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka kutokana na matokeo ya uchunguzi au ambaye ameamriwa kulipa fidia au kurejesha mali yoyote katika kesi iliyofunguliwa kwa mujibu wa kifungu cha 176(3), huenda katika kesi hiyo hiyo kuamuriwa kulipa gharama zilizotajwa kwa kiasi kama kitakavyoelezwa katika amri.

(b) kila shirika ambalo kesi imefunguliwa kwa jina lake kama ilivyoelezwa hapo juu, itampasa kulipa kiasi au thamani ya pesa zozote au mali zinazofidiwa kutokana na matokeo ya kesi hiyo; na kiasi chochote ambacho shirika linapaswa kulipa kwa mujibu wa paragrafu hii kitakuwa ni malipo ya kwanza kwenye kiasi au mali zinazofidiwa;

(c) Isipokuwa kama kutokana na matokeo ya uchunguzi mashtaka yamefunguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka:-

(i) kila shirika lililoshughulikiwa na ripoti hiyo, ambapo mkaguzi aliteuliwa vyenginevyo kuliko chini ya kifungu cha 172 (b), litawajibika, isipokuwa kwa kadiri ambavyo mahakama inaelekeza vyenginevyo;

(ii) (waombaji kwa ajili ya uchunguzi, pale ambapo mkaguzi aliteuliwa chini ya kifungu cha 171, watawajibika kwa kadiri (kama wapo) mahakama itakavyoelekeza.

(2) Ripoti ya mkaguzi aliyeteuliwa vyenginevyo kuliko chini ya kifungu cha 171(b), inaweza, ikiwa anadhani inafaa, na kama mahakama itaagiza hivyo, kuingiza mapendekezo kuhusu maelekezo (kama yapo), ambayo anadhani ni muafaka, kutokana na uchunguzi wake, kutolewa chini ya kifungu cha 1(c).

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, gharama zozote au matumizi yaliyofanywa na Mkurugenzi wa Mashtaka katika au kuhusiana na kesi iliyofunguliwa kwa mujibu wa kifungu cha 176(3) (pamoja na matumizi

yaliyofanywa na Waziri kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hicho) zitahesabiwa kama gharama za uchunguzi zilizotokana na kesi.

(4) Matumizi anayopaswa kulipwa Waziri yaliyowekwa na kifungu kidogo cha (1)(a) na cha (1)(b), baada ya kutosheleza haki ya Waziri ya kulipwa, yatakuwa pia ni dhima ya kufidia watu wote dhidi ya dhima chini ya kifungu cha (1)(c); na dhima yoyote ile iliyowekwa na kifungu cha (1)(a), kama ilivyoelezwa awali, itakuwa ni dhima chini ya kifungu cha (1)(c); na mtu yeyote mwenye dhima chini ya kifungu cha (1)(a) au (1)(b) au ama paragrafu ya (i) au ya (ii) ya kifungu cha (1)(c) atakuwa na haki ya kupata mchango kutoka kwa mtu yeyote mwenye dhima chini ya kifungu kidogo kile kile au paragrafu ile ile, kama itakavyokuwa, kulingana na kiasi cha dhima zao za madeni.

Ripoti ya Mkaguzi kuwa ushahidi.

**178.** Nakala ya ripoti yoyote ya mkaguzi aliyeteuliwa chini ya masharti yaliyotangulia ya Sheria hii itaruhusiwa katika kesi yoyote ya kisheria kama ushahidi wa maoni ya mkaguzi kuhusiana na jambo lolote lililomo katika ripoti.

Uteuzi na madaraka ya wakaguzi kuchunguza umiliki wa kampuni.

**179.** Kanuni zinaweza kutungwa na Waziri mwenye dhamana ya fedha, au na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana au mamlaka nyengine iliyoundwa kwa ajili hiyo, kwa ajili ya uchunguzi wa umiliki wa kampuni yoyote au hisa zozote au dhamana au kwa madhumuni ya kuamua watu wa kweli ambao ni au wamekuwa na maslahi ya kifedha katika mafanikio au kushindwa kampuni au wanaweza kudhibiti au kushawishi kifedha sera zake.

Kuharibu, kuchana n.k. nyaraka za kampuni.

**180.**-(1) Ofisa wa kampuni au kampuni ya bima anayeharibu, anayechana, anayeghushi au ni mshiriki katika uharibifu, uchanaji au udanganyifu wa hati inayoathiri au inayohusiana na mali ya kampuni au mambo, au kufanya au ni mshiriki katika kufanya uingizaji wa uongo katika hati hiyo, anatenda kosa, isipokuwa akithibitisha kuwa hakuwa na nia ya kuficha hali ya mambo ya kampuni au kupingana na sheria.

(2) Mtu huyo kama ilivyoelezwa hapo juu, ambaye kwa udanganyifu anachukua, au anafanya uachaji katika hati yoyote au ni mshiriki katika kuchukua, kubadilisha kwa udaganyifu au kuacha kwa udanganyifu, katika hati yoyote kama hiyo, anatenda kosa.

(3) Mtu anayetiwa hatiani kwa kosa chini ya kifungu hiki atafungwa kwa muda usiozidi miaka mitatu au kutozwa faini isiyozidi shilingi milioni mbili au yote mawili.

(4) Katika kifungu hiki, "hati" ni pamoja na taarifa iliyorikodiwa kwa namna yoyote.

Kuwakinga watetezi na wafanyakazi wa benki.

**181.** Hakuna chochote katika masharti yaliyotangulia ya Sehemu hii kitakachohitaji kuwekwa wazi mahakamani au kwa Mrajis au kwa mkaguzi aliyeteuliwa na Mahakama au Mrajis:-

(a) na wakili kuhusu mawasiliano yoyote ya upendeleo yaliyofanywa kwake katika wadhifa huo, isipokuwa kuhusiana na jina na anuani ya mteja wake; au

(b) na benki ya kampuni kuhusu taarifa yoyote kwa masuala yoyote ya wateja wao zaidi ya kampuni.

Uchunguzi wa kampuni za kigeni.

**182.**-(1) Masharti ya Sehemu hii yatatumika kwa kampuni za kigeni na mashirika yaliyoandikishwa nje ya Zanzibar ambayo wakati wowote yamefanya biashara katika Zanzibar, kama zinavyotumika kwa kampuni zilizoandikishwa chini ya Sheria hii, lakini kwa kuzingatia mambo yaliyoenguliwa katika kifungu cha (2).

(2) Masharti yafuatayo hayatatumika kwa makampuni ya kigeni na mashirika yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1):-

(a) kifungu cha 171(1)(a) na (c) (ukaguzi ulioamuriwa juu ya kutumika kwenye kampuni au wanachama wake);

(b) kifungu cha 176(3) (uwezo wa kuleta mashtaka ya madai kwa niaba ya kampuni).

(3) Waziri anaweza kutunga kanuni kuhusu kutumia masharti yoyote ya Sehemu hii kwa kampuni za kigeni au mashirika mengine yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuzingatia marekebisho kama yatakavyoelezwa humo.

Gawio.

**183.**-(1) Kwa kuzingatia kifungu hiki, kampuni inaweza, katika mkutano mkuu, kutangaza gawio kuhusiana na kipindi chochote cha hesabu au kipindi chengine.

(2) Pale ambapo mapendekezo ya wakurugenzi wa kampuni kuhusiana na taarifa maalumu ya gawio inakataliwa au kubadilishwa na kampuni katika mkutano mkuu, taarifa kuhusiana na hilo itaingizwa katika ripoti ya wakurugenzi inayohusika ya kila mwaka na katika marejesho yanayohusika ya kila mwaka.

(3) Kampuni inaweza kulipa gawio:-

(a) kutokana na faida yake iliyopatikana ukitoa hasara yake iliyopatikana; au

(b) kutokana na faida ya mapato yake ukitoa hasara iliyopatikana kwenye mapato yake, kama imepatika au haikupatikana.

Isipokuwa kwamba wakurugenzi wawe wanaamini kwamba mara baada ya mgao kuwa umelipwa kampuni itakuwa na uwezo wa kutekeleza dhima zake zinazopaswa kulipwa, na thamani ya raslimali za kampuni itakayopatikana haitakuwa chini ya kiasi cha madeni yake.

(4) Bila ya kujali kitu chochote katika kifungu hiki, kampuni ya uwekezaji isiyokuwa na ukomo inaweza kulipa gawio kama inavyoweza kuwekwa na Waziri mwenye dhamana ya Fedha.

Wakurugenzi na Maofisa Wengine Uendeshajiwa Kampuni.

**184.** Kwa kuzingatia marekebisho yoyote, mambo maalumu, au upungufu uliomo katika Sheria hii au katika kanuni za kampuni, wakurugenzi wa kampuni wana madaraka yote yanayohitajika kwa ajili ya kuendesha, na kuongoza na kusimamia masuala ya uendeshaji wa shughuli za kampuni.

Wajibu wa wakurugenzi kutekeleza kwa nia njema.

**185.**-(1) Kwa kuzingatia kifungu hiki, mkurugenzi wa kampuni, wakati anatumia madaraka katika kutekeleza majukumu, lazima atekeleze kwa uaminifu na kwa nia njema katika kile mkurugenzi ambacho anaamini kuwa na maslahi bora ya kampuni.

(2) Mkurugenzi wa kampuni ambayo inamilikiwa kamili kama kampuni tanzu anaweza, wakati anapotumia madaraka au kutekeleza wajibu kama mkurugenzi anaweza, ikiwa anaruhusiwa moja kwa moja kufanya hivyo na kanuni za kampuni, kutekeleza katika njia ambayo anaamini ni yenye maslahi bora kwa kampuni mama ya kampuni tanzu ingawa inaweza kuwa si yenye maslahi kwa kampuni tanzu.

(3) Mkurugenzi wa kampuni ambayo ni kampuni tanzu (lakini si kampuni tanzu inayomilikiwa kamili) anaweza, wakati anatumia madaraka au kutekeleza wajibu kama mkurugenzi, ikiwa ameruhusiwa moja kwa moja kufanya hivyo na kanuni za kampuni na kwa makubaliano ya kabla ya wamiliki wa hisa (zaidi ya kampuni tanzu yake), kutekeleza katika njia ambayo anaamini ni kwa maslahi ya kampuni mama ya kampuni tanzu hiyo ingawa inaweza kuwa si kwa maslahi bora ya kampuni tanzu.

(4) Mkurugenzi wa kampuni iliyoandikishwa kutekeleza ubia kati ya wamiliki wa hisa anaweza, wakati akitumia madaraka au kutekeleza majukumu kama mkurugenzi kuhusiana na utekelezaji wa ubia, kutekeleza kwa namna ambayo anaamini ni kwa maslahi bora ya mmiliki wa hisa au wamiliki wa hisa, ingawa inaweza kuwa si kwa maslahi bora ya kampuni.

Wakurugenzi kuzingatia maslahi ya wafanyakazi.

**186.**-(1) Mambo ambayo wakurugenzi wa kampuni wanapasa kuzingatia katika utekelezaji wa majukumu yao ni pamoja na, zaidi ya maslahi ya wanachama, maslahi ya wafanyakazi wa kampuni.

(2) Wajibu uliowekwa na kifungu hiki juu ya wakurugenzi ni dhima kwao kwa ajili ya kampuni yao na unatekelezeka kwa njia ile ile kama wajibu mwengine wowote wa dhamana kampuni inayoudai kwa wakurugenzi wake.

Mamlaka kutumiwa kwa madhumuni yanayofaa.

**187.** Mkurugenzi atatumia mamlaka yake kwa madhumuni yanayofaa.

Wajibu wa wakurugenzi wa kuwa waangalifu.

**188.** Mkurugenzi anadaiwa na kampuni wajibu wa kuwa muangalifu, ujuzi na bidii ambayo ingetumika katika hali inayolingana na mtu mwenye busara mwenye:-

(a) ujuzi na uzoefu ambao unaweza kutarajiwa kwa mtu aliye katika wadhifa kama mkurugenzi; na

(b) ujuzi wowote maalumu na uzoefu ambao mkurugenzi anao.

Idadi ya wakurugenzi.

**189.** Kila kampuni, isipokuwa kampuni yenye mwanachama mmoja, itakuwa na angalau wakurugenzi wawili.

Katibu.

**190.** Kila kampuni itakuwa na Katibu.

Ukatazaji wa baadhi ya watu kuwa wakurugenzi pekee au katibu.

**191.** Kampuni haitakuwa na:-

(a) katibu wa kampuni au shirika mkurugenzi pekee ambaye ni mkurugenzi pekee wa kampuni; au

(b) mkurugenzi wa kampuni pekee au shirika ambaye ni katibu wa kampuni.

Kuepusha vitendo kufanywa na mtu mwenye nyadhfa mbili kama mkurugenzi na katibu.

**192.** Masharti yanayotaka au kuidhinisha jambo kufanywa na au kwa mkurugenzi na katibu hayatatoshelezwa kwa kutekelezwa kwake na au kwa mtu huyo huyo anayekaimu kama mkurugenzi na kama au badala ya katibu.

Uhalali wa matendo ya wakuruge-nzi.

**193.** Matendo ya mkurugenzi au meneja yatakuwa halali bila ya kujali hitilafu yoyote ambayo baadaye itabainika katika uteuzi wake au sifa yake.

Vikwazo juu ya kuteuliwa au kutangazwa mkurugenzi.

**194.**-(1) Mtu hataweza kuteuliwa kuwa mkurugenzi wa kampuni kwa kanuni, na wala hatateuliwa kuwa mkurugenzi au mkurugenzi wa kampuni anayependekezwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotolewa kwa ajili ya mkurugenzi aliyekusudiwa wa kampuni iliyokusudiwa, au katika taarifa badala ya muhtasari wa ununuzi wa hisa uliowasilishwa kwa Mrajis na au kwa niaba ya kampuni, isipokuwa, kabla ya usajili wa kanuni au uchapishaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa au utoaji wa taarifa badala ya muhtasari wa ununuzi wa hisa, kama itakavyokuwa, yeye mwenyewe au kwa wakala wake ameidhinisha kwa maandishi:-

(a) ametia saini na kuwasilisha kwa Mrajis kwa ajili ya usajili ridhaa ya maandishi kutekeleza kama mkurugenzi; na

(b) ama:-

(i) ametia saini mkataba idadi ya hisa si chini ya zile zinazomstahikia, kama zipo; au

(ii) amechukua kutoka kwenye kampuni na amelipa au amekubali kulipa hisa zake zinazomstahikia, kama zipo; au

(iii) ametia saini na kuwasilisha kwa Mrajis kwa ajili ya usajili ahadi kwa maandishi kuchukua kutoka kwenye kampuni na kulipia hisa zake zinazomstahikia, kama zipo; au

(iv) alitayarisha na kuwasilisha kwa Mrajis kwa ajili ya usajili tamko la kisheria kwamba idadi ya hisa, si chini ya zile zinazomstahikia, kama zipo, zimesajiliwa kwa jina lake.

(2) Iwapo mtu ametia saini na kuwasilisha ahadi kama ilivyoelezwa kabla kuchukua na kulipa hisa zake zinazomstahikia, kuhusiana na hisa hizo, atakuwa katika nafasi sawa kama kwamba ametia saini mkataba kwa idadi ya hisa zinazohusika.

(3) Marejeo katika sehemu hii kuhusu hisa zinazomstahikia mkurugenzi au mkurugenzi anayependekezwa itafahamika kuwa ni hisa zinazomstahikia zinazohitajika wakati wa uteuzi au ndani ya kipindi kilichowekwa kwa kurejea wakati wa uteuzi, na marejeo yaliyomo humo kuhusu hisa zinazostahiki zitafahamika ipasavyo.

(4) Wakati wa kuomba usajili wa mkataba na kanuni za kampuni, muombaji atawasilisha kwa Mrajis orodha ya watu ambao wameridhia kwa wakurugenzi wa kampuni, na, kama orodha hii ina jina la mtu yeyote ambaye hajaridhia hivyo, mwombaji atatozwa faini.

(5) Sehemu hii haitatumika kwa:-

(a) kampuni ambayo haina mtaji wa hisa, au

(b) kampuni binafsi;

(c) kampuni ambayo ilikuwa kampuni binafsi kabla ya kuwa kampuni ya umma; au

(d) kampuni yenye mmiliki wa hisa mmoja; au

(e) muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotolewa na au kwa niaba ya kampuni baada ya kumalizika muda wa mwaka mmoja kutoka tarehe ambayo kampuni ilikuwa na haki ya kuanza biashara.

Sifa za wakurugenzi kuwa na hisa.

**195.**-(1) Bila ya kuathiri vikwazo vilivyowekwa na kifungu cha 194, utakuwa wajibu wa kila mkurugenzi ambaye kwa kanuni za kampuni anastahiki kuwa na hisa maalumu, na ambaye bado hajawa na hisa hizo, kupata hisa zinazomstahikia ndani ya miezi miwili baada ya uteuzi wake, au ndani ya muda mfupi kama inavyoweza kuwekwa na kanuni hizi.

(2) Kwa madhumuni ya masharti yoyote katika kanuni zinazohitaji mkurugenzi au meneja kumiliki hisa maalumu zinazomstahikia, mwenye waranti wa hisa hatahesabiwa kuwa mmiliki wa hisa iliyoainishwa katika waranti huo.

(3) Nafasi ya mkurugenzi wa kampuni itakuwa wazi kama mkurugenzi ndani ya miezi miwili kutoka tarehe ya kuteuliwa kwake, au ndani ya muda mfupi kama unavyoweza kuwekwa na kampuni, hajapata hisa zinazomstahikia, au kama baada ya kumalizika muda ya kipindi kilichoelezwa au katika muda mfupi anasita wakati wowote kumiliki hisa zake zinazomstahikia.

(4) Mtu anayeacha nafasi chini ya kifungu hiki atakuwa hawezi kuteuliwa tena kuwa mkurugenzi wa kampuni hadi atakapopata hisa zinazomstahikia.

(5) Endapo baada ya kumalizika muda wa kipindi kilichotajwa au muda mfupi mtu yeyote anatekeleza kama mkurugenzi wa kampuni, atatozwa faini kwa kila siku kati ya kumalizika muda ulioelezwa au muda mfupi au siku ile aliyoacha kuwa na sifa, kama itakavyokuwa, na siku ya mwisho ambayo imethibitishwa kuwa alitekeleza kama mkurugenzi.

Uteuzi wa wakurugenzi kupigiwa kura kwa mtu mmoja.

**196.**-(1) Katika mkutano mkuu wa kampuni nyengine zaidi ya kampuni binafsi, pendekezo kuhusu la kuteua watu wawili au zaidi kama wakurugenzi wa kampuni kwa azimio moja halitafanywa, isipokuwa azimio la kufanya hivyo limekubaliwa kabla kwa mkutano bila ya kupingwa na kura hata moja.

(2) Azimio lililopitishwa linalokiuka kifungu hiki litakuwa batili hata kama lilipingwa au la wakati wa kupitishwa kwake:

Isipokuwa kwamba:-

(a) kifungu hiki kidogo hakitachukuliwa kuwa kinaondoa utekelezaji wa kifungu cha 194; na

(b) ambapo azimio lililopendekezwa hivyo limepitishwa, hakuna sharti la kuteuliwa tena moja kwa moja wakurugenzi waliostaafu kwa kukiuka uteuzi mwengine litatumika.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, pendekezo la kuidhinisha uteuzi wa mtu au kuteua mtu kwa uteuzi litachukuliwa kama pendekezo la uteuzi wake.

(4) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitatumika kwa azimio la kubadilisha kanuni za kampuni.

Uondoaji wa wakurugenzi.

**197.**-(1) Kampuni inaweza kwa azimio la kawaida kumuondoa mkurugenzi kabla ya kumalizika muda wa kipindi chake cha ofisi, bila ya kujali kitu chochote katika kanuni zake au makubaliano yoyote baina ya kampuni na yeye.

(2) Taarifa maalumu itahitajika ya azimio lolote la kumuondoa mkurugenzi chini ya kifungu hiki au kumteua mtu badala ya mkurugenzi aliyeondolewa katika mkutano ambao yeye ameondolewa, na baada ya kupokea taarifa ya azimio linalokusudia kumuondoa mkurugenzi chini ya kifungu hiki kampuni papo hapo itapeleka nakala yake kwa mkurugenzi anayehusika, na mkurugenzi (kama yeye ni mwanachama wa kampuni au la) atakuwa na haki ya kusikilizwa kuhusu azimio katika mkutano.

(3) Pale ambapo taarifa imetolewa ya azimio lililokusudiwa kumuondoa mkurugenzi chini ya kifungu hiki na mkurugenzi anayehusika kuwasilisha vielelezo kwa maandishi kwa kampuni (visivyozidi urefu unaokubalika) na kuomba kutolewa taarifa yao kwa wanachama wa kampuni, kampuni, isipokuwa vielelezo vimechelewa mno kupokewa na kampuni kwa ajili ya kufanya hivyo: -

(a) itaeleza katika taarifa yoyote ya azimio iliyotolewa kwa wanachama wa kampuni ukweli wa vielelezo vilivyotayarishwa; na

(b) itapeleka nakala ya vielelezo kwa kila mwanachama wa kampuni ambaye taarifa ya mkutano alipelekewa (ama kabla au baada ya kupokewa vielelezo na kampuni);

na kama nakala ya vielelezo havikupelekwa kama ilivyoelezwa kabla kwa sababu vilipokelewa vimechelewa mno au kwa sababu ya kushindwa kampuni, mkurugenzi anaweza (bila ya kuathiri haki yake ya kusikilizwa kwa maelezo ya mdomo) kutaka kwamba vielelezo visomwe katika mkutano.

Isipokuwa kwamba nakala za vieleleo hailazimiki kupelekwa na vielelezo havihitaji kusomwa katika mkutano huo, ikiwa kwa maombi ama ya kampuni au ya mtu mwengine yeyote anayedai kuathiriwa, mahakama itaridhika kwamba haki zilizotolewa na kifungu hiki vinatumika vibaya kupata umaarufu usiohitajika kwa jambo lenye kashfa; na korti inaweza kuamuru gharama za kampuni juu ya maombi chini ya kifungu hiki kulipwa kamili au sehemu na mkurugenzi, bila ya kujali kwamba yeye hakushiriki katika maombi.

(4) Nafasi iliyopatikana kutokana na kuondolewa mkurugenzi chini ya kifungu hiki, kama haikujazwa katika mkutano ambao yeye ameondolewa, inaweza kujazwa kama nafasi iliyoachwa wazi kwa muda.

(5) Mtu anayeteuliwa kuwa mkurugenzi katika nafasi ya mtu aliyeondolewa chini ya kifungu hiki atahesabiwa, kwa madhumuni ya kubainisha wakati ambao yeye au mkurugenzi mwengine yeyote anapaswa kustaafu, kama kwamba alikuwa mkurugenzi katika siku ambayo mtu ambaye aliteuliwa katika nafasi yake kwa mara ya mwisho aliteuliwa kuwa mkurugenzi.

(6) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachochukuliwa kuwa kinamnyima mtu aliyeondolewa kwa mujibu wa kifungu hiki fidia au uharibifu unaolipwa kwake kuhusiana na kusitishwa uteuzi wake kama mkurugenzi au uteuzi wowote unaomalizika nao kama mkurugenzi au unaoshusha hadhi kutokana na uwezo wowote wa kumuondoa mkurugenzi ambao unaweza kuwepo mbali na kifungu hiki.

Kustaafu wakurugenzi kwa umri maalumu.

**198.-**(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara hii, hakuna atakayeweza kuteuliwa kama mkurugenzi wa kampuni chini ya kifungu hiki iwapo wakati wa uteuzi wake alikuwa hajatimiza umri wa miaka ishirini na moja au ametimiza umri wa miaka sabini.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki kama ilivyoelezwa kabla, mkurugenzi wa kampuni ambaye yuko chini ya kifungu hiki atalazimika kuacha kazi yake wakati wa kuhitimisha mkutano mkuu wa kuanzia mwaka wa pili baada ya kufikia umri wa miaka sabini:

Isipokuwa kwamba matendo yaliyofanywa na mtu akiwa mkurugenzi yatakuwa halali bila ya kujali kwamba baadaye itagundulikana kwamba uteuzi wake ulikuwa umesitishwa kwa mujibu wa kifungu hiki.

(3) Ambapo mtu anastaafu kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), hakuna masharti ya kuteuliwa moja kwa moja wakurugenzi wanaostaafu katika kukiuka uteuzi mwengine yatakayotumika; na kama katika mkutano ambao yeye anastaafu nafasi haikujazwa inaweza kujazwa kama nafasi ya muda.

(4) Hakuna chochote katika masharti yaliyotangulia ya kifungu hiki kitakachozuia uteuzi wa mkurugenzi katika umri wowote, juu ya umri wa miaka kumi na nane au kumtaka mkurugenzi kustaafu wakati wowote, kama uteuzi wake ni au ulifanywa au kuthibitishwa na kampuni katika mkutano mkuu, lakini taarifa maalumu itahitajika kuhusu azimio la kumteua au kuidhinisha uteuzi wa mkurugenzi kuweza kutumika kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki na taarifa yake iliyotolewa kwa kampuni na na kampuni kwa wanachama lazima ieleze au lazima iwe imeeleza umri wa mtu ambaye inamuhusu.

(5) Mtu aliyeteuliwa tena kuwa mkurugenzi bada ya kustaafu kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, au ameteuliwa katika nafasi ya mkurugenzi aliyestaafu, atachukuliwa, kwa madhumuni ya kubainisha wakati ambapo yeye au mkurugenzi mwengine anayetaka kustaafu, kama kwamba alikuwa mkurugenzi katika siku ambayo mkurugenzi anayestaafu mara ya mwisho aliteuliwa kabla ya kustaafu kwake, lakini, isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu kidogo hiki, kustaafu mkurugenzi kwa kurejea kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) kilichoelezwa hakutazingatiwa katika kuamua wakati wakurugenzi wengine wowote wanaopaswa kustaafu.

(6) Kampuni itakuwa chini ya kifungu hiki kama si kampuni binafsi au kama, ikiwa ni kampuni binafsi, ni kampuni tanzu ya shirika lililoandikishwa katika Zanzibar ambalo si kampuni binafsi; na kwa

madhumuni ya kifungu chengine chochote cha Sheria hii ambacho kinahusu kampuni chini ya kifungu hiki, kampuni itachukuliwa kuwa chini ya kifungu hiki bila ya kujali kwamba yote au mojawapo ya masharti yaliyotajwa limetolewa au kubadilishwa na kanuni za kampuni.

Wajibu wa wakurugenzi kubainisha umri kwa kampuni.

**199.-**(1) Mtu yeyote ambaye ameteuliwa au akijua amependekezwa kuteuliwa kuwa mkurugenzi wa kampuni chini ya kifungu cha 198 katika wakati ambao ametimiza umri wowote wa kustaafu unaomuhusu yeye kama mkurugenzi ama chini ya Sheria hii au chini ya kanuni za kampuni atatoa taarifa ya umri wake kwa kampuni.

Isipokuwa kwamba kifungu hakitatumika kuhusiana na kuteuliwa tena mtu baada ya ukomo wa uteuzi uliopita kama mkurugenzi wa kampuni.

(2) Mtu yeyote ambaye:-

(a) anashindwa kutoa taarifa ya umri wake kama inavyotakiwa na kifungu hiki; au

(b) anafanya kazi kama mkurugenzi chini ya uteuzi wowote ambao ni batili au umekatishwa kwa sababu ya umri wake; atatozwa faini kwa kila siku ambayo ukiukaji unaendelea au ambayo anaendelea kufanya kazi kama ilivyoelezwa awali.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2), mtu ambaye amefanya kazi kama mkurugenzi chini ya uteuzi ambao ni batili au umekatishwa atachukuliwa kuwa ameendelea kufanya hivyo katika kipindi chote kuanzia uteuzi batili au tarehe ambayo uteuzi ulikatishwa, kama itakavyokuwa, mpaka siku ya mwisho ambayo yeye ameonesha kuwa alifanya hivo.

Masharti kuhusu wafilisiwa wasioruhusiwa wanaofanya kazi kama wakurugenzi.

**200.-**(1) Kama mtu yeyote ambaye ni mfilisiwa ambaye hajaruhusiwa anafanya kazi kama mkurugenzi wa, au moja kwa moja au si moja kwa moja anashiriki katika au anajishughulisha katika usimamizi wa kampuni yoyote isipokuwa kwa idhini ya mahakama ambayo iliamua kuwa yeye amefilisika, yeye atafungwa akitiwa hatiani kwa muda usiozidi miaka miwili, au kutozwa faini isiyozidi shilingi milioni moja au adhabu zote mbili.

(2) Idhini ya mahakama kwa ajili ya madhumuni ya kifungu hiki haitatolewa isipokuwa taarifa kuhusu nia ya kuombwa kwake imepelekwa kwa mpokeaji rasmi, na itakuwa ni wajibu wa mpokeaji rasmi, kama yeye ana maoni kuwa ni kinyume na maslahi ya umma kuwa maombi yoyote kama hayo yakubaliwe, kuhudhuria kwenye kusikilizwa maombi na kupinga kukubaliwa kwake.

(3) Katika kifungu hiki, tamko "kampuni" linajumuisha kampuni ambayo haijasajiliwa na kampuni ambayo imeandikishwa nje ya Zanzibar ambayo ina mahali imara pa biashara ndani ya Zanzibar, na tamko "mpokeaji rasmi" maana yake ni mpokeaji rasmi katika kufilisika na linajumuisha mtu aliyeteuliwa rasmi chini ya Sheria ya Kufilisika.

Uwezo wa kuwazuia watu laghai kuendesha kampuni.

**201.**-(1) Ambapo:-

(a) mtu ametiwa hatiani kwa kosa lolote kuhusiana na utangazaji, uundaji, au usimamizi wa kampuni; au

(b) wakati wa kuifunga kampuni hiyo, inaonekana kwamba mtu.

(i) amekuwa na hatia, kwa kosa (kama ametiwa hatiani au la) la kufanya biashara kwa kughushi; au

(ii) (vyenginevyo ametiwa hatiani, wakati akiwa ofisa wa kampuni, kwa udanganyifu wowote kuhusiana na kampuni au ukiukaji wowote wa wajibu wake kwa kampuni;

mahakama inaweza kutoa amri kwamba mtu, bila ya idhini ya mahakama, hatakuwa mkurugenzi wa au kwa njia yoyote, iwe moja kwa moja au si moja kwa moja au kushiriki katika usimamizi wa kampuni kwa kipindi kisichozidi miaka mitano kama itakavyoelezwa kwenye amri.

(2) Katika kifungu kidogo kilichotangulia tamko "mahakama", kuhusiana na kutoa amri dhidi ya mtu yeyote kwa mujibu wa paragrafu ya (a) ililomo ndani yake, ni pamoja na mahakama ambayo yeye imemtia hatiani, na mahakama yoyote yenye mamlaka ya kuifunga kampuni, na kuhusiana na utoaji wa idhini ina maana mahakama yoyote yenye mamlaka ya kuifunga kampuni ambayo idhini inatafutwa.

(3) Mtu mwenye nia ya kuomba kutolewa amri chini ya kifungu hiki na mahakama yenye mamlaka ya kuifunga kampuni, atatoa taarifa si chini ya siku kumi ya nia yake kwa mtu ambaye dhidi yake amri inatafutwa, na katika kusikiliza maombi, mtu wa mwisho aliyetajwa anaweza kujitokeza na yeye mwenyewe kutoa ushahidi au kuwaita mashahidi.

(4) Maombi kwa ajili ya kutoa amri chini ya kifungu hiki na mahakama yenye mamlaka ya kuifunga kampuni yanaweza kufanywa na mpokeaji rasmi, au mfilisi wa kampuni au na mtu yeyote ambaye ni au amekuwa mwanachama au mdai wa kampuni; na katika kusikiliza maombi yoyote ya amri chini ya kifungu hiki na mpokeaji rasmi au mfilisi, au maombi yoyote ya idhini chini ya kifungu hiki na mtu ambaye amri imetolewa dhidi yake kwa maombi ya mpokeaji rasmi au mfilisi, mpokeaji rasmi au mfilisi atajitokeza na kuitanabahisha mahakama jambo lolote ambalo analiona linafaa na anaweza yeye mwenyewe kutoa ushahidi au kuwaita mashahidi.

(5) Amri inaweza kutolewa kwa mujibu wa paragrafu ndogo ya (ii) ya paragrafu (b) ya kifungu kidogo cha (1) ya kifungu hiki bila ya kujali kwamba mtu anayehusika anaweza kuwa na kesi ya jinai kuhusu mambo ambayo amri inatakiwa itolewe, na kwa madhumuni ya paragrafu ndogo ya (ii) iliyoelezwa tamko "ofisa" itakuwa ni pamoja na mtu yeyote ambaye maelekezo au miongozo yake wakurugenzi wamezoea kuitekeleza.

(6) Kama mtu yeyote anatekeleza kwa kukiuka amri iliyotolewa chini ya kifungu hiki, kuhusiana na kila kosa, akitiwa hatiani atafungwa gerezani kwa muda usiozidi miaka miwili, au kutozwa faini isiyozidi shilingi milioni moja, au adhabu zote mbili.

Dhima binafsi kwa deni za kampuni ambapo mtu anatekeleza wakati hana sifa.

**202.**-Mtu anawajibika binafsi kwa deni zote za kampuni zinazohusika kama wakati wowote:-

(a) kwa kukiuka amri ya kutokuwa na sifa yeye anashiriki katika usimamizi wa kampuni; au

(b) kama mtu ambaye anashiriki katika usimamizi wa kampuni, yeye anatenda au yuko tayari kutenda kwa maelekezo aliyopewa bila ya idhini ya mahakama na mtu ambaye yeye anajua wakati huo kuwa yuko chini ya amri ya kutokuwa na sifa au kuwa mfilisiwa asiyeruhusika.

Ukatazaji wa malipo yasiyokuwa na kodi kwa wakurugenzi.

**203.**-(1) Si halali kwa kampuni kumlipa mshahara mkurugenzi (iwe kama mkurugenzi au vyenginevyo) usiokatwa kodi ya mapato au vyenginevyo ulioheasabiwa kwa kurejea kwenye kumbukumbu au kutafautiana na kiasi cha kodi ya mapato yake, au kwenye au na kiwango au kiwango sanifu cha kodi ya mapato.

(2) Sharti lolote lililomo katika kanuni za kampuni, au katika mkataba wowote au katika azimio lolote la kampuni au muongozo wa kampuni, kwa ajili ya malipo kwa mkurugenzi ya mshahara kama ilivyoelezwa kabla litakuwa na athari kama kwamba ni sharti kwa ajili ya malipo, kama kiasi cha jumla chini ya kodi ya mapato, kiasi halisi ambacho kinatolewa hasa.

Ukatazaji wa mikopo kwa wakurugenzi.

**204.**-(1) Si halali kwa kampuni kutoa mkopo kwa mtu yeyote ambaye ni mkurugenzi wake au mkurugenzi wa kampuni yake ya hisa, au kuingia katika dhamana yoyote au kutoa dhamana yoyote kuhusiana na mkopo uliotolewa kwa mtu kama huyo kama ilivyoelezwa kabla na mtu mwengine yoyote:

Isipokuwa kwamba hakuna kitu katika kifungu hiki kitakachotumika ama:-

(a) kwa jambo lolote lililofanywa na kampuni ambayo wakati huo ni kampuni binafsi yenye msamha; au

(b) kwa jambo lolote lililofanywa na kampuni tanzu, ambapo mkurugenzi ni kampuni yake ya hisa; au

(c) bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (2), kwa jambo lolote lililofanywa kumpa mtu yeyote kama ilivyoelezwa kabla fedha za kukimu matumizi yaliyofanywa au kwa kutumiwa na yeye kwa madhumuni ya kampuni au kwa madhumuni ya kumuwezesha kutekeleza vyema majukumu yake kama ofisa wa kampuni; au

(d) kwa kampuni ambayo shughuli zake za kawaida ni pamoja na kukopesha fedha au kutoa dhamana kuhusiana na mikopo iliyotolewa na watu wengine, kwa jambo lolote lililofanywa na kampuni katika mwenendo wa kawaida wa shughuli hiyo.

(2) Paragrafu (c) ya kifungu kidogo cha (1) haitaidhinisha kutoa mkopo wowote, au kuingia katika dhamana yoyote, au kutoa kinga yoyote, isipokuwa ama:-

(a) kwa kupata kibali cha kampuni kabla kilichotolewa katika mkutano mkuu ambao madhumuni ya matumizi na kiasi cha mkopo au kiwango cha dhamana au kinga, kama itakavyokuwa, kimebainishwa; au

(b) kwa sharti kwamba, ikiwa idhini ya kampuni haikutolewa kama ilivyoelezwa kabla katika au kabla ya mkutano mkuu wa mwaka unaofuata, mkopo utalipwa au dhima chini ya dhamana au kinga itaruhusiwa, kama itakavyokuwa, ndani ya miezi sita tangu mwisho wa mkutano huo.

(3) Endapo idhini ya kampuni haikutolewa kama inavyotakiwa na sharti lolote lile, wakurugenzi walioidhinisha utoaji wa mkopo, au kuingia katika dhamana, au utoaji wa kinga, watakuwa na dhima ya pamoja na ya mmoja mmoja kuifidia kampuni kwa hasara yoyote iliyotokana na hatua hiyo.

Idhini ya kampuni inahitajika kwa malipo kwa mkurugenzi kwa hasara ya kuacha wadhifa, n.k.

**205.** Si halali kwa kampuni kufanya kwa mkurugenzi wa kampuni yeyote malipo kwa njia ya fidia kwa hasara ya kuacha ofisi, au kama mazingatio kwa au kuhusiana na kustaafu kwake kutoka ofisi, isipokuwa maelezo kuhusiana na malipo yaliyopendekezwa (ikiwa ni pamoja na kiasi chake) yamewekwa wazi kwa wanachama wa kampuni na pendekezo kukubaliwa na kampuni.

Idhini ya kampuni inahitajika kwa malipo yoyote kuhusiana na uhaulishaji wa mali zake kwa mkurugenzi kwa hasara ya kuacha wadhifa, n.k.

**206.**-(1) Si halali kuhusiana na uhaulishaji wa yote au sehemu yoyote ya biashara au mali ya kampuni kwa ajili ya malipo yoyote yanayopaswa kufanywa kwa mkurugenzi yeyote wa kampuni kwa njia ya fidia kwa hasara ya kuacha ofisi, au kama mazingatio kwa au kuhusiana na kustaafu kwake kutoka ofisi, isipokuwa maelezo kuhusiana na malipo yaliyopendekezwa (ikiwa ni pamoja na kiasi chake) yamewekwa wazi kwa wanachama wa kampuni na pendekezo kukubaliwa na kampuni.

(2) Pale ambapo malipo yanayoelezwa hapa kuwa ni kinyume cha sheria yamefanywa na mkurugenzi wa kampuni, kiasi kilichopokewa kitachukuliwa kuwa kimepokewa na yeye kwa dhamana ya kampuni. Wajibu wa mkurugenzi kubainisha malipo kwa hasara ya kuacha wadhifa, n.k. yaliyofanywa kuhusiana na uhaulishajiwa hisa katika kampuni 207. (1) Pale ambapo, kuhusiana na uhaulishaji kwa watu wowote zote au yoyote ya hisa katika kampuni, ukiwa ni uhaulishaji uliosababishwa na:-

(a) fursa iliyotolewa na chombo cha jumla cha wamiliki wa hisa;

(b) fursa iliyotolewa na au kwa niaba ya shirika jengine kwa mtazamo kuwa kampuni itakuwa kampuni tanzu yake au kampuni tanzu ya kampuni yake ya hisa;

(c) fursa iliyotolewa na au kwa niaba ya mtu binafsi kwa lengo la kupata haki ya kutumia uwezo au kudhibiti uwezo wa si chini ya moja ya thuluthi moja ya nguvu ya kupiga kura katika mkutano wowote mkuu wa kampuni; au

(d) fursa nyengine yoyote ambayo ni sharti la kukubalika kwa kiwango fulani;

malipo yatapasa kulipwa kwa mkurugenzi wa kampuni kwa njia ya fidia kwa hasara ya kuacha ofisi, au kama mazingatio kwa au kuhusiana na kustaafu kwake kutoka ofisi, utakuwa ni wajibu wa mkurugenzi huyo kuchukua hatua zote zinazofaa kupata taarifa kuhusiana na malipo yaliyopendekezwa (ikiwa ni pamoja na kiasi chake) yataingizwa kwenye au kupelekwa na taarifa yoyote ya fursa iliyotolewa kwa ajili ya hisa zao, ambayo inatolewa kwa wamiliki wa hisa wowote.

(2) Iwapo:-

(a) mkurugenzi yeyote anashindwa kuchukua hatua zinazostahili kama ilivyoelezwa kabla; au

(b) mtu yeyote ambaye ametakiwa kwa utaratibu unaofaa na mkurugenzi yeyote kuingiza taarifa zilizoelezwa katika au kuzipeleka pamoja na taarifa yoyote kama ilivyoelezwa kabla anashindwa kufanya hivyo, atatozwa faini.

(3) Iwapo:-

(a) mahitaji ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hayakutekelezwa kuhusiana na malipo yoyote kama yalivyotajwa humo; au

(b) kufanywa malipo yaliyopendekezwa, kabla ya uhaulishaji wa hisa zozote katika kutekeleza fursa iliyotolewa, hakukuidhinishwa na mkutano ulioitishwa kwa madhumuni ya wamiliki wa hisa ambao wanahusiana na fursa iliyotolewa na wamiliki wengine wa hisa za daraaja sawa kama ya hisa zozote zilizoelezwa;

fedha zozote zilizopokewa na mkurugenzi kutokana na malipo hayo zitachukuliwa kuwa alizipokea kuwa dhamana kwa watu wowote ambao waliuza hisa zao kama matokeo ya fursa iliyotolewa, na gharama zilizotumiwa na yeye katika kusambaza fedha hizo miongoni mwa watu hao zitalipwa na yeye na hazitatokana na fedha hizo.

(4) Endapo wamiliki wa hisa waliotajwa katika paragrafu (b) ya kifungu kidogo cha (3) si wanachama wote wa kampuni na hakuna sharti lililowekwa na kanuni kwa ajili ya kuitisha au kuratibu mkutano huo kama ulivyotajwa katika paragrafu hiyo, masharti ya Sheria hii na ya kanuni za kampuni zinazohusiana na mikutano mikuu ya kampuni, kwa ajili hiyo, yatatumika kwa ajili ya mkutano ama bila mabadiliko au na marekebisho kama Waziri kwa maombi ya mtu yeyote anayehusika anavyoweza kuelekeza kwa madhumuni ya kuyaoanisha na mazingira ya mkutano.

(5) Iwapo katika mkutano ulioitishwa kwa madhumuni ya kuidhinisha malipo yoyote kama inavyotakiwa na paragrafu (b) ya kifungu kidogo cha (3) akidi haikutimia na, baada ya mkutano kuakhirishwa hadi tarehe ya baadaye, akidi haikutimia tena; malipo yatachukuliwa kwa madhumuni ya kifungu kidogo hicho kuwa yameidhinishwa.

Masharti ya nyongeza kwa vifungu vya 206, 207 na 208.

**208.**-(1) Pale ambapo katika mashauri ya kurudisha malipo yoyote yaliyopatika kwa mujibu wa kifungu cha 206(1) na (2) au vifungu vya 207(1) na (3) kwa dhamana, inabainishwa kwamba:-

(a) malipo yalifanywa katika kutekeleza mpango wowote uliokubaliwa kama sehemu ya mkataba kwa ajili ya uhaulishaji unaohusika au ndani ya mwaka mmoja kabla au miaka miwili baada ya kuwa mkataba huo au fursa iliyotolewa iliyopelekea hiyvo; na

(b) kampuni au mtu yeyote ambaye kwa ajili yake uhaulishaji alishiriki katika mpango huo;

malipo yatachukuliwa, ila kwa kadri itakapothibishwa kinyume chake, kuwa mojawapo ambayo vifungu vidogo vilivyotajwa vitatumika.

(2) Ikiwa kuhusiana na uhaulishaji wowote kama ulivyotajwa katika ama kifungu cha 206 au cha 207:-

(a) gharama ya kulipwa kwa mkurugenzi wa kampuni ambaye ofisi yake itafutwa au ambaye atastaafu kutoka ofisi kwa hisa zozote katika kampuni zinazomilikiwa na yeye ni zaidi ya bei ambayo ingeweza wakati huo kupatikana na wamiliki wengine wa hisa kama hizo; au

(b) mazingatio yanayofaa yametolewa kwa mkurugenzi yeyote kama huyo; ziada au thamani ya fedha ya mazingatio, kama itakavyokuwa, kwa madhumuni ya sehemu hiyo, yatafahamika kuwa malipo yaliyotolewa kwake kwa njia ya fidia kwa kupoteza ofisi au kama mazingatio kwa au kuhusiana na kustaafu kwake kutoka ofisi.

(3) Marejeo katika vifungu vya 205, 206 na 207 kuhusu malipo yaliyofanywa kwa mkurugenzi yeyote wa kampuni kwa njia ya fidia kwa kupoteza ofisi, au kwa mazingatio ya au kuhusiana na kustaafu kwake kutoka

ofisi, hayajumuishi malipo yoyote halali ya uharibifu uliotokana na uvunjaji wa mkataba au ya pensheni kuhusiana na huduma za nyuma, na kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki tamko "pensheni" linajumuisha posho la kustaafu, kiinua mgongo au malipo kama hayo.

(4) Hakuna chochote katika vifungu vya 206 na 207 kitakachochukuliwa kuathiri uendeshaji wa utawala wa sheria yoyote unaohitaji kutoa taarifa kuhusiana na malipo yoyote kama hayo kama yalivyotajwa humo au kuhusiana na malipo mengine yoyote kama hayo yaliyofanywa au yanayotaka kufanywa kwa wakurugenzi wa kampuni.

Daftari la umiliki wa hisa za wakurugenzi, n.k.

**209.**-(1) Kila kampuni itaweka daftari kuhusiana na kila mkurugenzi wa kampuni (amabyo si kampuni yake ya hisa) idadi, maelezo na kiasi cha hisa zozote katika au dhamana za kampuni au shirika jengine lolote, lililo kampuni tanzu ya kampuni au kampuni ya hisa, au kampuni tanzu ya kampuni ya hisa ya kampuni, ambazo zinamilikiwa na au dhamana kwa ajili yake au ambayo yeye ana haki yoyote kuwa mmiliki (kama kwa malipo au la):

Isipokuwa kwamba daftari halilazimiki kujumuisha hisa katika shirika lolote ambalo ni kampuni tanzu inayomilikiwa kamili na shirika jengine, na kwa madhumuni haya shirika litachukuliwa kuwa kampuni tanzu inayomilikiwa na nyengine kama halina wanachama isipokuwa lile shirika jengine na lile shirika jengine ni kampuni tanzu zinazomilikiwa kamili na ni zake au wateuliwa wake.

(2) Pale hisa zozote au dhamana zinarikodiwa au zinasita kurikodiwa katika daftari kuhusiana na mkurugenzi yeyote kwa sababu ya biashara alizofanya wakati yeye ni mkurugenzi, daftari pia litaonesha tarehe ya na gharama au mazingatio mengine kwa ajili ya biashara hiyo.

Isipokuwa kwamba pale ambapo hakuna muda kati ya makubaliano kwa ajili ya biashara yoyote na kukamilika kwake, tarehe itakuwa ile ya makubaliano.

(3) Aina na kiwango cha maslahi ya mkurugenzi au haki katika hisa zozote au dhamana zilizorikodiwa kuhusiana na yeye katika daftari lililoelezwa vitaoneshwa kama yeye anataka hivyo katika daftari.

(4) Kampuni haitaathiriwa na kitu chochote kilichofanyika kwa madhumuni ya kifungu hiki na taarifa ya au kuwekwa katika uchunguzi kuhusu haki ya mtu yeyote kuhusiana na hisa zozote au dhamana.

(5) Daftari lililoelezwa, bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, litahifadhiwa kwenye ofisi ya kampuni iliyosajiliwa na itakuwa wazi kwa ukaguzi wakati wa saa za kazi (chini ya vizuizi vinavyofaa kama kampuni inavyoweza kuweka kwa kanuni zake au katika mkutano mkuu, ili si chini ya saa mbili kila siku zitaruhusiwa kwa ajili ya ukaguzi) kama ifuatavyo: -

(a) katika kipindi kuanzia siku kumi na nne kabla ya tarehe ya mkutano mkuu wa mwaka wa kampuni na kuishia siku tatu baada ya tarehe ya kumalizika kwake, litakuwa wazi

kwa ukaguzi wa mwanachama yeyote au mmiliki wa dhamana za kampuni; na

(b) katika kipindi hicho au kipindi chochote chengine, litakuwa wazi kwa ukaguzi wa mtu yeyote kwa niaba ya Mrajis.

Katika kuheasbu siku kumi na nne na siku tatu zilizotajwa katika kifungu hiki siku yoyote ambayo ni Jumamosi au Jumapili au ni sikukuu ya umma au benki haitahesabiwa.

(6) Bila ya kuathiri haki zilizotolewa na kifungu kidogo cha (5), Mrajis anaweza wakati wowote kuhitaji nakala ya daftari alililoelezwa au sehemu yake yoyote.

(7) Daftari lililoelezwa pia litatolewa wakati wa kuanza mkutano mkuu wa mwaka wa kampuni na kubaki wazi na kupatikana wakati wa kuendelea na mkutano kwa mtu yeyote anayehudhuria kwenye mkutano.

(8) Kama ukiukaji umefanyika katika kutekeleza kifungu kidogo cha (7), kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye ameshiriki katika ukiukaji atatozwa faini na kama ukiukaji umefanywa katika kutekeleza kifungu kidogo cha (1) na cha (2) vya kifungu hiki au kama ukaguzi wowote unahitajika chini ya kifungu unakataliwa au nakala yoyote inayotakiwa humo haikupatikana ndani ya muda wa kuridhisha, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye ameshiriki katika ukiukaji, atatozwa faini na pia faini kwa ukikaji.

(9) Kwa ukiukaji wowote kama huo, mahakama inaweza kutoa amri kulazimisha ukaguzi wa haraka wa daftari.

(10) Kwa madhumuni ya kifungu hiki:-

(a) mtu yoyote kwa mujibu wa miongozo au maelekezo ambayo wakurugenzi wa kampuni wamezoea kutekeleza atachukuliwa kuwa mkurugenzi wa kampuni; na

(b) mkurugenzi wa kampuni atachukuliwa kushikilia, au kuwa na maslahi yoyote au haki katika au juu ya, hisa zozote au dhamana ikiwa shirika jengine zaidi ya kampuni inayozishikilia yao au ambayo ina maslahi hayo au haki katika au juu yao, na ama

(i) shirika au wakurugenzi wake wamezoea kutekeleza kulingana na miongozo yake au maelekezo; au

(ii) yeye ana haki ya kutumia au kudhibiti utumiaji wa thuluthi moja au zaidi ya nguvu ya kupiga kura katika mkutano wowote mkuu wa shirika hilo.

Maelezo katika hesabu za mishahara ya wakurugenzi, pensheni, n.k.

**210.-**(1) Katika hesabu zozote za kampuni zilizowasilishwa kwake katika mkutano mkuu, au katika taarifa iliyoambatanishwa nazo, chini na kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki, mtaoneshwa kwa kadiri ambavyo taarifa imo katika vitabu vya kampuni na nyaraka au ambavyo kampuni ina haki ya kupata taarifa hiyo kutoka kwa watu wanaohusika:-

(a) kiasi cha jumla cha malipo ya mishahara ya wakurugenzi;

(b) kiasi cha jumla cha malipo ya wakurugenzi cha pensheni au pensheni ya zamani; na

(c) kiasi cha jumla ya malipo ya fidia yoyote kwa wakurugenzi au wakurugenzi wa zamani kwa kutoka kwenye ofisi.

(2) Kiasi kinachopasa kuoneshwa chini ya paragrafu (a) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:-

(a) kitakuwa ni pamoja na mishahara yoyote iliyolipwa kwa au iliyopokewa na mtu yoyote kuhusiana na huduma yake alipokuwa mkurugenzi wa kampuni ya au kuhusiana na huduma zake wakati ni mkurugenzi wa kampuni, kama mkurugenzi wa kampuni tanzu yake yoyote au vyenginevyo kuhusiana na usimamizi wa masuala yoyote ya kampuni au kampuni yake tanzu; na

(b) kitatafautisha baina ya mishahara kuhusiana na huduma alipokuwa mkurugenzi, kama wa kampuni au kampuni yake tanzu, na malipo mengine;

Kwa madhumuni ya ya kifungu hiki tamko "mishahara" kuhusiana na mkurugenzi, ni pamoja na ada na asilimia, pesa zozote zilizolipwa kwa njia ya gharama, posho kwa kadiri ambavyo pesa hizo zinakatwa kwa kodi ya mapato katika Protect ya Fate mchango wowote uliolipwa kuhusiana naye chini ya mpango wowote wa pensheni na makadirio ya thamani ya fedha ya faida yoyote zilizopokewa na yeye vyenginevyo zaidi ya pesa taslimu.

(3) Kiasi kinachopasa kuoneshwa chini ya paragrafu (b) ya kifungu kidogo cha (1) kilichoelezwa:-

(a) hakitakuwa ni pamoja na pensheni yoyote iliyolipwa au iliyopokewa chini ya mpango wa pensheni kama mpango ni wa namna kwamba michango yake ni mikubwa ya kutosha kwa ajili ya kuudumisha mpango huo, lakini isipokuwa kama ilivyoelezwa kabla kitakuwa ni pamoja na pensheni yoyote iliyolipwa au kupokewa kuhusiana na huduma zozote za mkurugenzi au mkurugenzi wa zamani wa kampuni kama walivyotajwa katika kifungu kidogo cha (2), iwapo kwa au na yeye au, juu ya uteuzi wake au kwa utegemezi juu ya au uhusiano mwengine na yeye, kwa au na mtu mwengine yeyote; na

(b) kitatafautisha kati ya pensheni kuhusiana na huduma kama mkurugenzi, iwe wa kampuni au kampuni yake tanzu, na pensheni nyengine;

Kwa madhumuni ya kifungu hiki tamko "pensheni" ni pamoja na posho yoyote baada ya kustaafu, kiinua mgongo baada ya kustaafu au malipo yanayofanana na hayo, na tamko " mpango wa pensheni " maana yake ni mpango kwa ajili ya utoaji wa pensheni kuhusiana na huduma kama mkurugenzi au vyenginevyo ambao unadumishwa kamili au katika sehemu kwa njia ya michango, na tamko "mchango" kuhusiana na mpango wa pensheni maana yake ni malipo yoyote (ikiwa ni pamoja na mchango wa bima) yanayolipwa kwa madhumuni ya mpango na au kuhusiana na watu wanaotoa huduma ambayo pensheni itatolewa au inaweza kutolewa chini ya mpango huo, isipokuwa kwamba haijumuishi malipo yoyote kuhusiana na watu wawili au zaidi kama kiasi kinacholipwa kuhusiana na kila mmoja wao hakijuilikani.

(4) Kiasi kinachopasa kuoneshwa chini ya paragrafu (c) ya kifungu kidogo cha (1) kilichoelezwa:-

(a) kitajumuisha pesa zozote zilizoplipwa au kupokewa na mkurugenzi au mkurugenzi wa zamani kwa njia ya fidia kwa hasara ya kutoka kwenye ofisi kama mkurugenzi wa kampuni au kwa hasara, wakati ni mkurugenzi wa kampuni au juu ya au kuhusiana na kukoma kwake kuwa mkurugenzi wa kampuni au ofisi nyengine yoyote kuhusiana na kusimamia masuala ya kampuni au ya ofisi yoyote kama mkurugenzi au vyenginevyo kuhusiana na kusimamia masuala ya kampuni yake tanzu yoyote; na

(b) kitatafautisha kati ya fidia inayohusiana na ofisi ya mkurugenzi awe wa kampuni au wa kampuni yake tanzu, na fidia kuhusiana na ofisi nyengine;

na kwa madhumuni ya kifungu hiki marejeo kwenye fidia kwa hasara ya kutoka kwenye ofisi itajumuisha kulipwa kama mazingatio kwa au kuhusiana na kustaafu mtu kutoka ofisi.

(5) Kiasi kinachopasa kuoneshwa chini ya kila paragrafu ya kifungu kidogo cha (1) kilichoelezwa:-

(a) kitakuwa ni pamoja na pesa zote zilizolipwa na au kupokewa kutoka:-

(i) kwenye kampuni; na

(ii) kwenye kampuni tanzu za kampuni, na

(iii) mtu mwengine yeyote;

Isipokuwa pesa zinazopasa kutolewa maelezo kwa kampuni au kwa kampuni zake tanzu zozote au daraja yoyote ya wanachama hao; na

(b) kitatafautisha, kuhusu kiasi kinachopasa kuoneshwa chini ya paragrafu (c) ya kifungu kidogo cha (1) kilichoelezwa, kati ya kiasi kilicholipwa na au kupokewa kutoka kwenye kampuni, kampuni tanzu za kampuni na watu wengine zaidi ya kampuni tanzu.

(6) Viasi vinavyopasa kuoneshwa chini ya kifungu hiki kwa mwaka wa fedha wowote vitakuwa ni pesa zilizopokewa kuhusiana na mwaka huo, wakati wowote zilipolipwa, au kwa pesa ambazo hazikupokewa kuhusiana na kipindi, pesa zilizolipwa katika kipindi cha mwaka, hata hivyo, pale ambapo:-

(a) pesa zozote hazikuoneshwa katika hesabu kwa mwaka unaohusika wa fedha kwa msingi kuwa mtu aliyezipokea anapaswa kuzitolea maelezo kama ilivyoelezwa katika paragrafu (a) ya kifungu kidogo cha (5), lakini dhima hiyo baada ya hapo imeondolewa kabisa au sehemu au haitatekelezwa ndani ya kipindi cha miaka miwili; au

(b) pesa zozote zilizolipwa kwa njia ya posho la matumizi zimekatwa kwa Mamlaka ya Kodi baada ya mwisho wa mwaka unaohusika wa fedha;

pesa hizo kwa kiwango ambacho dhima iliondolewa au haikutekelezwa au zimelipwa kama ilivyoelezwa kabla, kama itakavyokuwa, hazitaoneshwa katika hesabu za kwanza ambazo inawezekana kuoneshwa, au katika taarifa iliyoambatanishwa humo, na zitatafautishwa na viasi vitakavyoonehwa humo bila sharti hili.

(7) Pale ambapo ni lazima kufanya hivyo kwa madhumuni ya kuonesha tafauti yoyote inayotakiwa na kifungu hiki kuoneshwa humo, wakurugenzi wanaweza kugawanya malipo yoyote kati ya mambo ambayo yamelipiwa au yamepokewa katika namna amabayo wanafikiri ni muafaka.

(8) Kama kuhusiana na hesabu zozote masharti ya kifungu hiki hayakutekelezwa, utakuwa ni wajibu wa wakaguzi wa kampuni ambao wanachunguza hesabu kwa pamoja kuingiza katika ripoti yao, kwa kadiri wanavyoweza kufanya hivyo, maelezo yanayoainisha taarifa zinazohitajika.

(9) Katika kifungu hiki marejeo yoyote ya kampuni tanzu:-

(a) Kuhusiana na mtu ambaye ni au alikuwa, wakati alipokuwa mkurugenzi wa kampuni, mkurugenzi pia, kwa mujibu wa uteuzi wa kampuni hiyo, moja kwa moja au si moja kwa moja, wa shirika jengine lolote, chini ya paragrafu inayofuata, itajumuisha shirika hilo, kama ni au lilikuwa au la kwa kweli ni kampuni tanzu ya kampuni; na

(b) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2) na cha (3) vya kifungu hiki itachukuliwa kumaanisha kampuni tanzu wakati huduma zilipokuwa zikitolewa, na kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki itachukuliwa kumaanisha kampuni tanzu mara kabla kutoka kwenye ofisi kama mkurugenzi wa kampuni.

Maelezo katika hesabu za mikopo kwa maofisa, n.k.

**211.-**(1) Hesabu ambazo, kwa mujibu wa Sheria hii, zinapaswa kuwasilishwa kwenye kila kampuni katika mkutano mkuu, bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, zitakuwa na taarifa zinazoonesha:-

(a) kiasi cha mikopo yoyote iliyotolewa katika mwaka:-

(i) ofisa yoyote wa kampuni; au

(ii) mtu yeyote ambaye, baada ya kutoa mkopo, anakuwa katika mwaka huo ofisa wa kampuni;

na kampuni au kampuni tanzu yake au na mtu mwengine yeyote chini ya dhamana kutoka au juu ya kinga inayotolewa na kampuni au kampuni tanzu yake (ikiwa ni pamoja na mikopo yoyote ambayo ililipwa katika mwaka huo); na

(b) kiasi cha mikopo yoyote iliyotolewa kwa namna iliyoelezwa kabla kwa ofisa yoyote au mtu yeyote kama ilivyoelezwa wakati wowote kabla ya mwaka wa fedha wa kampuni na deni wakati wa kumalizika kwake.

(2) Kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hakitahitajika kujumuishwa katika hesabu taarifa za:

(a) mkopo uliofanywa katika mwenendo wa kawaida wa shughuli za kampuni au kampuni tanzu yake, ambapo shughuli za kawaida za kampuni au kampuni tanzu yake, au itakavyokuwa, kampuni tanzu, ni pamoja na kukopesha fedha, au

(b) mkopo uliotolewa na kampuni au kampuni tanzu yake kwa mfanyakazi wa kampuni au kampuni tanzu, kama itakavyokuwa, kama mkopo hauzidi shilingi elfu arubaini na kuthibitishwa na wakurugenzi wa kampuni au kampuni tanzu, kama itakavyokuwa, kuwa umefanywa kwa mujibu wa utaratibu uliopitishwa au ambao utapitishwa na kampuni au kampuni tanzu kuhusiana na mikopo kwa wafanyakazi wake;

usiokuwa, katika hali yoyote, mkopo uliotolewa na kampuni chini ya dhamana kutoka au juu ya kinga inayotolewa na kampuni tanzu yake au mkopo uliotolewa na kampuni tanzu ya kampuni chini ya dhamana kutoka au juu ya kinga inayotolewa na kampuni au kampuni yake tanzu.

(3) Kama katika hesabu yoyote kama ilivyoelezwa kabla masharti ya kifungu hiki hayakutekelezwa, itakuwa ni wajibu wa wakaguzi wa kampuni ambao wanachunguza hesabu kwa pamoja kuingiza katika ripoti mizania ya kampuni, kadiri wanavyoweza kufanya hivyo, maelezo yanayofafanua taarifa zinazotakiwa.

(4) Marejeo katika kifungu hiki kwa kampuni tanzu yatachukuliwa kumaanisha kampuni tanzu katika mwisho wa mwaka wa fedha wa kampuni (kama ni kampuni tanzu au la katika tarehe ya mkopo).

Wajibu wa jumla wa kuweka bayana kwa madhumuni ya vifungu vya 210, 211 na 212.

**212.-**(1) Ni wajibu wa mkurugenzi wa kampuni yoyote kutoa taarifa kwa kampuni kuhusu masuala yanayohusiana na yeye mwenyewe kama itakavyolazimika kwa madhumuni ya vifungu vya 209 na 210 na ya kifungu cha 211 isipokuwa kwa kadiri vinavyohusiana na mikopo iliyotolewa na kampuni au na mtu mwengine yeyote chini ya dhamana kutoka au juu ya kinga inayotolewa na kampuni, kwa ofisa huyo.

(2) Taarifa yoyote itakayotolewa kwa madhumuni ya kifungu cha 209 itakuwa kwa maandishi, na kama haikuwasilishwa katika mkutano wa wakurugenzi, mkurugenzi anayeitoa atachukua hatua za kuridhisha kuhakikisha kuwa inaletwa na kusomwa katika mkutano unaofuatia wa wakurugenzi baada ya kutolewa.

(3) Kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kitatumika:-

(a) kwa madhumuni ya kifungu cha 210 kuhusiana na maofisa wengine zaidi ya wakurugenzi; na

(b) kwa madhumuni ya kifungu cha 210 na kifungu cha 211 kuhusiana na watu ambao ni au wamekuwa wakati wowote katika miaka mitano iliyotangulia maofisa; kama inavyotumika kuhusiana na wakurugenzi.

(4) Mtu yeyote ambaye anakiuka masharti yaliyotangulia ya kifungu hiki atatozwa faini.

Wakurugenzi kubainisha maslahi yao katika mikataba.

**213.-**(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, itakuwa ni wajibu wa mkurugenzi wa kampuni ambaye kwa njia yoyote, iwe moja kwa moja au si moja kwa moja ana maslahi katika mkataba au mkataba uliopendekezwa na kampuni kutangaza aina ya maslahi yake katika mkutano wa wakurugenzi wa kampuni.

(2) Kwa mkataba uliopendekezwa tamko linalotakiwa na kifungu hiki kutolewa na mkurugenzi litatolewa katika mkutano wa wakurugenzi ambao suala la kuingia katika mkataba linazingatiwa kwa mara ya kwanza, au kama mkurugenzi katika tarehe ya mkutano huo hakuwa na maslahi katika mkataba uliopendekezwa, katika mkutano unaofuatia wa wakurugenzi uliofanyika baada ya yeye kuwa na maslahi, na katika hali ambapo mkurugenzi anakuwa na maslahi katika mkataba baada ya kutiwa saini, tamko litatolewa katika mkutano wa kwanza wa wakurugenzi unaofanyika baada ya mkurugenzi kuwa na maslahi.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, taarifa ya jumla iliyotolewa kwa wakurugenzi wa kampuni na mkurugenzi kuhusu kwamba yeye ni mwanachama wa kampuni iliyoainishwa au shirika na kwamba anapasa kuchukuliwa kuwa ana maslahi katika mkataba wowote ambao unaweza, baada ya tarehe ya kutolewa taarifa, kuingiwa na kampuni hiyo au kampuni, litachukuliwa kuwa ni tamko la kutosha kuhusu maslahi kuhusiana na mkataba wowote uliotiwa saini.

Isipokuwa kwamba hakuna taarifa ya namna hiyo itakayokuwa na athari isipokuwa ama iwe imetolewa katika mkutano wa wakurugenzi au mkurugenzi awe amechukua hatua zinazostahili kuhakikisha kuwa inaletwa na kusomwa katika mkutano unaofuatia wa wakurugenzi baada ya kutolewa.

(4) Mkurugenzi yeyote ambaye atashindwa kutekeleza masharti ya kifungu hiki atatozwa faini.

(5) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachochukuliwa kuathiri utekelezaji wowote wa utawala wa sheria unaowazuia wakurugenzi wa kampuni kuwa na maslahi yoyote katika mikataba na kampuni.

Daftari la wakurugenzi na makatibu.

**214.**-(1) Kila kampuni itaweka katika ofisi yake iliyosajiliwa daftari la wakurugenzi wake na makatibu.

(2) Daftari litakuwa na maelezo yafuatayo kuhusiana na kila mkurugenzi, yaani:-

(a) kwa mtu binafsi, jina lake la kwanza la sasa na jina la ukoo au jina lolote la kwanza la zamani na jina la ukoo, anuani ya makaazi yake ya kawaida, utaifa wake, na kama utaifa wake si utaifa wa asili, utaifa wake wa asili, kazi yake, kama ipo, maelezo ya kurugenzi nyengine zozote alizoshikilia na, kwa kampuni chini ya kifungu cha 199, tarehe yake ya kuzaliwa; na

(b) kwa shirika, jina lake la kujiandikisha na ofisi yake iliyosajiliwa au ofisi kuu:

Isipokuwa kwamba haitakuwa lazima daftari kuwa na maelezo ya kurugenzi zilizoshikiliwa na mkurugenzi katika makampuni ambazo kampuni ni kampuni tanzu inayomilikiwa kamili, au ambazo ni kampuni tanzu zinazomilikiwa aidha ama za kampuni au kampuni nyengine ambayo ni kampuni tanzu inayomilikiwa kamili, na kwa madhumuni ya paragrafu hii, shirika litachukuliwa kuwa kampuni tanzu inayomilikiwa kamili na kampuni nyengine kama haina wanachama isipokuwa ile kampuni nyengine na kwamba ile kampuni tanzu inayomilikiwa kamili ya kampuni nyengine; na wateuliwa wake au wao.

(3) Daftari lililoelezwa litakuwa na taarifa zifuatazo kuhusiana na katibu au, ambapo kuna makatibu wa pamoja, kuhusiana na kila mmoja wao, yaani:-

(a) kwa mtu binafsi, jina lake la kwanza la sasa na jina la ukoo na jina la kabila lake, kama lipo, jina la kwanza la zamani na jina la ukoo na anuani ya makaazi yake ya kawaida; na

(b) kwa shirika, jina lake la kujiandikisha na ofisi za usajili.

(4) Kampuni ndani ya vipindi vilivyotajwa katika kifungu cha (5), itawasilisha kwa Mrajis marejesho katika fomu zilizowekwa zenye maelezo yaliyoainishwa katika daftari lililoelezwa na taarifa katika fomu iliyowekwa ya mabadiliko yoyote miongoni mwa wakurugenzi wake au kwa katibu wake au maelezo yoyote yaliyomo katika daftari, yanayobainisha tarehe ya mabadiliko.

(5) Vipindi vilivyotajwa katika kifungu kidogo cha (4) ni vifuatayo, yaani.

(a) kipindi ambacho marejesho yaliyoelezwa yanapaswa kuwasilishwa kitakuwa ni kipindi cha siku kumi na nne kutoka uteuzi wa wakurugenzi wa kwanza wa kampuni; na

(b) kipindi ambacho taarifa iliyoelezwa ya mabadiliko inapaswa kutumwa itakuwa siku kumi na nne tokea ilipotolewa.

(6) Daftari linalopaswa kuwekwa chini ya kifungu hiki wakati wa saa za kazi (chini ya vikwazo vinavyoridhisha kama kampuni inavyoweza kuweka kwa kanuni zake au katika mkutano mkuu, ili kwamba si chini ya saa mbili kila siku litaruhusiwa kwa ajili ya ukaguzi) litakuwa wazi kwa ukaguzi wa mwanachama yeyote wa kampuni bila malipo na wa mtu mwengine yeyote, kwa malipo kama vile kampuni inavyoweza kuagiza, kwa kila ukaguzi.

(7) Kama ukaguzi wowote unaohitajika chini ya kifungu hiki unakataliwa au kama kutakuwa na ukiukaji katika kutekeleza kifungu cha (1), (2), (3) au (4) vya kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

(8) Kwa ukataaji wowote, mahakama inaweza kutoa amri kulazimisha ukaguzi wa haraka wa daftari.

(9) Kwa madhumuni ya kifungu hiki:-

(a) mtu ambaye maelekezo na miongozo yake wakurugenzi wa kampuni wamezoea kutekeleza atachukuliwa kuwa ni mkurugenzi na ni ofisa wa kampuni;

(b) tamko "jina la kwanza" ni pamoja na lakabu;

(c) kwa mtu wa rika moja au mtu ambaye kwa kawaida hujuilikana kwa jina tafauti na jina lake la ukoo, tamko "jina la ukoo" linamaanisha cheo hicho;

(d) marejeo ya jina la kwanza la zamani au jina la ukoo halijumuishi:-

(i) kwa mtu wa rika moja au mtu ambaye kwa kawaida hujuilikana kwa jina tafauti na jina lake lake la ukoo, jina ambalo alijuilikana kabla ya kutumia au kupata cheo; au

(ii) kwa mtu mwengine yeyote, jina la kwanza la zamani au jina la ukoo ambapo jina hilo au jina la ukoo, lilibadilishwa au liliachwa kutumiwa kabla ya mtu anayeitwa jina hilo hajatimiza umri wa miaka kumi na nane au limebadilishwa au limeachwa kutumiwa kwa kipindi ambacho si chini ya miaka ishirini, au

(iii) kwa mwanamke aliyeolewa, jina au jina la ukoo ambalo yeye alikuwa anajuilikana kabla ya kuolewa.

Mikataba ya kazi ya wakurugenzi kuwa wazi kwa ukaguzi.

**215.-**(1) Chini ya masharti yafuatayo, kila kampuni itaweka katika mahali panapofaa:-

(a) kwa kila mkurugenzi ambaye mkataba wake wa kazi na kampuni ni wa maandishi, nakala ya mkataba huo;

(b) kwa kila mkurugenzi ambaye mkataba wake wa kazi na kampuni si wa maandishi, makubaliano ya maandishi yanayoainisha masharti yake; na

(c) kwa kila mkurugenzi ambaye ameajiriwa chini ya mkataba wa kazi na kampuni tanzu ya kampuni, nakala ya mkataba huo au, kama si wa maandishi, makubaliano ya maandihi yanayoainisha masharti yake.

(2) Nakala zote na makubaliano yanayowekwa na kampuni kulingana na kifungu kidogo cha (1) zitatunza mahali pamoja.

(3) Zifuatazo ni sehemu zinazofaa kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1):-

(a) ofisi iliyosajiliwa ya kampuni;

(b) mahali ambapo daftari la wanachama wake limewekwa (kama ni pengine zaidi ya ofisi yake iliyosajiliwa).

(4) Kila kampuni itawasilisha taarifa katika fomu iliyowekwa kwa Mrajis wa Kampuni kuhusu mahali ambapo nakala na mikataba zinawekwa kufuatana na kifungu kidogo cha (1), na mabadiliko yoyote katika mahali hapo, isipokuwa katika hali ambayo wakati wote zimehifadhiwa katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni.

(5) Kila nakala na makubaliano yanayotakiwa na kifungu kidogo cha (1) kuwekwa yatakuwa wazi kwa ukaguzi wa mwanachama yeyote wa kampuni bila ya malipo.

(6) Iwapo:-

(a) ukiukaji umefanywa katika kutekeleza kifungu kidogo cha (1); au

(b) ukaguzi unaotakiwa chini ya kifungu kidogo cha (5) unakataliwa; kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini na, kwa ukiukaji unaoendelea faini ya kila siku kwa ukiukaji.

(7) Katika hali ya kukataliwa ukaguzi unaotakiwa chini ya kifungu kidogo cha (5) wa nakala au mkataba, mahakama inaweza kutoa amri kulazimisha ukaguzi haraka wa nayaraka hizo.

(8) Kifungu kidogo cha (1) kitatumika kwa mabadiliko ya mkataba wa kazi wa mkurugenzi kama kinavyotumika kwa mkataba.

Mkataba wa ajira wa wakurugenzi wa zaidi ya miaka mitano.

**216.-**(1) Kifungu hiki kinatumika kuhusiana na muda wowote wa mkataba ambapo ajira ya mkurugenzi na kampuni ambayo yeye ni mkurugenzi au, ambapo yeye ni mkurugenzi wa kampuni ya hisa, ajira yake kuliko katika kampuni (kama ni chini ya makubaliano ya awali au chini ya mkataba mpya aliotiliana saini katika kuutekeleza huo), kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu ambao ajira:-

(a) hauwezi kuvunjwa na kampuni kwa taarifa; au

(b) unaweza kuvunjwa katika mazingira maalumu yaliyoainishwa.

(2) Katika hali yoyote ambapo:-

(a) mtu ameajiriwa au anataka kuajiriwa na kampuni chini ya makubaliano ambayo hayawezi kuvunjwa na kampuni kwa taarifa au yanaweza kuvunjwa katika mazingira maalumu tu; na

(b) zaidi ya miezi sita kabla ya kumalizika muda wa kipindi ambacho yeye ameajiriwa au anataka kuajiriwa, kampuni inaingia katika mkataba wa ziada (vyenginevyo kuliko kwa mujibu wa haki iliyotolewa na au chini ya makubaliano ya awali juu ya upande mwengine kwa makubaliano hayo) ambayo yeye anataka kuajiriwa na kampuni au, ambapo yeye ni mkurugenzi wa kampuni ya hisa ndani ya kikundi.

(3) Kifungu hiki kinatumika kama kwamba kwa kipindi ambacho yeye anataka kuajiriwa chini ya mkataba huo wa ziada paliongezwa kipindi zaidi sawa na kipindi ambacho hakijamalizika cha makubaliano ya awali.

(4) Kampuni haitaingiza katika mkataba muda kama uliotajwa katika kifungu kidogo cha (1), isipokuwa muda huo kwanza umekubaliwa kwa azimio la kampuni katika mkutano mkuu na, kwa mkurugenzi wa kampuni ya hisa, kwa azimio la kampuni katika mkutano mkuu.

(5) Hakuna idhini inayohitajika kutolewa chini ya kifungu hiki na shirika lolote isipokuwa liwe ni kampuni kwa maana ya Sheria hii, au kama ni kampuni tanzu inayomilikiwa kamili ya shirika lolote, popote lilipoandikishwa.

(6) Azimio la kampuni la kuidhinisha muda kama uliotajwa katika kifungu kidogo cha (1) halitapitishwa katika mkutano mkuu wa kampuni isipokuwa makubaliano ya maandishi yanayobainisha mkataba unaopendekezwa ulioingiza muda yanapatikana kwa ukaguzi wa wanachama wa kampuni; mote muwili:-

(a) katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni si chini ya siku kumi na tano zinazomalizika tarehe ya mkutano; na

(b) katika mkutano wenyewe.

(7) Muda ulioingizwa katika mkataba kinyume na kifungu hiki, kwa kiasi kwamba unakiuka sehemu hii, ni batili; na mkataba huo na, katika hali ambapo kifungu kidogo cha (2) kinatumika, mkataba wa awali unachukuliwa kuwa na muda unaoipa haki kampuni ya kuuvunja wakati wowote kwa kutoa taarifa inayofaa.

Taarifa katika nyaraka za biashara

**217.**-(1) Kila kampuni, katika nyaraka zote za shughuli ambazo jina la kampuni linaonekana juu au ndani yake ambazo zimetolewa au kupelekwa na kampuni kwa mtu yeyote katika sehemu yoyote ya nchi, itaeleza katika herufi zinazosomeka kuhusiana na kila mkurugenzi kama shirika, jina la shirika, na kuhusiana na kila mkurugenzi kama mtu binafsi, maelezo yafuatayo:-

(a) jina lake la sasa, au ufupisho wake, na majina ya ukoo ya sasa;

(b) majina yoyote ya zamani na majina ya ukoo;

Isipokuwa kwamba, kama hali maalumu imetokea ambayo inaifanya kwa maoni ya Mrajis kuwa na haja ya kutolewa msamaha, Mrajis anaweza, kwa amri kuutoa, chini ya masharti kama yatakavyoelezwa katika amri, msamaha wa yote au sehemu ya majukumu yaliyowekwa na kifungu hiki kidogo.

(2) Kama kampuni inakiuka katika kutekeleza kifungu hiki, kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji akitiwa hatiani kwa kila kosa atatozwa faini isiyozidi laki tano, na kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki, ambapo shirika ni ofisa wa kampuni, ofisa yeyote wa shirika atachukuliwa kuwa ofisa wa kampuni.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki:-

(a) tamko "mkurugenzi" linajumuisha mtu yeyote amabye maelekezo au miongozo yake wakurugenzi wa kampuni wamezoea kutekeleza na tamko "ofisa" litafahamika ipasavyo.

(b) tamko "ufupisho" ni pamoja na ufupisho unaotambuliwa wa jina, na paragrafu (b) na (c) za kifungu kidogo cha (9) cha kifungu cha 214 kitatumika kwa madhumuni ya kifungu hicho.

Kuepuka Masharti Katika Vifungu vya Mikataba Vinavyowa-ondoshea Maofisa Dhima Masharti kuhusu dhima za maofia na wakaguzi.

**218.** Bila kuathiri masharti yanayoyofuata, sharti lolote, kama limo katika kanuni za kampuni au katika mkataba wowote na kampuni au vyenginevyo, kwa ajili ya kumsamehe ofisa yeyote wa kampuni au mtu yeyote (kama ni ofisa wa kampuni au siye) aliyeajiriwa na kampuni kama mkaguzi kuepukana na, au kumfidia kwa, dhima yoyote ambayo kwa mujibu wa utawala wa sheria yoyote ingemuelekea kuhusiana na uzembe wowote, ukiukaji, ukwepaji wa wajibu au uvunjaji wa uaminifu ambao yeye anaweza kuingia hatiani kuhusiana na kampuni litakuwa batili.

Isipokuwa kwamba:-

(a) hakuna chochote katika kifungu hiki kitakchotumika kuizuia kampuni kununua na kudumisha kwa ofisa yeyote au mkaguzi bima ya dhima yoyote; na

(b) bila ya kujali kitu chochote katika sehemu hii, kampuni inaweza, kulingana na sharti lolote kama ilivyoelezwa, kumfidia ofisa yeyote au mkaguzi kwa dhima yoyote aliyoipata katika kutetea kesi yoyote, iwe ya madai au jinai ambayo hukumu imetolewa kumpendelea yeye au katika ambayo yeye ameachiwa huru au katika kuhusiana na maombi yoyote chini ya kifungu cha 261 ambapo unafuu imetolewa kwake na mahakama.

Utaratibu na Usuluhishi Uwezo wa kuelewana na wadai na wanachama.

**219.**-(1) Pale ambapo maelewano au utaratibu unapendekezwa kati ya kampuni na wadai wake au kundi lao lolote au kati ya kampuni na wanachama wake au kundi lao lolote, mahakama inaweza kutoa amri ya, kwa maombi katika njia ya muhtasari wa kampuni au mdai yoyote au mwanachama wa kampuni, au, katika hali ya kampuni kuvunjwa, na mfilisi, kuitisha mkutano wa wadai au kundi la wadai, au wa wanachama wa kampuni au kundi la wanachama, kama itakavyokuwa, kwa namna mahakama itakavyoelekeza.

(2) Kama wengi kwa idadi wanaowakilisha robo tatu katika thamani ya wadai au kundi la wadai au wanachama au kundi la wanachama, kama itakavyokuwa, waliohudhuria na kupiga kura ama wenyewe au kwa kutumia wakala katika mkutano huo, kukubaliana na maelewano yoyote au utaratibu, maelewano hayo au utaratibu huo, ikiwa ulithibitishwa na mahakama, utakuwa na nguvu za kisheria juu ya wadai wote au kundi la wadai, au juu ya wanachama au kundi la wanachama, kama itakavyokuwa, na pia juu ya kampuni au, katika hali ya kampuni kuvunjwa, juu ya mfilisi na matawi ya kampuni.

(3) Amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki haitakuwa na athari hadi nakala ya kanuni iliyothibitishwa ya amri imewasilishwa kwa Mrajis kwa ajili ya usajili, na nakala ya kila amri hiyo itaambatanishwa kwenye kila nakala ya mkataba ya kampuni uliotolewa

baada ya amri kutolewa, au katika hali ya kampuni kufungwa, kwa mfilisi na matawi ya kampuni.

(4) Kama kampuni inakiuka katika kutekeleza kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa kila nakala ambayo ukiukaji umefanywa.

(5) Katika kifungu hiki na katika kifungu cha 220 tamko "kampuni" lina maana ya kampuni yoyote inayoweza kuvunjwa chini ya Sheria hii, na tamko "utaratibu" ni pamoja na ugawaji mpya wa mtaji wa hisa wa kampuni kwa uunganishaji wa hisa za daraja zote tafauti au kwa ugawanyaji wa hisa katika hisa za daraja mbali mbali au kwa njia hizo zote mbili.

Taarifa kuhusu kuelewana na wadai na wanachama.

**220.-**(1) Pale ambapo mkutano wa wadai au kundi la wadai au wa wanachama au kundi la wanachama unaitishwa chini ya kifungu cha 219:-

(a) pamoja na kila taarifa inayoitisha mkutano ambayo inapelekwa kwa mdai au mwanachama, yatapelekwa pia maelezo yanayofafanua athari za mapatano au utaratibu na hasa kufafanua maslahi yoyote ya wakurugenzi wa kampuni hiyo, ama kama wakurugenzi au kama wanachama au kama wa kampuni au vyenginevyo, na athari iliyopo ya mapatano au utaratibu; na, kadiri ambavyo ni tafauti na athari katika maslahi kama hayo ya watu wengine.

(b) katika kila taarifa inayoitisha mkutano ambayo inatolewa kwa tangazo, pataingizwa ama taarifa hiyo kama ilivyoelezwa awali au taarifa ya mahali ambapo na namna ambayo wadai au wanachama na wenye haki ya kuhudhuria mkutano wanaweza kupata nakala ya taarifa hiyo kama ilivyoelezwa awali.

(2) Pale ambapo maelewano au utaratibu unaathiri haki za wamiliki wa hisa za kampuni, taarifa iliyoelezwa itatoa maelezo yanayolingana kuhusiana na wadhamini wa hati yoyote kwa ajili ya kuhakikisha utoaji dhamana kama inavyohitajika kutolewa kuhusiana na wakurugenzi wa kampuni.

(3) Endapo taarifa iliyotolewa kwa tangazo ni pamoja na taarifa kuwa nakala za maelezo yanayoeleza athari za mapatano au utaratibu uliopendekezwa zinaweza kupatikana na wadai au wanachama na wenye haki ya kuhudhuria kwenye mkutano huo, kila mdai au mwanachama atakuwa, akipeleka maombi katika namna iliyoelezwa na taarifa, atapewa na kampuni bila ya malipo nakala ya taarifa hiyo.

(4) Endapo kampuni inakiuka katika kutekeleza matakwa yoyote ya kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini, na kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki mfilisi yeyote wa kampuni na mdhamini yeyote wa hati kwa ajili ya kuhakikisha utoaji wa dhamana za kampuni atachukuliwa kuwa ni ofisa wa kampuni.

Isipokuwa kwamba mtu huyo hatakuwa na dhima chini ya kifungu kidogo hiki ikiwa mtu huyo ataonesha kuwa ukiukaji ulitokana na kukataa mtu mwengine yeyote, akiwa mkurugenzi au mdhamini wa wamiliki wa dhamana, kusambaza taarifa zilizolazimika kwa maslahi yake.

(5) Ni wajibu wa mkurugenzi yeyote wa kampuni na wa mdhamini yeyote wa wamiliki wa dhamana za kampuni kutoa taarifa kwa kampuni kuhusu masuala yanayomhusu yeye mwenyewe kama inavyoweza kulazimika kwa madhumuni ya kifungu hiki, na mtu yeyote ambaye anakiuka katika kutekeleza kifungu kidogo hiki atatozwa faini.

Masharti kuhusu kurahisisha uundaji upya na uunganishaji wa kampuni.

**221.-**(1) Pale ambapo maombi yamepelekwa mahakamani chini ya kifungu cha 219 kusitishwa maelewano au utaratibu uliopendekezwa kati ya kampuni na watu wowote kama waliotajwa katika kifungu hicho, na imeoneshwa mahakamani kwamba maelewano au utaratibu umependekezwa kwa madhumuni ya au kuhusiana na mpango kwa ajili ya uundaji upya wa kampuni yoyote au kampuni zozote au uunganishaji wa kampuni zozote mbili au zaidi, na kwamba chini ya mpango huo zote au sehemu yoyote ya ahadi au mali ya kampuni yoyote inayohusika katika mpango (katika kifungu hiki inayojuilikana kama "kampuni inayohaulisha") inataka kuhamishiwa kwenye kampuni nyengine (katika kifungu hiki inayojuilikana kama "kampuni inayohaulishiwa"), mahakama inaweza, ama kwa amri inayozuia maelewano au utaratibu au kwa amri yoyote ya baadaye, kuweka sharti kwa yote au lolote kwa mambo yafuatayo:-

(a) uhaulishaji kwa kampuni inayohaulishiwa wa yote au sehemu yoyote ya ahadi na ya mali au madeni ya kampuni yoyote inayohaulisha;

(b) utoaji au umilikaji na kampuni inayohaulishiwa ya hisa zozote, dhamana, sera au maslahi mengine kama hayo katika kampuni hiyo ambayo chini ya mapatano au utaratibu yanataka kutolewa au kumilikiwa na kampuni hiyo kwa au kwa ajili ya mtu yeyote;

(c) uendelezaji na au dhidi ya kampuni inayohaulishiwa wa kesi yoyote inayosubiri na au dhidi ya kampuni yoyote inayohaulisha;

(d) ufutaji, bila kuvunjwa, wa kampuni yoyote inayohaulisha;

(e) kuweka sharti kwa mtu yeyote, ambaye ndani ya muda na kwa namna kama mahakama inavyoelekeza, kujitoa kwenye maelewano au utaratibu;

(f) masuala ya muafaka, ya matokeo na ya nyongeza yanayolazimika kuhakikisha kwamba uundaji upya au uunganishaji utatekelezwa kikamilifu na kwa ufanisi.

(2) Iwapo amri chini ya kifungu hiki inaweka sharti kwa ajili ya uhaulishaji wa mali au madeni, mali hiyo, kwa mujibu wa amri, itahaulishwa kwa na kuwekwa katika, na madeni hayo, kwa mujibu wa amri, yatahaulishwa kwa na kuwa madeni ya kampuni iliyohaulishiwa, na kwa

mali yoyote, kama amri inaelekeza hivyo, itaondolewa malipo yoyote ambayo kwa mujibu wa mapatano au utaratibu yatasita kuwa na athari.

(3) Iwapo amri imetolewa chini ya kifungu hiki, kila kampuni ambayo imetolewa amri hiyo itatayarisha nakala iliyothibitishwa ya hati yake ya kupelekwa kwa Mrajis kwa ajili ya usajili ndani ya siku saba baada ya kutolewa amri, na kama ukiukaji utafanywa katika kutekeleza kifungu kidogo hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

(4) Katika kifungu hiki tamko "mali" ni pamoja na mali, haki na uwezo wa namna yoyote, na tamko "madeni" ni pamoja na wajibu.
(5) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu cha 219, tamko "kampuni" katika kifungu hiki ni pamoja na kampuni yoyote nyengine zaidi ya kampuni ndani ya maana ya Sheria hii.

Uwezo wa kumiliki hisa za wamiliki wa hisa wanaojitoa kwenye mpango au mkataba uliokubaliwa na wengi.

**222.-**(1) Pale ambapo mpango au mkataba unaohusu uhaulishaji wa hisa au daraja la hisa katika kampuni (katika kifungu hiki inajuilikana kama "kampuni inayohaulisha") kwa kampuni nyengine, kama ni kampuni ndani ya maana ya Sheria hii au siyo (katika kifungu hiki inajuilikana kama "kampuni tinayohaulishiwa"), ndani ya miezi minne baada ya kutoa kwa ajili hiyo na kampuni inayohaulishiwa umekubaliwa na wamiliki si chini ya sehemu tisa katika kumi katika thamani ya hisa ambazo zinahusika katika uhaulishaji (zaidi ya hisa ambazo tayari zinamilikiwa katika tarehe ya kutoa na, au na mteuliwa kwa, kampuni inayohaulishiwa au kampuni yake tanzu), kampuni inayohaulishiwa inaweza, wakati wowote ndani ya miezi miwili baada ya kumalizika muda wa miezi minne ulioelezwa, kutoa taarifa katika namna iliyowekwa kwa mmiliki yeyote wa hisa aliyejitoa kwamba inataka kuchukua hisa zake, na wakati taarifa hiyo inapewa kampuni inayohaulishiwa itakuwa, isipokuwa kwa maombi yaliyotolewa na mmiliki wa hisa aliyejitoa ndani ya mwezi mmoja kutoka tarehe ambayo ilipewa taarifa mahakama inadhani inafaa kuamuru vyenginevyo, na haki na wajibu wa kuzichukua hisa hizo kwa masharti ambayo, chini ya mpango au mkataba, hisa za wamiliki wa hisa waliokubali zitahamishiwa kwenye kampuni iliyohamishiwa.

Isipokuwa kwamba ambapo hisa katika kampuni inayohaulisha za draja lile lile au daraja zile zile kama hisa ambazo uhaulishaji umehusu tayari zinamilikiwa kama ilivyoelezwa awali kwa thamani kubwa iliyozidi kwa moja ya kumi ya jumla ya thamani yao na ile ya hisa (zaidi ya zile ambazo tayari zinamilikiwa kama ilivyoelezwa) ambazo zimehaulishwa, masharti yaliyotangulia ya kifungu kidogo hiki hayatatumika isipokuwa:-

(a) kampuni iliyohaulishiwa inatoa masharti sawa kwa wamiliki wote wa hisa (zaidi ya wale ambao tayari wanamiliki kama ilivyoelezwa awali) ambazo zimehaulishwa, au ambapo hisa hizo ni pamoja na hisa za daraja tafauti ya kila daraja yao; na

(b) wamiliki ambao wanakubali mpango kuliko mkataba, pamoja na kumiliki si chini ya sehemu tisa katika kumi ya thamani za hisa (zaidi ya zile ambazo tayari

zinamilikiwa kama ilivyoelezwa awali) ambazo zimehamishwa, si chini ya robo tatu ya idadi ya wamiliki wa hisa hizo.

(2) Pale ambapo katika kutekeleza mpango wowote au mkataba kama ilivyoelezwa, hisa katika kampuni zinahamishiwa kwenye kampuni nyengine au mteuliwa wake, na hisa hizo pamoja na hisa nyengine zozote katika kampuni iliyotajwa kwanza zinazomilikiwa na, au na mteuliwa kwa niaba ya, kampuni inayohaulishiwa au kampuni yake tanzu katika tarehe ya uhaulishaji ina au inajumuisha sehemu tisa katika kumi ya thamani za hisa katika kampuni iliyotajwa kwanza au ya daraja yoyote ya hisa hizo, basi:-

(a) kampuni iliyohaulishiwa ndani ya mwezi mmoja tokea tarehe ya uhaulishaji (isipokuwa juu ya uhaulishaji uliopita katika kutekeleza mpango au mkataba tayari umetekeleza matakwa haya) itatoa taarifa kuhusu uhaulishaji huo kwa namna ambayo imewekwa kwa wamiliki wa hisa zilizobaki au wa hisa zilizobaki za daraja hiyo, kama itakavyokuwa, ambao hawakujitoa katika mpango au mkataba; na

(b) mmiliki yeyote anaweza ndani ya miezi mitatu kutoka tarehe aliyopewa taarifa kuitaka kampuni inayohaulishiwa kuchukua hisa zinazohusika;

na ambapo mmiliki wa hisa anatoa taarifa chini ya paragrafu (b) ya kifungu kidogo hiki kuhusiana na hisa yoyote, kampuni inayohaulishiwa itakuwa na haki na wajibu wa kuchukua hisa hizo kwa masharti ambayo chini ya mpango au mkataba hisa za wamiliki wa hisa waliokubali zilihamishiwa kwake, au kwa masharti mengine kama yanavyoweza kukubaliwa au kama mahakama kwa maombi ama ya kampuni inayohaulishiwa au mmiliki wa hisa itakavyoona inafaa.

(3) Pale ambapo taarifa imetolewa na kampuni inayohaulishiwa chini ya kifungu kidogo cha (1) na mahakama, kutokana na maombi yaliyotolewa na mmiliki wa hisa alaiyejitoa, haikuamuru vyenginevyo, kampuni iliyohaulishiwa, baada ya kumalizika muda wa mwezi mmoja kutoka tarehe ambayo taarifa ilitolewa, au, kama ombi kwenye mahakama hiyo la mmiliki wa hisa aliyejitoa linasubiri, baada ya maombi kukataliwa, itapeleka nakala ya taarifa kwa kampuni inayohaulisha pamoja na hati ya uhaulishaji iliyotekelezwa kwa niaba ya mmiliki wa hisa na mtu yeyote aliyeteuliwa na kampuni inayohaulishiwa na kwa niaba yake mwenyewe na kampuni inayohaulishiwa, na kulipa au kuhaulisha kwa kampuni inayohaulisha kiasi au mazingatio mengine yanayowakilisha bei inayolipwa na kampuni inayohaulishiwa kwa hisa ambazo kwa mujibu wa kifungu hiki kampuni hiyo ina haki ya kupata, na kampuni inayohaulisha baada ya hapo itaisajili kampuni iliyohamishiwa kama mmiliki wa hisa hizo.

Isipokuwa kwamba hati ya uhaulishaji haitahitajika kwa ajili ya hisa yoyote ambayo kwayo waranti wa hisa kwa wakati huo haujalipwa.

(4) Pesa zozote zilizopokewa na kampuni inayohaulisha chini ya kifungu hiki zitalipwa katika akaunti tafauti ya benki, na pesa zozote na mazingatio mengine yoyote yaliyopokewa yatamilikiwa na kampuni kama dhamana kwa watu kadhaa wenye haki ya hisa zinazohusiana na pesa zilizoelezwa au mazingatio mengine yalipokewa.

(5) Katika kifungu hiki, tamko "mmiliki wa hisa aliyejitoa" ni pamoja na mmiliki wa hisa ambaye haukuridhia mpango au mkataba na mmiliki wa hisa yeyote ambaye ameshindwa au alikataa kuhaulisha hisa zake kwa kampuni inayohaulishiwa kwa mujibu wa mpango au mkataba.

Wachache Suluhisho mbadala kuhusu kuivunja kampuni utokeapo uoneaji.

**223.-**(1) Mjumbe yeyote wa kampuni ambaye analalamika kwamba mambo ya kampuni yanafanywa kwa njia ya kikandamizaji kwa baadhi ya sehemu ya wanachama (ikiwa ni pamoja na yeye mwenyewe) au, katika suala linaloangukia ndani ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 176, anaweza kupeleka maombi mahakamani kwa njia ya rufaa kwa ajili ya kutolewa amri chini ya kifungu hiki.

(2) Kama katika rufaa yoyote mahakama inaona kwamba:-

(a) mambo ya kampuni yanafanywa kama ilivyoelezwa awali; na

(b) kuivunja kampuni kungeathiri sehemu hiyo ya wanachama, lakini vyenginevyo matukio yangehalalisha utoaji wa amri ya uvunjaji kwa misingi kuwa ilikuwa ni haki na usawa kwamba kampuni lazima ivunjwe;

mahakama inaweza, kwa nia ya kumaliza masuala yaliyolalamikiwa, kutoa amri kama inavyoona inafaa, kama kwa ajili ya kurekebisha uendeshaji wa mambo ya kampuni katika siku zijazo, au kwa ajili ya ununuzi wa hisa za wanachama wowote wa kampuni na wanachama wengine wa kampuni au na kampuni na, katika hali ya ununuzi na kampuni, kwa ajili ya kupunguza ipasavyo mtaji wa kampuni, au vyenginevyo.

(3) Iwapo amri chini ya kifungu hiki inafanya mabadiliko yoyote katika au kuongeza chochote katika mkataba wowote wa kampuni au kanuni, basi, bila ya kujali kitu chochote katika kifungu chengine chochote cha Sheria hii lakini bila ya kuathiri masharti ya amri, kampuni inayohusika haitakuwa na uwezo bila idhini ya mahakama ya kufanya mabadiliko yoyote zaidi katika au kuongeza kwenye mkataba au kanuni ambayo hayalingani na amri iliyotolewa, lakini, bila ya kuathiri masharti yaliyotangulia ya kifungu hiki kidogo, mabadiliko au nyongeza yaliyofanywa na amri yatakuwa na atahri sawa kama kwamba yamefanywa kihalali kwa azimio la kampuni na masharti ya Sheria hii yatatumika kwa mkataba au kanuni kama zilizvyobadilishwa au kuongezwa ipasavyo.

(4) Nakala iliyothibitishwa ya amri yoyote chini ya kifungu hiki inayobadilisha au kuongeza, au kutoa ruhusa ya kubadilisha au kuongeza, mkataba wa kampuni au kanuni, ndani ya siku kumi na nne baada ya kufanya hivyo, itawasilishwa na kampuni kwa Mrajis kwa usajili na kama kampuni

inakiuka katika kutekeleza kifungu kidogo hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini.

(5) Ombi chini ya kifungu hiki, halitazuia haki yoyote ya mdai au mchangiaji ya kuwa na kampuni kuvunjwa na mahakama chini ya Sheria ya Ufilisi, lakini kwa ombi la mchangiaji mahakama lazima iridhike kwamba haki za wachangiaji zitaathiriwa na ombi chini ya kifungu hiki.

## SEHEMU YA VII
## UFUNGAJI WA KAMPUNI KWA HIARI YA WAJUMBE

Maazimio kwa, na kuanza kwa, ufungaji wa hiari Mazingira ambayo kampuni inaweza kufungwa kwa hiari.

**224.**-(1) Kampuni inaweza kufungwa kwa hiari :-

(a) kwa muda (wowote) uliowekwa kwa mijibu wa kanuni za kampuni kutokana na kipindi hicho kumalizika, au tukio (lolote) linapotokea, matokeo yaliyoorodheshwa na kampuni ya kuvunjika kwake, na azimio la hiari la kuifunga kampuni lililopitishwa katika mkutano mkuu wa kampuni;

(b) iwapo kampuni itafungwa kwa kupitishwa azimio maalum la hiari.

(c) iwapo kampuni itafungwa kwa kupitishwa azimio maalum kutokana na sababu za madeni na kutoweza kuendelea na biashara, na kushauriwa kuifunga kampuni hiyo.

(2) Katika sheria hii ufafanuzi wa "azimio la ufungaji wa hiari wa kampuni" maana yake ni azimio lililoptishwa chini ya kijifungu cha (1).

(3) Azimio lililopitishwa chini ya mstari (a) wa kijifungu kidogo cha (1), vilevile katika azimio maalumu chini ya mstari (b) na azimio la ziada chini ya mstari (c), yatapelekwa na kusajiliwa na mrajis wa makampuni ndani ya kipindi cha siku 15.

Ilani ya azimio la kufunga.

**225.**-(1) Pale ambapo kampuni imepitisha azimio la kuifunga kampuni hiyo kwa hiari, ndani ya kipindi cha siku 14 baada ya kupitisha azimio hilo, itato notisi ya kulitangaza azimio hilo katika gazeti.

(2) Iwapo kampuni itashindwa kutekeleza masharti ya kifungu hichi, kampuni na kila afisa atawajibika kwa kosa hilo na kulipa faini, na kulipa faini ya kila siku kwa kuendelea na kosa hilo.
Kwa madhumuni ya kijifungu hichi mfilisi(mfunga hesabu) atajulikana kama ni afisa wa kampuni.

Kuanza ufungaji.

**226.**-(1) Ufungaji wa kampuni kwa hiari utachukuliwa umeanza wakati wa upitishaji wa azimio la ufungaji huo.

Matokeo ya azimio la ufungaji wa kampuni Kuepusha kuhamisha hisa, n.k. baada ya azimio la kufunga.

**227.** Kwa kesi ya ufungaji wa kampuni kwa hiari, kampuni kuanzia siku ya ufungaji huo itasita kuendesha biashara zake isipokuwa inaweza kutakiwa kufanya hivyo kwa faida ya ufungaji huo.

Imefafanuliwa kwamba, mamlaka na ushirika wa kampuni bila ya kuathiri chochote katika masharti yake, kampuni itaendelea hadi itakapokuwa imevunjwa.

**228.** Uhaulishaji wowote wa hisa, zilizokuwa hazijafanyiwa uhaulishaji, au pamoja na kizuizi cha mfilisi, na mabadiliko yoyote yaliyopo ya wajumbe wa kampuni, yaliyofanywa baada ya muda wa uanzaji wa ufungaji wa kampuni kwa hiari, ni batili.

Azimio la kulipa madeni Kiapo cha kufilisika.

**229.** Inapotokea kupendekezwa kufungwa kampuni kwa hiari, wakurugenzi (au, inapotokea kampuni ina zaidi ya wakurugenzi wawili, wengi wao) wanaweza kufanya mkutano wa wakurugenzi kuazimia kisheria kwa kufanya ukaguzi ndani ya masuala yote ya kampuni na baada ya kufanya hivyo watatoa pendekezo kwamba kampuni itaweza kulipa madeni yake yote, pamoja na kiwango halisi cha riba, ndani ya kipindi kisichozidi miezi 12 kuanzia siku ya ufungaji, kama ilivyoelezwa katika azimio.

(2) Azimio hilo la wakurugenzi halitokuwa na athari kwa sheria hii isipokuwa -

(a) limefanywa ndani ya wiki 5 mara tu baada ya tarehe iliyopitishwa kwa azimio la kuifunga kampuni, au kwa tarehe hiyo lakini kabla ya kupitishwa kwa azimio na;

(b) imejumuisha maelezo ya mali na madeni ya kampuni kwa kipindi cha mwisho wa utekelezaji kabla ya kufanywa kwa azimio.

(3) Azimio litapelekwa kwa mrajis wa makampuni kabla ya kumalizika kwa siku 15 mara tu kufuatia tarehe ambayo azimio limepitishwa.

(4) Mkurugenzi yoyote anaeazimia chini ya kifungu hichi bila ya kuwa na sababu za msingi kwa pendekezo kwamba kampuni italipa madeni yake yote, pamoja kiwango halisi cha riba, ndani ya kipindi kilichowekwa atawajibika kwa kosa na kutumikia kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miaka miwili, au kutozwa faini isiyopungua shilingi laki sita na isiyozidi shilingi milioni mbili, au zote.

(5) Iwapo kampuni imefungwa kwa mujibu wa azimio lililopitishwa ndani ya wiki 5 baada ya kufanya azimio, na madeni yake (pamoja kiwango halisi cha riba) hayajalipwa au kutolewa yote ndani ya kipindi kilichowekwa, itachukuliwa (isipokuwa itaoneshwa vyenginevyo) kwamba mkurugenzi hajawa na sababu za msingi kwa pendekezo lake.

(6) Iwapo azimio limetakiwa chini ya kijifungu cha (3) kuwasilishwa kwa mrajis na haliwasilishwa ndani ya kipindi kilichowekwa na kijifungu hicho, kampuni na kila afisa atawajibika kwa kosa kwa kulipa faini na atalipa faini kwa kila siku kwa kuendelea kuvunja masharti hayo.

**230.** Inapotokea ufungaji wa kampuni ambao umefanywa na kuazimiwa na wakurugenzi kisheria chini ya kifungu cha 229 ni " ufungaji wa hiari wa kampuni kwa wajumbe"; na inapotokea ufungaji wa kampuni ambao haujafanywa kwa mujibu wa azimio ni "ufungaji wa hiari wa kampuni kwa wadai".

Tofauti baina ya ufungaji wa hiari wa "wajumbe" na "wadai".

**231.**-(1) Katika ufungaji wa kampuni kwa hiari ya wajumbe, kampuni katika mkutano mkuu itateua mfunga hesabu mmoja au zaidi kwa madhumuni ya kufunga shughuli za kampuni na mgawanyo wa mali zake.

Uteuzi wa mfunga hesabu.

(2) Uteuzi wa mfunga hesabu utapelekea uwezo wote wakurugenzi kusitia, isipokuwa pale ambapo kampuni katika mkutano mkuu au mfunga hesabu ataondosha vikwazo vya kuendelea kwao.

**232.**-(1) Kama nafasi itakuwa wazi kwa kifo, au vinginevyo katika ofisi ya mfunga hesabu alieteuliwa na kampuni, kampuni katika mkutano mkuu inaweza, chini ya makubaliano na wadai wake, kujaza nafasi.

Uwezo wa kujaza nafasi katika ofisi ya mfunga hesabu.

(2) Kwa madhumuni hayo mkutano mkuu utaitishwa na mchangiaji yeyote au, kama kulikuwa na zaidi ya mfunga hesabu mmoja, na wafunga hesabus wanaoendelea.

(3) Mkutano utafanyika katika namna zinazoelezwa na Sheria hii au katiba, au kwa namna kama vile, juu ya maombi ya mchangiaji yoyote au kwa wafunga hesabu wanaondelea, utaamuliwa na Mahakama.

**233.**-(1) Katika tukio la kufunga kampuni lenye kuendelea kwa zaidi ya mwaka mmoja, mfunga hesabu ataitisha mkutano mkuu wa kampuni katika mwisho wa mwaka wa kwanza kuanzia ufungaji ulipoanza, na kila mwaka unaofuata, au siku itakayoonekana infaa ndani ya miezi 3 kutoka mwisho wa mwaka au muda mwengine ambao Waziri inaweza kuruhusu.

Mkutano mkuu wa kampuni katika kila mwisho wa mwaka.

(2) Mfunga hesabu atawasilisha katika mkutano hesabu za kazi alizozifanya, na utekelezaji wa kazi za ufungaji, katika mwaka unaofuata;

(3) Kama mfunga hesabu itashindwa kuzingatia kifungu hiki, atatozwa faini.

**234.**-(1) Mara baada ya kampuni kufungwa kikamilifu, mfunga hesabu ataweka hesabu za kuifunga kampuni, kuonyesha jinsi kazi ilivyofanywa na mali za kampuni zilivyokusanywa, na baadae kuitisha mkutano mkuu wa kampuni kwa lengo la kutoa hesabu, na kutoa maelezo yake.

Mkutano wa mwisho kabla ya kufutwa.

(2) Mkutano utaitishwa kwa tangazo katika Gazeti Rasmi, linalobainisha wakati wake, mahali na malengo na kuchapishwa angalau mwezi mmoja kabla ya mkutano.

(3) Ndani ya wiki moja baada ya mkutano, mfunga hesabu atatuma kwa Mrajis wa Makampuni nakala ya hesabu, na atawasilisha kwake kumbukumbu za mkutano na tarehe yake.

(4) Iwapo nakala hazikutumwa au kumbukumbu hazikufanywa kwa mujibu wa kijifungu cha (3), mfunga hesabu atatozwa faini na, kwa kuendelea kukiuka, faini ya kila siku.

(5) Iwapo akidi haikutimia kwenye mkutano huo, mfunga hesabu atapaswa, badala ya kumbukumbu zilizotajwa hapo juu, kufanya kumbukumbu kwamba mkutano umeitishwa kihalali na kwamba akidi ya kijifungu cha (3) hahaikutimia kwa ajili ya kuweka kumbukumbu inaonesha imezingatiwa.

(6) Kama mfunga hesabu itashindwa kuitisha mkutano mkuu wa kampuni kama inavyotakiwa na kijifungu cha (1) atatozwa faini.

Athari ya ufilisi wa kampuni.

**235.** Sehemu hii inatumika ambapo mfunga hesabu ana maoni kuwa kampuni haitaweza kulipa madeni yake kwa ukamilifu (pamoja na riba kwa kiwango rasmi) ndani ya kipindi kilichotajwa katika tamko la wakurugenzi chini ya kifungu cha 229.

(2) Mfunga hesabu atapaswa-

(a) kuitisha mkutano wa wadai siku ambayo si zaidi ya siku ya 28 baada ya ile siku ambayo yeye amekuwa na maoni hayo;

(b) kupeleka matangazo ya mkutano wa wadai kwa wadai kwa njia ya posta na baada ya siku zisizopungua saba kabla ya siku ambayo mkutano huo umepangwa kufanyika;

(c) kusababisha taarifa ya mkutano wadai kutangazwa mara moja katika Gazeti Rasmi na mara moja angalau katika magazeti mawili yanayosambazwa katika maeneo ambayo kampuni inafanya shughuli zake Zanzibar katika kipindi husika), na

(d) katika kipindi ambacho kabla ya siku ambayo mkutano wa wadai utafanyika, kuwapatia wadai bila ya malipo taarifa kuhusu masuala ya kampuni kama ambavyo watahitaji; na taarifa ya mkutano wa wadai itaeleza wajibu ulowekwa na aya ya (d) hapo juu.

(3) Mfunga hesabu pia atapaswa -

(a) kuweka tamko katika fomu iliyowekwa kuhusu masuala ya kampuni;

(b) kuweka tamko hilo katika mkutano wa wadai; na

(c) kuhudhuria na kuagiza katika mkutano huo.

(4) Taarifa kuhusu shughuli za kampuni zitathibitishwa kwa hati ya kiapo na mfunga hesabu ataonesha:

(a) maelezo ya mali za kampuni hiyo, madeni na madai;

(b) majina na anwani za wadai wa kampuni;

(c) dhamana walizoekewa kwa mtiririko;

(d) tarehe za dhamana kwa mtiririko; na

(e) maelezo ya zaidi au mengine kama ilivyoelekezwa.

(5) Endapo mahala pakuu pa biashara pa kampuni Zanzibar yapo katika maeneo mbalimbali kwa nyakati tofauti katika kipindi husika, wajibu uliowekwa na kifungu cha (2)(c) unatumika tofauti katika uhusiano na kila moja ya maeneo hayo.

(6) Endapo kampuni haina mahala pa biashara Zanzibar katika kipindi husika, marejeo katika kifungu cha (2) (c) na (5) kwa mahala pakuu pa shughuli za kampuni Zanzibar marejeo ni ofisi yake ya iliyosajiliwa.

(7) Katika kifungu hiki "kipindi husika" maana yake ni kipindi cha miezi 6 mara kabla ya siku iliotumwa matangazo ya kuitisha mkutano wa kampuni ambao iliamuliwa kwamba kampuni ifungwe kwa hiari.

(8) Kama mfunga hesabu bila sababu ya msingi atashindwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, atatozwa faini.

Kubadilika kuwa ufungaji hiari wa wadai.

**236.** Kuanzia siku ambayo mkutano wa wadai ulifanyika chini ya kifungu cha 235, Sheria hii ina athari kama;

(a) tamko la wakurugenzi chini ya kifungu 229 halikutolewa, na

(b) mkutano wa wadai na mkutano wa kampuni ambayo iliamuliwa kwamba kampuni ifungwe kwa hiari ilikuwa ni mikutano iliyoitishwa chni ya kifungu 138 katika Sura inayofuata na ufungaji wa kampuni utapaswa kuwa wa hiari kutokana na wadai.

Mrajis wa Kampuni anaweza kuifuta isiyohai kwenye daftari la usajili.

**237.**-(1) Pale ambapo Mrajis ana sababu ya kuamini kwamba kampuni haifanyi biashara au haiendeshi shughuli yeyote, anaweza kutuma barua kwa kampuni kwa njia ya posta kuhoji kama kampuni inafanya biashara zake au inaendesha shughuli yeyote.

(2) Kama Mrajis hajapokea jibu lolote ndani ya siku thelathini tangu kutuma barua, atatuma ndani ya siku kumi na nne baada ya kumalizika muda wa kipindi hicho kwa kampuni barua nyengine iliyosajiliwa posta inayofanya marejeo barua ya kwanza, na kueleza kuwa hakuna jibu alilopokea, na kwamba kama jibu hatopokea barua la barua ya pili ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe yake, ilani itachapishwa katika Gazeti Rasmi kwa lengo la kufuta jina la kampuni kwenye daftari la usajili.

(3) Kama Mrajis ama itapata jibu kwamba kampuni haifanyi biashara au haiendeshi shughuli yeyote, au ndani ya siku thelathini baada ya kutuma barua ya pili ya hakupokea jibu lolote, anaweza kuchapisha katika Gazeti la Rasmi, na kutuma kwa kampuni kwa njia ya posta, taarifa kwamba baada ya kumalizika muda wa miezi mitatu kuanzia tarehe ya tangazo jina la kampuni iliyotajwa humo itakuwa, isipokuwa sababu zitaonesha vyenginevyo, limefutwa kwenye daftari ta usajili na kampuni itafutwa:

Isipokuwa kwamba, Mrajis hatotakiwa kutuma barua iliyotajwa katika kifungu cha (1) na (2) katika hali yoyote ambapo kampuni yenyewe au mkurugenzi au katibu wa kampuni iliyomuomba kuifuta kampuni kwenye daftari la usajili au iliyomuarifu kuwa haifanyi shughuli yeyote.

(4) Iwapo, katika hali yoyote ambapo kampuni inafungwa, Mrajis ana sababu ya kuamini ama kwamba hakuna msimamizi, au kwamba masuala ya kampuni yamefungwa kikamilifu, na marejesho yavyotakiwa kufanywa na msimamizi (mfunga hesabu) hayakupatikana kwa kipindi cha miezi sita mfululizo, Mrajis atatangaza katika Gazeti Rasmi na kutuma kwa kampuni au mfunga hesabu, kama wapo, ilani kama kama ni ilivyotolewa katika kijifungu cha (3).

(5) Katika kumalizika kipindi cha muda uliotajwa katika ilani hiyo, Mrajis anaweza, isipokuwa sababu nyenginezo zimeoneshwa awali na kampuni au mfunga hesabu, kama hali inavyoweza kuwa, kufuta jina lake kwenye daftari la usajili, na itachapisha ilani ya yake katika Gazeti Rasmi, na juu ya uchapishaji huo wa ilani katika Gazeti Rasmi kampuni itafutwa:

Ispokuwa kwamba -

(a) dhima, kama ipo, ya kila mkurugenzi, afisa na mwanachama wa kampuni itaendelea na inaweza kutekelezwa kama kampuni ulikuwa bado haijafutwa, na

(b) hakuna chochote katika kijifungu hiki kitakachoathiri nguvu ya mahakama kuifunga kampuni ambayo jina lake limefutwa kwenye rejista.

(6) Kama kampuni au mwanachama yeyote au wadai wake anahisi hajaridhika na kampuni ambayo jina lake limefutwa kwenye rejista, Mahakama juu ya maombi yaliyotolewa na kampuni au mwanachama au wadai kabla ya kumalizika muda wa miaka kumi kutoka kuchapishwa katika Gazeti Rasmi tangazo anaweza, kama ataridhika kwamba kampuni wakati ilipofutwa ilikuwa ikifanya biashara na kendesha shughuli zake, au vinginevyo kwamba ni haki ya kuwa kampuni kurejeshwa kwenye rejista, ili jina la kampuni ya kurejeshwa kwa kujiandikisha, na juu ya kuthibitishwa nakala ya amri kuwasilishwa kwa Mrajis kwa ajili ya usajili, kampuni utachukuliwa imeendelea kuwepo kama jina lake halikifutwa, na Mahakama kwa amri inaweza kutoa maagizo hayo na kuweka masharti yatakayoonekana yanafaa kwa ajili ya kuweka kampuni na watu wengine wote katika msimamo huo kwa karibu kama kwamba jina la kampuni alikuwa na halikufutwa.

(7) Ilani itakayopelekwa chini ya sehemu hii kwa mfunga hesabu inaweza kutumwa kwa mfunga hesabu katika pahala pake pa mwisho panapojulikana anapofanya shughuli zake, na barua au tangazo litakalopelekwa chini ya sehemu hii kwa kampuni inaweza kutumwa kwa kampuni katika ofisi zake zilizosajiliwa au, kama haina ofisi iliyosajiliwa, kwa kupitia baadhi ya maafisa wa kampuni, au kama hakuna afisa wa kampuni ambaye jina na anuani inajulikana na Mrajis, inaweza kutumwa kwa kila aina ya watu ambao waliomo kwenye mkataba, kushughulikiwa na yeye katika anwani zilizotajwa katika mkataba.

## SEHEMU YA VIII
## KAMPUNI ZILIZOANDIKISHWA NJE YA ZANZIBAR

**238.**-(1) Sehemu hii itatumika kwa kampuni zote za kigeni, yaani, kampuni zilizoandikishwa nje ya Zanzibar ambazo baada ya siku maalumu, zinaanzisha sehemu ya biashara katika Zanzibar, na kwa kampuni zilizoandikishwa nje ya Zanzibar, ambazo kabla ya siku maalumu, zinaanzisha sehemu ya biashara ndani ya Zanzibar na kuendelea kuwa na mahali imara pa biashara ndani ya Zanzibar siku hiyo maalumu na baada ya siku hiyo maalumu.

Masharti Kuhusu Uanzishwaji wa Sehemu za Biashara Katika Zanzibar Kampuni ambazo Sehemu ya VII inatumika.

(2) Kampuni ya kigeni yoyote haitahesabiwa kuwa na mahali pa biashara katika Zanzibar kwa kufanya kwake biashara tu kupitia wakala katika Zanzibar katika nafasi ya biashara ya wakala.

**239.**-(1) Kila kampuni ya kigeni ambayo, baada ya siku maalumu, itaanzisha mahali pa biashara katika Zanzibar na kila kampuni ya kigeni ambayo katika siku maalumu ina mahali pa biashara katika Zanzibar ndani ya mwezi mmoja wa uanzishwaji wa mahali pa biashara au ndani ya miezi sita tangu siku maalumu, itawasilisha kwa Mrajis kwa ajili ya usajili:-

Nyaraka, n.k. kuwasilishwa kwa Mrajis na kampuni za kigeni zinazofanya biashara katika Zanzibar.

(a) nakala iliyothibitishwa ya katiba, sheria au mkataba na kanuni za kampuni au hati nyengine inayounda au kufafanua katiba ya kampuni, na, kama hati haikuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza, tafsiri yake iliyothibitishwa;

(b) orodha ya wakurugenzi na katibu wa kampuni yenye maelezo yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (2);

(c) majina na anuani za baadhi ya watu mmoja au zaidi wakaazi wa Zanzibar walioidhinishwa kukubali kwa niaba ya kampuni kuhudumia mwenendo na taarifa yoyote inayotakiwa kutolewa kuhusu kampuni.

(2) Orodha iliyotajwa katika paragrafu (b) ya kifungu kidogo cha (1) itakuwa na maelezo yafuatayo, yaani -

(a) kuhusiana na kila mkurugenzi;

(i) kwa mtu binafsi, jina lake la kwanza na jina lake la ukoo na jina la kwanza lolote la zamani na jina la ukoo, anuani ya makaazi yake ya kawaida, utaifa

wake na kazi yake ya biashara ikiwa ipo, au kama hana kazi ya biashara lakini anashikilia ukurugenzi mwengine wowote au kurugenzi, maelezo ya ukurugenzi huo au ya mmojawapo wa kurugenzi hizo; au

(ii) (kwa shirika, jina lake la shirika na ofisi yake iliyosajiliwa au ofisi yake kuu;

(b) kuhusiana na katibu au, ambapo kuna makatibu wa pamoja, kuhusiana na kila mmoja wao:-

(i) kwa mtu binafsi, jina lake la kwanza la sasa na jina lake la ukoo, jina lolote la kwanza la zamani na jina la ukoo na anuani ya makaazi yake ya kawaida; na

(ii) kwa shirika, jina lake la shirika na ofisi iliyosajiliwa;

Isipokuwa kwamba, ambapo washirika wote katika kampuni ni makatibu wa pamoja wa kampuni, jina na ofisi kuu ya kampuni inaweza kuelezwa badala ya maelezo yaliyotajwa katika paragrafu (b) ya kifungu hiki;

Paragrafu (b), (c) na (d) ya kifungu cha 214(9) zitatumika kwa madhumuni ya utayarishaji wa marejeo katika kifungu kidogo kwa majina ya kwanza ya sasa na ya zamani na majina ya ukoo ya sasa na ya zamani kama yanavyotumika kwa ajili ya utayarishaji wa marejeo hayo katika kifungu hicho.

Uwezo wa kampuni ya kigeni kumiliki ardhi.

**240.** Kampuni ya kigeni ambayo imewasilisha kwa Mrajis nyaraka na maelezo yaliyotajwa katika kifungu cha 225(1) na madhali imesajiliwa, itakuwa na uwezo sawa wa kumiliki ardhi katika Zanzibar kwa mujibu wa Sheria ya Umiliki wa Ardhi ya Mwaka 1994, kama kwamba ni kampuni iliyoandikishwa chini ya Sheria hii.

Marejesho kuwasilishwa kwa Mrajis na kampuni ya kigeni nyaraka n.k. zinapobadilishwa.

**241.** Kama mabadiliko yoyote yamefanywa katika:-

(a) mkataba, sheria, au katiba na kanuni za kampuni ya kigeni au chombo chochote kama ilivyoelezwa awali; au

(b) wakurugenzi au katibu wa kampuni ya kigeni au maelezo yaliyomo katika orodha ya wakurugenzi na katibu; au

(c) majina au anuani za watu walioidhinishwa kukubali kutoa huduma kwa niaba ya kampuni ya kigeni;
kampuni, ndani ya muda uliowekwa, itawasilisha kwa Mrajis marejejesho kwa ajili ya usajili yenye maelezo yaliyowekwa ya mabadiliko.

Hesabu za kampuni ya kigeni.

**242.**-(1) Kila kampuni ya kigeni, katika kila mwaka wa kalenda, itatayarisha mizania ya hesabu ya faida na hasara na, kama kampuni ni

kampuni ya hisa, hesabu za vikundi katika fomu, na zenye maelezo hayo na ikiwa ni pamoja na hati hizo, kama ilivyo chini ya masharti ya Sheria hii (kwa kuzingatia, hata hivyo, msamaha wowote uliowekwa), kama ingalikuwa ni kampuni ndani ya maana ya Sheria hii, ingetakiwa kutayarisha na kuwasilisha katika kampuni kwenye mkutano mkuu, na kuwasilisha nakala za nyaraka hizo kwa Mrajis.

(2) Kama hati yoyote kama ilivyotajwa katika kifungu cha (1) haikuandikwa katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza, itaambatanishwa pamoja nayo nakala iliyothibitishwa ya tafsiri yake.

Wajibu wa kutaja jina la kampui ya kigeni, kama ni yenye ukomo, na nchi ambapo iliandikishwa.

**243.** Kila kampuni ya kigeni: -

(a) katika kila muhtaasari wa ununuzi wa hisa unaokaribisha michango kwa ajili ya hisa zake au dhamana katika Zanzibar itataja nchi ambayo kampuni imeandikishwa; na

(b) itaonesha kwa uwazi katika kila mahali ambapo inaendesha biashara katika Zanzibar jina la kampuni na nchi ambayo kampuni imeandikishwa; na

(c) kuwezesha jina la kampuni na la nchi ambayo kampuni imeandikishwa kuelezwa katika hati za Kirumi zinazosomeka katika ankara na karatasi za barua, na katika matangazo yote na machapisho mengine rasmi ya kampuni; na

(d) kama dhima ya wanachama wa kampuni ni yenye ukomo, kuwezesha taarifa ya jambo hilo kuelezwa katika hati za Kirumi zinazosomeka katika muhtasari wa ununuzi wa hisa kama ilivyoelezwa awali na katika ankara zote, karatasi za barua, matangazo na machapisho mengine rasmi ya kampuni katika Zanzibar, na kubandikwa katika kila mahali ambapo inaendesha biashara yake.

Huduma kwa kampuni ya kigeni.

**244.** Mchakato wowote au taarifa inayotaka kupelekwa kwa kampuni ya kigeni itakuwa imeshughulikiwa ipasavyo na mtu yeyote ikiwa imewasilishwa kwa mtu yeyote ambaye jina lake limepelekwa kwa Mrajis chini ya masharti yaliyotangulia ya Sehemu hii na kuwekwa au kupelekwa kwa njia ya posta kwa anuani ambayo imewasilishwa hivyo.

Isipokuwa kwamba:-

(a) Ambapo kampuni yoyote inakiuka katika kuwasilisha kwa Mrajis jina na anuani ya mtu ambaye ni mkaazi wa Zanzibar ambaye ameidhinishwa kukubali kwa niaba ya kampuni kuhudumia mchakato au taarifa; au

(b) Kama wakati wowote watu wote ambao majina na anwani zao zilizowasilishwa wamekufa au wamesita kuishi Zanzibar, au wamekataa kukubali kuhudumia kwa niaba ya kampuni, au kwa sababu yoyote haziwezi kuhudumiwa;

(c) Hati inaweza kupelekwa kwa kampuni kwa kuiweka au kuipeleka kwa njia ya posta kwenye sehemu yoyote ya biashara iliyowekwa na kampuni katika Zanzibar.

Usajili kutolewa taarifa kampuni ya kigeni inaposita kuwa na mahali pa biashara Zanzibar.

**245.** Kama kampuni yoyote ya kigeni inaacha kuwa na mahali pa biashara katika Zanzibar, itatoa taarifa papo hapo kuhusu hali hiyo kwa Mrajis, na kutoka tarehe ambayo taarifa imetolewa, wajibu wa kampuni wa kuwasilisha hati yoyote kwa Mrajis utakoma.

Adhabu.......

**246.** Kama kampuni yoyote ya kigeni itakiuka katika kutekeleza masharti yoyote yaliyotangulia ya Sehemu hii, kampuni, na kila ofisa au wakala wa kampuni ambaye kwa kujua na kwa makusudi anaidhinisha au kuruhusu ukiukaji, atatozwa faini, au, katika hali ya kosa kuendelea, kutozwa faini kwa kila siku ambao ukiukaji unaendelea.

Tafsiri za vifungu vya 225 mpaka 232.

**247.** Kwa madhumuni ya masharti yaliyotangulia ya Sehemu hii:-

"iliyothibitishwa" linamaanisha kuthibitishwa katika namna iliyowekwa kuwa ni nakala halisi au tafsiri sahihi;

"mkurugenzi" kuhusiana na kampuni linajumuisha mtu yeyote ambaye maelekezo au miongozo yake wakurugenzi wa kampuni wamezoea kutekeleza;

"mahali pa biashara" ni pamoja na ofisi ya uhaulishaji wa hisa au ofisi ya usajili wa hisa;

"muhtasari wa ununuzi wa hisa" lina maana sawa kama linavyotumika kuhusiana na kampuni iliyoandikishwa chini ya Sheria hii.

"katibu" linajumuisha mtu yeyote anayeshikilia nafasi ya katibu kwa jina lolote analoitwa.

Muhtasari wa Ununuzi wa Hisa Utiaji tarehe katika muhtasari wa ununuzi wa hisa na taarifa zinazopasa kuwemo ndani yake.

**248.**-(1) Si halali kwa mtu yeyote kutoa, kusambaza au kugawa katika Zanzibar muhtasari wa ununuzi wa hisa wowote unaotoa hisa za kuchangia katika au dhamana za kampuni iliyoandikishwa au inayotaka kuandikishwa nje ya Zanzibar, kama kampuni imeanzisha au haikuanzisha, au itakapoundwa itaanzisha au haitaanzisha, mahali pa biashara katika Zanzibar isipokuwa muhtasari wa ununuzi wa hisa uwe umetiwa tarehe na:-

(a) unajumuisha maelezo kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) hati inayounda au kufafanua katiba ya kampuni;

(ii) sheria, masharti yana nguvu ya kisheria, ambayo kwayo au ambayo chini yake uandikishwaji wa kampuni ulifanyika;

(iii) anuani katika Zanzibar ambapo hati iliyotajwa, sheria au masharti, au nakala zake, na kama zimo

katika lugha nyengine isiyokuwa Kiswahili au Kiingereza au tafsiri zake zilizothibitishwa katika namna iliyowekwa, zinaweza kukaguliwa;

(iv) tarehe ambayo na nchi ambayo kampuni iliandikishwa;

(v) kama kampuni imeanzisha mahali pa biashara katika Zanzibar, na kama imefanya hivyo, anuani ya ofisi yake kuu katika Zanzibar.

(b) kwa kufuata masharti ya kifungu hiki, inaeleza mambo yaliyotajwa katika kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Isipokuwa kwamba masharti ya paragrafu ndogo za (i), (ii) na (iii) za paragrafu (a) ya kifungu kidogo hiki havitatumika kwa muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotolewa zaidi ya miaka miwili baada ya tarehe ambayo kampuni ilikuwa na haki ya kuanza biashara, na katika utekelezaji wa masharti ya kanuni za Sheria hii kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki, paragrafu yake ya 2 itakuwa na athari kwa mbadala, kwa ajili ya marejeo ya kanuni, ya marejeo ya katiba ya kampuni.

(2) Sharti lolote linalohitaji au kulazimisha maombi ya hisa au dhamana kuondoa utekelezaji wa matakwa yoyote yaliyowekwa kwa mujibu wa pargrafu (a) au (b) ya kifungu kidogo cha (1), au linalodai kuathiri taarifa ya mkataba wowote, hati au jambo ambalo halikutajwa makhsusi katika muhtasari wa ununuzi wa hisa, litakuwa batili.

(3) Si halali mtu yeyote katika Zanzibar kutoa fomu ya maombi kwa ajili ya hisa katika katika au dhamana za kampuni au kampuni inayokusudiwa kama ilivyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki isipokuwa fomu imetolewa pamoja na muhtasari wa ununuzi wa hisa ambao unafuata masharti ya Sehemu hii na suala lenyewe katika Zanzibar haliendi kinyume na masharti ya kifungu cha 237.

Isipokuwa kwamba kifungu hiki hakitatumika ikiwa imeoneshwa kwamba fomu ya maombi ilitolewa kuhusiana na mwaliko wa moja kwa moja kwa mtu kuingia katika mkataba wa kugharimia kuhusiana na hisa au dhamana.

(4) Itokeapo kutofuata au kukiuka matakwa yoyote yanayowekwa na paragrafu (a) na (b) za kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mkurugenzi au mtu mwengine anayehusika na muhtasari wa ununuzi wa hisa hatakuwa na dhima yoyote kwa sababu ya kutofuata au kukiuka, kama:-

(a) kwa suala lolote ambalo lilifichwa, anathibitisha kuwa hakuwa na habari nalo; au

(b) anathibitisha kuwa kutofuata au kukiuka kulitokana na kosa la kweli kwa upande wake; au

(c) kutofuata au kukiuka kulihusiana na mambo ambayo, kwa maoni ya mahakama inayoshughulikia kesi inayohusika, yalikuwa hayana umuhimu au vyenginevyo, kwa maoni ya mahakama hiyo, kwa kuzingatia mazingira yote ya kesi, yalipaswa kusamehewa.

Isipokuwa kwamba, katika tukio la kushindwa kuingiza katika muhtasari taarifa zinazohusu masuala yaliyomo katika kanuni, hakuna mkurugenzi au mtu mwengine ambaye atakuwa na dhima yoyote kuhusiana na kushindwa huko isipokuwa imethibitika kuwa alikuwa na habari ya mambo ambayo yalifichwa.

(5) Sehemu hii: -

(a) haitatumika kwa suala la kutoa kwa wanachama waliopo au wamiliki wa dhamana za kampuni waliomo kwenye muhtasari wa ununuzi wa hisa au fomu ya maombi inayohusiana na hisa katika au, dhamana za kampuni, kama mwombaji wa hisa au dhamana atakuwa na haki au la ya kukataa ili kuwapendelea kuwa na watu wengine; na

(b) ila kwa kadri ambavyo inahitajika muhtasari wa ununuzi wa hisa kutiwa tarehe, haitatumika kwa utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa kuhusiana na hisa au dhamana ambazo ni au zitakuwa katika hali zote sawa na hisa au dhamana zilizotolewa kabla na kwa wakati huo zinashughulikiwa au kuzabuniwa kwenye masoko ya hisa yaliyopo Zanzibar.

Lakini, kwa kuzingatia yaliyoelezwa awali, sehemu hii itatumika kwa muhtasari wa ununuzi wa hisa au fomu ya maombi iwe imetolewa kwa au kwa kuzingatia uundaji wa kampuni au baadaye;

(6) Hakuna chochote katika kifungu hiki, kikomo au kupunguza dhima yoyote ambayo mtu yeyote anaweza kuwa nayo chini ya sheria ya jumla ya Sheria hii, mbali na sehemu hii.

Uondoaji wa kifungu cha 234 na ulegezaji wa Jadweli ya Tatu kwa baadhi ya mihutasari.

**249.**-(1) Ambapo:-

(a) inapendekezwa kutoa kwa umma kwa muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotoa kwa jumla hisa zozote katika au dhamana za kampuni iliyoandikishwa au itakayoandikishwa nje ya Zanzibar, kama kampuni imeanzisha au haijaanzisha, au wakati itakapoundwa itaanzisha au haitaanzisha mahali pa biashara katika Zanzibar; na

(b) maombi yamefanywa kwenye soko lolote la hisa katika Zanzibar kutaka ruhusa kwa ajili ya hisa hizo au dhamana kushughulikiwa katika au kuzabuniwa katika sko hilo la hisa;

kunaweza kwa ombi la mwombaji kutolea na au kwa niaba ya soko hilo la hisa hati ya msamaha, yaani, hati ambayo, kwa kuzingatia mapendekezo (kama yalivyoelezwa katika ombi) kuhusiana na mamabo menegine kuhusu utoaji wa hisa au dhamana na kuhusu vikwazo vyoyote juu ya idadi na daraja ya watu ambao watapewa hiyo fursa, kufuata matakwa ya kanuni kutakuwa kuzito mno.

(2) Ikiwa hati ya msamaha imetolewa, na kama mapendekezo yaliyoelezwa awali yamezingatiwa na maelezo na taarifa zinazohitajika kuchapishwa kuhusiana na na maombi ya ruhusa kwenye soko la hisa zimechapishwa, basi:-

(a) muhtasari wa ununuzi wa hisa unaotoa maelezo na taarifa zilizoelezwa awali katika namna ambayo inatakiwa kuchapishwa utachukuliwa kuzingatia matakwa ya kanuni; na

(b) isipokuwa kwa kadiri inavyohitaji muhtasari wa ununuzi wa hisa kutiwa tarehe, kifungu cha 235 hakitatumika kwa utoaji wowote, baada ya ruhusa iliyoombwa kuwa imetolewa, wa muhtasari au fomu ya maombi yanayohusiana na hisa au dhamana.

Masharti kuhusu ridhaa ya wataalamu na ugawaji.

**250.-**(1) Si halali mtu yeyote kutoa, kusambaza au kugawa katika Zanzibar muhtasari wa ununuzi wa hisa wowote unaotoa furs ya kuchangia hisa au dhamana za kampuni iliyoandikishwa au inayotaka kuandikishwa nje ya Zanzibar, kama kampuni imeanzisha au haijaanzisha, au itakapoundwa itaanzisha au haitaanzishwa, mahali pa biashara katika Zanzibar:-

(a) kama, ambapo muhtasari wa ununuzi wa hisa una maelezo yanayodai kutolewa na mtaalamu, hajatoa, au ameondoa kabla ya utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa ajili ya usajili, ridhaa yake kwa maandishi kuhusu utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa pamoja na maelezo na katika fomu na muktadha ambao yameingizwa au haionekani katika muhtasari wa ununuzi wa hisa taarifa kwamba ametoa na hakuiodoa katika ridhaa yake kama ilivyoelezwa awali; au

(b) kama muhtasari wa ununuzi wa hisa hauna athari, ambapo maombi yamefanywa kwa kuuzingatia, ya kuwafanya watu wote wanaohusika kufungwa na masharti yote (zaidi ya vifungu vya adhabu) ya vifungu vya 58 na 59 kama vinavyotumika.

(2) Katika kifungu hiki tamko "mtaalamu" ni pamoja na mhandisi, mtathmini, mhasibu na mtu mwengine yeyote ambaye taaluma yake inatoa mamlaka kwa taarifa iliyotolewa na yeye, na kwa madhumuni ya kifungu hiki, taarifa hiyo itachukuliwa kuwa imejumuishwa kwenye muhtasari wa ununuzi wa hisa kama imo humo au katika ripoti au mkataba unaonekana kwenye uso wake au kwenye kumbukumbu zilizoingizwa humo au iliyotolewa humo.

Usajili wa muhtasari wa ununuzi wa hisa.

**251.**-(1) Si halali kwa mtu yeyote kutoa, kusambaza au kugawa katika Zanzibar muhtasari wa ununuzi wa hisa wowote unaotoa fursa ya kuchangia hisa katika au dhamana za kampuni iliyoandikishwa au inayotaka kuandikishwa nje ya Zanzibar, kama kampuni imeanzisha au haijaanzisha, au wakati wa kuundwa itaanzisha au haitaanzisha, mahali pa biashara katika Zanzibar, isipokuwa kabla ya utoaji huo, ugawaji au usambazaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa katika Zanzibar, nakala yake iliyothibitishwa na mwenyekiti na wakurugenzi wengine wawili wa kampuni kwamba baada ya kupitishwa kwa azimio la chombo kinachoongoza umewasilishwa kwa ajili ya usajili kwa Mrajis, na muhtasari unaeleza juu ya uso wake kwamba nakala imewasilishwa hivyo, na kumetiwa saini juu yake au kumeambatanishwa kwenye nakala:-

(a) ridhaa yoyote ya utoaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa inayotakiwa na kifungu cha 236;

(b) nakala ya mkataba wowote unaotakiwa na kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii kuelezwa katika muhtasari wa ununuzi wa hisa au, kwa mkataba si wa maandishi, mkataba unaotoa maelezo kamili, au, kwa muhtasari unaochukuliwa kwa mujibu wa hati iliyotolewa chini ya kifungu cha 235 kwa kuzingatia matakwa ya Jadweli hiyo, mkataba au nakala yake au maelezo ya mkataba inahitajika kupatikana kwa ajili ya ukaguzi kuhusiana na maombi chini ya kifungu hicho kwenye soko la hisa linalohusika, nakala au kama itakavyokuwa maelezo ya mkataba ule; na

(c) ambapo watu wanaotayarisha ripoti yoyote inayotakiwa na kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, wamefanya humo au, bila ya kutoa sababu, wameelezwa humo marekebisho yoyote kama yaliyotajwa katika kanuni, taarifa ya maandishi iliyotiwa saini na watu kuweka nje marekebisho na kutoa sababu hiyo.

(2) Marejeo katika kifungu kidogo cha (1)(b) kuhusu nakala ya mkataba unaotakiwa kutiwa saini au kuambatanishwa na nakala ya muhtasari wa ununuzi wa hisa, kwa mkataba ambao wote au sehemu yake umo katika lugha isiyokuwa ya Kiswahili au ya Kiingereza au utachukuliwa kama kumbukumbu ya nakala ya tafsiri ya mkataba wa Kiswahili au Kiingereza, au nakala iliyo na tafsiri kwa Kiswahili au Kiingereza za sehemu zilizomo katika lugha ya kigeni, kama itakavyokuwa, ikiwa ni tafsiri iliyothibitishwa katika namna iliyowekwa kuwa ni tafsiri sahihi, na kumbukumbu ya nakala ya mkataba inayotakiwa kupatikana kwa ajili ya ukaguzi itakuwa ni pamoja na kumbukumbu ya nakala ya tafsiri yake au nakala iliyo na tafsiri ya sehemu zake.

Adhabu kwa kukiuka vifungu vya 234, 235, 236 na 237.

**252.** Mtu yeyote ambaye akiwa anajua anahusika na utoaji, usambazaji au ugawaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa, au utoaji wa fomu ya maombi kwa ajili ya hisa au dhamana, kwa kukiuka masharti yoyote ya vifungu vya 234, 235, 236 na 237, atatozwa faini.

**253.** Kifungu cha 51 kitahusu kila muhtasari wa ununuzi wa hisa kinachotoa fursa ya kuchangia katika hisa au dhamana za kampuni iliyoandikishwa au inayotaka kuandikishwa nje ya Zanzibar, kama kampuni imeanzisha au haijaanzisha, au wakati wa kuundwa itaanzisha au haitaanzisha, mahali pa biashara katika Zanzibar, na kubalishana, kwa marejeo ya vifungu vya 48 ya marejeo ya kifungu cha 236.

Dhima kwa jamii kwa taarifa zisizokuwa sahihi kwenye muhtasari.

**254.-**(1) Ambapo hati yoyote ambayo hisa zozote katika au dhamana za kampuni iliyoandikishwa nje ya Zanzibar zinatolewa kwa ajili ya kuuzwa kwa umma, kama kampuni inayohusika ilikuwa kampuni ndani ya maana ya Sheria hii, ingechukuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 53 kuwa ni muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotolewa na kampuni, hati hiyo itachukuliwa kuwa, kwa madhumuni ya Sehemu hii, muhtasari wa ununuzi wa hisa uliotolewa na kampuni.

Tafsiri ya vifungu kuhusiana na muhtasari.

(2) Fursa ya kuchukua hisa au dhamana kwa ajili ya kuchangia au kuuza kwa mtu yeyote ambaye biashara yake ya kawaida au wakala, haitahesabiwa kuwa ni fursa kwa umma kwa madhumuni ya Sehemu hii.

(3) Katika Sehemu hii ya tamko "muhtasari wa ununuzi wa hisa ", "hisa", na "dhamana" yana maana sawa na kama yanavyotumika katika kuhusiana na kampuni ya iliyoandikishwa chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA IX
## MASHARTI YA JUMLA KUHUSU USAJILI

**255.-**(1) Kwa madhumuni ya usajili wa kampuni chini ya Sheria hii, kutakuwa na ofisi katika Zanzibar katika maeneo kama ambavyo Waziri ataelekeza.

Ofisi za usajili.

(2) Waziri anaweza kuteua Wasajili wasaidizi, kama yeye anadhani ni lazima kwa ajili ya usajili wa kampuni chini ya Sheria hii, na anaweza kutunga kanuni kuhusiana na kazi zao, na anaweza kumuondoa watu yeyote aliyeteuliwa hivyo.

(3) Kila Mrajis Msaidizi anaweza, chini ya maelekezo ya Mrajis, kufanya jambo lolote au shughuli yoyote ambayo Mrajis anaweza kisheria kufanya au anatakiwa na sheria hii kufanya, na kwa madhumuni hayo atakuwa na uwezo kamili, fursa na mamlaka ya Mrajis.

(4) Waziri anaweza kuagiza muhuri utayarishwe kwa ajili ya uthibitishaji wa nyaraka zinazohitajika kwa ajili ya au kuhusiana na usajili wa kampuni.

**256.-**(1) Kuhusiana na mamabo mbali mbali yaliyotajwa katika safuwima ya kwanza ya Jadweli iliyowekwa katika kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, chini ya mipaka inayowekwa na masharti ya kanuni hizo, kutalipwa kwa Mrajis ada mbali mbali maalumu zilizoainishwa katika safuwima ya pili ya Jadweli hiyo.

Ada.

(2) Waziri, kwa kushauriana na Mrajis, anaweza kutunga kanuni kuweka ada zinazopaswa kulipwa chini ya Sheria hii.

(3) Ada zote zinazolipwa kwa Mrajis kulingana na Sheria hii zitalipwa Hazina.

Ukaguzi, utoaji na ushahidi wa nyaraka zinazotunzwa na Mrajis.

**257.-**(1) Mtu yeyote anaweza:-

(a) kukagua nyaraka zinazowekwa na Mrajis, kwa malipo ya ada kama yanavyoweza kuwekwa na Waziri;

(b) kutaka hati ya kuandikishwa ya kampuni yoyote, au nakala au dondoo ya hati nyengine yoyote au sehemu yoyote ya hati nyengine yoyote, kuthibitishwa na Mrajis, kwa malipo ya cheti, nakala iliyothibitishwa au dondoo ya ada kama Waziri anavyoweza kuweka:

Isipokuwa kwamba:-

(i) kuhusiana na nyaraka zilizowasilishwa kwa Mrajis pamoja na muhtasari kwa mujibu wa paragrafu ndogo ya (i) ya paragrafu (b) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 49, haki zinazotolewa na kifungu kidogo hiki zitatumika tu wakati wa siku kumi na nne kuanzia tarehe ya uchapishaji wa muhtasari wa ununuzi wa hisa au kwa ruhusa ya Mrajis, na kuhusiana na nyaraka zilizowasilishwa kwa mujibu wa paragrafu (b) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 237 haki zilizotajwa zitatumika tu wakati wa siku kumi na nne kuanzia tarehe ya muhtsari wa ununuzi wa hisa au kwa ruhusa ya Mrajis; na

(ii) haki iliyotolewa na paragrafu (a) ya kifungu kidogo haitahusu nakala yoyote iliyopelekwa kwa Mrajis na mpokeaji au meneja wa yote au kiasi kikubwa cha mali yote ya kampuni, aliyeteuliwa kwa niaba ya wamiliki wa dhamana zozote za kampuni zilizopatikana kwa malipo yasiyokuwa na kiwango maalumu ya mpokeaji kuhusiana na masuala ya kampuni au ya maoni yoyote ya mpokeaji au mrithi wake au mpokeaji anaendelea au meneja wake, lakini tu kwa muhtasari wa ununuzi wa hisa, isipokuwa pale ambapo mtu anayedai haki ama ni au ni wakala wa mtu anayejieleza mwenyewe kwa maandishi kuwa ni mwanachama au mdai wa kampuni ambayo taarifa inahusiana nayo, na haki iliyotolewa na paragrafu (b) ya kifungu kidogo hiki itakuwa na mipaka kama hivyo.

(2) Hakuna utaratibu kwa ajili ya kulazimisha utoaji wa hati yoyote inayowekwa na Mrajis itatolewa kutoka mahakama yoyote ila kwa idhini

ya mahakama hiyo, na utaratibu wowote kama utatolewa utakuwa juu yake na taarifa kwamba umetolewa kwa idhini ya mahakama.

(3) Nakala ya, au dondoo kutoka, hati yoyote inayowekwa na kusajiliwa katika ofisi yoyote kwa ajili ya usajili wa kampuni, iliyothibitishwa kuwa ni nakala halisi kwa kutiwa saini na Mrajis (ambaye wadhifa wake rasmi haitakuwa lazima kuuthibitisha), itajuzu kuingizwa katika kesi zote za kisheria katika ushahidi halali sawa na hati halisi.

(4) Mtu yeyote kwa kudanganya anayejieleza mwenyewe kwa maandishi kwa madhumuni ya paragrafu ndogo ya (ii) ya kifungu kidogo cha (1) kuwa ni mwanachama au mdai wa kampuni atatozwa faini.

Kusimamia-wajibu wa kampuni kupeleka marejesho kwa Mrajis.

**258.**-(1) Kama kampuni, baada ya kufanya ukiukaji katika kuzingatia masharti yoyote ya Sheria hii ambayo inatakiwa iyafuate, inatoa au inapeleka kwa Mrajis marejesho yoyote, hesabu au hati nyingine, au kutoa taarifa kwake ya jambo lolote, inashindwa kurekebisha kasoro hiyo ndani ya siku kumi na nne baada ya kampuni kupewa taarifa ya kuitaka kufanya hivyo, mahakama inaweza, kutokana na maombi yaliyotolewa mahakamani na mwanachama yeyote au mdai wa kampuni au na Mrajis, kutoa amri kuielekeza kampuni na ofisa wake yeyote kurekebisha kasoro ndani ya muda kama utakavyoelekezwa katika amri.

(2) Amri kama hiyo yoyote inaweza kuweka sharti kwamba gharama zote za na zinazotokana na maombi zitalipwa na kampuni au na ofisa yeyote wa kampuni anayewajibika kwa ukiukaji.

(3) Hakuna chochote katika kifungu hiki katakachochukuliwa kuathiri utekelezaji wowote wa sheria inayotoa adhabu kwa kampuni au maofisa wake kuhusiana na ukiukaji wowote kama ilivyoelezwa awali.

## SEHEMU X
## MASHARTI MENGINEYO KUHUSIANA NA KAMPUNI ZA BENKI NA BIMA, NA JUMUIYA NYENGINE, UBIA NA KAMPUNI ZILIZOSAJILIWA

Masharti Kuhusu Kampuni za Benki na Bima Ukatazaji wa ubia wa benki wenye wanachama zaidi ya kumi.

**259.** Hakuna kampuni, chama, au ubia wenye watu zaidi ya kumi utakaofanywa kwa lengo la kufanyia biashara ya kibenki, isipokuwa kama imesajiliwa kama kampuni chini ya Sheria hii, au imeundwa kwa mujibu wa Sheria zinazoongoza mambo ya kibenki na taasisi za fedha,

Usajili wa kampuni ya benki yenye ukomo, wateja kupewa taarifa.

**260.**-(1) Pale ambapo kampuni ya benki ambayo ilikuwepo katika siku maalumu, inapendekeza kujiandikisha kama kampuni yenye ukomo, angalau siku thalathini kabla ya kujisajili, itatoa taarifa ya nia yake ya kujiandikisha kwa kila mtu ambaye ana akaunti ya benki na kampuni, ama kwa kumpelekea taarifa, au kwa kuipeleka kwa njia ya posta kwa, au kuipeleka kwa, anwani yake inayojulikana.

(2) Kama kampuni inaacha kutoa taarifa inayotakiwa na kifungu hiki, basi, kama kati ya kampuni mtu amabye kwa wakati huo ana maslahi katika akaunti ambayo ilipaswa kutolewa taarifa, na kadiri kuhusiana na akaunti mpaka wakati ambapo taarifa inatolewa, lakini si zaidi ya hapo au vyenginevyo, hati ya usajili yenye dhima yenye ukomo haitafanya kazi.

Benki na kampuni nyengine maalumu kuchapisha taarifa za vipindi.

**261.-**(1) Kila kampuni, kama kampuni ya benki yenye ukomo au kampuni ya bima au amana, akiba ya uzeeni, au jumuiya ya faida, kabla ya kuanzisha biashara, na pia katika Jumatatu ya kwanza ya mwezi wa Februari na Jumanne ya kwanza ya mwezi wa Agosti katika kila mwaka ambao inaendesha biashara, itatayarisha taarifa katika fomu iliyowekwa katika kanuni au inayokaribiana nayo kama hali inavyoruhusu.

(2) Nakala ya taarifa itawekwa katika mahali bayana katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni, na katika kila ofisi ya tawi au mahali ambapo biashara ya kampuni inafanyika.

(3) Kila mwanachama na kila mdai wa kampuni atakuwa na haki ya kupata nakala ya taarifa, kwa malipo ya pesa kama kampuni inavyoweza kuamua.

(4) Iwapo ukiukaji unafanywa katika kutekeleza kifungu hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini kwa ukiukaji.

(5) Kwa madhumuni ya Sheria hii kampuni ambayo inaendesha biashara ya bima pamoja na biashara nyengine yoyote moja au nyingi itachukuliwa kuwa ni kampuni ya bima.

Ukatazaji wa ubia wenye wanachama zaidi ya ishirini.

**262.** Hakuna kampuni, chama, au ubia wenye watu zaidi ya ishirini itakayoundwa kwa madhumuni ya kuendesha biashara yoyote (zaidi ya biashara ya kibenki) ambayo lengo lake ni upatikanaji wa faida kwa kampuni, chama, au ubia, au kwa wanachama wake binafsi, isipokuwa kama imesajiliwa kama kampuni chini ya Sheria hii, au imeanzishwa kwa mujibu wa baadhi ya sheria nyengine zinazohusika.

## SEHEMU XI
## JUMLA

Aina za madaftari, n.k.

263.-(1) Daftari lolote, fahirisi, kitabu cha kumbukumbu au kitabu cha hesabu linalotakiwa na Sheria hii kuwekwa na kampuni linaweza kuwekwa ama kwa kuingizwa taarifa katika vitabu vilivyojalidiwa au kwa kurikodi mambo yanayohusika kwa namna nyengine yoyote.

(2) Pale daftari lolote, fahirisi, kitabu cha kumbukumbu au kitabu cha hesabu haliwekwi kwa kuingiza taarifa katika kitabu kilichojalidiwa, lakini kwa njia nyengine, tahadhari ya kutosha itachukuliwa kwa ajili ya kulinda dhidi ya udanganyifu na kuwezesha kujuilikana kwake, na ambapo ukiukaji unafanywa katika kutekeleza kifungu kidogo hiki, kampuni na kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini na zaidi atatozwa faini kwa ukiukaji.

**264.**-(1) Hati inaweza kupelekwa kwenye kampuni kwa kuiweka kwenye au kuipelekaa kwa njia ya posta kwenye ofisi iliyosajiliwa ya kampuni katika Zanzibar. Upelekaji wa Hati Upelekaji wa hati.

(2) Hati inaweza kupelekwa kwa Mrajis kwa kuiweka kwenye au kuipeleka kwa njia ya posta kwenye ofisi yake.

**265.**-(1) Mrajis anaweza kutoa hati ya utendaji mzuri ili kuthibitisha kwamba kampuni fulani ipo kisheria, inazingatia mahitaji yote ya kiutawala kama na uwepo wake ndani ya Usajili rasmi, na imelipa ada zote za serikali, na hivyo ni katika utendaji mzuri. Hati ya Utendaji Mzuri.

(2) Kampuni inaweza, baada ya malipo ya ada iliyopangwa, kuomba kwa Mrajis hati ya utendaji mzuri, kwa maandishi kuandika na ikiambatanisha na ushahidi wa taarifa kutoka kwa mamlaka zinazohusika.

**266.** Hakuna mahakama chini ya Mahakama ya Hakimu Mkaazi itahukumu kosa lolote dhidi ya Sheria hii. Kuzingatia makosa.

**267.** Kama mtu yeyote katika marejesho yoyote, ripoti, hati, mizania, au hati nyengine, inayotakiwa na au kwa madhumuni ya masharti yoyote ya Sheria hii iliyotajwa katika Kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria hii kwa makusudi anatoa taarifa ya uongo katika hali yoyote, huku akijua kuwa ni uongo, anatenda kosa, na akitiwa hatiani atafungwa gerezani kwa muda usiozidi miaka miwili, au faini isiyozidi milioni mbili, au adhabu zote mbili. Adhabu kwa taarifa za uongo.

**268.** Kama mtu yeyote, anayehojiwa baada ya kula kiapo kilichoidhinishwa chini ya Sheria hii au katika hati yoyote ya kiapo au ushahidi wa kiapo katika au kuhusu uvunjaji wa kampuni yoyote au vyenginevyo katika au kuhusu jambo lolote linalotokana na Sheria hii, kwa makusudi na kwa rushwa anatoa ushahidi wa uongo, akitiwa hatiani atafungwa kwa muda usiozidi miaka saba, au faini isiyozidi milioni tano, au adhabu zote mbili. Adhabu kwa kusema uongo baada ya kuapa.

**269.**-(1) Popote ambapo sharti lolote katika Sheria linaeleza kwamba kampuni na/au kila ofisa wa kampuni na/au mtu mwengine yeyote atatozwa faini ya ukiukwaji, faini ya jumla na au adhabu nyengine yoyote ya pesa, kiasi cha kulipwa kitaamuliwa kwa namna ilivyowekwa katika Sheduli ya faini iliyoambatanishwa na Sheria hii. Masharti kuhusu faini ya ukiukwaji na faini kwa jumla na tafsiri ya "ofisa katika ukiukaji"

(2) Waziri kwa kushauriana na Mrajis anaweza kuirekebisha Sheduli ya Faini na marekebisho hayo yatakuwa na nguvu ya kisheria baada ya kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

(3) Kwa madhumuni ya sheria yoyote katika Sheria hii ambayo inaeleza kwamba ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji atatozwa faini au adhabu, tamko "ofisa ambaye anahusika katika ukiukaji" maana yake ni ofisa yeyote wa kampuni ambaye akiwa anajua na kwa makusudi anaidhinisha au anaruhusu ukiukaji, ukataaji au uvunjaji uliotajwa katika sheria.

Utoaji na ukaguzi wa vitabu kosa linapoakhirishwa kwa muda.

**270.-**(1) Kama kwa maombi yaliyopelekwa kwa Jaji wa Mahakama Kuu katika vyumba vya mahakama na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma imedhihirika kuwa kuna sababu ya kuamini kwamba mtu yeyote, wakati ni ofisa wa kampuni, alifanya kosa kuhusiana na usimamizi wa mambo ya kampuni hiyo na kwamba ushahidi wa kufanya kosa hilo utapatikana katika vitabu vyovyote au magazeti ya au yaliyo chini ya udhibiti wa kampuni amri inaweza kutolewa:-

(i) kumuidhinisha mtu yeyote aliyetajwa humo kuvikagua vitabu vilivyoelezwa au magazeti au lolote kati yao kwa madhumuni ya kuchunguza na kupata ushahidi wa kosa; au

(ii) kumtaka katibu wa kampuni au ofisa wake mwengine kama anavyoweza kutajwa katika amri kuvitoa vitabu au magazeti au lolote kati yao kwa mtu aliyeatajwa katika amri katika mahali palipotajwa.

(2) Kifungu kidogo cha (1) kitatumika pia kuhusiana na vitabu vyovyote au magazeti ya mtu anayeendesha biashara ya kibenki kwa kadiri kinavyohusiana na mambo ya kampuni hiyo, kama kinavyotumika kwa vitabu au magazeti ya au yaliyo chini ya udhibiti wa kampuni, ila kwamba hakuna amri kama ilivyotajwa katika paragrafu ya (ii) itatolewa kwa mujibu wa kifungu kidogo hiki.

Maombi ya faini.

**271.** Mahakama inayotoza faini yoyote chini ya Sheria hii inaweza kuelekeza kwamba yote au sehemu yake yoyote itatumika katika au kuelekea kwenye malipo ya gharama za kesi, au katika au kuelekea kwenye kumpa mtu zawadi mtu, ambaye habari au kuotokan na mashataka yake faini imepatikana.

Kuwakinga washtaki binafsi.

**272.** Hakuna kitu katika Sheria hii kuhusiana na taasisi ya kesi za jinai na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma kitakachochukuliwa kumtoa mtu yeyote kuanzisha au kuendelea na kesi yoyote kama hiyo.

Kinga kwa mawasiliano ya upendeleo.

**273.** Ambapo kesi imefunguliwa chini ya Sheria hii dhidi ya mtu yeyote na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hakuna kitu katika Sheria hii kitakachochukuliwa kumtaka mtu yeyote ambaye amekuwa mtetezi wa mshtakiwa kufichua mawasiliano yoyote ya upendeleo yanayofanywa kwake katika wadhifa huo.

Kesi za Kisheria Gharama katika matendo ya baadhi ya kampuni zenye ukomo.

**274.** Ambapo kampuni yenye ukomo ni mdai katika tendo lolote au kesi nyengine ya kisheria, hakimu yeyote mwenye mamlaka katika suala hilo, ikiwa inaonekana kwa ushahidi wa kutosha kuwa kuna sababu ya kuamini kwamba kampuni haitaweza kulipa gharama ya mshtakiwa kama akifanikiwa katika utetezi wake, anaweza kutaka dhamana ya kutosha itolewe kwa ajili ya gharama hizo, na anaweza kusitisha kesi yote mpaka dhamana itakapotolewa.

**275.**-(1) Kama katika kesi yoyote ya uzembe, ukiukaji, uvunjaji wa wajibu au uvunjaji wa uaminifu dhidi ya ofisa wa kampuni au mtu aliyeajiriwa na kampuni kama mkaguzi (kama yeye ni au si ofisa wa kampuni) inaonekana na mahakama inayosikiliza kesi hiyo kwamba ofisa au mtu ni au anaweza kuwajibika kuhusiana na uzembe, ukiukaji, uvunjaji wa wajibu au uvunjaji wa uaminifu, lakini kwamba yeye alitekeleza kwa uaminifu na kwa sababu, na kwamba, kwa kuzingatia mazingira yote ya kesi, ikiwa ni pamoja na yale yanayoambatana na uteuzi wake, alipaswa kusamehewa kwa uzembe huo, ukiukaji, uvunjaji wa wajibu au uvunjaji wa uaminifu, mahakama hiyo inaweza kumuondolea, ama kabisa au sehemu, dhima yake kwa masharti kama ambayo mahakama inaweza kuona inafaa. Uwezo wa mahakama kutoa nafuu katika maeneo mengine.

(2) Kama ofisa yeyote au mtu aliyeelezwa awali ana sababu ya kutuhumu kwamba madai yoyote yatafanywa au yangefanywa dhidi yake kuhusiana na uzembe wowote, ukiukaji, uvunjaji wa wajibu au uvunjaji wa uaminifu, yeye anaweza kuomba mahakama kwa ajili ya msamaha, na mahakama juu ya maombi yoyote kama hayo itakuwa na nguvu sawa ya kumsamehe kama chini ya kifungu hiki kama kwamba ingalikuwa ni mahakama ambayo kesi dhidi ya mtu huyo kwa uzembe, ukiukaji, uvunjaji wa wajibu au uvunjaji wa uaminifu ilikuwa imeletwa.

**276.** Maagizo yaliyotolewa na Mahakama Kuu chini ya Sheria hii yanaweza kutekelezwa katika namna ile ile kama maagizo yaliyotolewa katika kesi inayosubiri humo. Uwezo wa kutekeleza amri.

**277.**-(1), Waziri atakuwa na nguvu kwa kanuni zilizochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kubadilisha au kuongeza matakwa ya Sheria hii kuhusu mambo ya kuelezwa katika mizania ya kampuni, hesabu ya faida na hasara na hesabu za vikundi, na hasa za yale yaliyoelezwa katika kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii; na marejeo yoyote katika Sheria hii kwa kanuni zilizoelezwa zitafahamika kuwa zinarejea kwenye kanuni hizo pamoja na mabadiliko yoyote au nyongeza zilizofanywa na kanuni kwa wakati huo zinazotumika chini ya kifungu hiki. Uwezo wa kubadilisha jadweli na fomu.

(2) Waziri anaweza kwa kanuni:-

(a) baada ya Jadweli A, kanuni isipokuwa kwamba haziongezi kiasi cha ada ya kulipwa kwa Mrajis, na fomu iliyoainishwa katika kanuni; na

(b) kubadilisha au kuongeza kwenye Majadweli B, C, D, E na F katika Sheduli ya Kwanza, na fomu katika kanuni;

na jadweli yoyote au fomu inapobadilishwa, itachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, na baada ya hapo itakuwa na nguvu sawa kama kwamba ilikuwa imeingizwa katika mojawapo ya Sheduli za Sheria hii, lakini hakuna mabadiliko yaliyofanywa na Waziri katika Jadweli A yatakayoathiri kampuni yoyote iliyosajiliwa kabla ya mabadiliko, au kufuta kuhusiana na kampuni hiyo sehemu yoyote ya Jadweli hiyo.

(3) Pamoja na madaraka yaliyotolewa humu kabla na kifungu hiki, Waziri anaweza kuweka kanuni kuweka masharti kwa ajili ya yote au mambo yoyote ambayo kwa mujibu wa Sheria hii yanapaswa kuwekwa kwa idhini yake.

Kufuta. **278.** Dikrii ya Kampuni Sura ya 153 imefutwa

## SHEDULI YA KWANZA
## JADWELI A, B, C, D, E NA F
## SEHEMU YA I
## JADWELI A
## KANUNI ZA KUENDESHA KAMPUNI YA UMMA YENYE UKOMO WA HISA

Kufuta. **1.** Katika kanuni hizi:-

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Kampuni;

" kanuni " maana yake ni kanuni za kampuni;

"siku wazi" kuhusiana na muda wa taarifa maana yake ni muda ukitoa siku ambayo taarifa inatolewa au siku ambayo itaanza kutumika;

"mmiliki" kuhusiana na hisa maana yake ni mwanachama ambaye jina lake limeingizwa katika daftari la wanachama kama mmiliki wa;

"muhuri" maana yake ni muhuri wa kawaida wa kampuni;

"katibu" maana yake ni katibu wa kampuni au mtu mwengine yeyote aliyeteuliwa kufanya kazi za katibu wa kampuni.

Matamko yanayorejea kwenye maandishi, isipokuwa dhamiri nyengine imedhihirika, yatachukuliwa kujumuisha uchapishaji, lithografia, fotografia, na njia nyengine za kuwasilisha au kunakili maneno katika hali ya kuonekana.

Isipokuwa muktadha unataka vyenginevyo, maneno au matamko yaliyomo katika Kanuni hizi yatabeba maana sawa na zile zilzizomo katika Sheria au mabadiliko yoyote ya kisheria yaliyomo humo yanayotumika katika tarehe ambayo Kanuni hizi zinaifunga kampuni.

Jumla ya Hisa na Mabadiliko ya Haki. 2. Kwa madhumuni ya masharti ya Sheria hii, na bila kuathiri haki zozote zilizofungamana na hisa zilizopo, hisa yoyote inaweza kutolewa pamoja na haki au vizuizi, iwe kuhusiana na gawio, kupiga kura, marejesho ya mtaji au vyenginevyo kama ambavyo kampuni itaamua kwa azimio la kawaida.

**3.** Kwa madhumuni ya kifungu cha 67 cha Sheria, hisa zozote zinaweza, kwa uamuzi wa azimio la kawaida, kutolewa kwa shuruti, au kwa uchaguzi wa kampuni kuwa zina dhima, kuhesabiwa kwa masharti na kwa namna kama ambavyo kampuni kabla ya hisa kutolewa inaweza kuamua kwa azimio maalumu.

**4.** Iwapo katika wakati wowote jumla ya hisa inagawiwa katika daraja tafauti za hisa, haki zilizofungamana na daraja yoyote (isipokuwa imeelezwa vyenginevyo na masharti ya utoaji wa daraja hiyo) zinaweza kubadilishwa, iwe kampuni inavunjwa au la, kwa ridhaa ya maandishi ya wamiliki wa robo tatu za hisa zilizotolewa kwa daraja hiyo, au kwa uamuzi wa azimio maalumu lililopitishwa kwenye mkutano mkuu maalumu wa wamiliki wa hisa za daraja hiyo. Kwa kila mkutano huo mkuu maalumu masharti ya Kanuni hizi kuhusiana na mikutano mikuu yatatumika, lakini kwa namna ambayo akidi ya lazima itakuwa kwa uchache ni watu wawili wanaomiliki au wanaowakilisha kwa niaba thuluthi moja ya hisa zilizotolewa za daraja hiyo na kwamba kila mmiliki wa hisa wa daraja hiyo aliyepo yeye mwenyewe au kwa niaba anaweza kuomba kupiga kura.

**5.** Haki ambazo wamiliki wa hisa wamepewa za daraja yoyote, isipokuwa imeelezwa wazi na masharti ya utoaji wa hisa za daraja hiyo, hazitahesabiwa kuwa zimebadilishwa kwa kuanzisha au kutoa hisa zaidi zenye daraja sawa.

**6.** Kampuni inaweza kuutumia uwezo wake wa kulipa kamisheni iliopewa na kifungu cha 62 cha Sheria. Bila kuathiri masharti ya Sheria hii, kamisheni hiyo inaweza kutoshelezwa kwa kulipa fedha taslimu au mgao wa hisa zilizolipiwa kamili au zilzizolipiwa sehemu kwa namna moja na sehemu kwa namna nyengine.

**7.** Isipokuwa kama ilivyotakiwa na sheria, hakuna mtu atakayetambuliwa kuwa ni mmiliki wa hisa yoyote kwenye mfuko wowote, na kampuni haitafungika na au kulazimika kwa namna yoyote ile kuitambua (hata kama inaifahamu) hisa yoyote ya kawaida, inayoweza kutokea, ya baadaye au sehemu ya riba katika hisa yoyote au riba yoyote katika sehemu yoyote ya hisa au (isipokuwa imeelezwa vyengine katika Kanuni au sheria) haki nyengine zozote au maslahi kuhusiana na hisa isipokuwa haki halisi ya jumla iliyopo kwa mmiliki aliyesajiliwa.

Hati za Hisa.

**8.** Kila mwanachama, baada ya kuwa mmiliki wa hisa yoyote, atakuwa na haki bila ya kulipa kupata ndani ya miezi miwili baada ya kugawa au kupanga uhaulishaji (au ndani ya kipindi chengine kama ambavyo masharti ya utoaji yatakiweka) hati moja kwa hisa zote za daraja moja zinazomilikiwa naye (na, akihaulisha sehemu ya umiliki wa hisa zake za daraja yoyote, hati ya bakaa za umiliki huo) au hati nyingi kila moja kwa hisa yake moja au hisa zake zaidi ya moja baada ya kulipa kwa kila hati baada ya kiasi cha kuridhisha cha kwanza kama itakavyoamuliwa na wakurugenzi. Kila hati itapigwa muhuri na itaainisha idadi, daraja na namba ainishi (kama zipo) za hisa ambazo zinahusiana nayo na kiasi au viasi vilivyolipwa kwa ajili hiyo.

Isipokuwa kwamba, kuhusiana na hisa ya hisa nyingi zinazomilikiwa kwa pamoja na watu wengi, kampuni haitafungika kutoa zaidi ya hati moja, na utoaji wa hati moja ya hisa kwa mmiliki mmoja wa pamoja utatosheleza kwa utoaji wa wamiliki wote kwa pamoja.

**9.** Ikiwa hati ya hisa imefutika, imechakaa, imepotea au imeharibika inaweza kutolewa mpya kwa masharti (kama yapo) kama ushahidi au kinga na malipo ya gharama ilizoingia kampuni katika kuchunguza ushahidi kama ambavyo wakurugenzi wataamua lakini vyenginevyo bila ya malipo, na (katika hali ya ufutikaji au uchakavu) baada ya kuwasilisha hati kongwe.

**10.** Kampuni haitatoa, ama moja kwa moja au kwa kupitia, na iwapo kwa njia ya mkopo, dhamana, utoaji wa dhamana au vyenginevyo, mssada wowote wa kifedha kwa madhumuni ya au kuhusiana na ununuzi au uchangiaji uliofanywa na mtu yeyote au kwa ajili ya hisa yoyote katika kampuni au katika kampuni yake ya hisa, lakini hakuna kitu chochote katika kanuni hii kitakataza maingiliano ya kibiashara zilizotajwa katika masharti ya kifungu cha 63(1) cha Sheria.

Umiliki.

**11.** Kampuni itakuwa na umiliki wa mwanzo na wa juu kwenye kila hisa (ikiwa si hisa iliyolipiwa kamili) kwa pesa zote (kama zimelipwa sasa hivi au la) zilizotakiwa au zilizolipwa kwa muda maalumu uliowekwa kuhusiana na hisa; lakini wakurugenzi wanaweza wakati wowote kutangaza kwamba hisa yoyote ama yote au sehemu yake imesamehewa na masharti ya kanuni hii. Umiliki wa kampuni, kama upo, juu ya hisa utahusu kwenye kiasi chochote kinacholipwa kuhusiana nayo.

**12.** Kampuni inaweza kuuza, kwa namna ambayo wakurugenzi wameamua, hisa zozote zinazomilikiwa na kampuni ikiwa kiasi kuhusiana na umiliki kinalipwa sasa hivi na hakilipwi ndani ya siku kumi na nne zilizo wazi baada ya taarifa kwa maandishi kupewa mwenye hisa, au mtu anayestahiki kupewa kutokana na sababu ya kifo cha au kufilisika kwa mmiliki, kudai malipo na kueleza kwamba iwapo taarifa haikutekelezwa hisa zinaweza kuuzwa.

**13.** Ili kutekeleza uuzaji huo wakurugenzi wanaweza kumuidhinisha mtu kuhaulisha hisa alizouziwa, au kwa mujibu wa maelekezo ya mnunuzi wa hisa hizo. Mnunuzi atasajiliwa kama mmiliki wa hisa zilizomo katika uhaulishaji huo, na hatafungika kuona maombi ya pesa za kununulia, wala jina lake katika hisa halitaathiriwa na upungufu au kutofaa katika mwenendo kuhusiana na mauzo.

**14.** Mapato halisi ya mauzo yatapokewa na kampuni na kutumika katika malipo ya sehemu ya kiasi hicho kuhusiana na umiliki uliopo kama ambavyo yanalipwa sasa hivi, na bakaa, kama ipo, italipwa (baada ya kuwasilisha hati ya hisa zilizouzwa kwenye kampuni kwa ajili ya kufutwa na kwa kuzingatia umiliki kama huo kwa viasi ambavyo havilipwi sasa hivi kama ilivyokuwa kwenye hisa kabla ya mauzo) kwa mtu anayestahiki kumiliki hisa, katika tarehe ya mauzo.

Matangazo ya Hisa.

**15.** Kwa kuzinagatia masharti ya ugawaji, wakurugenzi wanaweza kila baada ya muda kutangaza kwa wajumbe kuhusiana na fedha zozote ambazo hazijalipwa juu ya hisa (kama ni kuhusiana na thamani ya msingi au bonsi) na si kwa masharti ya ugawaji huo yaliyofanywa ya kulipa katika nyakati maalumu, isipokuwa kwamba hakuna tangazo litakalozidi robo moja ya thamani ya msingi ya au kulipwa kwa chini ya mwezi mmoja kutoka tarehe iliyowekwa kwa ajili ya malipo ya tangazo la mwisho lililotangulia, na kila mwanachama (kwa kuzingatia kupata angalau siku kumi na nne za wazi za taarifa inayoainisha lini na wapi malipo yanapaswa kufanywa) atailipa kampuni kama inavyotakiwa na taarifa kiasi kilichotangazwa juu ya hisa zake. Tangazo linaweza kutakiwa kulipwa kwa awamu. Tangazo linaweza, kabla ya kupokewa na kampuni kiasi kinachohusika, kufutwa lote au sehemu yake na malipo ya tangazo yanaweza kufutwa yote au sehemu yake. Mtu ambaye anatangaziwa atakuwa na dhima juu ya matangazo yaliyotolewa kwa ajili yake bila ya kujali uhaulishaji wa baadaye wa hisa zilizotolewa tangazo.

**16.** Tangazo litahesabiwa kuwa limetolewa katika wakati ambao azimio la wakurugenzi la kuidhinisha tangazo lilipitishwa.

**17.** Wamiliki wa pamojan wa hisa watakuwa kwa pamoja na mmoja mmoja na dhima ya kulipa matangazo yote yanayohusiana nao.

**18.** Iwapo tangazo linabakia bila ya kulipwa baada ya kufika wakati wake na linalipika, mtu ambaye kiasi cha kulipwa kinamthibitikia atalipa riba juu ya kiasi ambacho hakijalipwa kutoka siku ambayo kilipaswa kulipwa na kulipika mpaka wakati ambapo malipo halisi yalipofanywa kwa kima kilichowekwa na masharti ya ugawaji wa hisa, ikiwa hakuna kima kilichowekwa, kwa kima kisichozidi asilimia tano kwa mwaka kama watakavyoamua wakurugenzi, lakini wakurugenzi wanaweza kuondoa malipo ya riba hiyo yote au sehemu.

**19.** Kiasi kinacholipika kuhusiana na hisa inayogawiwa au katika tarehe yoyote iliyowekwa, kama ni kuhusiana na thamani ya msingi au bonsai au kama mkupuo wa tangazo, kitahesabika kuwa tangazo, na kama hakikulipwa masharti ya kanuni yatatumika kama kwamba kiasi kilipitwa na wakati na kulipika kwa kuzingatia tangazo.

**20.** Kwa kuzingatia masharti ya ugawaji, wakurugenzi wanaweza, kuhusu utoaji wa hisa, kutafautisha baina ya wamiliki kulingana na jumla ya matangazo ya kulipiwa na mara za kulipa.

**21.** Wakurugenzi wanaweza, kama wanaona inafaa, kupokea kutoka mwanachama yeyote anayetaka kutanguliza malipo, yote au sehemu ya fedha ambazo hazikutangazwa na hazikulipwa juu ya hisa zinazomilikiwa naye, na juu ya fedha zote au fedha zozote ziizotangulizwa hivyo zinaweza (mpaka pale ambapo fedha hizo, isipokuwa kwa kitangulizi hicho, zitakapokuwa zimelipwa) kulipa riba kwa kiasi ambacho hakizidi (isipokuwa kampuni katika mkutano mkuu itaelekeza vyenginevyo) asilimia sita kwa mwaka, kama ambavyo itakubaliwa baina ya wakurugenzi na wanachama wanaolipa kiasi hicho kama kutangulizi.

Uhaulishaji wa Hisa.

**22.** Hati ya uhaulishaji wa hisa yoyote itakuwa katika umbo lolote lile la kawaida au umbo jengine lolote ambalo wakurugenzi wataelekeza na itatekelezwa na au kwa niaba ya mhaulishaji na, isipokuwa hisa imelipwa kamili, na au kwa niaba ya anayehaulishiwa, na mhaulishaji atahesabika kubakia mmiliki wa hisa mpaka jina la anayehaulishiwa linapoingizwa katika daftari la wanachama kuhusiana na uhaulishaji huo.

**23.** Mkurugenzi anaweza kukataa kusajili uhaulishaji wa hisa ambayo haijalipiwa kamili kwa mtu ambaye hawajamthibitisha na wanaweza kukataa kusajili uhaulishaji wa hisa ambayo kampuni ina umiliki.

**24.** Wakurugenzi wanaweza pia kukataa kusajili uhaulishaji isipokuwa kama:-

(a) umeletwa ofisini au mahali pengine wakurugenzi watakapoteua, na umeambatatana na hati ya hisa inazohusiana nazo, na ushahidi mwengine kama ambavyo wakurugenzi watataka kuonesha haki ya mhaulishaji kufanya uhaulishaji huo; na

(b) umehusu daraja moja tu la hisa; na

(c) inawahusu wahaulishiwa wasiozidi wanne.

**25.** Iwapo wakurugenzi wanakataa uhaulishaji, ndani ya siku sitini baada ya tarehe uhaulishaji ulipoombwa kwenye kanuni, watapeleka kwa mhaulishiwaji taarifa ya kukataa.

**26.** Usajili wa uhaulishaji wa hisa au uhaulishaji wowote wa daraja yoyote ya hisa unaweza kusitishwa katika wakati na kwa vipindi (visivyozidi siku thalathini katika mwaka) kama watakavyoamua wakurugenzi.

**27.** Hakuna ada itakayotozwa na kampuni kwa usajili wa hati yoyote ya uhaulishaji au waraka mwengine kuhusiana na au kuathiri jina kwenye hisa yoyote.

Urithishaji wa Hisa.

**28.** Itokeapo kufa mwanachama, mtu aliye hai wa wale walio hai kama marehemu alikuwa ni mmiliki wa pamoja, na wawakilishi binafsi wa marehemu kama alikuwa mmiliki wa pekee au peke yake aliye hai miongoni mwa wamiliki wa pamoja, watakuwa ndio watu peke yao wanaotambuliwa na kampuni kuwa wana jina kuhusu maslahi kwenye hisa zake; lakini hakuna jambo hapa litakalotoa mali ya mwanachama aliyefariki kutoka dhima yoyote kuhusiana na hisa yoyote ambayo ilikuwa inamilikiwa kwa pamoja na yeye.

**29.** Mtu yeyote ambaye anastahiki kupata hisa kutokana na kifo au kufilisika mwanachama anaweza, baada ya ushahidi kutolewa kama itakavyotakiwa na wakurugenzi na kwa kuzingatia masharti yaliyomo humu, ama kuchagua kwa taarifa kwa kampuni inayotaka kusajiliwa kuwa ni mmiliki wa hisa, au kuchagua kuwa na mtu aliyeteuliwa na yeye kusajiliwa kama mhaulishiwaji ambapo katika hali hiyo atatekeleza hati muafaka ya uhaulishaji.

**30.** Ikiwa mtu ambaye ana haki hiyo atachagua kusajiliwa yeye binafsi, atawasilisha au atapeleka taarifa kwenye kampuni kwa maandishi iliyotiwa saini na yeye mwenyewe ikieleza kwamba anachagua hivyo. Ikiwa atachagua kuwa na mtu mwengine kusajiliwa atathibitisha uchaguzi wake kwa kutekeleza uhaulishaji wa hisa hizo kwa yule mtu. Kanuni zote zinazohusu haki ya kuhaulisha hisa zitatumika kwa taarifa au uhalishaji huo kama kwamba ilikuwa hati ya uhaulishaji iliyotekelezwa na mwanachama na kama kwamba kifo au kufilisika hakukutokea.

**31.** Mtu yeyote ambaye anastahiki kupata hisa kutokana na kifo au kufilisika mwanachama atakuwa na haki amabyo kwayo angestahiki kama yeye angekuwa mmiliki aliyesajiliwa wa hisa, isipokuwa kwamba, kabla hajasajiliwa kama mmiliki wa hisa, hatastaki kuhusiana na hisa hiyo kutekeleza haki yoyote inayotolewa kwa uanachama kuhusiana na mikutano ya kampuni.

Upotezaji wa Hisa.

**32.** Iwapo tangazo linabakia bila ya kulipwa baada ya kupita muda wake na kulipika, wakurugenzi wanaweza kumpa mtu ambaye anastahiki si chini ya siku kumi na nne zilizo wazi taarifa kumtaka alipe malipo ya kiasi ambacho hakijalipwa, pamoja na riba yoyote ambayo imapatikana.

**33.** Taarifa itataja mahali ambapo malipo yatafanywa na itaeleza kwamba endapo taarifa haitatekelezwa, hisa zinazohusiana na tangazo lililotolewa zitapotea.

**34.** Endapo taarifa haikutekelezwa, hisa yoyote ambayo ilitolewa kwayo, kabla ya malipo yaliyotakiwa na taarifa kuwa yamefanywa, itapotezwa kwa azimio la wakurugenzi kuhusiana na jambo hilo na upoteaji huo utajumuisha gawio lote au fedha nyengine zinazolipwa kuhusiana na hisa zilizopotezwa na ambazo hazikulipwa kabla ya upotezaji.

**35.** Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, hisa iliyopotezwa inaweza kuuzwa, kugawiwa tena au vyenginevyo kuachwa kwa masharti na kwa namna ambayo wakurugenzi wataelekeza ama kwa mtu ambaye kabla ya upotezaji alikuwa ni mmiliki au kwa mtu mwengine yeyote, na wakati wowote kabla ya uuzaji, ugawaji mpya au hali nyengine upotezaji unaweza kufutwa kwa masharti ambayo wakurugenzi wanaona yanafaa. Ambapo kwa madhumuni ya upotezwaji wake hisa iliyopotezwa inataka kuhaulishwa kwa mtu yeyote, wakurugenzi wanaweza kuidhinisha mtu kutekeleza hati ya uhaulishaji wa hisa inayohusika.

**36.** Mtu ambaye hisa zake zozote zimepotezwa atasita kuwa mwanachama kuhusiana na hisa zilizopotezwa na atawasilisha kwenye kampuni ili ifutwe hati ya hisa zilizopotezwa, lakini atabakia kuwa na dhima kwenye kampuni kwa fedha zote ambazo, katika tarehe ya upotezaji, zilikuwa zilipwe na yeye kwa kampuni kuhusiana na hisa, lakini dhima yake itasita ikiwa na ambapo kampuni imepokea malipo kamili ya fedha zote kuhusiana na hisa, lakini wakurugenzi wanaweza kufuta malipo yote au sehemu yake au kulazimisha malipo bila ya punguzo kwa thamani ya hisa kwa wakati wa upotezaji kwa mazinagtio yoyote yaliyopokelewa waliyokuwa nayo.

**37.** Tangazo la kisheria la mkurugenzi au katibu kwamba hisa imepotezwa katika tarehe iliyotajwa katika tangazo litakuwa ni ushahidi wa mwisho wa taarifa zilizoelezwa humo dhidi ya watu wote ambao wanadai kuwa na haki kwenye hisa, na tangazo, (kwa kuzingatia utekelezaji wa hati ya uhaulishaji ikiwa ni lazima) litajenga jina zuri kwenye hisa, na mtu ambaye hisa inaondolewa hatafungika kuona utekelezaji wa mazingatio, kama yapo, wala haki yake kwenye hisa haitaathiriwa na upungufu wowote au kutofaa kwa taratibu kuhusiana na upotezaji au uondoaji wa hisa.

**38.** Masharti ya kanuni hizi kuhusiana na upotezaji zitatumika katika hali ambayo hapajalipwa kiasi chochote ambacho kwa masharti ya utoaji wa hisa kinapaswa kulipwa katika wakati maalumu uliowekwa, ama kwenye hisabu ya thamani ya msingi ya hisa, au kwa njia ya bonasi, kama kwamba malipo hayo yalifanywa kwa tangazo lililotolewa na kutolewa taarifa.

Kubadilisha Hisa Kuwa Bidhaa

**39.** Kampuni inaweza kwa azimio la kawaida kubadilisha hisa zozote zilizolipwa kuwa bidhaa, na kubadilisha tena bidhaa zozote kuwa hisa zilizolipwa za kiwango chochote.

**40.** Wamiliki wa bidhaa wanaweza kuzihaulisha, au sehemu yake yoyote, kwa namna ile ile, na kwa kuzingatia kanuni zile zile, kuhusiana na kwa kuzingatia hisa ambazo bidhaa zilizotokana nazo zingeweza kuwa kabla ya kubadilishwa zingeweza kuhaulishwa, au karibu na hivyo kadiri hali itakavyoruhusu; na wakurugenzi kila baada ya muda wataweka kiasi cha chini cha bidhaa zinazoweza kuhaulishwa lakini kwa namna ambayo hakitazidi idadi ya msingi ya hisa ambazo kutoka kwao bidhaa ziliibuka.

**41.** Wamiliki wa bidhaa watakuwa, kulingana na bidhaa zinazomilikiwa na wao, na haki zile zile, fursa na manufaa kuhusiana na gawio, kupiga kura kwenye mikutano ya kampuni na masuala mengine kama kwamba walimiliki hisa ambazo kutoka kwao bidhaa ziliibuka, lakini fursa au manufaa hayo (isipokuwa kushiriki katika gawio na faida za kampuni na katika raslimali wakati wa kufungwa) hazitatolewa kwa kiasi cha bidhaa ambazo, kama zingekuwa katika hisa, zingetolewa fursa au manufaa hayo.

**42.** Masharti hayo ya kampuni kama yanavyotumika kwenye hisa zilizolipwa yatatumika kwenye bidhaa, na maneno "hisa" na "mmiliki wa hisa" yatajumuisha "bidhaa" na "mmiliki wa bidhaa".

Marekebi-sho ya Mtaji

**43.** Kampuni kila baada ya kipindi inaweza, kwa azimio la kawaida:-

(a) kuongeza jumla ya hisa zake kwa hisa mpya za kiasi ambacho azimio linaweka;

(b) kuunganisha na kugawa zote au jumla yoyote ya hisa zake katika hisa za kiasi kikubwa kuliko hisa zake za sasa;

(c) kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 71(1)(d) cha Sheria, kugawanya hisa zake zilizopo, au zozote kati yao, katika hisa za kiasi kidogo kuliko kilichowekwa na katiba ya jumuiya;

(d) kufuta hisa amabazo, katika tarehe ya kupitisha azimio, hazijachukuliwa au hazijakubaliwa kuchukuliwa na mtu yeyote na kupunguza kiasi cha jumla ya hisa zake kwa kiasi cha hisa ambazo zimefutwa.

**44.** Kila itakapotokea kwamba kutokana na kuunganishwa hisa mwanachama yeyote atakuwa na haki ya sehemu ya hisa, wakurugenzi wanaweza, kwa niaba ya wanachama hao, kuuza hisa zinazowakilisha sehemu kwa bei nzuri kabisa inayopatikana kwa mtu yeyote (pamoja na kuzingatia masharti ya Sheria hii) na kuigawa faida hiyo ya mauzo kwa sehemu zinazowiana miongoni mwa wanachama hao, na wakurugenzi wanaweza kuidhinisha mtu kutekeleza hati ya uhaulishaji kwa au kwa mujibu wa maelekezo ya mnunuzi. Mhaulishiwaji hatafungika kuona maombi ya fedha ya kununulia wala haki yake kwenye hisa haitaathiriwa na kasoro yoyote au kutofaa kwa taratibu kuhusiana na mauzo.

**45.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria, kampuni inaweza kwa azimio maalumu kupunguza jumla ya hisa zake, fedha yoyote ya mtaji wa akiba au akaunti yoyote ya bonasi ya hisa kwa namna yoyote.

Mikutano Mikuu

**46.** Kampuni itaitisha mkutano mkuu katika kila mwaka kama mkutano wake mkuu wa mwaka zaidi ya mikutano myengine katika mwaka ule, na itaainisha mikutano hiyo katika taarifa za kuiitisha; na si zaidi ya miezi kumi na tano itamalizika baina ya tarehe ya mkutano mmoja mkuu wa mwaka wa kampuni na ule wa mwaka mwengine.

**47.** Mikutano myengine yote mikuu isiyokuwa mikutano mikuu ya mwaka itaitwa mikutano mikuu ya dharura.

**48.** Wakurugenzi wanaweza, kila wanapoona inafaa, kuitisha mkutano mkuu wa dharura, na mkutano mkuu wa dharura utaitishwa kutokana na ulazima, au, kwa kukosekana, unaweza kuitishwa kwa dharura, kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 138 cha Sheria. Itokeapo wakati wowote hapana idadi ya kutosha ya wakurugenzi ya kuwezesha kuitisha mkutano, mkurugenzi yoyote au wanachama wawili wowote wa kampuni wanaweza kuitisha mkutano kwa namana ile ile kadiri inavyoyumkinika kama vile ambavyo mikutano inaweza kuitishwa na wakurugenzi.

Taarifa ya Mikutano Mikuu.

**49.** Kila mkutano mkuu utaitishwa kwa taarifa ya maandishi ya siku wazi ishirini na maoja. Taarifa itaainisha wakati na mahali pa mkutano na sura ya jumla ya shughuli na, kwa mkutano mkuu wa mwaka, itauainisha mkutano kuwa ni wa aina hiyo;

Isipokuwa kwamba mkutano wa kampuni unaweza kuitishwa kwa taarifa ya muda mfupi ikiwa imekubaliwa hivyo:-

(a) kwa mkutano mkuu wa mwaka, kwa wanachama wote wanaostahiki kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano huo; na

(b) kwa mkutano mwengine wowote kwa idadi kubwa ya wanachama wenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura katika

mkutano, idadi hiyo ikiwa kwa pamoja wanamiliki si chini ya asilimia 95 ya thamani ya msingi ya hisa inayowapa haki hiyo.

**50.** Kwa kuzingatia masharti ya kanuni na vizuizi vyovyote vilivyowekwa juu ya hisa zozote, taarifa itapewa wanachama wote, kwa watu wote wanaostahiki kuwa na hisa kwa kifo au kufilisika mwanachama na kwa wakurugenzi na wakaguzi. Uachaji wa bahati mbaya wa kutoa taarifa ya mkutano kwa, au kutokupata taarifa ya mkutano na, mtu yeyote anayestahiki kupata haitabatilisha taratibu za mkutano.

Taratibu za Mikutano Mikuu.

**51.** Shughuli yote itahesabika kuwa ni maalumu ile ambayo inajadiliwa kwenye mkutano mkuu wa dharura, na pia ile inayojadiliwa kwenye mkutano mkuu wa mwaka, ukiacha kutangaza gawio, mazingatio ya hesabu, na ripoti za wakurugenzi na wakaguzi, uchaguzi wa wakurugenzi kuchukua nafasi ya wale waliostaafu na uteuzi wa, na kupanga mafao ya wakaguzi.

**52.** Hakuna shughuli itakayojadiliwa kwenye mkutano mkuu wowote isipokuwa akidi ya wajumbe imetimia wakati wa mkutano unaoendelea na shughuli; watu wawili wenye haki ya kupiga kura juu ya shughuli itakayojadiliwa, kila mmoja wao akiwa ni mwanachama au wakala wa mwanachama au mwakilishi aliyeidhinishwa kabla wa shirika, atakuwa ni akidi.

**53.** Endapo ndani ya nusu saa kutoka wakati uliopangwa kufanyika mkutano akidi haijatimia, au endapo wakati mkutano unaendelea akidi ikasita kutimia, mkutano utakuwa umeahirishwa mpaka siku kami le ya wiki inayofuata, wakati ule ule na mahali pale pale au mpaka siku nyengine wakati mwengine kama wakurgenzi watakavyoamua.

**54.** Mwenyekiti, kama yupo, wa bodi ya wakurugenzi au ikiwa hayupo mkurugenzi mwengine aliyeteuliwa na wakurugenzi ataendesha mkutano kama mwenyekiti wa mkutano mkuu na, iwapo yupo mkurugenzi mmoja tu aliyehudhuria na anataka kukaimu, atakuwa mwenyekiti.

**55.** Endapo kwenye mkutano wowote hakuna mkurugenzi anayetaka kukaimu kama mwenyekiti au endapo hakuna mkurugenzi aliyehudhuria ndani ya dakika kumi na tano baada ya muda uliopangwa wa kuendesha mkutano, wanachama waliopo watachagua mmoja wapo miongoni mwao kuwa mwenyekiti wa mkutano.

**56.** Mkurugenzi, bila ya kujali kuwa yeye si mjumbe, atastahiki kuhudhuria na kuzungumza kwenye mkutano mkuu na kwenye mkutano mwengine wowote wa wamiliki wa hisa za daraja yoyote katika kampuni.

**57.** Mwenyekiti anaweza, kwa ridhaa ya mkutano wowote ambao akidi imetimia na ikiwa ameelekezwa hivyo na mkutano, kuakhirisha mkutano kutoka wakati mmoja hadi wakati mwengine na kutoka mahali pamoja hadi mahali pengine, lakini hakuna shughuli nyengine itakayofanywa kwenye mkutano wowote ulioakhirishwa isipokuwa shughuli ambayo ingeweza kushughulikiwa vyema katika mkutano kama usingeakhirishwa. Mkutano unapoakhirishwa kwa muda wa siku kumi na nne au zaidi, kwa uchache siku wazi saba na sura ya jumla ya shughuli itakayojadiliwa kwenye mkutano ulioakhirishwa.

**58.** Katika mkutano wowote mkuu azimio lililowekwa kupigiwa kura kwenye mkutano litaamuliwa kwa kuinua mikono isipokuwa upigaji wa kura (kabla au katika kutangaza matokeo ya kuinua mikono) umeombwa:-

(a) na mwenyekiti;

(b) na angalau wajumbe wawili wenye haki ya kupiga kura kwenye mkutano huo; au

(c) na mjumbe au wajumbe wanaowakilisha si chini ya sehemu moja katika kumi ya haki zote za kupiga kura za wajumbe wote wenye haki ya kupiga kura katika mkutano huo; au

(d) na mjumbe au wajumbe wanaomiliki hisa wenye haki ya kupiga kura kwenye mkutano zikiwa hisa zenye jumla ya pamoja zimelipwa sawasawa kwa kiasi kisichopungua sehemu moja katika kumi ya jumla yote iliyolipwa kwa hisa zote zilizotoa haki; na

(e) na mtu ambaye ni wakala wa mjumbe atakuwa ni sawasawa na matakwa ya mjumbe.

**59.** Isipokuwa kwamba uchaguzi ulioombwa ufanywe hivyo, tangazo la mwenyekiti kwamba azimio kwa kuinua mikono limepitishwa au limepitishwa bila ya kupingwa, au kwa wingi wa kura, au halikupitishwa, au halikupitishwa kwa wingi wa kura na uingizwaji wake kwenye kumbukumbu za mkutano utakuwa ni ushahidi wa uamuzi huo.

**60.** Ombi la kutaka upigaji wa kura linaweza, kabla ya upigaji wa kura kufanywa, kuondolewa.

**61.** Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 54, iwapo upigaji kura umeombwa utafanywa kwa namna ambayo mwenyekiti ataelekeza, na matokeo ya upigaji kura yatahesabika kuwa ni uamuzi wa mkutano ambao upigaji kura uliombwa.

**62.** Endapo idadi za kura zitalingana, kama ni kwenye kuinua mikono au katika upigaji wa kura, mwenyekiti wa mkutano atakuwa na haki ya kura ya uamuzi zaidi ya kura nyengine yoyote aliyonayo.

**63.** Upigaji wa kura ulioombwa katika uchaguzi wa mwenyekiti au juu ya suala la kuakhirishwa utafanywa pale pale. Upigaji wa kura ulioombwa kwa suala jengine lolote utafanywa ama pale pale au katika wakati mwengine usiozidi siku thalathini baada ya upigaji wa kura kuombwa kama mwenyekiti wa mkutano atakavyoelekeza, na shughuli nyengine yoyote isipokuwa hiyo ambayo imeombewa upigaji wa kura inaweza kuendeshwa na kuwekwa upande kwa muda upigaji wa kura.

**64.** Azimio kwa maandishi lililotekelezwa na au kwa niaba ya kila mjumbe ambaye angestahiki kulipigia kura kama lingependekezwa kwenye mkutano mkuu ambao yeye alihudhuria litakuwa na athari kama kwamba lilipitishwa kwenye mkutano mkuu ulioitishwa na kufanywa, na linaweza kuwa na hati zinazofanana kila moja ikitekelezwa na au kwa niaba ya mjumbe mmoja au zaidi ya mmoja.

Kura za Wajumbe.

**65.** Kwa kuzingatia haki zozote au vizuizi vyoyote vilivyofungamana na hisa yoyote au daraja yoyote ya hisa, katika kuinua mikono kila mjumbe (akiwa ni mtu binafsi) aliyepo yeye mwenyewe au (likiwa shirika) akiwapo baada ya kuidhinishwa kabla kama mwakilishi, yeye mwenyewe akiwa si mjumbe mwenye haki ya kupiga kura, na katika kupiga kura kila mjumbe atakuwa na kura moja kwa kila hisa ambayo anaimiliki.

**66.** Kwa wamiliki wa pamoja kura ya mkuu wao ambaye anapiga kura, ama yeye mwenyewe au kwa kuwakilishwa, itakubaliwa kwa kuenguliwa kura nyengine za wamiliki wenzake washirika; na kwa madhumuni hayo ukubwa utaamuliwa kwa mpangilio ambao majina yamekaa katika daftari la wanachama.

**67.** Mjumbe ambaye mali yeke imeteuliwa meneja chini ya kifungu cha 34 cha Sheria ya Maradhi ya Akili, anaweza kupiga kura, ama kwa kuinua mikono au kwa kupiga kura, kwa meneja wake, na meneja huyo anaweza, wakati wa kupiga kura, kupiga kura kwa niaba.

**68.** Hakuna mjumbe atakayekuwa na haki ya kupiga kura katika mkutano mkuu au katika mkutano mwengine wa wamiliki wa hisa za daraja yoyote ya hisa katika kampuni isipokuwa matangazo yote au viasi vyote vinavyopaswa kulipwa na yeye kuhusiana na hisa katika kampuni ziwe zimelipwa.

**69.** Hakuna pingamizi itakayotolewa juu ya sifa ya mpiga kura yoyote isipokuwa katika mkutano au mkutano ulioakhirishwa ambao kura inayopingwa imepigwa, na kila kura ambayo haikupingwa katika mkutano huo itakuwa halali kwa madhumuni yote. Pingamizi yoyote iliyotolewa katika wakati muafaka itawasilishwa kwa mwenyekiti wa mkutano, ambaye uamuzi wake utakuwa wa mwisho na wenye kuthibitisha.

**70.** Katika kupiga kura voti zinaweza kupewa mtu mwenyewe au kwa niaba. Mjumbe anaweza kuteua zaidi ya wakala mmoja kuhudhuria katika upigaji wa kura.

**71.** Hati inayomteua wakala itakuwa ya maandishi inayotekelezwa na au kwa niaba ya mteuaji au ya wakala wake aliyeidhinishwa kabla kwa maandishi, au endapo mteuaji ni shirika, ama chini ya muhuri, au chini ya saini ya ofisa au mwanasheria aliyeidhinishwa kabla. Wakala si lazima awe mwanachama wa kampuni.

**72.** Hati inayomteua wakala na idhini yoyote ambayo kwayo inatekelezwa nakala ya idhini hiyo iliyothibitishwa rasmi au kwa namna nyengine kama ilivyoidhinishwa na wakurugenzi itawekwa kwenye ofisi iliyosajiliwa ya kampuni au katika mahali pengine ndani ya Zanzibar kama ilivyoainishwa kwa madhumuni hayo katika taarifa inayoitisha mkutano, si chini ya saa 48 kabla ya wakati wa kuendesha mkutano au mkutano ulioakhirishwa ambao mtu aliyetajwa anapendekeza kupiga kura, au, kwa upande wa upigaji wa kura, si chini ya saa 24 kabla ya wakati uliopangwa kwa ajili ya upigaji wa kura, na ikikiukwa hati ya wakala haitahesabika kuwa ni halali.

**73.** Hati inayomteua wakala itakuwa katika fomu ifuatayo au katika fomu inayokaribiana nayo kama hali inavyoruhusu:
"____________________ Yenye ukomo __________________________
Mimi/sisi _____________________ wa. ___________________ tukiwa _____________ni mwanachama/wanachma wa kampuni iliyotajwa hapo juu, hapa tunamteua __________________ wa _____________________.
Au akikosekana, ______________ wa __________________
kama wakala wangu/wetu kunipigia/kutupigia kura kwa niaba yangu/yetu kwenye (mkutano wa mwaka au wa dharura, kama hali itakavyokuwa) mkutano mkuu wa kampuni utakaofanyika siku ya ______ tarehe __________, 20__, na kwenye kuakhirishwa kokote kwa mkutano huo.
Imetiwa saini siku ya ____________________ tarehe __________, 20 __,"

**74.** Pale ambapo inatakiwa kuwapatia wanachama fursa ya kupiga kura kuunga mkono au kupinga azimio hati ya kuteua wakala itakuwa katika fomu inayofuata au fomu inayokaribiana nayo kama hali inavyoruhusu:
"____________________ Yenye ukomo __________________________
Mimi/sisi ____________________wa.____________________ tukiwa _____________ni mwanachama/wanachama wa kampuni iliyotajwa hapo juu, hapa tunamteua, ___________________ wa _____________________
au akikosekana, ______________ wa __________________ kama wakala wangu/wetu kunipigia/kutupigia kura kwa naba yangu/yetu kwenye (mkutano wa mwaka au wa dharura, kama hali itakavyokuwa) mkutano mkuu wa kampuni utakaofanyika siku ya ______tarehe__________, 20__, na kwenye kuakhirishwa kokote kwa mkutano huo.
Imetiwa saini siku ya ____________________ tarehe __________, 20 __,"

*Fomu hii itatumika kuunga mkono /kupinga maazimio n.k. isipokuwa imeelekezwa vyenginevyo, wakala atapiga kura kama anavyoona yeye inafaa au kuacha kupiga kura.

**75.** Hati inayomteua wakala itahesabika kumpa uwezo wa kutaka au kujumuika katika kutaka uchaguzi.

**76.** Kura iliyotolewa kwa mujibu wa masharti ya hati ya wakala, au kwa mwakilishi aliyeidhinishwa kabla wa shirika itakuwa halali bila ya kujali kuwa uamuzi wa kabla ulipokewa na kampuni kwenye ofisi yake iliyosajiliwa (au mahali pengine ambapo hati hiyo au wakala uliwasilishwa kabla) kabla ya kuanza mkutano au mkutano ulioahirishwa ambao wakala unatumika.

Mashirika Yanayowakilishwa na Wawakilishi Kwenye Mikutano

**77.** Shirika lolote ambalo ni mwaanachama wa kampuni kwa azimio la wakurugenzi wake au chombo chengine kinachotawala kinamuidhinisha mtu ambaye linafikiri anafaa kutenda kama mwakilishi wake kwenye mkutano wowote wa kampuni au wa daraja yoyote ya wanachama wa kampuni, na mtu aliyeidhinishwa hivyo atastahiki kutekeleza uwezo sawa kwa niaba ya shirika ambalo analiwakilisha kama ule ambao shirika lile lingeweza kutekeleza kama lilikuwa ni mwanachama mmoja wa kampuni.

Wakurugenzi.

**78.** Idadi ya wakurugenzi na majina ya wakurugenzi wa awali yataamuliwa kwa maandishi na wachangiaji wa katiba ya kujiunga au idadi

kubwa ya wao na mpaka uamuzi huo uliotolewa waliotia saini kwenye katiba ndio watakaokuwa wakurugenzi wa awali. Isipokuwa kwamba imeamuliwa vyengine kwa azimio la kawaida, idadi ya wakurugenzi haitahusishwa na kiwango cha juu lakini haitakuwa chini ya wakurugenzi wawili.

**79.** Sifa ya kumiliki hisa kwa wakurugenzi inaweza kuwekwa na kampuni katika mkutano mkuu, na isipokuwa na mpaka hapo itakapowekwa sifa yoyotye haitatakiwa.

Uwezo na Majukumu ya Wakurugenzi.

**80.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria, katiba na kanuni na maelekezo yoyote yalitolewa na azimio maalumu lolote, shughuli za kampuni zitaendeshwa na wakurugenzi, ambao wanaweza kutumia uwezo wote wa kampuni. Hakuna mabadiliko ya katiba au kanuni na hakuna maelekezo yatakayobatilisha tendo lolote lililotekelezwa kabla na wakurugenzi ambalo vyenginevyo lingekuwa halali. Uwezo uliotolewa katika kifungu hiki kwa wakurugenzi hautapunguzwa na uwezo wowote maalumu uliotolewa kwa wakurugenzi na kanuni na mkutano wa wakurugenzi ambao akidi imetimia unaweza kutumia uwezo wote ambao unaweza kutumiwa na wakurugenzi.

**81.** Wakurugenzi kwa hati ya idhini ya kisheria wanaweza kumteua mtu yeyote kuwa wakala au ajenti wa kampuni kwa madhumuni na kwa masharti kama watakavyoamua, ikiwemo uwezo wa wakala au ajenti kukasimu madaraka yake yote au baadhi ya madaraka yake.

**82.** Wakurugenzi wanaweza kutumia uwezo wote wa kampuni kukopa pesa, na kuweka rahani au kutoza ada biashara yake, mali na mtaji ambao haujatumika, au sehemu yake yoyote, na kutoa dhamana, dhamana ya bidhaa, na dhamana nyengine ama moja kwa moja au kama dhamana kwa deni yoyote, dhima au jukumu la kampuni la mshirika yoyote wa tatu.

**83.** Kampuni inaweza kutumia uwezo iliyopewa kampuni na kifungu cha 126 hadi 129 cha Sheria kuhusiana na kuweka daftari la tawi, na wakurugenzi wanaweza (kwa kuzingatia vifungu hivyo) kuweka na kubadilisha kanuni kama wanavyoona inafaa wakihishimu uwekaji wa daftari laina hiyo lolote.

Uteuzi wa Wakurugenzi na Maslahi Yao.

**84.** Wakurugenzi wanaweza kuteua mmoja au zaidi katika idadi yao kwenye cheo cha mkurugenzi mtendaji au ofisa mtendaji mwengine yeyote chini ya kampuni na wanaweza kuingia katika makubaliano au utaratibu na mkurugenzi yoyote kwa uajiri wake kwa kampuni au kwa utoaji wake wa huduma zozote nje ya mawanda ya majukumu yake ya kawaida ya mkurugenzi. Uteuzi, makubaliano au utaratibu wa namna hiyo wowote, unaweza ukafanywa kwa masharti ambayo wakurugenzi watayaweka na wanaweza kumlipa mukurugenzi kama huyo yeyote kwa huduma zake kama wanavyoona inafaa. Uteuzi wowote wa mkurugenzi kwenye cheo cha utendaji utamalizika ikiwa atasita kuwa mkurugenzi, lakini bila ya kuathiri madai yoyote kuhusiana na fidia kutokana na kuvunjwa mkataba wa kazi baina ya mkurugenzi na kampuni. Mkurugenzi mtendaji ambaye anashikilia cheo chengine chochote cha utendaji hatawajibika kustaafu kwa mzunguko.

**85.** Mkurugenzi ambaye kwa njia yoyote, ama moja kwa moja au si moja kwa moja anayependelea mkataba au mkataba anayependekeza mkataba na kampuni atatangaza maumbile ya mapendekezo yake katika mkutano wa wakurugenzi kwa mujibu wa kifungu cha 213 cha Sheria.

**86.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria, na kwa sharti kwamba amewatambulisha wakurugenzi maumbile na mawanda manufaa yake ya mali, mkurugenzi bila ya kujali cheo chake:-

(a) anaweza kuwa mshirika kwa, au vyenginevyo kunufaika katika, shughuli yoyote au utaratibu wa kampuni au ambao kampuni ndani yake inanufaika;

(b) anaweza kuwa mkurugenzi au ofisa mwengine wa, au kuajiriwa na, au mshirika katika shughuli yoyote au utaratibu wowote, au vyenginevyo kunufaika katika shirika lolote lililokuzwa na kampuni au ambalo kampuni linaweza kunufaika;

(c) hatawajibika, kwa sababu ya cheo chake, kwa kampuni kwa fursa yoyote ambayo anapata kutokana na cheo hicho au malipo ya ajira au fursa nyengine anazopata kama mkurugenzi au ofisa wa, au kutoka maslahi yake kwenye, kampuni nyengine isipokuwa kampuni inaelekeza vyenginevyo.

Isipokuwa kwamba hakuna kitu kilichomo humu kitamuidhinisha mkurugenzi au shirika lake kuwa mkaguzi wa kampuni.

**87.** Kwa madhumuni ya kanuni ya 76 na 77:-

(a) Taarifa ya jumla iliyotolewa kwa wakurugenzi kwamba mkurugenzi anapaswa kuonekana kuwa ana maslahi ya aina na mawanda yaliyoainishwa katika taarifa katika shughuli yoyote au utaratibu wowote ambao mtu aliyeainishwa au kundi la watu lina maslahi itahesabika kuwa ni ubainishaji kwamba mkurugenzi ana maslahi katika shughuli hiyo ya aina na mawanda yaliyoainishwa; na

(b) Maslahi ambayo mkurugenzi hana taarifa nayo na haistahiki kudhani kuwa nayo hayatahesabika kuwa ni maslahi yake.

**88.** Hundi zote, hati za ahadi, rasimu, hawala na hati nyengine za mapatano, na risiti zote za fedha inazolipwa kampui, zitatiwa saini, kukubaliwa, kuthibitishwa au vyenginevyo kutekelezwa kwa namna ambayo wakurugenzi kila baada ya muda kwa azimio wataelekeza.

**89.** Wakurugenzi watawezesha kumbukumbu za vikao kuandikwa katika vitabu vinavyotunzwa kwa madhumuni ya:- Kumbukumbu za Mikutano.

(a) uteuzi wote wa maofisa unaofanywa na wakurugenzi;

(b) majina ya wakurugenzi wote waliopo kwenye kila mkutano wa wakurugenzi na kila kamati ya wakurugenzi;

(c) maazimio yote na mwenendo wa mikutano yote ya kampuni, ya wamiliki wa kila daraja ya hisa katika kampuni, na ya wakurugenzi, na ya kamati za wakurugenzi.

Malipo na Matumizi; Viinua Mgongo na Pensheni.

**90.** Malipo ya wakurugenzi yataamuliwa kwa azimio la kawaida la kampuni na, isipokuwa kwamba azimio linataka vyenginevyo, malipo hayo yatahesabika kupatikana kutoka siku hadi siku. Wakurugenzi wanaweza pia kulipwa matumizi ya usafiri, hoteli na matumizi mengine waliyofanya kwa namna inayokubalika katika kuhudhuria na kurejea kutoka kwenye mikutano ya wakurugenzi au kamati yoyote ya wakurugenzi au mikutano mikuu au mikutano myengine ya wamiliki wa hisa za daraja yoyote au dhamana za kampuni au vyenginevyo kuhusiana na shughuli za kampuni.

**91.** Wakurugenzi kwa niaba ya kampuni wanaweza kulipa kiinuamgongo au pensheni au posho wakati wa kustaafu kwa mkurugenzi yeyote amabye alishika dhamana ya ofisi nyengine yoyote aliyolipwa mshahara au mahali pa faida na kampuni au kwa mjane wake au wategemezi wake na wanaweza kutoa michango kwa mfuko wowote na kutoa malipo kwa ajili ya ununuzi au utoaji wa kiinua mgongo hicho, pensheni au posho.

Ubatilishaji na Uondoaji wa Wakurugenzi.

**92.** Cheo cha mkurugenzi kitakuwa wazi iwapo mkurugenzi:-

(a) atasita kuwa mkurugenzi kwa mujibu wa kifungu chochote cha Sheria au anakatazwa na sharia kuwa mkurugenzi; au

(b) akiwa muflisi au anafanya mipango yoyote au muungano wowote na wakopeshaji wake kwa ujumla; au

(c) anakuwa na akili isiyokuwa timamu; au

(d) anajiuzulu ofisi yake kwa taarifa ya maandishi kwa kampuni; au

(e) atakuwa kwa zaidi ya miezi sita mfululizo amekuwa hayupo bila ya ruhusa ya wakurugenzi kwenye mikutano ya wakurugenzi iliyoendeshwa katika kipindi hicho na wakurugenzi wakaazimia kwamba cheo chake kiwe wazi.

Uteuzi na Kustaafu Wakurugenzi.

**93.** Kampuni kwa azimio la kawaida inaweza kumteua mtu anayetaka kufanya kazi kama mkurugenzi ama kujaza nafasi tupu au kuwa mkurugenzi wa ziada.

**94.** Wakurugenzi wanaweza kumteua mtu ambaye yuko tayari kuwa mkurugenzi, ama kwa kujaza nafasi au kama mkurugenzi wa ziada, isipokuwa kwamba jumla ya idadi ya wakurugenzi haitazidi idadi iliyowekwa na au kwa mujibu wa kanuni hizi. Mkurugenzi alyeteuliwa hivyo atashika madaraka tu mpaka mkutano mkuu wa mwaka unaofuata, na kisha atakuwa na haki ya kuchaguliwa tena.

**96.** Kampuni inaweza kwa azimio la kawaida, ambalo taarifa maalumu imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 148 cha Sheria, kumuondoa mkurugenzi yeyote kabla ya kumalizika muda wa kipindi chake cha ofisi bila ya kujali kitu chochote katika kanuni hizi au katika makubaliano yoyote

kati ya kampuni na mkurugenzi. Kuondolewa huko hakutaathiri madai yoyote mkurugenzi anayoweza kuwa nayo kuhusu madhara yaliyotokana na uvunjaji wa mkataba wowote wa huduma kwa kampuni.

**97.** Kampuni inaweza kwa azimio la kawaida kumteua mtu mwengine katika nafasi ya mkurugenzi aliyeondolewa kutoka ofisi chini ya kanuni iliyotangulia, na bila ya kuathiri mamlaka ya wakurugenzi chini ya kanuni ya 85 kampuni inaweza kwa azimio la kawaida kumteua mtu yeyote kuwa mkurugenzi ama kujaza nafasi au kuwa mkurugenzi wa ziada.

**98.** Bila ya kuathiri masharti ya kanuni, wakurugenzi wanaweza kusimamia mikutano yao kama wanavyofikiri inafaa. Masuala yanayotokana na mkutano yataamuliwa kwa kura nyingi. Katika hali ya usawa wa kura, mwenyekiti atakuwa na kura ya pili ya uamuzi. Mkurugenzi anaweza, na katibu kwa ombi la mkurugenzi huyo, ataitisha mkutano wa wakurugenzi. Haitakuwa lazima kutoa taarifa ya mkutano wa wakurugenzi kwa mkurugenzi yeyote ambaye hayuko Zanzibar. Taratibu za Wakurugenzi.

**99.** Akidi ya lazima kwa ajili ya maingiliano ya biashara ya wakurugenzi inaweza kuwekwa na wakurugenzi, na isipokuwa hivyo itakuwa wawili.

**100.** Wakurugenzi wanaoendelea wanaweza kuchukua hatua bila ya kujali lolote katika upungufu wa idadi yao, lakini, kama idadi yao imepungua chini ya idadi iliyowekwa kama akidi, wakurugenzi wanaoendelea au mkurugenzi anaweza kuchukua hatua kwa madhumuni ya kujaza nafasi tu au ya kuitisha mkutano mkuu.

**101.** Wakurugenzi wanaweza kuteua mmoja miongoni mwao kuwa mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi na kuamua kipindi ambacho yeye atashikilia ofisi. Isipokuwa kwamba yeye hataki kufanya hivyo, mkurugenzi aliyetuliwa ataongoza kila mkutano wa wakurugenzi ambao yeye amehudhuria. Lakini kama hakuna mwenyekiti aliyeteuliwa, au kama yeye hataki kuwa mwenyekiti wa mkutano, au kama katika mkutano wowote mwenyekiti hayupo ndani ya dakika tano baada ya wakati uliowekwa kwa ajili ya kufanya mkutano, wakurugenzi waliopo wanaweza kuchagua mmoja miongoni mwao kuwa mwenyekiti wa mkutano.

**102.** Wakurugenzi wanaweza kukasimu madaraka yao yoyote kwa kamati yoyote yenye mkurugenzi mmoja au zaidi; kamati yoyote iliyoundwa hivyo katika kutekeleza waliyokasimiwa hivyo watafuata kanuni zozote ambazo zinaweza kuwekwa juu yao na wakurugenzi. Chini ya kanuni hizo, mwenendo wa mikutano ya kamati yenye wajumbe wawili au zaidi utaongozwa na kanuni zinazosimamia mwenendo wa miktano ya wakurugenzi kwa kadiri zinavyoweza kutumika.

**103.** Matendo yanayofanywa na mkutano wa wakurugenzi au wa kamati ya wakurugenzi au na mtu yeyote anayekaimu kama mkurugenzi, bila ya kujali kwamba ni baadaye itadhihirika kwamba kulikuwa na baadhi ya kasoro katika uteuzi wa mkurugenzi yoyote kama huyo, au kwamba yeyote kati yao alionekana kuwa hastahili madaraka, au aliacha madaraka, au

alikuwa hana haki ya kupiga kura, yatakuwa halali kama kwamba kila mtu wa namna hiyo alikuwa kihalali ameteuliwa na alikuwa anastahiki na alikuwa ameendelea kuwa mkurugenzi na alikuwa na haki ya kupiga kura.

**104.** Azimio kwa maandishi, lililotiwa saini na wakurugenzi wote wenye haki ya kupewa taarifa ya mkutano wa wakurugenzi, au wa kamati ya wakurugenzi, litakuwa halali na lenye kutumika kama kwamba lilikuwa limepitishwa katika mkutano wa wakurugenzi au (kama hali itakavyokuwa) kamati ya wakurugenzi ulioitishwa na uliofanyika, na unaweza kuwa na nyaraka kadhaa katika fomu zinazofanana kila moja ikiwa imetiwa saini na mmoja au zaidi ya wakurugenzi.

**105.** Ila kama iliyoelezwa katika kanuni, mkurugenzi hatapiga kura katika mkutano wa wakurugenzi au wa kamati ya wakurugenzi juu ya azimio lolote linalohusu jambo ambalo yeye, ama moja kwa moja au si moja kwa moja, ana maslahi au wajibu ambao ni wa kitu na ambao unakinzana au unaweza kukinzana na maslahi ya kampuni. Bila ya kuathiri na kwa mujibu wa masharti ya Sheria, maslahi ya mtu ambaye anahusiana na mkurugenzi yatahesabiwa kama maslahi ya mkurugenzi.

**106.** Mkurugenzi hatahesabiwa katika akidi iliyohudhuria katika mkutano kuhusiana na azimio ambalo yeye hana haki ya kulipigia kura.

**107.** Kampuni inaweza kwa azimio la kawaida kusimamisha au kulegeza kwa kiasi chochote, ama kwa jumla au kuhusiana na jambo lolote makhsusi, masharti yoyote ya kanuni yenye kumzuia mkurugenzi kupiga kura katika mkutano wa wakurugenzi au wa kamati ya wakurugenzi.

**108.** Ambapo mapendekezo yanazingatiwa kuhusu uteuzi wa wakurugenzi wawili au zaidi kwa dhamana au ajira katika kampuni au shirika lolote ambalo kampuni ina maslahi, mapendekezo yanaweza kugawanywa na kuzingatiwa uhusiano na kila mkurugenzi peke yake na (madamu yeye hajazuiliwa kwa sababu nyengine kupiga kura) kila mmoja wa wakurugenzi wanaohusika atakuwa na haki ya kupiga kura na kuhesabiwa katika akidi kuhusiana na kila azimio isipokuwa kuhusu uteuzi wake mwenyewe.

**109.** Kama hoja imeibuka katika mkutano wa wakurugenzi au wa kamati ya wakurugenzi kuhusu haki ya mkurugenzi ya kupiga kura, hoja inaweza, kabla ya kuhitimisha mkutano, kutapelekwa kwa mwenyekiti wa mkutano na uamuzi wake kuhusiana na mkurugenzi yeyote mwengine zaidi ya yeye mwenyewe utakuwa wa mwisho na wenye kufunga mjadala.

Katibu

**110.** Katibu atateuliwa na wakurugenzi kwa kipindi, katika malipo hayo na kwa masharti watakayoona yanafaa; na katibu yeyote aliyeteuliwa hivyo anaweza kuondolewa na wao.

**111.** Sharti la Sheria au kanuni zinazotaka au kuidhinisha kufanywa jambo na au kwa mkurugenzi na katibu halitatosheleza kwa kufanywa na au kwa mtu huyo huyo anayekaimu wote kama mkurugenzi na kama, au kwa niaba ya, katibu.

Muhuri.

**112.** Muhuri utatumiwa kwa idhini ya wakurugenzi tu au ya kamati ya wakurugenzi iliyoidhinishwa na wakurugenzi. Wakurugenzi wanaweza kuamua nani atatia saini waraka wowote ambao umepigwa na isipokuwa imeamuliwa vyenginevyo utatiwa saini na mkurugenzi na katibu au na mkurugenzi wa pili.

Gawio na Akiba.

**113**. Bila ya kuathiri kifungu cha 184 cha Sheria, kampuni inaweza kwa azimio la kawaida kutangaza gawio kwa mujibu wa haki ya wanachama wanaohusika, lakini hakuna litakalozidi kiasi kilichopendekezwa na wakurugenzi.

**114.** Bila ya kuathiri masharti ya Sheria, wakurugenzi wanaweza kila baada ya muda kulipa kwa wanachama gawio la mpito kama inavyoonekana na wakurugenzi kukubalika kutokana na faida ya kampuni iliyopo kwa ajili ya kugawana.

**115.** Wakurugenzi wanaweza, kabla ya kupendekeza gawio lolote, kuweka kando nje ya faida ya kampuni kiasi ambacho wanafikiri kinafaa kama akiba ambayo au akiba ambazo, kwa busara ya wakurugenzi, zitatumika kwa madhumuni yoyote ambayo faida ya kampuni inaweza kutumika ipasavyo, na katika kusubiri matumizi, kwa busara kama hiyo, zinaweza ama kutumika katika biashara ya kampuni au kuwekezwa katika miradi (zaidi ya hisa za kampuni) kama wakurugenzi wanavyoweza kila baada ya muda kuona inafaa. Wakurugenzi wanaweza pia bila ya kuweka faida kwenye akiba kuhaulisha faida yoyote ambayo wanaweza kufikiria kuwa ni busara kutoigawa.

**116.** Isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo na masharti yaliyofungwa kwenye hisa, gawio lote litatangazwa na kulipwa kulingana na kiasi kilicholipwa kwenye hisa inayohusiana na gawio linalolipwa. Gawio lote litagawanywa na kulipwa kwa uwiano kwa kiasi kilicholipwa kwa hisa wakati wa mgao wowote au migao yoyote katika kipindi ambacho gawio linalipwa; lakini kama hisa yoyote inatolewa kwa masharti kwamba itastahiki gawio kutoka tarehe fulani, hisa hiyo itastahiki gawio hilo ipasavyo.

**117.** Mkutano wowote mkuu unaotangaza gawio unaweza, kwa mapendekezo ya wakurugenzi, unaweza kuelekeza malipo ya gawio hilo lote au sehemu kwenye ugawaji wa raslimali na, ambapo ugumu wowote umejitokeza kuhusiana na ugawaji, wakurugenzi wanaweza kutatua ugumu huo, na hasa wanaweza kutoa vyeti vya sehemu na kuweka thamani kwa ajili ya ugawaji wa raslimali yoyote na wanaweza kuamua kwamba malipo ya fedha yatafanywa kwa wanachama wowote kuhusu kulipa thamani iliyowekwa ili kurekebisha haki za wanachama, na wanaweza kuweka raslimali zozote katika mifuko ya dhamana.

**118.** Gawio lolote, riba ama fedha nyengine zinazolipwa taslimu kuhusiana na hisa zinaweza kulipwa kwa hundi iliyopelekwa kwa njia ya posta kwa anwani iliyosajiliwa ya mmiliki au, kwa wamiliki wa pamoja, kwa anuani iliyosajiliwa ya mmoja wa wamiliki wa pamoja ambaye ni wa kwanza jina lake kuandikishwa katika daftari la wanachama, au kwa mtu ambaye na anuani ambayo mmiliki au wamiliki wa pamoja wanaweza

kuelekeza kwa maandishi. Kila hundi au waranti wa namna hiyo utalipwa kwa utaratibu wa mtu ambaye anapelekewa, na malipo ya hundi yatakuwa huduma nzuri iliyotolewa na kampuni. Mmiliki mmoja yeyote wa wamiliki wawili au zaidi wa pamoja anaweza kutoa risiti ya kutekelezwa kwa gawio lolote au fedha nyengine iliyolipwa kuhusiana na hisa zinazomilikiwa na wao kama wamiliki wa pamoja.

**119.** Hakuna gawio au fedha nyengine zinazolipwa kuhusiana na zitakazozalisha riba dhidi ya kampuni isipokuwa imeelezwa vyenginevyo na haki zilizoambatana na hisa.

**120.** Gawio lolote ambalo limebakia bila ya kuchukuliwa kwa muda wa miaka kumi na mbili kuanzia tarehe ambayo malipo yalikuwa yafanywe, kama wakurugenzi wataamua hivyo, litafutwa na kusita kubaki kuwa ni deni kwa kampuni.

Hesabu.

**121.** Wakurugenzi watawezesha kuwekwa vitabu vya hesabu kuhusiana na:-

(a) fedha zote zilizopokelewa na kutumiwa na kampuni na mambo ambayo yanahusiana na mapato na matumizi yaliyofanyika;

(b) mauzo na manunuzi yote ya bidhaa yaliyofanywa na kampuni; na

(c) rasilimali na madeni ya kampuni.

Vitabu sahihi havitahesabiwa kuwa vimewekwa kama havikuwekwa vitabu hivyo vya hesabu kama inavyohitajika kutoa sura ya kweli na ya haki ya hali ya mambo ya kampuni na kuelezea shughuli zake za kibiashara.

**122.** Vitabu vya hesabu vitawekwa katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni, au, chini ya kifungu cha 154(4) cha Sheria, katika mahali pengine au mwahala mwengine kama wakurugenzi wanavyoona inafaa, na daima vitakuwa wazi kwa ukaguzi wa wakurugenzi.

**123.** Mwanachama yeyote (kwa kweli) hatakuwa na haki yoyote ya kukagua rikodi zozote za hesabu au kitabu chengine au hati ya kampuni isipokuwa kama ilivyotolewa na sheria au kuidhinishwa na wakurugenzi au kwa azimio la kawaida la kampuni.

**124.** Wakurugenzi watawezesha, kwa mujibu wa vifungu vya 156, 158 na 164 vya Sheria, kutayarishwa na kuwekwa mbele ya kampuni kwenye mkutano mkuu faida na hasara, mizania, maelezo ya mtiririko wa fedha, hesabu za makundi (kama zipo) na taarifa kama zinavyoelezwa katika vifungu hivyo.

**125.** Kwa mujibu wa kifungu cha 169 cha Sheria, nakala ya hesabu za kampuni za kila mwaka kuwasilishwa mbele ya kampuni kwenye mkutano mkuu pamoja na nakala ya ripoti ya mkurugenzi na ripoti ya mkaguzi si chini ya siku ishirini na moja kabla ya tarehe ya mkutano itapelekwa kwa kila mwanachama wa, na kila mmiliki wa dhamana wa, kampuni. Isipokuwa

kwamba kanuni hii haitahitaji kwamba nakala ya hati hizo kupelekwa kwa mtu yeyote ambaye anwani yake kampuni haiitambui au kwa zaidi ya mmoja wa wamiliki wa pamoja wa hisa zozote au dhamana.

Faida Kufanywa Mtaji.

**126.** Wakurugenzi wanaweza, kwa idhini ya azimio la kawaida la kampuni:-

(a) kuamua kuifanya mataji sehemu yoyote ya kiasi ambacho kwa wakati unaohusika kipo katika mapato ya akaunti yoyote ya akiba ya kampuni au mapato ya akaunti ya faida na hasara au vyenginevyo yanayopatikana kwa ajili ya kugawiwa, na kwamba kiasi hicho kifanywe mtaji kwa wanachama ambao wangekuwa na haki nao kama ungegawanya kwa njia ya gawio na katika uwiano sawa na kutumia kima hicho ama katika au kuelekezwa kwenye kulipa kiasi chochote ambacho kwa wakati unaohusiaka hakijalipwa kwa hisa zozote zinazomilikiwa na wanachama hao au katika kulipa kamili katika hisa zilizotolewa au dhamana za kampuni zitakazotengwa na kugawiwa;

(b) kutayarisha masharti ya utoaji wa hati za sehemu au kwa malipo ya fedha taslimu au vyenginevyo kama wanavyofikiri inafaa kwa ajili ya hisa au dhamana zinazoweza kugawika katika sehemu, na kumuidhinisha mtu yeyote kuingia katika makubaliano kwa niaba ya wajumbe wote wenye haki ya kufanya hivyo na kampuni unaohusu kugawanywa kwao wao, kulipwa kikamilifu hisa zozote au dhamana ambazo wao wana haki kwenye mtaji huo, na makubaliano yoyote yaliyofanywa chini ya mamlaka hayo yatakuwa madhubuti na yanayowafunga wanachama wote.

**127.** Wakaguzi watateuliwa na majukumu yao kuratibiwa kwa mujibu wa vifungu vya 166-169 cha Sheria. Ukaguzi.

**128.** Taarifa yoyote inayotolewa kwa au na mtu kwa mujibu wa kanuni itakuwa katika maandishi isipokuwa kwamba taarifa inayoitisha mkutano wa wakurugenzi haitakuwa na haja ya kuwa katika maandishi. Kampuni inaweza kutoa taarifa yoyote kwa mwanachama ya ama binafsi au kwa kupeleka kwa njia ya posta katika bahasha iliyolipiwa yenye anwani iliyosajiliwa ya mwanachama, au kwa kuiweka katika anuani hiyo. Ambapo taarifa imepelekwa kwa njia ya posta, upelekaji wa taarifa utachukuliwa kuwa umetekelezwa vizuri kwa kutiwa anuani inayofaa, kutayarisha, na kuitia posta barua yenye taarifa, na kuwa imetekelezwa kwa kumalizika muda wa saa (sabiini na mbili) baada ya barua yenye taarifa hiyo kutiwa posta. Mwanachama ambaye anwani yake iliyosajiliwa haimo ndani ya Zanzibar na ambaye anatoa kwa kampuni anuani iliyomo ndani ya Zanzibar ambayo taarifa zake zinaweza kupelekwa atakuwa na haki ya kupokea taarifa yoyote kutoka kwenye kampuni. Matangazo.

**129.** Taarifa inaweza kutolewa na kampuni kwa wamiliki wa pamoja wa hisa kwa kutoa taarifa kwa mmiliki wa pamoja wa kwanza jina lake kuandikishwa katika daftari la wanachama kuhusiana na hisa.

**130.** Taarifa inaweza kutolewa na kampuni kwa watu wenye haki kwenye hisa katika matokeo ya kifo au kufilisika mwanachama na kuipeleka au kuiwasilisha, kwa njia yoyote ile iliyoidhinishwa na kanuni, kwa kupelekewa kwa majina, au kwa lakabu za wawakilishi wa marehemu, au mdhamini wa mfilisiwa, au kwa maelezo yoyote kama hayo, katika anuani, kama ipo, ndani ya Zanzibar iliyotolewa kwa madhumuni hayo na watu wanaodai kuwa na haki hiyo. Mpaka pale ambapo anuani hiyo imetolewa, taarifa inaweza kutolewa kwa njia yoyote ile ambayo ingeweza kutolewa kama kifo au kufilisika kusingetokea.

**131.** Mwanachama aliyehudhuria, ama yeye mwenyewe au kwa wakala, mkutano wowote wa kampuni au ya wamiliki wa daraja yoyote ya hisa katika kampuni utachukuliwa kuwa amepokea.

Fidia.

**132.** Kwa mujibu wa masharti ya Sheria, lakini bila ya kuathiri fidia yoyote ambayo mkurugenzi vyenginevyo ingemstahikia, kila mkurugenzi au ofisa mwengine au mkaguzi wa kampuni atalipwa fidia kutokana na raslimali za kampuni dhidi ya zozote alizoingia katika kutetea kesi yoyote, iwe ya madai au jinai, ambayo hukumu imetolewa kwa kumpendelea yeye au ambayo yeye ameachiwa huru au kuhusiana na jambo lolote chini ya kifungu cha 262 cha Sheria ambalo nafuu imetolewa kwake na mahakama kutokana na dhima ya uzembe, ukiukaji, uvunjaji wa wajibu au uvunjaji wa uaminifu kuhusiana na masuala ya kampuni.

## SEHEMU YA II
## KANUNI KWA AJILI YA UENDESHAJI WA KAMPUNI BINAFSI ZENYE UKOMO WA HISA

Kanuni zilizomo katika Sehemu ya I ya Jadweli A zitatumika ispokuwa kifungu cha 22.

**1.** Kampuni ni kampuni binafsi na kwa mnasaba huo:-

(a) haki ya kuhaulisha hisa inazuiwa kwa namna ambayo imewekwa humu;

(b) idadi ya wanachama wa kampuni haizidi khamisini kama ilivyoelezwa zaidi katika Sheria;

(c) mualiko wowote wa umma kuchangia kwenye hisa zozote au dhamana za umma unakatazwa;

(d) kampuni haitakuwa na uwezo kutoa hati za hisa kwa mmiliki.

**2.** Wakurugenzi wanaweza, kwa uamuzi wao wenyewe na bila ya kuhusisha sababu yoyote kwenye uamuzi huo, kukataa kusajili uhaulishaji wowote wa hisa yoyote, kama ni hisa iliyolipiwa kamili au la.

## JADWELI B
## FOMU YA KATIBA YA KUUNGANA YA KAMPUNI YENYE UKOMO WA HISA

**1.** Jina la kampuni ni "________________________Yenye ukomo".

**2.** Ofisi iliyosajiliwa ya kampuni ipo _____________________

**3.** Malengo ya kuanzishwa kampuni ni,

**4.** Dhima ya wanachama ina ukomo.

**5.** Jumla ya hisa ya kampuni ni shilingi _____________ zilizogawanya katika hisa _______ za shilingi ________ kila moja.

SISI, watu ambao majina na anwani zao yameandikwa, tunataka kuwekwa katika kampuni, kwa mujibu wa katiba hii ya ushirikiano, na tunakubali kuchukua idadi ya hisa katika mtaji zilizoainishwa pembeni mwa majina yetu.

| Majina, anwani na maelezo ya mchangiaji | Idadi ya hisa zilizochukuliwa na kila mchangiaji | Saini za wachangiaji |
|---|---|---|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |

Jumla ya hisa zilizochukuliwa _________________________________

Shahidi (mwanasheria nayefanya kazi) kwa saini hizo hapo juu.

Jina: ………………………………
Anwani: ……………………………
………………………
Sifa : ……………………………………
Tarehe ___ mwezi wa __________, 20___

Saini:

MUHURI

## JADWELI C
## FOMU YA KATIBA NA KANUNI ZA USHIRIKIANO ZA KAMPUNI YENYE UKOMO WA DHAMANA, NA ISIYOKUWA NA MTAJI WA HISA

**1.** Jina la kampuni ni "____________________________Yenye ukomo".

**2.** Ofisi iliyosajiliwa ya kampuni ipo _____________________

**3.** Malengo ya kuanzishwa kampuni ni,

**4.** Dhima ya wanachama ina ukomo.

**5.** Kila mwanachama wa kampuni anaahidi kuchangia kwenye raslimali za kampuni endapo itafungwa wakati yeye ni mwanachama, au ndani ya mwaka mmoja baadaye, kwa ajili ya kulipa deni na dhima za kampuni ilizoingiliana mikataba kabla ya yeye kusita kuwa mwanachama, na gharama, ada na matumizi ya kuifunga kampuni, na kwa ajili ya kurekebisha haki za wachangiaji miongoni mwao, kiasi kama kitakavyohitajika kisichozidi shilingi ……………..…………..

SISI, watu ambao majina na anwani zao yameandikwa, tunataka kuwekwa katika kampuni, kwa mujibu wa katiba hii ya ushirikiano.

| Majina, anwani na kazi za mchangiaji | Saini za wachangiaji |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |
| 4. | |
| 5. | |

Shahidi wa saini hizo hapo juu.
Jina :………………………………………
Anwani :………………………………..…
Sifa :………………………………………
Saini :……………………………………..
Tarehe ___ mwezi wa __________, 20___

## KANUNI ZA USHIRIKIANO ZA KAMPUNI ZINAZOTANGULIA KATIBA YA USHIRIKIANO

Fasili.

**1.** Katika kanuni hizi :-

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Kampuni;

"kanuni " maana yake ni kanuni za kampuni;

"siku wazi" kuhusiana na kipindi cha taarifa maana yake ni kipindi ukitoa siku ambayo taarifa inatolewa au inahesabika kutolewa na siku ambayo kwa ajili ya siku hiyo inatolewa au ambayo itaanza kutumika;

"muhuri" maana yake ni muhuri wa kawaida wa kampuni;

"Katibu" maana yake ni mtu yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya katibu wa kampuni.

Matamko yanayorejea kwenye maandishi, isipokuwa kwamba dhamiri nyengine imejitokeza, yatachukuliwa kujumuisha marejeo kwenye uchapishaji, lithografia, upigaji wa picha, na njia nyengine za kuwakilisha au kutoa upya maneno katika umbo linaloonekana.

Isipokuwa kama muktadha unahitaji vyenginevyo, maneno au matamko yaliyomo katika kanuni hizi yatakuwa na maana sawa na zile zilizomo katika Sheria au mabadiliko yoyote ya kisheria yaliyomo humo yanayotumika katika tarehe ambayo kanuni hizi zinaifunga kampuni.

Wanachama.

**2.** Idadi ya wanachama ambayo kampuni inapendekeza kusajiliwa ni …….. lakini wakurugenzi wanaweza kila baada ya kipindi wakasajili idadi zaidi ya wanachama.

**3.** Wachangiaji wa katiba ya ushirikiano na watu wengine ambao wakurugenzi watawaingiza kwenye uwanachama watakuwa ni wanachama wa kampuni.

Mkutano Mkuu.

**4.** Kampuni katika kila mwaka itafanya mkutano mkuu kama mkutano wake mkuu wa mwaka zaidi ya mikutano myengine yoyote katika mwaka huo, na itauainisha mkutanao hivyo katika taarifa ya kuuitisha; na si zaidi ya miezi kumi na tano itapita baina ya tarehe ya mkutano mkuu wa mwaka wa kampuni na ule unaofuata:

Isipokuwa kwamba maadamu kampuni inaitisha mkutano wake mkuu wa mwaka wa kwanza ndani ya miezi kumi na nane ya kuandikishwa kwake, au katika mwaka unaofuata. Mkutano mkuu wa mwaka utafanyika katika wakati na mahali kama wakurugenzi watakapoainisha.

**5.** Mikutano mikuu yote zaidi ya mikutano mikuu ya mwaka itaitwa mikutano mikuu ya dharura.

**6.** Wakurugenzi wanaweza, wakati wowote wanaofikiri unafaa, kuitisha mkutano mkuu wa dharura, na mikutano mikuu ya dharura pia itaitishwa kwa ombi, au, kwa ukiukaji, unaweza kuitishwa na waombaji, kama ilivyoelezwa na kifungu cha 137 cha Sheria. Kama wakati wowote hakuna ndani ya Zanzibar wakurugenzi wa kutosha wa kutimiza akidi, mkurugenzi yeyote au wanachama wowote wawili wa kampuni wanaweza kuitisha mkutano mkuu wa dharura kwa karibu namna ile ile kama ambavyo mikutano inaweza kuitishwa na wakurugenzi.

Taarifa ya Mkutano Mkuu.

**7.** Kila mkutano mkuu utaitishwa kwa taarifa ya siku ishirini na moja kamili kwa uchache kwa maandishi. Taarifa itaainisha mahali, siku na saa ya mkutano na, kwa shughuli maalumu, hali ya jumla ya hiyo shughuli:

Isipokuwa kwamba mkutano wa kampuni, bila ya kujali kwamba umeitishwa kwa taarifa ya muda mfupi kuliko ule ulioainishwa katika kanuni hii utafahamika kwamba umeitishwa kihalali kama umekubaliwa -

(a) kwa mkutano ulioitishwa kama mkutano mkuu wa mwaka, na wanachama wote wenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura; na

(b) kwa mkutano mwengine wowote, idadi ya wingi wa wanachama wenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano, ikiwa ni wingi wa pamoja unaowakilisha si chini ya asilimia tisiini na tano ya haki zote za kupiga kura katika mkutano ule wa wanachama wote.

**8.** Bila ya kuathiri masharti ya kanuni, taarifa itatolewa kwa wanachama wote, kwa watu wote wenye haki ya hisa kwa matokeo ya kifo au kufilisika mwanachama na kwa wakurugenzi na wakaguzi. Uachaji kwa bahati mbaya katika kutoa taarifa ya mkutano kwa, au kutopokelewa taarifa ya mkutano na, mtu yeyote mwenye haki ya kupokea taarifa hakutabatilisha mwenendo wa mkutano huo.

Utaratibu wa Mikutano Mikuu.

**9.** Shughuli yoyote itachukuliwa kuwa ni maalumu ambayo inatekelezwa wakati wa mkutano mkuu wa dharura, na pia ile ambayo inatekelezwa wakati wa mkutano mkuu wa mwaka, isipokuwa kutangaza gawio, kuzingatia hesabu, mizania, na ripoti za wakurugenzi na wakaguzi, uchaguzi kujaza nafasi ya wale waliostaafu na uteuzi wa, na uwekaji wa malipo ya wakaguzi.

**10.** Hakuna shughuli itakayotekelezwa katika mkutano wowote mkuu isipokuwa akidi ya wanachama ipo wakati mkutano unaendelea na shughuli; watu wawili, wenye haki ya kupiga kura kuhusu shughuli inayotekelezwa, kila mmoja akiwa mwanachama au wakala wa mwanachama au mwakilishi aliyeidhinishwa kihalali wa shirika, watakuwa akidi.

**11.** Kama ndani ya nusu saa kutoka wakati wa kufanyika mkutano akidi haipo, au kama wakati mkutano unaendelea akidi haipo, mkutano utaakhirishwa hadi siku kama ile ya mkutano katika wiki ijayo, wakati huo huo na mahali pale pale, au siku nyengine na katika wakati mwengine na mahali pengine kama wakurugenzi watakavyoamua.

**12.** Mwenyekiti, kama yupo, wa bodi ya wakurugenzi au ikiwa hayupo mkurugenzi mwengine aliyeteuliwa na wakurugenzi ataongoza kama mwenyekiti wa mkutano mkuu, lakini kama mwenyekiti wala mkurugenzi mwengne (kama yupo) hayupo ndani ya dakika kumi na tano baada ya wakati uliowekwa kwa ajili ya kufanya mkutano na wakataka kukaimu, wakurugenzi waliopo watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa mwenyekiti wa mkutano huo, na kama kuna mkurugenzi mmoja tu aliyehudhuria na anakubali kukaimu, yeye atakuwa mwenyekiti.

**13.** Kama katika mkutano wowote hakuna mkurugenzi aliye tayari kukaimu kama mwenyekiti au kama hakuna mkurugenzi ndani ya dakika kumi na tano baada ya wakati uliowekwa kwa ajili ya kufanya mkutano,

wanachama waliopo watachagua mmoja miongoni mwao kuwa mwenyekiti wa mkutano huo.

**14.** Mwenyekiti anaweza, kwa idhini ya mkutano wowote ambao akidi ipo (na atakuwa kama hivyo akiongozwa na mkutano), kuakhirisha mkutano kila baada ya muda na kutoka mahali hadi mahali, lakini hakuna shughuli itakayotekelezwa wakati wa mkutano wowote ulioakhirishwa zaidi ya shughuli ambayo ingeweza kutekelezwa vizuri wakati wa mkutano kama uakhirishaji usingefanyika. Wakati mkutano ukiakhirishwa kwa siku kumi na nne au zaidi, angalau taarifa ya siku saba kamili ya mkutano ulioakhirishwa itatolewa inayobainisha wakati na mahali pa mkutano na hali ya jumla ya shughuli itakayotekelewa. Ila kama ilivyoelezwa awali haitakuwa lazima kutoa taarifa yoyote ya kuakhirishwa au ya shughuli itakayotekelezwa kwenye mkutano ulioakhirishwa.

**15.** Katika mkutano wowote mkuu azimio lililowasilishwa kupigiwa kura na mkutano litaamuliwa kwa kunyoosha mikono isipokuwa uchaguzi (kabla au wakati wa kutangaza matokeo ya mikono iliyonyooshwa) uombwe:-

(a) na mwenyekiti, au

(b) na wanachama angalau watatu waliopo wenyewe au kwa kutumia wakala; au

(c) na mwanachama yeyote au wajumbe waliohudhuria wenyewe au kwa kutumia wakala na wanaowakilisha si chini ya moja ya kumi ya haki zote za kupiga kura za wanachama wote wenye haki ya kupiga kura kwenye mkutano.

Isipokuwa kwamba uchaguzi ulihitaji tamko la mwenyekiti kwamba azimio katika kunyoosha mikono limepitishwa bila ya kupingwa, au kwa wingi makhsusi, au lilipingwa na kuingizwa jambo hilo katika kitabu cha kumbukumbu za mikutano ya kampuni kutakuwa ni ushahidi wa ukweli wa suala linalohusika bila ya ushahidi wa idadi au uwiano wa kura zilizorikodiwa kuunga mkono au kupinga azimio hilo.

Ombi kwa ajili ya uchaguzi linaweza, kabla ya uchaguzi kufanyika, kuondolewa.

**16.** Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kanuni ya 18, kama uchaguzi umeombwa kihalali utafanywa kwa namna kama mwenyekiti atakavyoongoza, na matokeo ya uchaguzi yatachukuliwa kuwa ni azimio la mkutano ambao uchaguzi uliombwa.

**17.** Ikitokea kura kuwa sawa, iwe kwenye kunyoosha mikono au kwa kupiga kura, mwenyekiti wa mkutano huo atakuwa na haki ya kura ya pili au ya uamuzi.

**18.** Upigaji wa kura ulioombwa juu ya uchaguzi wa mwenyekiti, au juu ya suala la kuakhirishwa mkutano, utafanyika palepale. Upigaji wa kura ulioombwa juu ya suala jengine lolote utafanyika pale pale au wakati

mwengine kama mwenyekiti wa mkutano atakavyoelekeza, na shughuli nyengine yoyote zaidi ya ile ambayo iliombewa upigaji kura inaweza kuendelea na wakati upigaji wa kura ukisubiri.

**19.** Azimio la maandishi linalotekelezwa na au kwa niaba ya kila mwanachama ambaye angekuwa na haki ya kupiga kura juu yake kama lilipendekezwa katika mkutano mkuu ambao yeye alihudhuria litakuwa na athari kama vile lilipitishwa katika mkutano mkuu kihalali ulioitishwa na uliofanyika, na linaweza kuwa na nyaraka nyingi katika fomu inayofanana kila moja ikitekelezwa na au kwa niaba ya mwanachama mmoja au zaidi.

Kura ya Wanachama.

**20.** Kila mwanachama atakuwa na kura moja.

**21.** Hakuna mwanachama atakayekuwa na haki ya kupiga kura katika mkutano wowote mkuu isipokuwa fedha yote ambayo inapaswa kulipwa na yeye kwa wakati huo kwa kampuni iwe imelipwa.

**22.** Katika uchaguzi kura inaweza kutolewa ama kwa mwenyewe binafsi au kwa kutumia wakala.

**23.** Hati inayomteua wakala itakuwa katika maandishi iliyotiwa saini na mteuaji au wakili wake aliyeidhinishwa kwa maandishi, au, kama mteauaji ni shirika, ama kwa kupigwa muhuri au kwa kutiwa saini na ofisa au wakili aliyeidhinishwa kihalali. Wakala si lazima kuwa mwanachama wa kampuni.

**24.** Hati inayomteua wakala na hati ya idhini au mamlaka nyengine, kama ipo, ambayo imetiwa saini au mthibitishaji rasmi alithibitisha nakala ya hati au idhini itawekwa katika ofisi ya kampuni iliyosajiliwa au katika mahali pengine ndani ya nchi kama ilivyoainishwa kwa ajili hiyo katika taarifa ya kuitisha mkutano, si chini ya saa arubaini na nane kabla ya wakati wa kufanya mkutano wa mkutano ulioakhirishwa ambao mtu aliyetajwa katika hati anapendekeza kupiga kura, au, kwa uchaguzi, si chini ya saa ishirini na nne kabla ya wakati uliowekwa kwa ajili ya kufanya uchaguzi, na katika ukiukaji hati ya wakala haitachukuliwa kuwa ni halali.

**25.** Hati ya kuteua wakala itakuwa katika fomu ifuatayo au fomu inayokaribiana sana nayo kadiri hali inavyoruhusu:

"______________________ Yenye ukomo

Mimi / sisi ______________________ wa ____________________ kama _________________

mwanachama / wanachama wa kampuni iliyotajwa hapo juu, hapa tunamteua _____________________ wa ______________________, au akikosekana yeye, ______________ wa ___________________ kama mwakilishi wangu / wetu kupiga kura kwa ajili yangu / yetu kwa niaba yangu / yetu katika mkutano wa (mwaka au dharura, kama itakavyokuwa) wa mwaka wa kampuni utakaofanywa siku ______ ya __________, 20__, na wakati wowote utakapoakhirishwa.

Imetiwa saini leo siku ya ______________________ mwezi wa __________, 20__, "

**26.** Ambapo inahitajika kuwapa wanachama fursa ya kupiga kura kuunga mkono au kupinga azimio hati ya kuteua wakala itakuwa katika fomu ifuatayo au fomu inayokaribiana nayo kadiri hali inavyoruhusu: -

"__________________________ Yenye ukomo
"Mimi/sisi ____________________ wa ___________________ kama __________________
mwanachama/wanachama wa kampuni iliyotajwa hapo juu, hapa tunamteua ___________________ wa ____________________ au akikosa yeye, _____________ wa _________________ kama mwakilishi wangu / wetu kupiga kura kwa ajili yangu / yetu kwa niaba yangu / yetu katika mkutano wa (mwaka au dharura, kama itakavyokuwa) utakaofanywa siku ______ ya__________, 20__, na wakati wowote utakapoakhirishwa.

Imetiwa saini leo siku ya ______________________ mwezi wa __________, 20__, "

Fomu hii itatumika katika kuunga mkono* / kupinga azimio. Kama haikuelezwa vyengine, wakala atapiga kura kama anavyodhani inafaa.

* Kata yoyote isiyohitajika.

**27.** Hati ya kuteua wakala itachukuliwa kutoa mamlaka ya kudai au kujiunga katika kudai uchaguzi.

**28.** Kura iliyotolewa kwa mujibu wa masharti ya hati ya wakala, au uchaguzi uliodaiwa na wakala, au kwa mwakilishi aliyeidhinishwa kihalali wa shirika utakuwa halali bila ya kujali uamuzi uliopita wa mamlaka ya mtu aliyepiga kura au kudai uchaguzi isipokuwa taarifa ya uamuzi ilipokelewa na kampuni katika ofisi yake iliyosajiliwa (au mahali pengine ambapo hati ya wakala ilikuwa kihalali imewasilishwa) kabla ya kuanza mkutano au mkutano ulioakhirishwa ambao uwakilishi unatumika.

Mashirika Yanayofanya Kazi kwa Uwakilishi Katika Mikutano.

**29.** Shirika lolote ambalo ni mwanachama wa kampuni linaweza kwa azimio la wakurugenzi wake au chombo chengine cha uongozi kumuidhinisha mtu kama linavyoona inafaa kuwa mwakilishi wake katika mkutano wowote wa kampuni, na mtu aliyeidhinishwa atakuwa na haki ya kutumia madaraka kwa niaba ya shirika ambalo yeye analiwakilisha kama vile ambayo shirika lingeweza kutumia kama lingekuwa mwanachama binafsi wa kampuni.

Wakurugenzi.

**30.** Idadi ya wakurugenzi na majina ya wakurugenzi wa kwanza yataamuliwa kwa maandishi na wanachama wa mkataba wa chama au wengi wao na mpaka uamuzi utakapotolewa watiaji saini wa mkataba wa chama watakuwa ndio wakurugenzi wa kwanza. Isipokuwa kwamba imeamuliwa vyenginevyo na azimio la kawaida, idadi ya wakurugenzi haitakuwa na ukomo wowote lakini itakuwa si chini ya wawili.

**31.** Malipo ya wakurugenzi yataamuliwa kila baada ya muda na kampuni katika mkutano mkuu. Malipo hayo yatachukuliwa kuchumwa kutoka siku hadi siku. Wakurugenzi watalipwa pia gharama zote kusafiri, hoteli na matumizi mengine yaliyofanywa ipasavyo na wao katika kuhudhuria na kurudi kutoka mikutano ya wakurugenzi au ya kamati yoyote ya wakurugenzi au mikutano mkuu wa kampuni au kuhusiana na shughuli za kampuni.

Uwezo wa Kukopa

**32.** Mkurugenzi anaweza kutumia madaraka yote ya kampuni ya kukopa fedha, na kuweka rahani au kulipa ahadi yake na mali, au sehemu yake yoyote, na kutoa dhamana, dhamana ya bidhaa na dhamana nyengine, ama moja kwa moja au kama dhamana ya deni lolote, dhima au wajibu wa kampuni au mtu yeyote wa tatu.

Mamlaka na Majukumu ya Wakurugenzi

**33.** Bila ya kuathiri masharti ya Sheria, mkataba na kanuni na maagizo yoyote yaliyotolewa na azimio maalumu, shughuli za kampuni zitasimamiwa na wakurugenzi, ambao wanaweza kutumia madaraka yote ya kampuni. Hakuna mabadiliko ya mkataba au kanuni na maelekezo yatabatilisha kitendo kilichotekeleza kabla na wakurugenzi ambacho vyenginevyo kingekuwa halali. Madaraka yanayotolewa na kanuni hii hayatapunguza na nguvu yoyote maalumu waliyopewa wakurugenzi na kanuni na mkutano wa wakurugenzi ambao akidi ipo unaweza kutumia madaraka yote yanayoweza kutumiwa na wakurugenzi.

**34.** Wakurugenzi wanaweza kwa nguvu ya wakili kumteua mtu yeyote kuwa mwanasheria au wakala wa kampuni kwa madhumuni hayo na kwa masharti kama watakayoweka, ikiwa ni pamoja na mamlaka ya wakili au wakala kugawa yote au yoyote ya madaraka yake.

**35.** Hundi zote, hati za ahadi, rasimu, hawala na nyaraka nyengine zinazobadilishika, na risiti zote kwa fedha zinazolipwa kwa kampuni, zitatiwa saini, kutolewa, kukubalika, kuthibitishwa, au vyenginevyo kutekelezwa, kama hali itakavyokuwa, kwa namna ambayo wakurugenzi kila baada ya muda kwa azimio wataamua.

**36.** Wakurugenzi watawezesha kumbukumbu kuwekwa katika vitabu vilivyotolewa kwa ajili ya:-

(a) ya uteuzi wote wa maofisa uliofanywa na wakurugenzi;

(b) ya majina ya wakurugenzi waliokuwepo katika kila mkutano wa wakurugenzi na wa kamati yoyote ya wakurugenzi;

(c) ya maazimio yote na kumbukumbu katika mikutano yote ya kampuni, na ya wakurugenzi, na ya kamati ya wakurugenzi.

Kutokuwa na Sifa Wakurugenzi

**37.** Ofisi ya mkurugenzi itakuwa wazi kama mkurugenzi:-

(a) bila ya ridhaa ya kampuni katika mkutano mkuu anashikilia ofisi yoyote nyengine ya faida chini ya kampuni; au

(b) amefilisika au anafanya mpango wowote au ushirikiano na wakopeshaji wake kwa ujumla; au

(c) atakoma kuwa mkurugenzi kwa mujibu wa masharti yoyote ya Sheria au anapigwa marufuku na sheria kuwa mkurugenzi; au

(d) anakuwa hana akili timamu; au

(e) amejiuzulu wadhifa wake kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa kampuni; au

(f) moja kwa moja au si moja kwa moja kuwa na maslahi katika mkataba na kampuni na anashindwa kutangaza aina ya maslahi yake kwa namna iliyotakiwa na sheria.

Mkurugenzi hatapiga kura kuhusiana na mkataba wowote ambao yeye ana maslahi au jambo lolote linalotokana nao, na kama yeye anafanya hivyo kura haitahesabiwa.

**38.** Kampuni inaweza kwa azimio la kawaida kumteua mtu ambaye yuko tayari kufanya kazi kama mkurugenzi kujaza nafasi au kuwa mkurugenzi wa ziada.

**39.** Wakurugenzi wanaweza kumteua mtu ambaye yuko tayari kuwa mkurugenzi, ama kujaza nafasi au kama mkurugenzi wa ziada, lakini ili kwamba jumla ya idadi ya wakurugenzi haitazidi kwa wakati wowote idadi iliyowekwa na au kwa mujibu wa kanuni hizi. Mkurugenzi yeyote aliyeteuliwa hivyo atashika madaraka mpaka mkutano mkuu wa mwaka ujao, na kisha atakuwa na haki ya kuchaguliwa tena.

**40.** Kampuni inaweza kwa azimio la kawaida, ambalo taarifa maalumu imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 148 cha Sheria, kumuondoa mkurugenzi yeyote kabla ya kumalizika kipindi chake cha ofisi bila ya kujali kitu chochote katika kanuni au makubaliano yoyote kati ya kampuni na mkurugenzi huyo. Kuondolewa huko kutakuwa bila ya kuathiri madai yoyote mkurugenzi anayoweza kuwa nayo kutokana na uharibifu kwa uvunjaji wa mkataba wowote wa huduma kati yake na kampuni.

**41.** Kampuni inaweza kwa azimio la kawaida kumteua mtu mwengine katika nafasi ya mkurugenzi aliyeondolewa katika ofisi chini ya kanuni iliyotangulia hapo juu. Bila ya kuathiri madaraka ya wakurugenzi chini ya kanuni ya 40 kampuni katika mkutano mkuu inaweza kumteua mtu yeyote kuwa mkurugenzi ama kujaza nafasi au kama mkurugenzi wa ziada.

Mikutano ya Wakurugenzi.

**42.** Kwa mujibu wa masharti ya kanuni, wakurugenzi wanaweza kusimamia mikutano yao kama wanavyofikiri inafaa. Masuala yanayotokea katika mkutano yataamuliwa kwa wingi wa kura. Katika hali ya usawa wa kura, mwenyekiti atakuwa na kura ya pili au kura ya uamuzi. Mkurugenzi anaweza, na katibu kwa ombi la mkurugenzi huyo, kuitisha mkutano wa wakurugenzi. Haitakuwa lazima kutoa taarifa ya mkutano wa wakurugenzi kwa mkurugenzi yeyote ambaye hayupo Zanzibar.

**43.** Akidi ya lazima kwa ajili ya kutekeleza shughuli inaweza kuwekwa na wakurugenzi, na isipokuwa kama haikuwekwa itakuwa wawili.

**44.** Wakurugenzi wanaoendelea wanaweza kufanya kazi bila ya kujali nafasi yoyote, lakini ikiwa na maadamu idadi yao imepungua chini ya idadi iliyowekwa na au kwa mujibu wa kanuni za kampuni kama akidi ya lazima ya wakurugenzi, wakurugenzi wanaoendelea au mkurugenzi anayeendelea anaweza kufanya kazi kwa madhumuni ya kuongeza idadi ya wakurugenzi kutimiza idadi hiyo, au ya kuitisha mkutano mkuu wa kampuni, lakini si kwa madhumuni mengine.

**45.** Wakurugenzi wanaweza kumteua mmoja miongoni mwao kuwa mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi na kuamua kipindi ambacho yeye atashikilia ofisi. Isipokuwa kama yeye hataki kufanya hivyo, mkurugenzi aliyeteuliwa ataongoza kila mkutano wa wakurugenzi ambao yeye yupo. Lakini kama hakuna mwenyekiti aliyeteuliwa, au kama yeye hataki kuwa mwenyekiti, au kama katika mkutano wowote mwenyekiti hayupo ndani ya dakika tano baada ya wakati uliowekwa kwa ajili ya kufanya mkutano, wakurugenzi waliopo wanaweza kumchagua mmoja miongoni kuwa mwenyekiti wa mkutano.

**46.** Wakurugenzi wanaweza kukasimu madaraka yao yoyote kwa kamati yoyote yenye wakurugenzi mmoja au zaidi; kamati yoyote iliyoundwa hivyo itakuwa katika utekelezaji wa mamlaka iliyokabidhiwa inafuata kanuni zozote ambazo zinaweza kuwekwa juu yao na wakurugenzi. Bila ya kuathiri kanuni nyengine yoyote, mikutano ya kamati yenye wanachama wawili au zaidi itaongozwa na kanuni zinzosimamia mikutano ya wakurugenzi maadamu zinaweza kutumika.

**47.** Matendo yote yaliyofanywa na mkutano wa wakurugenzi au wa kamati ya wakurugenzi au na mtu yeyote anayekaimu kama mkurugenzi, bila ya kujali kwamba baadaye ilibainika kwamba kulikuwa na kasoro katika uteuzi wa mkurugenzi yeyote, au kwamba yeyote kati yao alikuwa hastahiki kushika madaraka, au alikuwa ameacha ofisi, au alikuwa hana haki ya kupiga kura, yatakuwa halali kama vile kila mmoja wa watu hao alikuwa ameteuliwa kihalali na alikuwa na sifa na aliendelea kuwa mkurugenzi na alikuwa na haki ya kupiga kura.

**48.** Azimio kwa maandishi, lililotiwa saini na wakurugenzi wote wenye haki ya kupokea taarifa ya mkutano wa wakurugenzi, au wa kamati ya wakurugenzi, litakuwa halali na kutumika, kama kwamba lilikuwa limepitishwa katika mkutano wa wakurugenzi au (kama itakavyokuwa) wa kamati ya wakurugenzi ulioitishwa kihalali na uliofanyika, na unaweza kuwa na nyaraka nyingi katika fomu zinazofanana kila moja iliyotiwa saini na mkurugenzi mmoja au zaidi.

Katibu.

**49.** Katibu atateuliwa na wakurugenzi kwa kipindi, kwa malipo na kwa masharti wanayoona yanafaa; na katibu yeyote aliyeteuliwa hivyo anaweza kuondolewa na wao.

**50.** Masharti ya Sheria au kanuni hizi yanayotaka au kuidhinisha kitu kufanywa na au kwa mkurugenzi na katibu hayatatoshelezwa kwa kufanywa kwake na au kwa mtu huyo huyo anayefanya kazi kama mkurugenzi na kama, au badala ya, katibu.

**51.** Muhuri utatumika kwa idhini ya wakurugenzi tu au ya kamati ya wakurugenzi iliyoidhinishwa na wakurugenzi. Wakurugenzi wanaweza kuamua nani atatia saini hati yoyote ambayo imepigwa muhuri na isipokuwa kwamba imeamuliwa vyenginevyo itatiwa saini na mkurugenzi na katibu au na mkurugenzi wa pili. Muhuri.

**52.** Wakurugenzi watawezesha kuwekwa vitabu vya hesabu vinavyofaa kuhusiana na:- Hesabu.

(a) fedha zote zilizopokelewa na kutumiwa na kampuni na mambo yanayohusiana na mapato na matumizi ambayo hufanyika;

(b) mauzo yote na ununuzi wa bidhaa unaofanywa na kampuni; na

(c) rasilimali na madeni ya kampuni.

Vitabu vya raslimali havitahesabiwa kuwa vimewekwa kama hakutawekwa vitabu vya hesabu vya lazima vyenye kuonesha hali ya ukweli na ya haki ya shughuli za kampuni na kuelezea shughuli zake za biashara.

**53.** Vitabu vya hesabu vitatunzwa kwenye ofisi iliyosajiliwa ya kampuni, au chini ya kifungu cha 154(4) cha Sheria, katika mahali pengine au maeneo mengine kama wakurugenzi watakavyoona inafaa, na vitakuwa daima wazi kwa ukaguzi wa wakurugenzi.

**54.** Mwanachama yeyote hatakuwa na haki yoyote ya kukagua kumbukumbu zozote za uhasibu au kitabu chengine au hati ya kampuni isipokuwa kama ilivyotolewa na sheria au ilivyoidhinishwa na wakurugenzi au kwa azimio la kawaida la kampuni.

**55.** Wakurugenzi kila baada ya muda kwa mujibu wa vifungu vya 156, 158 na 164 vya Sheria, watawezesha kutayarishwa na kuwekwa mbele ya kampuni katika mkutano mkuu, hesabu za faida na hasara, mizania, hesabu za vikundi, ikiwa zipo, na ripoti kama zilizvyoelezwa katika vifungu hivyo.

**56.** Kwa mujibu wa kifungu cha 165 cha Sheria, nakala ya hesabu za kampuni za kila mwaka kuwasilishwa mbele ya kampuni katika mkutano mkuu pamoja na nakala ya ripoti ya mkurugenzi na ripoti ya mkaguzi wa haitapelekwa chini ya siku ishirini na moja kabla ya tarehe ya mkutano kwa kila mwanachama, na kwa kila mmiliki wa dhamana za kampuni. Isipokuwa kwamba kanuni hii haitahitaji nakala ya hati hizo kupelekwa kwa mtu yeyote ambaye anwani yake kampuni haiitambui au zaidi ya mmoja wa wamiliki wa pamoja wa dhamana yoyote.

**57.** Wakaguzi atateuliwa na majukumu yao yatawekwa kwa mujibu wa vifungu vya 166-169 vya Sheria. Ukaguzi.

**58.** Taarifa yoyote inayopasa kutolewa kwa au na mtu kwa mujibu wa kanuni itakuwa kwa maandishi isipokuwa kwamba taarifa ya kuitisha mkutano wa wakurugenzi haina lazima ya kuwa kwa maandishi. Kampuni inaweza kutoa taarifa yoyote kwa mwanachama ama binafsi au kwa Matangazo.

kumpelekea kwa njia ya posta katika bahasha iliyolipiwa yenye anwani ya mwanachama ya ofisi yake iliyosajiliwa, au kwa kuitua katika anuani hiyo. Ambapo taarifa imepelekwa kwa njia ya posta, kupelekwa taarifa hiyo kutachukuliwa kuwa kumetekelezwa vizuri kwa kuwekwa anwani sahihi, kulipiwa kabla, na kutiwa posta barua yenye taarifa, na kuweza kutekelezwa kabla ya kumalizika muda wa saa sabiini na mbili baada ya barua yenye taarifa kutiwa posta. Mwanachama ambaye anwani yake iliyosajiliwa haimo ndani ya Zanzibar na ambaye anatoa kwa kampuni anuani iliyomo ndani ya Zanzibar ambayo taarifa zinaweza kupelekwa kwake atakuwa na haki ya kupewa taarifa kwa anuani hiyo, lakini vyenginevyo hakuna mwanachama kama huyo atakayekuwa na haki ya kupokea taarifa yoyote kutoka kwenye kampuni.

| Majina, anuani na maelezo ya mteja | Idadi ya Hisa zilizochukuliwa na | Saini ya kila mteja ya wanachama |
|---|---|---|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |

Jumla ya hisa zilizochukuliwa ________________________________

Saini ya aliyewashuhudia hao hapo juu

Jina: ....................................................

Anuani: ................................................

Sifa: ....................................................

Sahihi: .................................................

Tarehe hii siku ya ___ ___________, 20__

## JADWELI D
## KATIBA NA KANUNI ZA USHIRIKIANO ZA KAMPUNI YENYE UKOMO WA DHAMANA NA YENYE MTAJI WA HISA

Katiba ya Ushirikiano

ni

**1.** Jina la kampuni ni "__________________________Yenye Ukomo".

**2.** Ofisi iliyosajiliwa ya kampuni ipo _____________________

**3.** Malengo ambayo kwayo kampuni imeundwa ni,

**4.** Dhima ya wanachama ina ukomo.

**5.** Kila mwanachama wa kampuni anaahidi kuchangia kwenye raslimali za kampuni endapo itafungwa wakati yeye akiwa ni mwanachama, au ndani ya mwaka mmoja baadaye, kwa ajili ya kulipa madeni na dhima za kampuni zilizotiliana saini mkataba kabla ya yeye kusita kuwa mwanachama, na gharama, malipo na matumizi ya ufungaji, na kwa ajili ya kurekebisha haki za wachangiaji miongoni mwao, kima ambacho kitahitajika kisichozidi shilingi …………………..

**6.** Jumla ya hisa za kampuni itakuwa na shilingi ______________ zilizogawanywa katika hisa ____________ za shilingi ____________ kila moja.

Sisi, watu ambao majina yao na anwani zao zimeandikwa, tunataka kuanzisha kampuni, kufuatana na mkataba huu wa ushirikiano, na kutokana na hivyo tunakubali kuchukua idadi ya hisa katika mtaji wa kampuni zilizoainishwa sambamba na majina yetu.

| Majina, anwani na maelezo ya mchangiaji | Idadi ya hisa zilizochukuliwa na kila mchangiaji | Saini za wachangiaji |
|---|---|---|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |

Saini ya aliyewashuhudia hao hapo juu.
Jina: ……………………………………......…
Anwani: ……………………………….....…
Sifa : …………………………………......…
Saini : ……………………………….....…
Tarehe ____ mwezi wa ____________, 20___

**KANUNI ZA USHIRIKIANO ZA KAMPUNI KUTANGULIA KATIBA YA USHIRIKIANO**

**1.** Idadi ya wanachama ambao kampuni inapendkeza kusajiliwa ni …………., lakini wakurugenzi wanaweza kila baada ya kipindi kusajili wanachama zaidi.

**2.** Kanuni za Jadweli A iliyowekwa kwenye Sheduli ya Sheria ya Kampuni zitachukuliwa kuwa zimeingizwa kwenye kanuni hizi na zitatumika kwa kampuni.

**3.** Sisi, watu ambao majina yao na anwani zao zimeandikwa, tunataka kuanzisha kampuni, kufuatana na mkataba huu wa ushirikiano, na kutokana na hivyo tunakubali kuchukua idadi ya hisa katika mtaji wa kampuni zilizoainishwa sambamba na majina yetu.

| Majina, anwani na kazi ya mchangiaji | Saini za wachangiaji |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |
| 4. | |
| 5. | |

Saini ya aliyewashuhudia hao hapo juu.
Jina: …………………………………..……
Anwani: ……………………………………
Sifa : ……………………………………….
Saini : ………………………………………
Tarehe ____ mwezi wa ___________, 20___

## JADWELI E
## KANUNI ZA UENDESHAJI WA KAMPUNI BINAFSI YA MWANACHAMA MMOJA YENYE UKOMO

Tafsiri

**1.** Katika tafsiri ya kanuni hizi maneno yafuatayo yatakuwa na maana zifuatazo isipokuwa pale ambapo zinakirihi au zinapingana na kanuni za suala linalohusika:-

"mkurugenzi mbadala mteule" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na mwanachama mmoja kuwa mkurugenzi mteuliwa katika hali ya kukosekana mkurugenzi mteule;

"kampuni" au "kampuni hii" maana yake ni XYZ (Kampuni ya Mwanachama Mmoja-Binafsi) yenye ukomo;

"wakurugenzi" au "bodi ya wakurugenzi" maana yake ni bodi ya wakurugenzi ambayo itakuwa na mkurugenzi mmoja tu au zaidi ya mkurugenzi mmoja endapo watachaguliwa chini ya masharti yanayofaa ya Sheria hii;

"kwa maandishi" mana yake ni yenye kuandikwa kwa mkono au kwa kupigwa chapa au kuandikwa kifungu kwa mkono na kifungu kwa kupigwa chapa au kwa kutumia jiwe au kwa taipureta au kwa kibadala chengine cha uandishi;

"mwanachama mkurugenzi" maana yake ni mtu anayekuwa mkurugenzi kutokana na kuwa mwanachama wa kampuni kwa mujibu wa kifungu kidogo (h) cha kifungu cha 187;

"mkurugenzi mteule" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na mwanachama mmoja kuwa mkurugenzi endapo atafariki mwanchama mmoja pekee;

"kampuni binafsi" maana yake ni kampuni binafsi ambayo si kampuni ya mwanachama mmoja;

"kanuni " maana yake ni kanuni ya Kanuni za Kampuni za Mwanachama Mmoja;

"kifungu" maana yake ni kifungu cha Sheria ya Kampuni; na

"mkurugenzi pekee" maana yake ni mkurugenzi wa kampuni ambaye kwa wakati huu ni mkurugenzi pekee na ni mwanachama mmoja wa kampuni.

Utangulizi

**2.** Sharti lolote la Sheria au taratibu na kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hiyo ambazo zinatumika kuhusiana na kampuni binafsi yenye ukomo wa hisa iliyoundwa chini ya Sheria hii, kama hapana sharti jengine lolote linaloeleza vyenginevyo, litatumika kuhusiana na kampuni ya mwanchama mmoja kama inavyotumika kuhusiana na kampuni ambayo imeundwa na watu wawili au zaidi au yenye wanachama wawili au zaidi.

Kampuni ya Mwanchama Mmoja

**3.** Kampuni ni kampuni ya mwanachama mmoja na kwa kuwa ni kampuni binafsi yenye ukomo wa hisa:-

(a) haitatoa mwaliko kwa umma wa kuchangia hisa yoyote ya kampuni;

(b) kampuni haitasajili hisa yoyote au hisa zozote kwa jina la watu wawili au zaidi kumiliki hisa moja au zaidi mmoja mmoja au kwa pamoja; na

(c) idadi ya wanachama wa kampuni itabakia kuwa mmoja.

**HISA**

**4.** kampuni inaweza kuongeza jumla ya hisa za msingi kulingana na kifungu cha 70 na 72.

**5.** Cheti au vyeti vya hisa vitatolewa vikiwa na muhuri wa kampuni na vitatiwa sini na mkurugenzi mwanachama, na endapo amefariki, na mkurugenzi mteule na katibu.

**6.** Kampuni inaweza, baada ya kupitisha azimio maalumu, kutoa hisa zaidi au kuhaulisha hisa zilizopo au sehmu yake kufanya idadi ya wanachama kuwa wawili au zaidi kulingana na taratibu lakini itakuwa kampuni ya binafsi baada ya hapo.

**7.** Kampuni haitahaulisha hisa zote za mwanachama pekee kwa watu wawili au zaidi au sehemu ya hisa za mwanacham pekee kwa mtu au watu wengine au kugawa hisa zaidi kwa mtu yeyote zaidi ya mwanachama pekee au, wakati wowote, kuruhusu kuhaulisha hisa au ugawaji wa hisa au yote mawili na hivyo kupelekea idadi ya wanachama kuwa wawili au zaidi, isipokuwa kwa idhini ya azimio maalumu la kubadilisha hadhi kutoka kampuni ya mwanachama mmoja kuwa kampuni binafsi na kubadilisha kanuni zake ipasavyo.

**8.** Mwanachama pekee anaweza kuhaulisha hisa zake zote kwa mtu mmoja kwa idhini ya azimio la kawaida ambapo kampuni itabakia kuwa ya mwanachama mmoja kama ilivyokuwa kabla ya uhaulishaji huo.

**9.** Mtu ambaye jina lake limesajiliwa kuwa ni mwanachama katika daftari la wanachama atastahiki kupata, ndani ya siku tisiini baada ya kugawa au ndani ya siku arubaini na tano za maombi ya usajili wa uhaulishaji, cheti chenye muhuri chenye kuainisha hisa moja au hisa nyingi zinazomilikiwa naye.

Uhaulishaji na Uwasilishaji wa Hisa

**10.** Uhaulishaji na uwasilishaji wa hisa utakuwa kwa mujibu wa masharti ya vifungu vya 80 hadi 87.

**11.** Endapo mwanachama pekee atafariki, uwezo wa kusajili au kukataa uhaulishaji wa hisa utatekelezwa na katibu na mkurugenzi mteule kwa mujibu wa taratibu.

**12.** Ikiwa kampuni inagawa hisa zaidi au hisa zinazomilikiwa na mwanachama pekee zinahaulishwa kwa pamoja au kwa sehemu na kwa kufanya hivyo kampuni inakuwa kampuni binafsi, ukweli kwamba imebadilika kutoka kampuni ya mwanachama pekee na kuwa kampuni binafsi na idadi ya wanachama wake imeongezeka kuwa wawili au zaidi utarikodiwa katika daftari la wanachama pamoja na tarehe ya tukio hilo na taarifa za wanachama.

**13.** Uhaulishaji wa hisa kwa warithi halali utarikodiwa katika daftari la wanachama na katibu na mkurugenzi mteule.

Kubadilisha Hadhi.

**14.** Kampuni inaweza kujibadilisha kutoka kampuni binafsi ya mwanachama mmoja kuwa kampuni binafsi kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 4.

**15.** Mkutano mkuu, utakaoitwa mkutano mkuu wa mwaka, utaitishwa, kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 137 na kanuni ya 5.

**16.** Mikutano yote mikuu ya kampuni ukiacha mkutano mkuu wa mwaka kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 138 itaitwa mikutano mikuu ya dharura na italazimika kufanywa kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 5.

**17.** Katibu atahudhuria mikutano yote ya kampuni lakini hatakuwa na kura.

Taarifa na Mwenendo wa Mikutano Mikuu.

**18.** Iwapo sheria inaainisha kipindi cha wakati cha kutoa taarifa ya mkutano wowote wa wanachama au mkurugenzi au wakurugenzi, matakwa ya sheria yatachukuliwa kuwa yamefuatwa ikiwa katibu na wanachama wanaarifiwa kuhusu mkutano na wanahudhuria mkutano huo isipokuwa kwamba kwa mkutano mkuu wa mwaka kipindi cha muda cha kutoa taarifa kwa mkaguzi wa kampuni kitakuwa si chini ya siku ishirini na moja.

**19.** Mwanachama pekee aliyehudhuria yeye mwenyewe au kwa kuwakilishwa atafanya akidi ya mkutano mkuu isipokuwa kwamba katibu hataweza kumwakilisha mwanachama pekee.

**20.** Ikiwa mwanchama pekee anafanya maamuzi yoyote ambayo yanatakiwa kuchukuliwa katika mkutano wa bodi au katika mkutano mkuu au kwa njia ya azimio na uamuzi huo ukawasilishwa na mwanachama pekee kwa maandishi, ndani ya siku tatu baada ya maamuzi hayo kutolewa, kwa kampuni kwa kuingizwa katika kitabu cha kumbukumbu na kurikodiwa, maamuzi hayo yatakuwa halali kama kwamba yamekubaliwa katika mkutano huo.

Mkurugenzi.

**21.** Kampuni itakuwa daima na mwachama pekee kama mkurugenzi lakini, inaweza kuwa na idadi nyengine ya wakurugenzi ambao wanatimiza masharti kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 90.

**22.** Bodi ya mkutano mkuu haitakuwa na uwezo wa kumuondoa mwanachama mkurugenzi lakini mwanachama pekee (mwanachama

mkurugenzi) atakuwa na uwezo wa kumuondoa mkurugenzi yeyote, mtendaji mkuu au katibu kwa kupitishs azimio.

**23.** Mkurugenzi atakuwa na uwezo kama ulivyoainshwa katika kifungu cha 36.

**24.** Mkurugenzi atateua mtendaji mkuu kwa mujibu wa vifungu vya 17 na 38.

Katibu

**25.** Mkurugenzi ataelekeza kumbukumbu kuweka katika vitabu kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 152.

**26.** Kampuni binafsi ya mwanachama pekee yenye ukomo itateua katibu kwa mujibu wa vifungu vya 191, 192 na kanuni ya 6 ambaye atakuwa na wajibu wa kutekeleza kazi ambazo kwa kawaida zinatekelezwa na katibu chini ya sheria ya mashirika na kawaida ya ukatibu.

**27.** Katibu atateuliwa wakati wa kuandikisha kampuni na badaye siku ile ile au siku inayofuata kujiuzulu kwake au kuondolewa au endapo amefariki ndani ya siku saba baada ya tukio.

**28.** Mkurugenzi pekee hatakuwa katibu wa kampuni.

Mikataba na Mwana-chama Pekee.

**29.** Mkataba baina ya kampuni na mwanachama pekee utafanywa kulingana na masharti ya kanuni ya 8.

**30.** Kampuni inaweza kutangaza gawio na kulipa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 184.

Hesabu.

**31.** Mkurugenzi au wakurugenzi watawezesha kuweka vitabu vinavyofaa vya hesabu kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 154 na, kama inavyotakiwa na vifungu vya 156, 158 na 164, atawezesha kutayarishwa na kuwasilishwa kwenye mkutano mkuu wa kampuni hesabu za faida na hasara au hesabu za mapato na matumizi na mizania ambazo zimeshakaguliwa na ripoti kama zinavyotajwa katika vifungu hivyo. Katika vipengele vyote zitakuwa zinafuata masharti ya vifungu vya 154 na 160.

**32.** Kwa muda wote ambapo kampuni ina mkurugnzi mmoja tu, matakwa ya kifungu cha 241 kitachukuliwa kuwa kimefuatwa iwapo mizania na hesabu za faida na hasara zimethibitishwa na mkurugenzi pekee.

**33.** Wakaguzi watateuliwa na majukumu yao yataratibiwa kwa mujibu wa masharti ya vifungu vya 166 hadi 169.

Muhuri.

**34.** Mkurugenzi atatoa hifadhi yenye usalama kwa ajili ya muhuri na muhuri hautapigwa kwenye waraka wowote isipokuwa kwa idhini ya azimio la bodi ya wakurugenzi au kwa idhini ya kamati ya mkurugenzi ambayo imeidhinishwa kwa mnasaba huo na mwanachama mkurugenzi na katibu au mtu ambaye mkurugenzi anaweza kumteua kwa ajili hiyo; na mwanchama mkurugenzi na katibu au mtu mwengine kama ilivyoelezwa kabla atatia saini kila waraka ambao juu yake umepigwa muhuri wa kampuni mbele yao.

**JADWELI F**
**KATIBA NA KANUNI ZA KUJIUNGA**
**ZA KAMPUNI YENYE MTAJI WA HISA**

Katiba ya Chama

**1.** Jina la kampuni ni

**2.** Malengo ambayo kampuni imeundwa kwayo ni

Sisi, watu ambao majina yao na anwani zao yameandikwa, tunataka kuunda kampuni, kwa mujibu wa katiba hii ya chama, na kwa hivyo tunakubali kuchukua idadi ya hisa katika mtaji wa kampuni zilizowekwa sambamba na majina yetu.

| Majina, anwani na kazi ya mchangiaji | Saini ya mchangiaji |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |
| 4. | |
| 5. | |

Shahidi wa saini za hao hapo juu
Jina: ……………………………………………
Anwani: ……………………………………….
Sifa: ……………………………………………
Saini: ………………………………………….
Tarehe ____ mwezi wa __________, 20___

## KANUNI ZA USHIRIKIANO KUFUATANA NA KATIBA YA CHAMA ILIYOTANGULIA

**1.** Idadi ya wanachama ambayo kampuni inapendekeza kusajiliwa ni _____, lakini wakurugenzi wanaweza kila baada ya muda kusajili wanachama zaidi.

**2.** Jumla ya hisa za kampuni ni shilingi _________________ zilizogawanywa katika hisa _______ za shilingi _____________ kila moja.

**3.** Kampuni inaweza kwa azimio maalumu:-

(a) kuongeza jumla ya hisa kwa kima ambacho kitagawanywa katika hisa za kima ambacho azimio litakiweka;

(b) kuunganisha hisa zake kuwa hisa za kima kikubwa zaidi kuliko hisa zake zilizopo;

(c) kuzigawanya hisa zake katika hisa za kima kidogo zaidi kuliko hisa zake zilizopo;

(d) kufuta hisa zozote ambazo katika siku ya kupitisha azimio hazijachukuliwa au kukubaliwa kuchukuliwa na mtu;

(e) kupunguza jumla ya hisa zake kwa namna yoyote ile.

**4.** Kanuni za Jadweli A zilizowekwa katika Sheduli ya Sheria ya Kampuni (zaidi ya kanuni 34 hadi 36 kwa pamoja) zitachukuliwa kuwa zimejumuishwa kwenye kanuni hizi na zitatumiwa na kampuni.

Saini za wachangiaji

Tarehe ........... mwezi wa 20

Shahidi wa saini za hapo juu

**SHEDULI YA PILI**

*Kifungu cha 256*

**FAINI KWA UKIUKAJI, FAINI NA HATIA**

Zimetayarishwa chini ya kifungu cha …. cha Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2012

**1 Jina, kuanza na tafsiri "Faini ya ukiukwaji"**

1.1 Kwa madhumuni ya kifungu cha 256 cha Sheria hii, kima cha faini ya ukiukaji wa kila siku ni asilimia moja ya faini ambayo inatolewa kwa kosa lililotendwa kwa mara ya kwanza kwa kila siku ya ukiukaji.

**2 Adhabu ya Makosa chini ya Sheria hii**

2.1 Sheduli ya Sheria hii itatumika kuhusiana na namna ambayo makosa chini ya Sheria hii yanapaswa kuadhibiwa baada ya kutiwa hatiani.

2.2 Safu ya kwanza ya Sheduli inaainisha kosa chini ya Sheria hii. Safu ya pili ya Sheduli inaeleza maumbile ya jumla ya kosa. Safu ya tatu ya Sheduli inaonesha adhabu ya juu kabisa, kwa kutozwa faini au kufungwa au adhabu zote mbili, ambayo inaweza kutolewa kwa mtu aliyetiwa hatiani kwa kosa.

2.3 Viwango vya juu kabisa vifuatavyo vya adhabu vinahusu makosa chini ya Sheria hii:

(a) Daraja A - shilingi elfu arubaini. (Hii ni Daraja ya juu kabisa ya faini, iliyowekwa kwa makosa makubwa kabisa chini ya Sheria hii).

(b) Daraja B - shilingi elfu ishirini. (Daraja hii ya faini inahusu makosa makubwa)

(c) Daraja C - shilingi elfu kumi na tano. (Hii ni Daraja ya chini kabisa ya faini, iliyowekwa kwa makosa madogo madogo chini ya Sheria hii)

## SHEDULI

| **Kifungu cha Sheria kinacho-sababisha kosa** | **Aina ya kosa** | **Kiwango cha juu juu cha adhabu** |
|---|---|---|
| | **FAINI KWA UKIUKAJI** | |
| 7(7) | Kampuni kushindwa kutoa taarifa au kuwasilisha waraka wowote kwa Mrajis kama inavyotakiwa na kifungu cha 7(6). | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 9(3) | Kampuni kushindwa kumpa Mrajis taarifa ya kuongezeka idadi ya wanchama zaidi ya idadi iliyosajiliwa.<br>Kampuni kushindwa kufuata matakwa ya kifungu cha 19. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 19(8) | Bodi kubadilisha masharti ya katiba yake au kanuni bila ya ridhaa ya Mrajis. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 20(4) | Kampuni kushindwa kubadilisha jina baada ya kupewa maelekezo na Mrajis. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 21(4) | Kuuza au kuendesha biashara kwa kutumia vibaya maneno "yenye ukomo". | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 26(2) | Kampuni kushindwa kumpeleka mmoja wa wanachama wake nakala ya katiba au kanuni, zinapotakiwa na mwanachama. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 27(2) | Endapo katiba ya kampuni imebadilishwa, kutoa nakala ya katiba ambayo haina mabadiliko yakliyofanywa. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 32(3) | Kushindwa kutoa maelezo kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa Mrajis. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 66(3) | Kampuni kushindwa kudhibiti taarifa za punguzo lililoruhusuwia katika muhtasari wa ununuzi wa hisa inayotoa hisa kwa punguzo. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 70(2) | Kampuni kushindwa kutoa taarifa kwa Mrajis kuhusu kuungana, kugawika, kubadilika kukombolewa au kufutwa hisa. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 71(3) | Kampuni kushindwa kutoa taarifa kwa Mrajis kuhusu kuongezeka jumla ya hisa zaidi ya mtaji ualiosajiliwa. | Faini: ***[Daraja A]*** |

| **Kifungu cha Sheria kinacho-sababisha kosa** | **Aina ya kosa** | **Kiwango cha juu juu cha adhabu** |
|---|---|---|
| 78(5) | Kampuni kushindwa kuwasilisha nakala ya amri iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 78 kwa Mrajis. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 85(2) | Kampuni kushindwa kupeleka taarifa ya kukataa kuhaulisha hisa zozote au dhamana. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 87(2) | Kampuni kushindwa kukamilisha hati kufuatia mgawanyo au uhaulishaji. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 101(3) | Kampuni kushindwa kuwasilisha kwa Mrajis taarifa ya malipo ambayo wameyafanya wao au dhamana ambazo zinahitaji usajili. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 102(2) | Kampuni kushindwa kuwasilishwa kwa Mrajis taarifa za malipo juu ya mali iliyonunuliwa. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 113(2) | Kampuni kushindwa kuwa na ofisi iliyosajiliwa. | Faini: [***Daraja A]*** |
| 113(2) | Kampuni kushindwa kuchora au kubandika jina nje ya ofisi yake au mahali pa biashara. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 116(4) | Kampuni kushindwa kuweka daftari la wanachama, au kushindwa kupeleka taarifa kwa Mrajis kuhusu mahali ambapo dftari la wanachama linawekwa. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 117(4) | Kampuni kushindwa kuweka faharisi ya wanachama. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 125(3) | Kampuni kushindwa kutoa taarifa kwa Mrajis kuhusiana na daftari la ofisi tanzu. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 126(7) | Kampuni kushindwa kupeleka kwenye ofisi yake iliyosajiliwa nakala ya uingiaji kwenye daftari la ofisi tanzu, au kuweka nakala ya daftari lake la ofisi tanzu. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 129(3) | Kampuni kuwa na jumla ya hisa zinazoshindwa kufanya faida ya mwaka. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 130(3) | Kampuni isiyokuwa na jumla ya hisa kushindwa kuwasilisha marejesho ya mwaka. | Faini: ***[Daraja B]*** |

| **Kifungu cha Sheria kinacho-sababisha kosa** | **Aina ya kosa** | **Kiwango cha juu juu cha adhabu** |
|---|---|---|
| 131(2) | Kampuni kushindwa kukamilisha marejesho ya mwaka kufutana na kifungu cha 131. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 132(3) | Kampuni kushindwa kuambatanisha kanuni zinazotakikana kwenye marejesho ya mwaka. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 136(5) | Kampuni kukiuka kuitishaa mkutano mkuu wa mwaka. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 148(5) | Kampuni kushindwa kupelekwa nakala za azimio au makubaliano kwa Mrajis. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 151(4) | Kampuni kushindwa kuweka kumbu-kumbu za mikutano ya kampuni na ya bodi. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 164(3) | Kushindwa kupeleka hesabu za mwaka, ripoti ya wakurugenzi na ripoti ya mkaguzi kwa wale wanaostahiki kuzipata. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 166(3) | Kampuni kushindwa kutoa taarifa kwa Mahakama kwamba hakuna mkaguzi aliyeteuliwa au aliyeteuliwa tena. | Faini: ***[Daraja]*** |
| 167(4) | Kampuni kushindwa kutoa taarifa kwa Mahakama kwamba mkaguzi kaondolewa ofisini. | Fini: ***[Daraja C]*** |
| 209(8) | Kampuni kushindwa kuweka daftari la umiliki wa hisa la wakurugnzi, au kukataa ukaguzi wa daftari hilo au kushindwa kuwasilisha nakala inapotakiwa au kutoa daftari hilo kwenye mkutano mkuu wa mwaka. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 214(7) | Kampuni kushindwa kuweka daftari la wakurugenzi na makatibu, au kukataa ukaguzi wa daftari hilo au kushindwa kuwasilisha taarifa kwa Mrajis. | ***Faini: [Daraja A]*** |
| 215(6)(b) | Kampuni kushindwa kuweka mikataba ya kazi ya wakurugenzi, au kukataa ukaguzi wa mikataba hiyo au kushindwa kuwasilisha taarifa kwa Mrajis. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 219(4) | Kampuni kushindwa kuwasilisha nakala ya amri kwa Mrajis, au kushindwa kuambatanisha nakala ya amri kwenye katiba. | Faini: ***[Daraja B]*** |

| Kifungu cha Sheria kinacho-sababisha kosa | Aina ya kosa | Kiwango cha juu juu cha adhabu |
|---|---|---|
| 221(3) | Kampuni kushindwa kuwasilisha nakala ya amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 221 kwa Mrajis. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 223(4) | Kampuni kushindwa kuwasilishwa nakala ya amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 223 kwa Mrajis. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 247(4) | Kampumi kukiuka katika kufuata kifungu cha 247 (kusambaza nakala ya taarifa) | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 249(2) | Kampuni kushindwa kuweka daftari, faharisi, daftari la kumbukumbu au daftari la hesabu, n.k. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| | **FAINI** | |
| 19(7) | Shirika kubadilisha masharti ya katiba yake au kanuni zake bila ya ridhaa ya Mrajis. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 20(4) | Kampuni kushindwa kubadilisha jina baada ya kupewa maelekezo na Mrajis. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 21(4) | | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 45(3) | Kampuni binafsi kutoa hisa kwa umma au kugawanya hisa kwa dhamiri ya kutolewa hivyo. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 47(3)(b) | Kutoa waraka unaopingana na kanuni. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 48(2) | Kusambaza waraka ulitolewa unaopingana na kifungu cha 48. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 49(4) | Kusambaza waraka uliotolewa bila ya nakala kuwasilishwa kwa Mrajis, au uliowasilishwa bila ya kanuni zilizohitajika. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 56(4) | Kushindwa kufuata masharti yanayohusiana na kutoa maelezo kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 58(3) | Kampuni kushindwa kufuata kifungu cha 58 (masharti kuhusiana na kuomba, kugawanya hisa na dhamana). | Faini: ***[Daraja B]*** |

| **Kifungu cha Sheria kinacho-sababisha kosa** | **Aina ya kosa** | **Kiwango cha juu juu cha adhabu** |
|---|---|---|
| 59(3) | Kampuni kushindwa kufuata kifungu cha 59 (masharti kuhusiana na ugawaji wa hisa na dhamana kushughulikiwa kwenye soko la hisa). | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 60(3) | Kampuni kushindwa kuwasilisha kwa Mrajis marejesho ya mgawanyo. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 61(4) | Kampuni kushindwa kuwasilisha kwa Mrajis maelezo katika utaratibu uliowekwa kama ulivyoainishwa katika kifungu cha 61. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 62(2) | Kampuni kutoa msaada wa pesa kwa ajili ya kununua au kuchangia yenyewe au hisa za kampuni yenye kudhibiti hisa. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 74(4) | Kampuni kushindwa kutangaza azimio maalumu linalopunguza jumla ya hisa zake. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 94(4) | Kampuni kukataa kuruhusu wamiliki wa dhamana au wamiliki wa hisa kukagua daftari la wamiliki wa dhamana, au kukataa kutoa nakala ya hati ya mfuko. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 104(2) | Mtu kuruhusu utoaji wa dhamana, wa cheti cha hisa za dhamana bila ya uthibitisho wa cheti cha usajili kilichotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 103(3). | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 107(3) | Kushindwa kutoa taarifa kwa Mrajis kuhusu uteuzi wa mpokeaji au meneja, au kusita kwake kufanya kazi. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 109(2) | Ofias wa kampuni kuidhinisha au kuruhusu kitu kuachwa kutoka kwenye daftari la malipo. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 110(2) | Ofisa wa kampuni kukataa ukaguzi wa waraka wa malipo au wa daftari la malipo. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 113(2) | Kampuni kushindwa kuchora au kubandika jina lake nje ya ofisi yake au mahali pake pa biashara. | Faini: ***[Daraja]*** |
| 113(3) | Kampuni kushindwa kuchora jina lake kwenye muhuri wake au kushindwa kutaja jina lake na ofisi yake iliyosajiliwa kwenye barua zake na machapisho yake. | Faini: [Daraja B] |

| **Kifungu cha Sheria kinacho-sababisha kosa** | **Aina ya kosa** | **Kiwango cha juu juu cha adhabu** |
|---|---|---|
| 113(4) | Kutumia muhuri au kutoa barua au ankara ambapo jina la kampuni au ofisi iliyosa-jiliwa haikutajwa kwa usahihi juu yake. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 114(2) | Kampuni kushindwa kueleza kima cha mtaji ambapo mtaji ulioidhinishwa umeelezwa. | Faini: ***[Grade B]*** |
| 115(6) | Kampuni kuanza biashara au kutumia uwezo wa kukopa kwa kukiuka kifungu cha 115(1). | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 119(3) | Kukataa kukaguliwa daftari la wanachama au kushindwa kupeleka nakala ya daftari hilo baada ya kuombwa. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 135(9) | Kushindwa kufuata masharti ya kifungu cha 138 (kuhusiana na mkutano uliokubaliwa kisheria au ripoti iliyokubaliwa kisheria). | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 140(2) | Kampuni kushindwa kueleza katika taarifa inayoitisha mkutano kwamba wanachama wanaweza kupiga kura kwa kuwakilishwa. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 141(4) | Wito wa kupiga kura kwa kuwakilishwa uliopelekwa kwa baadhi tu ya wanachama. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 145(7) | Ofisa wa kampuni aliyekiuka katika kusambaza azimio la wanachama kwa ajili ya mkutano wa kampuni. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 148(6) | Kampuni kushindwa kupeleka nakala za azimio au makubaliano kwa Mrajis. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 152(3) | Kukataa ukaguzi wa kumbukumbu za mkutano mkuu; kushindwa kupeleka nakala ya kumbukumbu kwa mjumbe anapoomba. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 161(4) | Mkurugenzi kuthibitisha hesabu ambazo hazifuati matakwa ya sheria. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 162(3) | Kutayarisha, kusambaza au kuwasilisha maelezo ya urari wa hesabu, hesabu ya faida na hasara na ripoti ya Mkaguzi bila kufuata masharti ya kifungu cha 162. | Faini: ***[Daraja A]*** |

| **Kifungu cha Sheria kinacho-sababisha kosa** | **Aina ya kosa** | **Kiwango cha juu juu cha adhabu** |
|---|---|---|
| 164(3) | Kushindwa kupeleka hesabu za mwaka, ripoti ya mkurugenzi na ripoti ya mkaguzi kwa wale wanaostahiki kuzipata. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 168(4) | Mtu ambaye hana sifa kujifanya ameteuliwa kuwa Mkaguzi. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 170(3) | Ofisa wa kampuni kushindwa kutoa madaftari au kutoa taarifa kufuatia amri chini ya kifungu cha 170. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 194(4) | Mtu ambaye hana sifa kuteuliwa kuwa mkurugenzi. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 195(5) | Mtu ambaye hana sifa anayekaimu kama mkurugenzi. | Faini: [Daraja B] |
| 199(2) | Mtu kushindwa kutoa taarifa inayohitajika ya umri au kukaimu kama mkurugenzi chini ya uteuzi usiofaa au uliositishwa. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 207(2)(b) | Mkurugenzi kushindwa kupeleka taarifa ya malipo ya hasara ya ofisi n.k. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 209(8) | Kampuni kushindwa kuweka daftari la umiliki wa hisa la wakurugenzi, kukataa ukaguzi wa daftari hilo au kushindwa kuwasilisha nakala inapohitajika au kuwa-silisha daftari hilo kwenye mkutano mkuu wa mwaka. | Faini: ***[Daraja]*** |
| 212(4) | Kushindwa kufuata masharti ya kifungu cha 212 (wajibu wa kufichua kwa madhumuni ya kifungu cha 209, 210 na 211). | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 213(4) | Mkurugenzi kushindwa kufichua maslahi katika zabuni. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 215(6)(b) | Kampuni kushindwa kuweka mikataba ya kazi ya wakurugenzi, au kukataa ukaguzi wa mikataba hiyo au kushindwa kutoa taarifa kwa Mrajis. | Faini: ***[Daraja C]*** |
| 220(4) | Kampuni kushindwa kufuata matakwa ya kifungu cha 220 (kusambaza taarifa za suluhu). | Faini: ***[Daraja B]*** |

| Kifungu cha Sheria kinacho-sababisha kosa | Aina ya kosa | Kiwango cha juu juu cha adhabu |
|---|---|---|
| 220(5) | Kushindwa mkurugenzi wa kampuni na mdhamini wa wanaomiliki dhamana kutoa taarifa kwa kampuni kuhusu masuala yanayohusu kifungu cha 233. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 232 | Kampuni ya kigeni kushindwa kufuata masharti ya Sehemu ya VI ya Sheria hii. | Faini: ***[Daraja A]*** |
| 238 | Kukiuka sharti lolote miongoni mwa masharti ya vifungu vya 234, 235, 236 and 237. | Faini: ***[Daraja B]*** |
| 245(4) | Mtu kueleza kwa uongo kuwa yeye ni mwanachama au mdai wa kampuni. | Faini: ***[Daraja]*** |
| 249(2) | Kampuni kushindwa kuweka daftari, faharisi, kumbukumbu au daftari la hesabu, n.k. | Faini: ***[Daraja ]*** |
| 255 | Kuuza au kuendesha biashara kwa kutumia vibaya maneno "yenye ukomo". | Faini: ***[Daraja]*** |
| | **Faini na Hatia** | |
| 32(4) | Maelezo ya uongo kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa yaliyowasilishwa kwa Mrajis chini ya kifungu cha 32. | Faini: ***[Daraja]*** |
| | Kampuni kushindwa kuchora jina lake kwenye muhuri. | Faini: ***[Daraja ]*** |
| 52(1) | Kushindwa kuamini maelezo kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa kwa Mrajis. | Faini: ***[Daraja]*** |
| 56(5) | Kushindwa kufuata masharti yanayohusu kutoa tamko kuhusu muhtasari wa ununuzi wa hisa. | Faini: ***[Daraja]*** |
| 75(3) | Mkurugenzi anayetoa hati ya kufilisika bila ya kuwa na sababu zinazostahiki kuhusu uamuzi wake. | |
| 153(4) | Mkurugenzi anayeshindwa kuchukua hatua zote zinazostahiki kuhakikisha kwamba kampuni infuata masharti ya kifungu cha 150 na 152 (hesabu za kampuni) | |
| 154(3) | Mkurugenzi anayeshindwa kufuata masharti ya kifungu cha 154. | |

| **Kifungu cha Sheria kinacho-sababisha kosa** | **Aina ya kosa** | **Kiwango cha juu juu cha adhabu** |
|---|---|---|
| 155(6) | Mkurugenzi anayeshindwa kuchukua hatua zote zinazostahiki kuhakikisha kwamba kampuni inafuata masharti ya kifungu cha 153 (hesabu kuonesha mtazamo wa uhalisi na ukweli/kufuata kanuni. | |
| 156(3) | Mkurugenzi anayeshindwa kufuata masharti ya kifungu cha 156 (wajibu wa kutayarisha hesabu za vikundi). | |
| 163(3) | Mkurugenzi anayeshindwa kuchukua hatua zote zinazostahiki kulingana na kifungu cha 163 (ripoti ya mkurugenzi). | |
| 180(3) | Ofisa wa kampuni anayeharibu, anayepo-potoa au anayeghushi kanuni. | |
| 200(1) | Muflisi ambaye anakaimu kama mkurugenzi. | |
| 201(6) | Mtu anayefanya jambo linalopingana na amri ya kubatilisha. | |
| 217(2) | Kampuni ambayo inakiuka kufuata kifungu cha 212 (majina ya wakurugenzi kutokea kwenye mawasiliano ya kampuni n.k.). | |
| 252 | Mtu ambaye kwa hiari yake anatoa maelezo ya uongo katika waraka wowote unaotakiwa kwa madhumuni ya masharti ya Sheria. | |
| 253 | Mtu ambaye kwa hiari yake na kwa kupewa rushwa anatoa ushahidi wa uongo chini ya masharti ya kifungu cha 253. | |

## MADHUMUNI NA SABABU

Katika utekelezaji wa mageuzi hayo ya mifumo ya uendeshaji wa biashara hapa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeona ipo haja ya kupitiwa na kutungwa upya sheria ya usajili wa makampuni itakayosaidia kuleta mageuzi ya mfumo mzima wa usajili wa makampuni hapa Zanzibar. Mapitio na marekebisho hayo yataweza kuondoa kasoro zilizokuwa zikijitokeza wakati wa uendeshaji wa biashara za makampuni.

Sheria ya usajili ya Makampuni *(Companies Decree Cap. 153)*, iliyopo hivi sasa inatokana na Sheria ya Makampuni ya Uingereza ya mwaka 1948 *(English Companies Act of 1948)* ambayo yenyewe imeshafanyiwa marekebisho mengi na ilifanyiwa mageuzi makubwa mwaka 1985 na yakafuatiwa na mengine yaliyopelekea kuwa na *"English Companies Act"* ya mwaka 2006.

Pamoja na kuwa sheria iliyopo sasa haiendani na wakati na utaratibu, vigezo na mifumo ya kimataifa, lakini pia haitoshelezi mahitaji ya kibiashara ya kisasa yanayokwenda sambamba na sayansi na teknolojia; na hivyo kupelekea kuwa ni kikwazo katika maendeleo ya uendeshaji wa shughuli za makampuni. Hivyo basi kwa kuzingatia mapungufu ya Sheria iliyopo sasa na athari zake, AMMS imeona ipo haja ya kupitiwa na kufanyiwa marekebisho ya sheria hiyo na kupendekezwa rasimu ya sheria mpya ya *"The Companies Act"*.

Rasimu ya sheria hii imetengenezwa kwa kuzingatia mwongozo utakaokwendana sambamba na mfumo wa uboreshaji wa mazingira ya uingiaji na utokaji wa biashara ambao ndio msingi wa mapendekezo ya mageuzi ya mifumo ya uendeshaji wa biashara hapa Zanzibar *(Business Entry, Exit and Security Registration Reforms).*

Mapendekezo ya mfumo wa kisheria wa uingiaji na utokaji wa biashara umefanywa kwa kuzingatia sio tu uzoefu mzuri wa utendaji kimataifa *(international best practices)*, lakini pia kwa ajili ya kukidhi haja ya wafanya biashara na wawekezaji hapa Zanzibar katika kurahisisha mwingiliano na ushindani wa kibiashara hapa Zanzibar.

Rasimu ya sheria inayopendekezwa imezingatia mambo muhimu yafuatayo:

(a) Idadi ya wanahisa: Lengo hapa ni kuanzisha na kurasimisha usajili wa kampuni inayomilikiwa na mtu mmoja au zaidi na kuweza kutambuliwa na sheria ambayo itampa nafasi hata mtu mmoja kuwekeza katika biashara ya uendeshaji wa kampuni.

Kwa mujibu wa kifungu cha 3(1) cha Sheria yetu ya Makampuni, kampuni inaweza kuanzishwa na kuanzia watu 2. Hata hivyo ingawa sheria za makampuni za Tanzania Bara na Kenya bado zina sharti hilo, sheria mpya ya makampuni ya Afrika ya Kusini na ile ya Uingereza ya mwaka 2006 zinaruhusu mtu mmoja au zaidi kuanzisha kampuni. Hali hii pia hivi sasa ndivyo ilivyo katika karibu Ulaya yote. Hata Marekani nako dhana ya msingi ni kuwa mtu mmoja anatosha kuanzisha kampuni/shirika.

Kukubalika kwa mtu mmoja kufungua kampuni (Kif. 3.1) kutaruhusu kutanuka kwa ulinzi wa shughuli za kampuni kwa watu binafsi ambao wanataka kuwekeza au kuanzisha biashara hapa Zanzibar kwani watakuwa wakipata haki na fursa sawa na wengine wenye malengo kama hayo. Hii itaongeza fursa za uwekezaji kwani *"Sole Proprietorship"* huwaweka watu katika hatari ya wao na familia zao kupoteza mali zao binafsi.

(b) Wajibu wa "Katiba na Kanuni za Kampuni" *(Role of Memorandum and Articles of Association)"*: Katiba na Kanuni za Kampuni ndio nyaraka za msingi za uanzishaji wa kampuni kama inavyotakiwa na kifungu cha 14 cha sheria. Katiba ya kampuni ndio inayoeleza, kati ya mambo mengine, madhumuni ya kuanzisha kampuni hiyo yaani kazi au biashara zitakazofanywa na kampuni hiyo *(Objects of the company)*.

Hii imetokana na haja ya kuweka mipaka ya uwezo wa wakurugenzi wa kampuni wa kutofanya lile lililo nje ya madhumuni ya kuanzishwa kwake na hivyo Mahakama kuwa na uwezo wa kuyatangaza yale yote yanayofanywa na kampuni nje ya madhumuni yake kuwa ni *"ultra vires"*. Hii inaonekana ilifanywa kwa madhumuni ya kuwalinda wenye hisa, wawekezaji, wadeni wa kampuni na hata jamii kwa ujumla.

Hata hivyo kutokana na kukuwa kwa ushindani wa kibiashara na uwekezaji, wanahisa, wawekezaji na hata wakurugenzi wa makampuni wamejikuta wakiweka *"objects"* za kampuni refu zinazoweza kuhakikisha kuwa kila aina ya kazi inayoweza kufikirika inaingizwa ili kutanua wigo wa kazi wa kampuni kujiweka salama na msingi wa *"ultra vires"*.

Hali hii ilisababisha utata mkubwa wa kisheria wa msingi huu kwani matendo ya kampuni yaliweza kupingwa mahakamani hata na kampuni yenyewe, mwanahisa, mwekezaji au mdeni ambaye amana yake au deni lake linatishiwa na kampuni husika au wakati mwengine hata na mtu wa tatu.

Athari nyengine ya msingi huu ni kuwa inaweka wajibu kwa yule anaeingia mkataba na kampuni kuhakikisha kwamba anaisoma kikamilifu katiba ya kampuni kabla ya kuingia nayo mkataba ili kujitosheleza kama kampuni inao uwezo wa kuingia mkataba huo.

Zaidi ya hayo, muathirika mkubwa zaidi wa msingi huu amekuwa ni mtu wa tatu ambaye hausiki na udhaifu uliopo kwenye mkataba lakini ni mfaidika na huduma zinazotokana na mkataba huo.

Ni kutokana na hali hii ndio maana nchi nyingi (kwa mfano Uingereza na Tanzania Bara) zimefanya marekebisho ya sheria zao za makampuni na kuutoa msingi huu wa *"ultra vires"* katika sheria zao za makampuni. Hata hivyo, mbali ya kwamba "Katiba ya Kampuni" haiweki tena mipaka juu ya uwezo wa kampuni wa kuingia kwenye mikataba, haimanishi kwamba wakurugenzi wanaweza kufanya lolote kwasababu nguvu zao zinadhibitiwa na sheria. Kwa mfano sheria inawazuia wakurugenzi kuingia mikataba ambayo watafaidika binafsi au watu walio karibu nao. Pia mchakato na utaratibu wa kampuni wa kuingia kwenye mikataba umeboreshwa zaidi ili kuweka mazingira mazuri zaidi ya uendeshaji wa biashara (Kif. 35-37 na 38-44).

(c) Ulinzi wa wanahisa wadogowadogo *(Protection of minority shareholders)*. Ingawa Sheria ya Makampuni iliyopo imezingatia miongozo ya Usimamizi wa makampuni/mashirika *(OECD Principles of Corporate Governance)* lakini kwa kuzingatia hali ya usasa bado yapo baadhi ya mapungufu; kwa mfano Sheria inamtaka mwanahisa kuhudhuria *"physically"* katika Mkutano Mkuu au kutuma mwakilishi. Athari ya sharti hili ni kukwaza ushiriki wa mwanahisa katika uendeshaji wa kampuni yake.

Hii ndio sababu ya misingi kuwekewa mkazo na kuimarishwa katika sheria mpya. Misingi hiyo ni

(i) Haki za wanahisa: Muongoza wa Usimamizi wa makampuni unapaswa kulinda haki za wanahisa na kurahisisha utumiaji wa haki hizo ikiwemo kushiriki katika kupitisha maamuzi ya msingi ya uendeshaji wa kampuni *"in person or in absentia"* (Kif. 150) ikiwemo ya kupiga kura, kuwachagua wajumbe wa bodi pamoja na kupanga malipo na marupurupu yao na ya wafanyakazi wa kampuni, kuihoji bodi, kuelewa taratibu zinazoongoza kampuni kibiashara pamoja na wakurugenzi kufanya kazi kwa uwazi *(transparent)* na kuweka mazingira yatakayowalinda wanahisa wote n.k.

(ii) Wanahisa kuwa na haki zinazowiana *(Equitable treatment of shareholders)*

Muongoza wa Usimamizi wa makampuni unapaswa kuhakikisha kuwa wanahisa wote, ikiwa ni pamoja na wanahisa wadogowadogo na wa kigeni wana haki zinazowiana kwa mujibu wa hisa zao na kwamba wawe na fursa ya kudai haki zao iwapo zitakiukwa. Msingi huu unasisitiza pia kulindwa kwa haki za wanahisa wadogowadogo dhidi ya vitendo viovu vya wanahisa wakubwa.

Wajumbe wa bodi pamoja na maafisa wa kampuni wanakiwa kuweka bayana iwapo kazi yoyote inayofanywa na kampuni ina maslahi binafsi kwao au kwa watu wanaohusiana nao.

(iii) Nafasi na wajibu wa wadau katika uendeshaji wa kampuni; Muongoza wa Usimamizi wa makampuni unapaswa kutambua haki za wadau zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na wawe na fursa ya kuzidai iwapo zitakiukwa.

Wadau hao, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi na vyama vyao vinavyowawakilisha wawe huru kuwasilisha malalamiko yao juu ya matendo yanayokiuka sheria na maadili kwa Bodi; na walindwe kwa kufanya hivyo.

(d) Uwezo/nguvu za Wakurugenzi *(Directors powers)*:

Sheria hii inakusudia kuweka vifungu vitakavyoweza kuwaongoza wakurugenzi kutotumia madaraka yao vibaya; kwani huu ni mmoja wa msingi muhimu wa ulinzi wa haki za wanahisa.

Kama ilivyoelezwa hapo, kwa vile wakurugenzi wamepewa nguvu zaidi katika uendeshaji wa kampuni kutokana na kuondolewa kwa dhana ya "ultra vires", sheria imeweka misingi madhubuti ya kuhakikisha wakurugenzi wanazingatia sheria, kanuni na maadili katika utendaji na uendeshaji wa kampuni. Misingi hiyo ni:-

(i) Wajibu wa kufanya kazi kisheria na kimaadili kwa maslahi ya kampuni na ya wafanyakazi wake ;

(ii) Wajibu wa kufanyakazi kwa malengo yaliyokusudiwa na sio ya kujipatia maslahi binafsi

(iii) Wajibu wa kufanya kazi kitaaluma na kujali zaidi kampuni ;

(iv) Wajibu wa kutojiweka katika nafasi ambapo maslahi ya kampuni na ya kwake binafsi yanakinzana.

(e) Kuweka wajibu kwa kampuni kuwa na regista la usajili wa stakabadhi za mikopo (*debentures)* katika afisi zao: Sheria ilivyo hivi sasa ni kwamba inafikiria tu kuwa kampuni itaweka rejista hilo. Hivyo sheria mpya inaweka ulazima kwa kampuni kuwa rejista hilo na kuwajibika kutoa taarifa kwa msajili wa makampuni juu ya mahali lilipo rejista hilo na iwapo mahali hapo patabadilishwa; hii ni kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wadai na umma pindipo zitakapohitajika juu ya mikopo ambayo kampuni imechukua na amana ambazo imetoa.

(f) Kupunguza hisa za kampuni na kuwalinda wadeni: Kwa mujibu wa sheria iliyopo hivi sasa, ili kuwalinda wadeni wa kampuni, kampuni hairuhusiwi kupunguza mtaji wake isipokuwa kwa masharti yaliyowekwa katika Sheria na tena kwa amri ya mahakama.

Kutokana na haja ya kuipunguzia kazi mahakama, kutokana na uhaba ilionao wa rasilimali watu na fedha, inapendekezwa, kama ilivyo kwa sheria ya makampuni ya Tanzania Bara, kuziruhusu kampuni, pale inapobidi, kupunguza mtaji wake, kwa sharti kwamba ni lazima iitangaze nia yake hiyo kwa umma na kuwataarifu wadeni ili, kama hawaridhiki na hilo, waweze kupinga mahakamani upunguzaji huo. Hali hii itaisaidia Mahakama kuwa na kazi ya kushughulikia kuchambua na kuyatolea maamuzi yale maombi yaliyopingwa tu.

(g) Kuweka mfumo wa usajili wa makampuni utakaoendana na vigezo vya usajili vya kimataifa ambapo pia utahamasisha utoaji wa huduma bora kwa makampuni, wanahisa na wawekezaji wote kwa kuhakikisha kwamba Usimamizi/endeshaji wa makampuni:

(i) unakuza uwazi, unaendana na kufuata sheria za nchi na kuhakisha kwamba mgawanyo wa madaraka mingoni mwa vyomba vya kusimamia na kutekeleza sheria unawekwa bayana;

(ii) unahakikisha kwamba taarifa zote muhimu zinazohusu kampuni, ikiwa ni pamoja na taarifa za fedha, utendaji na umiliki na uendeshaji wakampuni zinatolewa kwa wakati na usahihi;

(iii) wajumbe wa bodi za kampuni wanawajibika kwa kampuni na wanahisa, wanakutenda haki kwa wadau wote na wanazingatia sheria, kanuni, maadili na maslahi ya kampuni

(h) Kuweka na kuunganisha vifungu vya adhabu zitakazototolewa na mahakama iwapo mtu yoyote atakwenda kinyume na masharti ya sheria hii.

Kwa ujumla wa Mswada huu unajula ya Sehemu Kuu Kumi (10) ambazo zimegawika kwenye vifungu (278)

**ZANZIBAR** (ABUBAKARY KH. BAKAR)
8 Julai, 2013 ***Waziri wa Katiba na Sheria***

LIMEPIGWA CHAPA NA MPIGA CHAPA MKUU WA SERIKALI - 2013